BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Thelathini – Tarehe 17 Mei, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA KILIMO:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MHE. RITTA E. KABATI - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MHE. KUNTI Y. MAJALA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA KILIMO:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MWENYEKITI: Umepona? Katibu!

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Swali letu la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa linaelekezwa Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Na. 244

Kukamilisha Maboma ya Shule na Afya – Solwa

MHE. AHMED A. SALUM aliuliza:-

Katika Jimbo la Solwa tayari kuna maboma 158 ikiwemo shule za msingi, sekondari na afya na tayari tumeomba fedha ili kukamilisha maboma hayo:-

Je, ni kiasi gani cha fedha Jimbo hilo limepata ili kukamilisha maboma hayo?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/ 2019, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 29.9 kwa ajili ya kukamilisha maboma 2,392 ya shule za sekondari ambazo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga imepatiwa kiasi cha shilingi milioni 87.5 kwa ajili ya kukamilisha maboma saba ya shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na ukarabati/ujenzi wa vituo vya afya na zahanati 352 kwa gharama ya shilingi bilioni 184.6 ambapo kipaumbele ni ukamilishaji wa maboma yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi. Ukarabati wa vituo 352 unahusisha ukamilishaji wa maboma 199 ya vituo vya afya na zahanati.

Katika Halmashauri ya Wilaya Shinyanga, Serikali imefanya ukarabati wa Kituo cha Afya Samuye na Tinde kwa gharama ya shilingi milioni 900. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2019/2020 kupitia mapato yake ya ndani Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga imetenga kiasi cha shilingi milioni 140 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Salum.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, pamoja na majibu yasiyoridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ni mepesi mepesi sana, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivi, katika Jimbo la Solwa tuna maboma 158, kati ya hayo maboma 40 ni zahanati kwa maana zahanati 32 na nyumba za watumishi ni 10 na maboma 50 ni shule za msingi, 58 tupo kwenye sekondari kwa maana ya maabara. Fedha zinazohitajika ni zaidi ya bilioni 4.7 lakini sijaona *commitment* ya Serikali ya kuniambia kwamba katika mwaka huu wa fedha au mwaka unaofuata tutatenga kiasi fulani kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma haya. Kwa majibu haya, ninaona kabisa kwamba

hata miaka kumi hatuwezi kukamilisha maboma haya ambayo ni nguvu za wananchi tulikwenda kuyakamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Serikali inatoa *commitment* majibu sahihi kwa wananchi wa Jimbo la Solwa kwenda kukamilisha maboma haya hata kwa awamu tatu polepole ili tukamilishe maboma haya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza haya siyo majibu mepesi, kwa sababu Serikali imepeleka fedha shilingi bilioni 29.9 nchi nzima, siyo jambo dogo ni jambo kubwa na la kupongeza. Na Majimbo yote yamepata na Mheshimiwa Mbunge tumetaja kiasi cha fedha ambazo amepata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kumalizia maboma haya ya zahanati, msingi na sekondari ni jambo mtambuka, tunahusisha wadau mbalimbali wa elimu, Serikali yenyewe, Mheshimiwa Mbunge, halmashauri yake na wadau wengine, kwa hiyo hili jambo ni la pamoja. Niseme tu kwamba *commitment* kwa mfano Halmashauri ya Shinyanga wametenga fedha mapato ya ndani milioni 140 kumalizia maboma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza niseme tu kwamba wiki iliyopita Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tano imepeleka fedha shilingi bilioni 68.48 kumalizia maboma ya shule za msingi na halmashauri yake imepata. Kwa hiyo, hii ni *commitment* kubwa, tunaomba hizi fedha zitumike vizuri, cha muhimu wakurugenzi wa halmashauri wanapoleta maboma kule TAMISEMI wawasiliane na Wabunge wao ili wawe kwenye lugha moja, fedha zikienda Wabunge wajulishwe ili waweze kusimamia utekelezaji, fedha iweze kutumika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nimuulize swali Mheshimiwa Waziri katika Mkoa wa Mwanza, katika mgao wa fedha za maboma kwa ajili ya sekondari, Wilaya ya Kwimba haikupangiwa hata senti tano kwa maana hata boma moja, ilisahaulika na tayari tulikuwa tumeshaleta Shule za Sekondari za Wala, Kikubiji, Malya, Wungumarwa, Ndami, Mwabomba, Shilembo, Iseni na Mwangalanga. Mheshimiwa Waziri, tunaomba tupate majibu kwa nini Wilaya ya Kwimba katika mgao huo wa bilioni 29.9 ilirukwa yenye Majimbo mawili na tayari tulikuwa tumeshaweka majina.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Mbunge ameshawasilisha hoja yake hiyo Wizarani na nilimuahidi kwa niaba ya Wizara kwamba watakapoanza kugawa fedha za *EPFR* sekondari maeneo yote siyo kwake tu, maeneo yote ambayo yalivukwa kwa bahati mbaya maana huo haukuwa mpango mahsusi wa makusudi, ilikuwa ni bahati mbaya tu, tutazingatia Kwimba pamoja na maeneo mengine yote ambayo yalirukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niombe, wakati tunaomba taarifa hizi, ndiyo maana nikasema hapa Wakurugenzi na maafisa elimu wetu wa sekondari na msingi, wanapoombwa walete taarifa ya maboma TAMISEMI tunawaelekeza washauriane na kupeana taarifa na Wabunge ili wazungumze kwenye lugha moja. Imegundulika kuna maboma mengine yameletwa na Waheshimiwa Wabunge lakini kule wanasema kwamba hiyo siyo shida kubwa sana. Kwa hiyo, tumesema tunaposema tunahitaji maboma, wakurugenzi na maafisa elimu wakitoa taarifa wapitishe au kushauriana na Waheshimiwa Wabunge ili tuzungumze pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, fedha zikipelekwa kama zilivyopelekwa sasa, tumepeleka bilioni 29.9 kuna baadhi ya Wabunge hawakupewa taarifa, tumepeleka bilioni 68.48 wiki iliyopita, inawezekana Wabunge hawajui;

kwa hiyo, Wabunge wajulishwe ili wajue lakini kama kuna mahali pesa imeletwa kwenye halmashauri una hali mbaya sana kwenye shule ya msingi au sekondari, mkurugenzi anajua anaandika barua kwa Katibu Mkuu TAMISEMI anaomba kubadilisha matumizi ili kutibu shida kubwa, hii nyingine itaendelea kusubiri, asante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni wazi kwamba kwa nchi nzima tuna matatizo makubwa sana ya upungufu wa madarasa. Sasa nilitaka kujua Serikali ina mpango mkakati gani wa kuhakikisha kwamba walau kwa kila mwaka wanajenga madarasa kadhaa wakati wanajua kabisa kwamba *projection* ya idadi ya watoto wanaijua. Sasa nilitaka kujua wana mkakati gani mahsusi wa kuhakikisha kwamba hili tatizo walau kila mwaka watakuwa wanajenga madarasa kadhaa kwa kila mkoa na wilaya. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, mipango yetu imekaaje?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tumeona hiyo changamoto wakati ambapo watoto wanaenda kuingia kidato cha kwanza, darasa la awali na darasa la kwanza ilionekana kuna upungufu mkubwa wa madarasa. Tumeshawaelekeza wakurugenzi wanafahamu, mwaka huu *projection* darasa la saba wanamaliza wangapi, kwa hiyo *vacancy* itakuwa ni kiasi gani, *form four* wanamaliza wangapi, vivo hivyo kidato cha sita, wafanye hiyo kazi na kila halmashauri, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wameelekezwa lakini sisi kwenye bajeti tumetenga zaidi ya bilioni 90 kwa ajili ya kazi hiyo, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii. Pamoja na jitihada kubwa za Serikali zilizofanywa za kupeleka fedha kwa ajili ya kumalizia maboma, bado Wilaya ya Tanganyika kuna uhitaji mkubwa wa kumalizia majengo ambayo yalianzishwa kwa nguvu za wananchi hasa ya shule za sekondari Ablulamatam, Kapalamsenga, Tongwe na Mnyagala kwenye kituo cha afya. Je, ni lini Serikali itawaunga mkono wananchi ambao wamejitolea kwa kiwango kikubwa.

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunatambua kuna uhitaji mkubwa na kuna majengo ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi na wadau mbalimbali na Serikali yenyewe. Na ndiyo maana tuliekeza kwenye fedha ile ya maboma, kazi mojawapo ni kuchangia na kumalizia nguvu za wananchi. Na hata hizi ambazo zimepekwa sawa bilioni 68.48 ambayo ni wiki iliyopita tu, hizi fedha zina maelekezo, humu kuna fedha ambazo zinaenda kwenye ujenzi lakini pia kuna fedha za ku-*balance* ikama, kuna hoja ilikuwepo hapa kwamba kuna walimu wa kike shule moja hakuna walimu wa kiume, au walimu wa kiume hakuna walimu wa kike; wakurugenzi watumie fedha hii walimu walipwe ili waweze ku-*balance* kama kule halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo tumeomba, shule ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, fedha zimeenda kwenye halmashauri yake, ni wao sasa kuangalia je, hiyo fedha itumike namna gani. Lakini kadri tutakapopata uwezo tutakuwa tunazingatia maeneo ambayo yana changamoto kubwa ili kuweza kuondoa hiyo kero lakini hasa kuchangia na kushiriki katika nguvu za wananchi ili wasiendelee kulalamika.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa majibu mazuri, Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea! Swali linalofuata

linaulizwa na Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, ambalo linaelekezwa kwa ofisi ya TAMISEMI.

Na. 245

Hitaji la Vifaa – Tiba Hospitali ya Handeni

MHE. OMARI A. KIGODA aliuliza:-

Hospitali ya Handeni inahudumia karibu Majimbo manne lakini ina upungufu wa vifaa ambao unasababisha wagonjwa wengi kupewa rufaa:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza vifaa ili watu wengi wapate huduma?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Kandege, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri, Ofisi ya Rais –TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma inayofaa katika Hospitali ya Mji Handeni kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018 Serikali imeongeza vifaa tiba muhimu ambavyo ni; *ultra sound, urine chemistry analyzer, gene expert machine* na *cryotherapy machine.* Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya vifaa tiba kila mwaka na katika mwaka wa fedha 2019/ 2020 fedha zitakazotumika kununua vifaa tiba katika Hospitali ya Handeni ni shilingi milioni 96 ikiwa ni ongezeko la shilingi milioni 20 ikilinganishwa na bajeti ya vifaa tiba kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kuondoa msongamano kwenye Hospitali ya Halmashauri ya

Mji Handeni, Serikali katika mwaka wa fedha 2019/2020 imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Handeni. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi milioni 800 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Vituo vya Afya vya Kabuku na Mkata vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni sambamba na ununuzi wa vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 300 ili kuviwezesha vituo hivyo kutoa huduma bora. Serikali inazielekeza halmashauri kuendelea kutenga fedha kwenye bajeti zake kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa vifaa tiba.

MWENYEKITI: Ahsante. Mhesimiwa Omari Kigoda.

MHE. OMARI A. KIGODA: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza Bunge lililopita niliuliza kuhusu suala la ambulance na Mheshimiwa Waziri aliniambia tuendelee kutumia magari ya kawaida mpaka *ambulance* itakapopatikana. Tatizo la magari ya kawaida hayana vifaa maalum vya huduma ya kwanza kwa hiyo wagonjwa wengi wanaotoka pale hospitali kwenda hospitali nyingine wengi wanapoteza maisha njiani. Sasa nauliza tena, je, ni lini tena Serikali itaona umuhimu wa kuipatia Hospitali ya Handeni *ambulance*, asante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu kipekee kabisa nitumie fursa hii kuwapongeza Wabunge wa Mkoa wa Tanga maana maswali ya kuhusiana na afya wiki hii yamekuwa kila leo yakiulizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake ambalo anauliza juu ya umuhimu wa Serikali kuhakikisha kwamba inapatikana *ambulance* kama ambavyo tulishawahi kujibu

hapa, naomba niendelee kumsihi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa kupitia Wizara ya Afya ipo kwenye mchakato katika hatua za mwisho kuhakikisha kwamba *ambulance* zinanunuliwa. Na naamini katika maeneo ambayo yatakumbukwa kuhakikisha kwamba kile tulichoahidi kama Serikali tunatekeleza na yeye atapata. *(Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Hongoli.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Lupembe Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina vituo vinne na kimoja kipo kwenye ujenzi lakini vituo vyote hivi havina vifaa muhimu kama vile *Ultra sound* na *X-ray machines* pamoja na kwamba tunatoa huduma ya upasuaji katika Kituo cha Lupembe.

Je, ni lini Serikali italeta vifaa hivi muhimu sana kwa ajili ya kuwasaidia wananchi waweze kupima baadhi ya vipimo kwenye hivi vituo vya afya? Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hongoli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kabisa, kama kuna Wabunge ambao wanafuatilia masuala ya afya kwenye majimbo yao, ni pamoja na Mheshimiwa Hongoli na hivi karibuni alikuja ofisini na tukakubaliana. Amepata fursa ya Kituo cha Afya cha Kichiwa kinajengwa na naomba uniruhusu, ifike mahali nitaleta orodha ya jinsi ambavyo Serikali imefanya *commitment* na fedha ambazo tumeshalipa *MSD,* kinachosubiriwa ni vifaa kupelekwa. Kama ambavyo nimekuwa nikijibu kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha vituo vya afya vyote ambavyo vinajengwa vinapatiwa vifaa ili vitumike kama ambavyo tumekusudia. *(Makofi)*

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Moshi ilishaleta ombi Serikali Kuu la muda mrefu kidogo, zaidi ya miaka minne, mitano, kuomba kupandishwa hadhi kwa Zahanati za Kata za Longuo, Ng'ambo na Msaranga, lakini bahati mbaya mpaka leo Serikali haijatujibu na tuna tatizo la huduma ya miundombinu ya afya katika Manispaa ya Moshi kwa sababu hatuna hospitali ya wilaya na hospitali ya wilaya Serikali haikuwa tayari kutukubalia ombi letu. Je, ni lini hadhi ya vituo hivyo itapandishwa ili tuwe na vituo vya afya vya kutosha?

MWENYEKITI: Ahsante. Kupandisha hadhi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, uwepo wa zahanati umuhimu wake hauondoki kwa kuondoa zahanati kuifanya eti kituo cha afya, kwa hiyo msimamo wa Serikali kwanza ni suala la uwepo wa zahanati lakini pia na uwepo wa vituo vya afya. Pale ambapo inaonekana kwamba hakuna namna, baada ya kujiridhisha kwamba matakwa yote ya kutoka zahanati kwenda kituo cha afya, hapo ndipo Serikali tunafanya kupandisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sio rahisi kwa swali ambalo Mheshimiwa Mbunge ameuliza bila kujiridhisha kwamba yale matakwa ya kituo cha afya ambayo ni tofauti na zahanati yametimizwa. Inawezekana ndiyo maana na yeye mwenyewe anaridhika kwamba Serikali tunahakikisha tunajenga vituo vya afya tukizingatia ramani lakini pia na eneo ambalo zahanati zinatakiwa kuwepo na vituo vya afya vinatakiwa kuwepo.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kituo cha Afya cha Hamai kilichopo Wilayani Chemba kina upungufu mkubwa wa vifaatiba. Kituo hicho ndicho kinachotumika kama hospitali ya wilaya, kinahudumia wananchi wote wa Jimbo la Chemba, lakini pili, majirani zetu kwa maana ya Chilonwa na Jimbo la Kiteto mpakani kule. Sasa nataka kujua Wizara imejipangaje kutupatia vifaatiba zikiwemo *x-ray machines* pamoja na *ultrasound?* La pili suala zima la *ambulance* yetu, imechoka haitamaniki, haithamaniki. Nataka kupata majibu ya Waziri kuhusiana na hicho kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Jibu moja tu. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika jibu lililotangulia, kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba vituo vyote vya afya vinapelekewa vifaa. Niruhusu nichukue fursa hii kuiagiza *MSD* kuhakikisha kwamba zile oda zote ambazo zimepelekwa kuwe na msukumo wa kuhakikisha kwamba hivyo vifaa vinapatikana mapema ili viweze kutumika katika vituo vya afya kama Serikali tulivyokusudia. Pia ni ukweli usiopingika kwamba *MSD* safari hii wanakwenda kuagiza kutoka kwa *manufacturer,* sio habari ya kuagiza kutoka kwa mtu wa kati na kuna *specifications* ambazo lazima tuzingatie, lakini ni vizuri tukahakikisha jambo hili linafanyika mapema.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, lakini kwa niaba Mheshimiwa Mwambe.

Na. 246

Kutokamilika kwa Miradi ya REA – Momba

MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MHE. DAVID E. SILINDE) aliuliza:-

Zoezi la usambazaji wa umeme wa *REA* katika Wilaya ya Momba bado haujakamilika hadi sasa:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza mchakato wa kupeleka umeme katika kata ambazo hazijafikiwa na miradi hiyo katika Jimbo la Momba?

(b) Je, ni lini mradi wa kuwasha umeme Tarafa ya Kamsamba utakamilika?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Momba ina jumla ya vijiji 72, kati ya hivyo, Vijiji 13 vya Nkangano, Chiwanda, Isanga, Kakozi, Ndalambo, Chitete, Tindingoma, Ntungwa, Mkonko, Kamsamba, Masanyinta, Itumbula na Mpapa, vimepata umeme kupitia Mradi wa *REA II* na wateja wa awali 854 wameunganishiwa umeme. Jumla ya Vijiji 15 vya Halmashauri ya Momba vya Nakawale, Ikana, Ivuna, Ipatikana, Muungano, Myunga, Machindo, Mfuto, Isanga, Tindingoma na Kikozi vimepatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza unaoendelea kutekelezwa na Kampuni ya *STEG International Services.* Kazi za kupeleka umeme katika vijiji hivi itakamilika ifikapo mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa kilometa 168 za njia ya umeme wa msongo wa

kilovoti 33 na kilometa 109 za njia za umeme msongo kilovoti 0.4, kufunga transfoma 37 na kuunganisha wateja wa awali 1,775. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 11.23. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, mkandarasi ameshafunga transfoma 15 kati ya 21 na kuwasha umeme. Jumla ya wateja wa awali 244 wameunganishiwa umeme. Mkandarasi anaendelea na kazi ya kuvuta waya kufunga transfoma katika Vijiji vya Ipata, Mpui, Msungwe na Kapele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Kamsamba ilipatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA* awamu ya pili ambapo kazi ya kusambaza umeme katika baadhi ya vitongoji vya tarafa hiyo inaendelea chini ya *TANESCO* kwa bei ya shilingi 27,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kukamilika kwa Mradi wa *REA* awamu ya tatu, mzunguko wa kwanza, jumla ya vijiji 24 vitapatiwa umeme katika Halmashauri ya Momba. Vijiji 44 vilivyosalia vitapatiwa umeme katika Mradi wa *REA II,* mzunguko wa pili unaotarajia kuanza mwezi Julai, 2020.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri ametaja mkandarasi anayesimamia ujenzi kwenye hivyo vijiji, lakini amekuwa akifanya kazi hii kwa taratibu sana na analalamika kwamba hapewi pesa yake ya kukamilisha kazi zake kwa wakati. Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kutueleza hivi viporo vya *REA II* vitakamilika lini *specifically?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; matatizo yaliyopo Jimbo la Momba kwenye masuala haya ya umeme yanafanana moja kwa moja na shida pia zilizopo kwenye Jimbo la Ndanda, Wilaya ya Masasi, hasa zaidi kwenye Vijiji vya Mkwera, Mumburu, Chipite, Mdenga, Liputu, Ndoro pamoja na Mbaju pamoja na Kata za Msikisi na Mlingula. Vijiji hivyo nilivyovitaja vyote vinapitiwa na umeme mkubwa juu wa kilowati 33 lakini chini wanakokaa wananchi hakuna

umeme. Je, ni lini Serikali kwa makusudi kabisa itatekeleza kazi hii ya kushusha umeme walau kwenye vile vijiji vinavyopitiwa na umeme mkubwa unaoelekea Masasi?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri, nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri katika swali la msingi, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Mwambe katika maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni kweli yapo maeneo yaliyobaki katika utekelezaji wa *REA II* na maeneo yote yaliyobaki katika utekelezaji wa *REA II* yamechukuliwa na Mradi wa *REA III* unaoendelea sasa. Kwa maendeleo yote, hasa katika Jimbo la Mheshimiwa kama alivyotaja, eneo lote la kutoka Sumbawanga kwenda Tunduma kwenda mpaka Mpanda, yaliyobaki yote yamechukuliwa na Mradi wa *REA III* unaoendelea. Kwa hiyo nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya muuliza swali kwamba maeneo yote yaliyobaki yatachukuliwa na *REA III* inayoendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili, ni kweli kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mwambe; maeneo ya Ndanda, hasa eneo la Liputi pamoja na Mbemba pamoja na Kitongoji cha Ndoro, yako chini ya *line* inayopita *KVA* 33, lakini kama ambavyo nimeshatoa utaratibu na Mheshimiwa Mbunge anafahamu, hivi sasa *TANESCO* wanapeleka umeme katika vitongoji vyote hivyo. Bahati nzuri sana Kitongoji cha Ndoro kiko nyuma ya Sekondari ya Ndanda ambayo tayari ina umeme. Kwa hiyo, maeneo haya yatafanyiwa kazi na yatakamilishwa ifikapo mwisho wa mwezi Juni, mwaka huu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa, Wizara yenyewe inakuja, msubiri mtakuja kuuliza vizuri tu. Ndiyo, sasa nyumba

nzima imesimama, naelewa changamoto ya umeme, lakini Serikali inajitahidi.

Haya, Mheshimiwa Njeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nipende tu kuwashukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, waliweza kufanya ziara katika Jimbo la Mbeya Vijijini na katika ziara hiyo waliahidi kuwa wangepeleka umeme katika Kata za Maendeleo, Itawa na Shizuvi, ikiwa ni pamoja na vijiji vinavyolizunguka Jiji la Mbeya. Sasa je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye Kata za Maendeleo, Itawa na Shizuvi?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Mgalu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oran Njeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulitembelea Mkoa wa Mbeya, hususan Jiji la Mbeya na si chini ya mara mbili na kuwaahidi wananchi wa Kata za Maendeleo na Kata ambayo ameitaja ya Itawa, kwamba tutawapatia umeme na hususan katika mradi unaoendelea wa ujazilizi awamu ya pili, mzunguko wa kwanza, ambao hatua za manunuzi zimeshakamilika na kiasi cha shilingi bilioni 169 zimetengwa. Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa tisa ambayo itapata fursa ya ujazilizi awamu ya pili, mzunguko wa kwanza kama ambavyo imepata fursa ya ujazilizi awamu ya kwanza kutokana na mahitaji makubwa. Kwa hiyo nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na nimuahidi kwamba maeneo haya yatapatiwa umeme katika mradi ambao utaanza Julai, 2019. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ester Mahawe. Tunaendelea.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Maige.

MWENYEKITI: Hapana, ngojeni, tuwatendee haki wale watu wa nyuma kule; Mheshimiwa Malocha.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali katika *REA* awamu ya pili ilichukua umeme kutoka Mjini Sumbawanga na kupitisha katika jimbo langu kupeleka Mkoa wa Katavi maeneo ya Kibaoni bila kushusha umeme katika Vijiji vya Mbwilo, Mnazi, Kalumbaleza, Mpete, Mtapenda, Mfinga na Kizungu. Je, ni lini Serikali itashusha umeme katika maeneo hayo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze kwa kazi nzuri anayofanya kwenye jimbo lake na yeye mwenyewe anathibitisha tulishafanya ziara pia katika Mkoa wa Rukwa na Jimbo lake zaidi ya mara mbili. Nataka nimwarifu maeneo hayo ambayo ameyataja ambapo umeme ulipita wakati unaelekea Mkoa wa Katavi kwamba tumeshatoa maelekezo maeneo hayo yaingie kwenye *REA* awamu ya tatu, mzunguko wa pili unaoanza Julai, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo Mkandarasi Nakuroi anaendelea na kazi katika Mkoa wa Rukwa na hususan katika jimbo lake na maeneo ambayo tulitembelea pamoja yanaendelea na kazi vizuri na yatawashwa umeme kwa kipindi kinachoendelea. Kwa hiyo kwa maeneo haya na kwa kuwa umeme ulipita na nafurahi leo ninaposimama hapa pia kama ambavyo mnafahamu Rais wa Benki wa Dunia ameshatoa fursa ya mradi wa kusafirisha umeme katika msongo wa *KV* 400 ambao unaelekea Sumbawanga,

Mpanda, Nyakanazi, Kigoma, kwa hiyo kutakuwa na uhakika wa umeme katika maeneo aliyotaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami niulize swali dogo la nyongeza. Kuna kata iko pale inaitwa Kata ya Sirari, kata kubwa kabisa, ina wakazi zaidi ya 45,000, watu wana majumba mpaka ya milioni 200 pale; Kitongoji cha Nyamorege, Niroma, kuna maeneo ya Kimusi, tumezungumza na Waziri muda mrefu sana, watu wanahitaji umeme na wana uwezo wa kulipia. Ni lini hao watu watapata umeme kwenye hayo maeneo niliyoyataja kwa sababu watu wanahitaji umeme na wana nguvu za kulipa?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, ni kweli nilitembelea eneo hilo na kutoa maelekezo na nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa sababu anafahamu. Utekelezaji wa kupeleka umeme katika eneo hilo mpakani kabisa na Sirari umeshaanza na Kitongoji anachokisema cha Nyamorege ambacho kiko jirani sana na wilaya moja wapo ya mkoa wa kwanza kutoka Kenya tayari kuna umeme na wakandarasi kupitia kampuni yetu inayopeleka umeme vijijini kule Mara umeshaanza. Tarehe ya kumaliza kazi hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge ni tarehe 12 Juni, mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Maige.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nimetoka kuongea na rafiki yangu, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, hapa lakini nataka awatangazie wananchi wa Msalala. Halmashauri ya Msalala

Makao Makuu yake yako Ntobo na wameshahamia, lakini shughuli zote inabidi zifanyikie mjini, kwenda kutoa *photocopy,* hata shughuli za kibenki au za kiuhasibu kwa sababu ya ukosefu wa umeme. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye Kijiji cha Ntobo yalipo Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kwa dharura?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli, ni kama takribani nusu saa tumemaliza kuongea na Mheshimiwa Mbunge. Kazi ya kupeleka umeme katika Kijiji cha Ntobo ambacho kiko kilometa nane kutoka umeme unapoishia inaanza Jumatatu ijayo na tayari leo wakandarasi wamekwenda ku-*survey.* Niwape taarifa wananchi wa Msalala, hasa wa Ntobo, kwamba kuanzia wiki ijayo kazi ya kupeleka umeme kwenye kijiji kizima na vitongoji vya Ntobo inaanza Jumatatu wiki ijayo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Acha nione, Manyara, *Senior MP* Manyara, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Moja ya wilaya ambazo zilipata maeneo machache sana mwanzoni ni Wilaya ya Hanang na sasa bado changamoto ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aliniahidi kwamba atatembelea Hanang, mimi nasubiri naomba awaambie wananchi wa Hanang ni lini atakwenda kule ili kuona changamoto zile na tushirikiane naye ili tuweze kuondoa hizo changamoto?

MWENYEKITI: Ahsante. Lini mtaelekea huko? Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 2, mwezi ujao, baada ya bajeti yetu kumalizika tutafuatana mimi na Mheshimiwa Mbunge, twende kwenye jimbo lake. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Mwantum Haji Dau, Mbunge wa Viti Maalum, linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jami, Jinsia, Wazee na Watoto.

Na. 247

Tatizo la Kisukari, Shinikizo la Damu na Kansa

MHE. MWANTUMU DAU HAJI aliuliza:-

Kuna wagonjwa wa Kisukari, Shinikizo la Damu na Kansa wanapata shida kubwa ya kiafya:-

Je, Serikali ina mpango gani katika kuwapatia huduma ipasavyo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisukari, Shinikizo la Damu na Saratani ni kati ya magonjwa yajulikanayo kama magonjwa sugu au magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Magonjwa haya yamekuwa yakiongezeka sana duniani kote ikiwa ni pamoja na Nchi Zinazoendelea, Tanzania ikiwepo. Ongezeko hili lilianza kuonekana tangu miaka ya tisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Sera ya Afya ya Mwaka 2007, ilitoa tamko la kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Aidha, mnamo mwaka 2009, Serikali kupitia Wizara ya Afya, ilianzisha kitengo cha kushughulikia magonjwa yasiyo ya kuambukiza na kutengeneza mpango mkakati wa mwaka 2009 – 2015 na hivi sasa tunatekeleza mpango mkakati wa mwaka 2016 – 2020. Mwongozo huu unatekelezwa kuanzia ngazi ya hospitali ya kanda hadi zahanati. Huduma za Magonjwa ya Kisukari, Shinikizo la Damu pamoja na Saratani ni huduma ambazo katika hatua za awali zinapatikana katika ngazi ya kituo cha afya. Mgonjwa anapokuwa na magonjwa haya ambayo yapo katika hatua ya juu, hulazimika kupatiwa huduma za matibabu ambazo zinapatikana Hospitali za Kanda, Taifa, Rufaa za Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeboresha huduma ya magonjwa ya moyo ikiwemo Shinikizo la Damu kwa kufungua Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Hospitali za *Ocean Road,* Bugando, *KCMC,* Benjamin Mkapa na ipo mbioni kufungua huduma za saratani katika Hospitali ya Kanda ya Mbeya ili kupunguza mzigo kwa Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* ambayo kwa miaka mingi ni yenyewe pekee imekuwa ikitoa huduma kwa wagonjwa hao. Aidha, Serikali iko mbioni kuanzisha programu ya magonjwa yasiyoambukiza kama ilivyo kwa Programu za UKIMWI, *TB* na *Malaria* ili kufikisha huduma hizi katika ngazi ya zahanati na kuzipa mwonekano wa kipekee huduma za magonjwa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, natoa rai kwa wananchi kuhakikisha wanajikinga na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa kufanya mazoezi angalau mara tatu kwa wiki, kula mlo unaofaa, kutotumia tumbaku na bidhaa zake na kupunguza matumizi ya pombe.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwantumu Dau.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, suala alilosema Naibu Waziri ni suala zuri sana wala halina mjadala, lakini sasa Serikali haioni ni wakati sasa wa kufanya matibabu yakawa bure nchini hasa kwa wale waliokuwa hawana bima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Waziri ametoa rai kwamba watu waende kwenye mazoezi, kuhusu suala la mlo na mambo mengine, ni kweli lakini napenda kuishauri Serikali, je, ni kwa nini haitoi elimu kwa jamii namna ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukizika hasa haya ya *pressure*, sukari na shinikizo la damu? Ahsante.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Je, Serikali haioni sasa kuwaondolea matibabu yakawa bure nchini hasa kwa wale wasio na bima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu la pili, Mheshimiwa Waziri ametoa rahi hapa kwamba watu waende kwenye mazoezi, kuhusu suala la mlo na mambo mengine, ni kweli lakini napenda kuishauri Serikali. Serikali haitoi elimu kwa jamii namna ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukizwa hasa haya ya *pressure*, sukari na shinikizo la damu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwantumu Dau kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nianze kumpa tu maelezo ya awali kuhusiana na swali lake la kwanza ambalo ameliongelea. Magonjwa haya yasiyoambukizwa ni

magonjwa ambayo yana gharama sana na ni magonjwa ya kudumu. Naomba nitoe mfano, mgonjwa wa tatizo la figo ili kusafisha damu kwa wiki anahitaji kati ya laki saba na nusu mpaka milioni moja; na upandikizaji wa figo kwa sasa nchini tunafanya kwa takribani milioni 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mgonjwa wa kisukari anahitaji kati ya shilingi 50,000 mpaka 100,000 kutokana na idadi ya dawa; vivyo hivyo kwa mgonjwa ambaye ana shinikizo la damu. Kwa hiyo tumekuwa tunaona ongezeko kubwa sana na ndiyo maana utaona kwamba sisi kama Serikali tumeweka msisitizo mkubwa sana na tunataka kuanzisha *program* ya kitaifa; lengo ni kuanza kupambana kwasababu mwanzoni tulikuwa tunapambana na magonjwa ya kuambukiza. Unapomtibu malaria mtu leo hatorudi tena katika kituo chetu cha huduma za afya labda baada ya mwaka mmoja. Lakini mgonjwa ambaye anatatizo la kisukari, *pressure* na saratani, huyu anaingia katika mfumo wetu wa kudumu wa kupata huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo gharama za matibabu haya ni kubwa, na sisi kama Serikali ili kutoa nafuu kwa wananchi ndiyo sasa tunataka tuelekee katika mfumo wa bima ya wananchi wote na mwezi Septemba tunataka tulete Muswada huo ambao utaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mwananchi anakuwa na bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kipindi hiki cha awali msisitizo mkubwa ambao tunaendelea nao ni kutoa elimu. Tunatoa elimu kupitia Wizara, na ndiyo maana tuliona hata tumepiga marufuku matumizi ya *tv* zetu katika vituo vya afya ili viweze kutoa elimu kwa umma. Tunaongea na wenzetu wa *SUMATRA* ili hata katika vyombo vya usafiri elimu ya afya kwa umma.

Mheshimiwa Mwneyekiti, na mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, magonjwa haya ya kuambukiza yanazidi kukua; nitoe rai ya kuhakikisha kwamba tunatunza afya zetu na kutunza afya zetu ni kuhakikisha kwamba

tunakula mlo sahihi tunafanya mazoezi na tuhakikishe kwamba tunakuwa na matumizi ya wastani ya vileo ikiwa ni pamoja na pombe na sigara.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Sware

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kumekuwa na ongezeko kubwa sana hususan katika haya magonjwa yasiyoambukizwa kama saratani. Kuna shida kubwa sana ya kutambua magonjwa haya mpaka zinakuwa dalili au zile hatua za mwisho sana. Sasa Serikali haioni imefika wakati wa kuja na mkakati mahususi kwa kutoa elimu kujua hizo *symptoms* na kuboresha huduma katika vituo vyetu vya afya ili kuweza kutoa *diagnosis* inayotakiwa mapema? Ahsante

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Afya Dkt Ndungulile.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Sware kama lifuatavyo; na ameuliza swali moja zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyektii, ni kweli kansa nyingi ambazo tunaziona katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya zinakuja katika hatua za mwisho sana, na hili yote ni suala tu la elimu na hususan saratani ya shingo ya uzazi ambayo inawaathiri wanawake wengi sana. Wengi wanakuja katika hatua ya tatu na ya nne ambazo ni hatua za mwisho sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi kama Serikali tumeendelea kutoa elimu katika masuala haya magonjwa ya saratani, na tumeendelea vilevile kuhakikisha kwamba huduma za msingi za utambuzi tunazitoa na tunazitoa bure. Katika vituo vyetu vya afya utambuzi wa sarakani ya shingo ya uzazi tunazitoa hizi huduma bure, na mashine za *Clio therapy* tumeziwekeza sana kwa ajili ya matibabu ya awali ya saratani za shingo za kizazi, zipo.

Mheshimiwa mwenyekiti, na tumekwenda mbali, sasa hivi tunatoa chanjo ya kukinga saratani dhidi ya shingo ya kizazi. Kusudio letu ni kwamba takriban watoto mabinti 650,000 walio kati ya miaka tisa mpaka 14 tuweze kuwafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tumeendelea kuboresha huduma zetu za matibabu ya saratani. Pale *ocean road* tumefunga *linear accelerator* ambayo inaifanya Hospitali yetu ya *Ocean Road* kuwa hospitali ya kisasa kabisa katika matibabu ya mgonjwa wa kionzi. Vilevile tutafunga mashine ya *PET scan* ambayo itaifanya sasa Taasisi yetu iwe ni taasisi ya kisasa sana katika matibabu ya kansa ndani ya dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunaendelea kuboresha huduma hizi za matibabu ya saratani kule Bugando, wanatoa dawa lakini vile vile watatoa huduma za mionzi. Pia tunaendelea kuboresha kule *KCMC* ili waweze kutoa huduma za dawa na vile vile matibabu ya mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mikakati ya Serikali ipo na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunaendelea kutoa elimu kwa jamii ili waweze kufika katika vituo vya afya na kufanya uchunguzi na utambuzi wa ugonjwa wa kansa mapema iwezekanavyo.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ugonjwa wa dengue ni ugonjwa hatari sana na umekuwa ukiwa kwa kasi sana katika nchi yetu, lakini ugonjwa huu ni mgonjwa wa mlipuko kama magonjwa ya kipindupindu na magonjwa mengine, na Serikali imekuwa na utamaduni wa aidha wa kutibu bure au kwa gharama ya chini za matibabu.

Je, sasa Serikali ina mpango gani wa kutibu ugonjwa huu bure kwa wananchi ili waweze kupambana nao na usisambae katika nchi yetu?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna mlipuko wa ugonjwa wa dengue ndani ya nchi yetu na hadi kufikia wiki hii tuna *cases* 1901 katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani na Kilimanjaro pamoja na Singida ambayo imetambuliwa; na hawa mikoa mengine wengi walikuwa ni wagonjwa ambao wamepitia mkoa huu wa Dar es Salaam. Sisi kama Serikali tumeshaanza kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba tunaudhibiti ugonjwa huu wa dengue

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama nilivyosema hapo awali na katika taarifa zetu, ugonjwa huu hauna tiba, tunachokifanya ni kutibu zile dalili ambazo mgonjwa anakuja nazo ikiwa ni pamoja na matibabu ya homa, maumivu pamoja na upungufu wa maji ambao anakuwa nao. Changamoto kubwa ilikuwa katika katika upatikanaji wa vipimo. Sasa hivi niwahakikishie kwamba katika vituo vyetu vya umma vipimo vimepatikana na tumevisambaza katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga pamoja na hapa Dodoma. Kusudio letu ndani ya wiki moja ijayo tutapata vipimo tena ambavyo tutataka sasa tuvisambaze nchi nzima ili kuhakikisha kwamba tunaweza kubaini hizi *cases* za ugonjwa huu wa dengue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja kubwa katika maswali mengi ambayo tumekuwa tunayapata ni ugharamiaji ugonjwa huu wa dengue na husasan kwa wale wagonjwa wa bima. Niseme tu kwamba wagonjwa wa ugonjwa huu wa dengue wanapata matibabu kwasababu huu ni ugonjwa kama ugonjwa mwingine, na wanatibiwa na pale lilikuwa ni suala sasa la vipimo. Kwa wale wagonjwa ambao ni wagonjwa wa dengue ambao wanakadi ya bima za afya wanapokwenda katika vituo vya umma huduma ile ya vipimo wataipata bure. Tutazitoa hizi huduma za vipimo katika hospitali zetu za umma na kwasababu tumeshasambaza vipimo katika hospitali zetu za umma.

MWENYEKITI: Ahsante bado tuna Wizara hiyo hiyo, tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Fakharia Shomari Hamisi Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 248

Sera ya Matibabu Bure kwa Wazee Nchini

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS aliuliza:-

Sera ya Wazee imeelekeza kuwapatia wazee matibabu bure lakini utekelezaji wake haueleweki na pia una urasimu mkubwa.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa uhakika wa kuwaondolea kero na shida hizo wanazozipata wazee katika suala zima la matibabu yao?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Sera ya Afya ya Mwaka 2007 iliweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba wazee wanapata huduma bora za afya. Katika kutekeleza uamuzi huo Serikali ilitoa tamko la makundi maalum wakiwemo wazee wasio na uwezo kupatiwa huduma za afya bila malipo. Hata hivyo, changamoto iliyopo katia utekelezaji wa Sera hii ni ufinyu wa bajeti ikilinganishwa na mahitaji ya kuwapatia huduma za afya makundi hayo bila wao kuchangia gharama za huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali iko katika hatua za mwisho kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Ugharamiaji wa Huduma za Afya ambao lengo lake ni kuibua vyanzo

mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kugharamia huduma za afya *(Health Care Financing).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa vyanzo vilivyopendekezwa katika Mkakati huo ni uanzishwaji wa Bima ya Afya Moja (*Single National Health Insurance*) ambapo uchangiaji katika bima hiyo utakuwa ni wa lazima kwa wote walio na uwezo wa kuchangia.

Kulingana na tatifi zilizofanywa, njia hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza rasilimali fedha katika sekta ya afya na kuweza kugharamia makundi maalum yanayohitaji msamaha wa kulipia huduma za afya. Serikali inatarajia kuleta Muswada wa Bima ya Afya kwa wote mwezi Septemba, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwataka watoa huduma kutenga madirisha maalum kwa ajili ya kwuahudumia wazee na halmashauri ziwatambue na kuwapa kadi za wazee kwa ajili ya matibabu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fakharia

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza na pia kwa Mheshimiwa alivyonijivu kidogo inaleta afueni kwa wazee wetu lakini bado haijawa ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wazee bado wanaendelea kuteseka kupata matibabu yaliyobora.

Je, Wizara imefanya tathmini gani ya kuona kwamba wazee hawa wanaendelea kutunzwa na kwamba hawawezi kupata shida?

Swali la pili, kwa kuwa wazee wanahaki ya kutunzwa na kulelewa lakini hakuna sheria iliyotungwa ilhali Sera imetungwa tangu mwaka 2007 lakini sheria hadi hii leo haijatungwa; unategemea nini, kwamba Sera yako hii itaweza kufanyakazi na wazee hawa waweze kutunzwa?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Dkt. Ndungulile.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake ameuliza kwamba tumefanya tathmini na changamoto ni zipi. Changamoto kama nilivyosema, ni kwamba kwanza ni utambuzi wa wazee. Taifa letu limepata bahati, sasa hivi kadri tunavyoboresha sekta yetu ya afya umri wa wazee nao kuishi unazidi kuongezeka. Sasa hivi wastani wa Mtanzania kuishi ni miaka 64 na wengi miaka 64 bado wana afya njema, na kundi hili linazidi kukua kwasababu ya maboresho haya ambayo tumeyafanya katika sekta yetu ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwahiyo moja ya changamoto ambayo tunayo ni utambuzi wa hawa wazee. Ndiyo maana tumetoa rai kuhakikisha kwamba halmashauri zinaendelea kuwatambua na kuwapatia vitambulisho. Wizara tumetoa maelekezo ya kuwa na madirisha maalum kwa ajili ya kuwahudumia wazee, na hili tumeendelea kulifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini changamoto nyingine ambayo tumeibaini na ambayo sasa nayo tunataka kuitibu ni magonjwa ambayo yanawaathiri wazee ni magonjwa mahususi sana; na katika jibu langu la msingi kwa swali lililopita nilijibu kwamba sasa tunataka kwenda katika *National program* ya magonjwa yasiyoambukiza ambayo itakwenda mpaka chini kuhakikisha kwamba sasa wazee wale ambao magonjwa yao mengi ni yale magonjwa sugu basi waweze kupata huduma zao kule kule katika ngazi za kata na zahanati ambazo wanazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, changamoto nyingine ambayo tumeibaini na ambayo sasa tunataka kuitibu ni ugharamiaji wa matibabu kwa wazee

ambapo sasa tunataka mwezi Septemba tuje na muswada wa sheria ambao utakuwa na bima ya wananchi wote ambao sasa utaweza kufanya ugharamiaji wa matibabu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili linauliza ni lini Serikali italeta sheria ya wazee. Sera ambayo tunayo sasa hivi sisi kama Serikali tumeona imepitwa na wakati na sasa tuko katika hatua ya kufanya mapitio ya Sera hii ya Wazee ili iweze kuendana na mazingira ya kwetu ya sasa na baada ya hapo sasa Serikali itatafakari kama kuna umuhimu wa kuja na sheria mpya ya wazee.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ruth Mollel

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Pamoja na huduma bure kwa wazee bado tuna ule mkakati pia au huduma ambayo inatolewa kwa mama na mtoto hasa akina mama wanaokwenda kujifungua. Ni kweli inatakiwa iwe bure lakini ukweli *on the ground* akina mama hawa wanatakiwa kwenda na *kits,* na ninaushahidi wa ndugu yangu ambaye amejifungua watoto watatu juzi japokuwa hawakuwa riziki; alikwenda na kila kitu kwenda kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa changamoto hii ambayo bado watu wanakwenda na vifaa, ni kwa nini Serikali isipate taasisi zetu au *REPOA* au *ESRF* waweze kufanya utafiti kuona ni kwanini *kits* zinakuweko na kwanini wahusika hawapewi? maana yake mkienda nyinyi Mawaziri hamtapata ukweli lazima tupate mtu wa pembeni atakayefanya utafiti.

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Afya Dkt. Ndungulile, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Mollel Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunagharamia ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kujifungulia akina mama. Ninachokiona hapa ni changamoto ya uelewa kwa watoa huduma wetu wa afya. Mama anapokwenda kliniki anaambiwa ajiandae ili atakapopata dharura kabla hajafika katika kituo cha kutoa huduma ya afya endapo atapata dharura basi awe na vifaa ambavyo vinavyomsaidia. Hata hivyo vifaa hivi si mbadala wa vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya kuwa na vifaa vya kujifungulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaipokea hii changamoto na sisi tutaweza kutoa maelezo vizuri kwa watoa huduma wetu wa afya ili waweze kuzingatia misingi hii; kwasababu sisi kama Serikali tunagharamia vifaa na vifaa hivi tunavyo katika bohari yetu ya madawa.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje Mbunge wa Mpwapwa linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 249

Ujenzi wa Daraja la Godegode

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Daraja la Godegode limesombwa na maji wakati wa mvua za masika na daraja hilo ni kiungo kikubwa kati ya Jimbo la Kibakwe na Jimbo la Mpwapwa ambalo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya Mpwapwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja hilo ili kurudisha mawasiliano kati ya Wananchi na Kata za Godegode, Pwaga, Lumuma, Mbuga na Galigali?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli daraja la Godegode lilisombwa na maji wakati wa mvua kubwa iliyonyesha kipindi ha masika mwaka 2018. Kwa kuzingatia umuhimu wa daraja hilo, Serikali ina mpango wa kurudisha mawasiliano kati ya Mpwapwa na Kata ya Godegode, Pwaga, Lumuma, Mbuga na Galigali kwa kujenga Daraja jipya. Ujenzi wa Daraja hilo utaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/20 ambapo jumla ya shilingi milioni 325 imetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili. Kwa kuwa daraja lililosombwa na maji lilijengwa kwa gharama ya shilingi milioni 500 na limesombwa na maji, leo mnajenga daraja la shilingi milioni 325 hilo si ndiyo litachukuliwa mapema. Kwanini msiongeze fedha Mheshimiwa Naibu Waziri?

Swali la pili kwa kuwa barabara ya kutoka Mpwapwa, Lupeta, Mbori, Makutupa, Chamkoroma, Mlali mpaka Pandambili ni barabara muhimu sana kwa Majimbo mawili. Jimbo la Mheshimiwa Spika Mheshimiwa Ndugai Kongwa na Mpwapwa. Na kwa kuwa barabara hili huwa linatengewa fedha kidogo sana kwa ajili ya ukarabati.

Je, ni lini mtatenga fedha za kutosha ili barabara hii iweze kutengenezwa?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa maswali hayo Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti,

napenda kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Lubeleje, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Lubeleje, mimi siku hizi namuita mzee wa Godegode, anafuatilia sana ujenzi wa daraja hili na Godegode na maeneo mengine. Nikiri kwamba ni kweli, kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema, kwamba daraja hili lililokuwepo lilijengwa muda mrefu na lilijengwa kwa gharama alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, kwa milioni 500. Katika jibu langu la msingi nimezungumza juu ya kutenga milioni 325 kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuhakikishie kwanza Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hii itafanyika vizuri tunafanya shughuli ya ujenzi kwa kutumia utaratibu wa *design* and *construction.* Kwa maana hiyo niseme tu kwamba tumetenga milioni 325 kwa ajili ya ule usanifu ambao utachukua muda mfupi sana kwasababu tutafanyakazi wenyewe kupitia wakala halafu baadaye tutaanza kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nikuhakikishie Mheshimiwa Lubeleje ukiangali kwenye kitabu chetu cha bajeti ukurasa 323 utaona kwamba pamoja na fedha hizi nilizozitaja kwamba baada ya *design* tutaanza kujenga na tumetenga milioni 180 ili sasa *approach* ya Kilomita 6 kwenye daraja la Godegode ili ujenzi uende sambamba kwa hiyo kuna fedha zingine milioni 180 tumezitenga,

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalenga kwamba katika ujenzi wetu maeneo haya Godegode na maeneo mengine kusimamia vizuri ili gharama za ujenzi ziende chini huu ni mkakati wetu kama Wizara sio kama kujenga kwa fedha nyingi tumejipanga ili kusimamia vizuri gharama za ujezi ziweze kupungua. Mheshimiwa Lubereje utakubaliana na mimi kwamba sehemu ambapo daraja hili lipo ni sehemu ambayo imejengwa muda mrefu na mmomonyoko ni mkubwa na urefu wa daraja lile ni kubwa sana. Sasa tumejipanga kwamba kwenye daraja na godegode upande wa kulia

kwake kama unaelekea kibakwe kwa maana kwamba tutalijenga upande kulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalenga kwamba *span* ya daraja lile itakuwa fupi, sasa *span* ikiwa fupi gharama ya ujenzi zitapungua, *span* ikiwa fupi pia tutatumia muda ili wananchi haya waweze kupata huduma za kupita katika maeneo haya. Na kwa maana hiyo pia tumejipanga ndio maana nikasema tutakuwa na *approach* tutaboresha ili ku-*control* mmomonyoko ili daraja hili liwe bora. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lubereje nikutoe wasiwasi kwamba tumajipanga vizuri kwamba tumejipanga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu B Mheshimiwa Lubereje anasema kumekuwa bajeti ndogo katika eneo la mpwapwa, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mpwapwa ni kati ya Wilaya zilizokuwa katika Mkoa wa Dodoma ambayo ni Makao Makuu na Mpwapwa ndio wilaya pekee ambayo haijaunganishwa vizuri na mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumejipanga kama Serikali kufanya Mpwapwa iwe na barabara nzuri ili sasa iweze ku-*support* kazi nyingi ambazo zinafanyika katika Makao Makuu. Na kwa ushahidi tu Mheshimiwa Mbunge anafahamu tutaanza ujenzi wa lami kuanzia Mpwapwa kilometa kadhaa kuja kongwa. Lakini Mheshimiwa Lubereje nikuhakikishie kwamba kutoka Mpwapwa kwenda Gulwe kwenda Rudi, Chipogolo na penyewe tunasanifu kwa ajili ya ujenzi wa lami. Na barabara uliyo itaja barabara ya pandambili, Mlali Nghambi yapo kama maeneo manne matano ambayo tumeyatengea fedha za kutosha eeh...

MWENYEKITI: Ahsante

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): ...sehemu korofi tumetengea milioni 120 kuna daraja pia milioni 150, tatu kuna zaidi ya milioni 600 ambazo tumezipanga katika mwaka huu wa

fedha unaokuja ili kuifanya mpwapwa nao iweze kupata huduma za barabara.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa niaba ya waliodhurumiwa wote, naomba swali lao namba 250 lijibiwe.

Na.250

Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Kuwekwa Wazi kwa Umma

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF aliuliza:-

Ibara ya 130 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inataja kazi za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, moja ya kazi zake ni kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa Haki za za Binadamu na ukiukwaji wa msingi ya utwala bora.

(a) Je, kwa nini ripoti za tume hiyo haziwekwi wazi kwa uma?

(b) Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa kujenga utamaduni wa ripoti hizo kujadiliwa Bungeni?

MWENYEKITI: Umesema nini? Hebu uliza swali tena Mheshimiwa. Uliza tu swali.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Kwa niaba ya waliodhurumiwa katika haki za binadamu, naomba swali lao 250 lijibiwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa niaba yake Naibu Elimu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf Mbunge wa Mgogoni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijalijibu Mheshimiwa Ally Yussuf, amesema wadhurumiwa wote kwa hiyo inawezekana hata yeye kuna ambao amewadhurumu lakini naomba nijibu swali kama alivyouliza maana hakuuliza hivyo huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli kwamba Ibara ya 130 ya katiba ya Jamhuri ya Muugano ikiosomwa kwa pamoja na sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Na. 7 ya 2001) inaipa Tume mamlaka ya kufanya uchunguzi wa mambo yote yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu, kifungu cha 28(1)(a) mpaka (f) cha sheria hiyo (Na. 7 ya 2001) kinafafanua kuwa, tume baada ya kufanya uchunguzi na kuthibitisha kuwepo kwa uvunjifu wa haki za binadamu itawaslisha taarifa na mapendekezo yake kwenye mamlaka kusika kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 33 (1) (a) –(c) cha Sheria Na. 7 ya 2001 kinaitaka Tume kuwasilisha taarifa yake ya mwaka katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Mawaziri kupitia wanaoshughulikia masuala ya haki za binadamu kwa Tanzania Bara na Zanzabar, hata hivyo, Tume imekuwa ikitimiza jukuu hilo kwa mujibu wa sheria. Aidha, hakuna sheria yoyote inayokataza taarifa za Tume kujadiliwa Bungeni endapo Mbunge ataona kama kuna jambo la kuibua kutoka kwenye taarifa iliyowasilishwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Sulemain.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana jambo la kwanza nataka nimwambie Mheshimiwa Naibu Waziri nimerekebisha

waliodhurumiwa katika haki za Binadamu. Na ningeweza kujibu sana lakini sio wakati wake. Maswali yangu mawili, kituo cha haki za binadamu *LHRC* Tanzania huwa kinaweka wazi matukio yote makubwa ambayo yanayotokea nchini yakiwemo utekwaji, uteswaji, upoteaji, upigwaji risasi, kuonyesha bastola hadharani....

MWENYEKITI: Uliza swali sasa.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Ubambikizwaji...

MWENYEKITI: Uliza swali sasa

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Ripoti za Serikali hazibebi mambo mazito kama haya.

Swali la pili, nataka kujua ni *challenge* zipi ambazo serikali inazipata inapokwenda kutoa ripoti zake katika vikao vya kimataifa huku kukiwepo na ripoti mbadala za ndani zinazo kinzana na ripoti za Serikali?

MWENYEKITI: Ahsante sana majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ole Nasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli *Legal Human Right Center* mara nyingi hutoa ripoti yenyewe inavyoona kuwa mambo ya haki za binadamu yamekuwa yakiendelea nchini,

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria zetu zina ruhusu na inatoa uhuru wa maoni sio *Legal Human Right Center* hata watu binafsi mashirika mengine sio ya kiserikali kwa hiyo wanaongea mengi. Lakini katiba na sheria zetu zimetambua hasa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwamba ndio imepewa jukumu la kikatiba la kuhakikisha kwamba haki za binadamu zina heshimiwa na ndio imepewa fursa ya kusikiliza malalamiko mbalimbali. kwa hiyo, yoyote yule mwenye malalamiko na manunguniko kuhusiana na uvunjifu

wa haki za binadamu pamoja na ufunjivu wa taratibu za utawala bora waweze upeleka kwenye Tume kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ni changamoto gani tunapata huko tunapoenda nje kuhusiana na haki ya haki za binadamu, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba changamoto kubwa kuliko zote ni uposhwaji mkubwa sana unaofanywa na sio tu taasisi mbalimbali lakini vilevile mtu mmoja mmoja ikiwa na baadhi na wanasiasa. Lakini kama anavyofahamu hivi karibuni Serikali imeamua kuchukua hatua kuhakikisha kwamba kila upotoshwaji unaotolewa unajibiwa pale unapotolewa kwa sababu mara nyingi ni kwa ajili ya kuchafua sifa njema ya Taifa letu.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea, Mheshimiwa swali linalofuatwa linaulizwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo linaelekezwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 251

Mgogoro Kati ya Magereza na Wananchi wa Ukondamayo

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi la magereza na wananchi wa Kata ya Ukondamayo hususan Kijiji cha Tumaini umedumu kwa muda mrefu sasa.

Je, Serikali inachukua hatua gani kutatua na kumaliza mgogoro huu?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, kwa niaba, Mheshimiwa Mabula.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukujulisha kwambakwa sasa hakuna mgogoro wa ardhi kati ya kata ya Ukandamoyo hususani kijiji cha Tumaini na gereza la ilimo Urambo. Ni kweli hapo awali ulikuwepo mgogoro baina vya vijiji vinne mojawapo kijiji cha tumaini, Mgogoro huo ulitatuliwa na kuhitishwa mwaka 200 kwa kuhutimishwa mwaka 2000 kwa kushirikishwa viongozi kutoka wizira ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ardhi, Jeshi la Magereza, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tabora, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Urambo na Serikali ya vijiij vyote nine vilivyokuwa na mgogoro kikiwemo Kijiji cha Tumaini,

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho la mgogoro huo ni baada ya Jeshi la magereza kukubali kuotka eneo la jumla ya ekari 3,218 kwa vijiji vilivyokuwa na mgogoro mojawapo kijiji cha Tumaini wakapewa ekari 505, Imalamakoye ekari 195, Nsendakanoge ekari 1,655 na Itebulanda ekari 860.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha hati ya makubaliano ya hitimisho la mgogoro ilisainiwa na viongozi wa vijiji vyote vinne vilivyokuwa na mgogoro kikiwemo kijiji cha Tumaini na mawe ya mipaka yaani *beacons* yakawekwa upya kwa utambulisho wa namba Uv 66, Uv 69, Uv 107, Uv 35 na Uv 108.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niulize maswali ya nyongeza mawili kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimhakikishie Naibu Waziri aliyejibu maswali pamoja na Bunge kwa ujumla kwamba Mgogoro bado upo kati ya magereza na Kijiji cha Tumaini. Na uthibitisho ninao naomba nikukabidhi vithibitisho nilivyonavyo. Wananchi wanajua haki zao

wanajua *beacons* zilizowekwa na baadaye kuondolewa, kwa hiyo mgogoro bado upo sasa maswali mawili kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Serikali inasema imemamliza mgogoro wananchi wa kijiji cha Tumaini wanasema mgogoro bado upo. Je huoni kwamba kuna umuhimu wa wewe mwenyewe kwenda kuangalia nani anayesema ukweli na kutatua tatizo hili?

(ii) Kwa kuwa urambo kuna migogoro mingi kuhusiana na mipaka na hata ile inayopakana pori la akiba la ugala ikiwemo sehemu Indenda, Lunyeta, Uyumbu, Tevela pamoja na Ukondamoyo.

Je huoni Mheshimiwa Waziri kwamba utakapokwenda kutatua tatizo la Tumaini na magereza pia utatue migogoro mingine iliyopo hapa na ninapendekeza pia kwamba ufuatane na Waziri wa Maliasili kwa sababu pia vinahusiana pamoja?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa mgogoro kama ambavyo nimeeleza katika jibu langu la msingi na mgogoro huo ulitatuliwa lakini tukumbuke tu kwamba vijiji hivi vilipimwa mwaka 2013. Lakini wakati huo gereza lile lilipimwa mwaka 1988 maana yake gereza lilitanguliwa likiwa na ekari 10,416 baada ya kuwa na mgogoro walipunguza kiasi cha ekari 7,198 kama nilivyotaja kwa vijiji ambavyo nimevitaja kwenye jibu la msingi la gereza likabaki na ekari 3,218.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akilifuatilia hili suala la mgogoro na ana vielelezo vingi vya wananchi wake wakilalamika nipende kumkubalia alichosema kwamba twende pengine

tukaangalie uhakika uliopo nasema nipo tayari kwenda kwa ajili kuangalia mgogoro uliopo ili tuweze kuumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili alikuwa anaongelea mgogoro wa mipaka katika maeneo mengine ambao yanaingiza kwenye pori la akiba sasa niseme hili pia katika ule msafara wa mawazie nane walikuwa wakipitia migogoro hii yote ilikuwa imehusisha Wizara ya Maliasili, TAMISEMI lakini wakati huo huo aridhi na Mambo ya Ndani pia walikuwapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, cha msingi hapa ni kufanya ufuatiliaji wa kina kwanza tuone hivi vijiji alivyovitaja vya Senda, Tundu na Ukomola kama vipo kwenye vile vijiji 366 ambavyo vilikuwa vimeainishwa katika kile kitabu kibwa cha migogoro. Kama napo kutakuwa kuna shida basi nitakapokuwa nina-*solve* mgogoro wa hili gereza na vijiji vya tumaini basi tutafika na hili pori la akiba tuweze kuona nini cha kufanya. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge Muda wetu ndio huo wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni waliopo jukwaa la Spika, tunawageni 117 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga (Mb) Waziri wa Kilimo ambao ni *Engineer* Mathew Mitigumwe Katibu Mkuu wa Wizara hiyo karibu sana. Profesa Siza Tombo Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Obey Asery Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Ndugu Fred Kafero Mwakilishi *FAO* Tanzania, Ndugu Neema Sitta Mwakilishi *WFP* nchini, ndugu Timoth Liyaya mwakilishi wa *UNIDO*, tunaye Vianey Tweyendela, Mwakilishi Mkazi Agra-Tanzania, Dkt. Titus Mlengenya Kamani Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya ushirika, Ndugu Monica Mbega Mwenyekiti Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Dkt. Joe Kabisa Mwenyekiti Bodi ya Pamba, Profesa Susan Nchimbi Msola Mwenyekiti Bodi ya *TOSCI*, ndugu Elizabeth Makweba Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika wameambana na Wakurugenzi na wakuu wa idara na taasisi zilizo chaini ya Wizara hii ya kilimo. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Hasunga ambao ni familia yake. Ndugu Mary Hasunga mke wa Waziri karibu sana shemeji yetu. Tuna mtoto wa Mheshimiwa Waziri ambaye ambaye ni Eliza Hasunga karibu sana, na mwingine Scola Hasunga mtoto na Michael Hasunga hawa ndio watoto karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine 44 wa Mheshimiwa Waziri Hasunga ni wenyeviti na Makatibu wa CCM wa kata na vijiji kutoka Jimbo la Vwawa Mkoani Songwe, wakiongozwa na ndugu Neema Nzowa karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Kundi la pili la wageni wa Waheshimiwa Wabunge waliopo hapa leo tunae mgeni wa Mheshimiwa Omar Mgumba (Mb) Naibu Waziri wa Kilimo ambaye ni mke wake ndugu Husna Abbas Mgumba karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Mwita Waitara (Mb) Naibu Waziri TAMISEMI ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam na Mkoa wa Mara wakiongozwa na Baba yake mzazi, Mzee Mwikwambe Waitara karibu sana mzee wetu karibu sana *omghaka*. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Jumaa Aweso (Mb) Naibu Waziri wa maji na uwamwagiliaji, ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Mohamed Issa karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 55 wa Mheshimiwa Innoncent Bashungwa (Mb) naibu waziri wa Kilimo ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanatokea karagwe, Mkoani Kagera karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 31 wa Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma na wana *Club* ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wakiongozwa na Ndugu Petro Maitare. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 52 wa Mheshimiwa Justin Monko ambao ni Walimu na wanafunzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Singida toka Idara ya Menejimenti ya Kumbukumbu na Nyaraka kutoka Mkoani Singida, wakiongozwa na Lameck Sospeter. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni watatu wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ambao ni wafanyakazi wa Mufindi *Community Bank* ya Mufindi, Mkoani wa Iringa wakiongozwa na Meneja Mkuu wa Benki hiyo Ndugu Philip Raymond, karibuni. *(Makofi)*

Tuna Wageni 44 wa Mheshimiwa Agnes Marwa na Mheshimiwa Vedastus Mathayo ambao ni Madiwani, Wenyeviti pamoja na Makatibu wakiongozwa na Flora Tinga, Anna Madaraka, Prisca Mjarifu, Juma Songo na Bertha Bulemo, karibuni sana kwetu hapa, mmependeza sana kama anavyopendeza Mbunge wenu Agnes Marwa. *(Makofi/ Vigelegele)*

Tunao pia Wageni 24 wa Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Stella Andrea. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Esther Mmasi ambao ni Umoja wa Vijana wa CCM kutoka Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala *(KIU),* Kampasi ya Dar es Salaam. Karibuni sana kwetu.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Susan Lyimo ambao ni Ndugu Xavery Kunambi Mwenyekiti wa Baraza la Wazee CHADEMA Jimbo la Kinondoni na Ndugu Jane Makani, mdogo wake Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Lucy Magereli ambaye ni jamaa yake kutoka Mkoani Arusha Ndugu Martina Lukumay. *(Makofi)*

Tuna Wageni wawili wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni Wapiga kura wake kutoka Iringa Mjini Ndugu Marco Ng'umbi na Sabrina Ernest. Karibuni. *(Makofi)*

Naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa Jumatatu tarehe 20 Mei hadi Ijumaa tarehe 24 Mei Maafisa kutoka Idara ya Uhamiaji watakuwepo hapa Bungeni kwa ajili ya Usajili wa maombi ya Hati mpya za kusafiria *(Passport)*za kielektoniki. *(Makofi)*

Nyaraka muhimu, mnazotakiwa kuwa nazo ni pamoja na Kitambulisho cha Ubunge, picha moja ya *passport size* yenye *background* ya bluu. yenye *background* ya bluu, usilete nyeupe, Mheshimiwa Heche haitakubaliwa. Ya tatu nakala ya Hati ya kusafiria ya awali uliyonayo, usije na kipande cha kupigia kura na nne, kitambulisho cha uraia. Inafanyika wapi? Ukumbi Na.9 *ground floor,* Jengo la Utawala karibu na chumba cha maslahi. Waheshimiwa Wabunge wote wenye uhitaji wa hati hizo mpya za kusafiria mnaombwa kutumia fursa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mbunge wa Mafia anaomba, tangazo muhimu sana hili, anaomba niwatangazie Wabunge mnaopenda kuhudhuria mashindano ya kusoma *Quran* Tukufu kesho katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa saba mchana. Mnakaribishwa mkaone tukio muhimu hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyonayo hapa kwa hiyo...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ATASHASTA J. NDITIYE:) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MHE. PASCAL Y HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MBUNGE FULANI: Waziri Mkuu.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwakyembe. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Kariri na haya.

MWENYEKITI: Hivi kwa sababu ya muda nitachukua labla wawili tu. Tuna hoja nzito kweli kuanzia leo. Mheshimiwa Massare, Mheshimiwa Lyimo, Mheshimiwa Mwambe na Mheshimiwa Alberto, jana uliuliza wewe, waulize na wengine bwana Mheshimiwa Msigwa basi, tunaanza, jamani muda, mniwelewe, Bunge bado lipo kama una swali utauliza siku nyingine. Mheshimiwa Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Bunge letu, ni Bunge muhimu sana na hasa kipindi hiki cha Bajeti wakati tunapitisha Bajeti za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana jana wakati tunapitisha Bajeti ya Wizara ya Ulinzi, Katibu alipokuwa anatusomea vifungu hasa katika kile Kitabu cha Maendeleo aliishia *subvote* 2001 na akaacha vipengele vingine na baada ya hapo bado tulikuwa na muda na Mwenyekiti hakwenda kwenye *guillotine*. Kulikuwa na vifungu vitatu ambapo mimi mwenyewe nilikuwa na *interest* sana ya kuweza kusimama, kwa hiyo ina maana kwamba hatukumaliza kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo naomba kuuliza kama Bajeti ile ambayo ilipitishwa ni halali kwa sababu kuna vifungu vitatu, *subvote* 2002, *subvote* 2003, ambayo hii moja inahusu suala la utafiti na nyingine inahusu suala la fidia. Haya mambo yote hatukuyapitisha, sasa naomba kujua kama ni sawasawa ile Bajeti sasa imekuwa rasmi au tutafanya tena marudio ili tuweze kupitisha vifungu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, kwa sababu imekuwa na bahati nzuri sana tulimweleza na Mheshimiwa Mwambe alisimama, lakini Mwenyekiti

aliyekuwa amekaa kwenye kiti hakumruhusu. Kwa hiyo naomba mwongozo wako, kwa sababu kwa kweli saa nyingine kunakuwa kunakiukwa taratibu lakini tunaposimama kuomba utaratibu hatupewi nafasi. Kwa hiyo naomba kupata Mwongozo wako kama hii bajeti ni halali au sio halali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Yahaya.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7)kuhusu jambo ambalo limetokea leo mapema hapa katika jengo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya za Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na maswali ambayo limeulizwa na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, kuhusu magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kisukari na *pressure*, lakini katika nyumba hii ya kutunga sheria kumekuwa na hali ya hewa ambayo si rafiki kwa kipindi hiki cha baridi kulinganisha na hali ya Mji wa Dodoma. Kumekuwa na baridi kali sana siku nyingine katika nyumba hii, tunaomba Mwongozo wako ni lini, wasimamizi wa *weather condition* humu ndani watazingatia hali ya afya ya Wabunge ambao wengi wanakuja kuugua kulingana na kupata *cholesterol* zinazosababishwa na ubaridi mkali ulio katika nyumba hii. Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Bunge letu tumekuwa tukichagua Wawakilishi mbalimbali katika maeneo mbalimbali na Kimataifa, mojawapo ni Wabunge wa *PAP*, nataka nipate Mwongozo wako kwa sababu Bunge hili ndiyo limechagua Wawakilishi wa Bunge la *PAP*, sasa inapotokea Mbunge mwenzetu ambaye tulimchagua humu ndani anakuwa *suspended* wakati Bunge ambalo tulimchagua hatujajadili, hatujajua kosa lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua uhalali huo unatoka wapi? Kwa sababu hawa watu tunaowachagua kutuwakilisha hawajateuliwa na mtu? Ni Bunge tulipiga kura hapa wakatuwakilishe kwenye Mabunge mbalimbali, nataka nijue *mandate* ya hawa Wawakilishi wetu wanakuwa *suspended* vipi ili tuone tunakuwa tunaliwakilisha Taifa vipi, maana yake haya mambo mtu yuko kuwakilisha Taifa, halafu anasimamishwa tu na kiti hapo, bila Bunge kujadili na mtu anayewakilisha Taifa analeta sura nzuri ya Taifa, inatuchafua kama Taifa. Nataka nijue Bunge letu linakuwa na nguvu kiasi gani ya kuwalinda hawa tunaowachagua watuwakilishe katika nchi yetu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi pia kunipa nafasi ili meza yako itoe Mwongozo kwenye mambo ambayo yamekuwa yakiendelea ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna utaratibu kwamba Kiti, wakati fulani kinasitisha mijadala pamoja na miongozo, halafu siku ya pili hawaruhusu kwa sababu lile jambo linaonekana limetokea siku moja kabla. Nitatoa mfano, jana wakati wa mjadala wetu, Mheshimiwa Spika alitoa ufafanuzi kuhusiana na Sheria ya *Liquor and Intoxication Act*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambayo Sheria hii ilirekebishwa mwaka 1968, 1971, 1978 na 1982 iliyohalalisha gongo au nipa kuwa ni pombe halali isipokuwa utaratibu wake, sasa nataka kiti chako kitolee ufafanuzi na wewe ni Mwanasheria mbobezi kwenye sheria hizi zinasema nini ili kuwaondoa wananchi na hii sintofahamu kwa sababu kimsingi wakulima wanalima mazao yao ya shamba na wanapata hayo mazao kutokana na haya mazao.

Sasa je, Sheria zetu za Tanzania zinahalalisha pombe ya gongo ama hapana? Kiti chako kitolee ufafanuzi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe, lakini na wewe mambo mengine, mwezi Mtukufu huu, lakini ndiyo hivyo.

Nianze na hilo la Mwongozo Mheshimiwa Mwambe, ingawa *technically* halikutokea leo hapa, lakini kwa sababu Serikali imo ndani ya Bunge, hili suala la gongo au nipa, au aina yoyote ya pombe inayotengenezwa vijijini huko inayofanana na hayo, wengine wanaiita machozi ya simba na mengine yote hayo. Ukikutwa nayo utakamatwa, lakini Serikali watalifafanua yawezekana wasifafanue hapa sasa hivi, lakini kwa uelewa wangu ni kwamba na ndiyo maana sheria hiyo uliyoitaja ilitungwa hiyo miaka ya 1968 na ikafanyiwa marekebisho katikati hapo.

Lengo la Serikali lilikuwa ni zuri na bado ni zuri. Ndiyo maana Kiwanda cha Konyagi kilianzishwa, lengo ilikuwa ni kwamba kunakuwa na vituo vya kukusanya nipa au gongo chochote kile kama malighafi ili sasa Kiwanda kinunue kiende kika-*process* hiyo malighafi ili wananchi wetu wanapokunywa wanywe kitu ambacho kina afya na ubora katika matumizi yao na ni sawa tu na *walagi* ya Uganda, yote inatokana na hiyo.

Hata hivyo, niseme kwa upande wa Serikali walichukue hili halafu waje walitolee maelezo mazuri kwa sababu ndiyo ilikuwa shabaha ya Serikali na bado naamini kwamba hiyo ndiyo shabaha ya Serikali kwamba wananchi wetu tuwaondoe *gradually* hatua kwa hatua katika matumizi ya kinywaji hiko ambacho kina madhara kwa afya. Kwa sababu *purification* yake haijafikia ule ubora unaotakiwa. Kwa hiyo naiomba Serikali walichukue tu hilo waje watusaidie.

Mheshimiwa Lyimo, *again*, limetokea jana na Waheshimiwa Wabunge niwaombe sana, kuna kitu kimoja ambacho uwe umekalia hapa, au umekaa kwenye kiti kwenye Kamati, suala la kuhusu utaratibu maana ni Kanuni tunataka utuambie ni wapi Kanuni zimekiukwa? Huwezi ukasema Mwongozo, Taarifa, haiwezekani. Msikiweke Kiti katika hali ambayo si nzuri lakini ukisema kwa suala la utaratibu, nyumba itakusikiliza kwa sababu hatutaki kukiuka

Kanuni na kwa hiyo kwa jana, nataka niseme Bunge lilihojiwa kwa ujumla wake, kwa hiyo mafungu na kasma zote zile zimepitishwa rasmi na Bunge. Huo ndiyo Mwongozo wangu. *(Makofi)*

Naenda kwa jambo la Mheshimiwa Msigwa. Kanuni zetu zinasema tusiwahishe mambo, tunakatazwa kabisa, jana mmemsikia Mheshimiwa Spika, amelisemea hapa na ameelekeza linaenda wapi suala hili, mimi nasema natumia *Parliamentary Restraint*, ningelikuwa Mahakamani, nasema *Judiciary Restraint,* nijizuie kwa swali hilo hadi litakapo fika kule na baadaye litaletwa humu Bungeni. Litakapokuja sana, ndiyo utapata nafasi ya kuyasema hayo na kuuliza usaidiwe, bado haijafungwa, huo mlango haujafungwa. Uwe na subira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Yahaya, baridi, Waheshimiwa Wabunge, kwanza mmevaa nadhifu sana, nawaona Waheshimiwa Wabunge wa kiume wa kike, ndiyo nadhifu, koti safi, suti, lakini unasema, bado unasikia baridi?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

WABUNGE FULANI: Hapana hiyo.

MWENYEKITI: enhe, naona sasa, mara joto, mara baridi sana, mimi nadhani acha. Nalichukua tu kwa maana ni suala la kiutawala sana hili acha Katibu alichukue tuone itakuwaje. Mara nyingine ni kweli inakuwa baridi kweli kweli humu ndani, lakini mara nyingine inakuwa joto sana.

Kwa hiyo tuwe *in a balancing act* ya kutuwezesha kuweza kutekeleza majukumu yetu humu ndani vizuri bila kukwazika. Kwa hiyo Mheshimiwa Yahaya tunakushukuru sana kwa *observation* yako hiyo. Katibu!

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

MWENYEKITI: Ahsante mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hasunga una muda usiozidi saa moja kuwasilisha hoja yako.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba kufatia taarifa iliyowasilishwa leo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Bunge lako tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, inaliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika siku ya leo tukiwa wazima wa afya njema na kuendelea kuijalia nchi yetu amani na mshikamano na kujadili bajeti hii inayolenga kusukuma mbele kasi ya maendeleo ya kilimo na wakulima kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kuwa Waziri wa Kilimo. Pia ninamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanayofanya ya kusukuma maendeleo ya nchi hii ikiwemo sekta ya kilimo. Napenda kuwaahidi kwamba nitafanya kazi kwa kuongoza Wizara ya Kilimo kwa uaminifu, juhudi na maarifa ili kuhakikisha kuwa rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ya kilimo zinawafikiwa walengwa ili kuongeza tija na kuinua kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa hotuba yake ambayo iligusa maeneo mengi ikiwemo sekta ya kilimo. Aidha, nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha na kusimamia kilimo pamoja na maendeleo ya ushirika nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe mwenyewe na Naibu Spika, Dkt. Tulia Akson Mwansasu Mbunge pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa. Aidha, nitumie nafasi hii kuwapongeza Wabunge wote kwa umahiri wao mkubwa katika mijadala inayoendelea katika Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Makamu Mwenyekiti, Dkt. Christine Ishengoma (Mb). Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wizara na kutembelea baadhi ya maeneo kuona utekelezaji wa kazi za kilimo na kushauri namna ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara, bodi na taasisi zake. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba ushauri wao umezingatiwa na tutaendelea kushirikiana na kamati ili kuleta mageuzi ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa Sekta ya Kilimo. Serikali imepanga kubadilisha kilimo kutoka kuwa kilimo cha kujikimu na kuwa kilimo cha kibiashara kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2020/2025. Aidha, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo umesisitiza mapinduzi ya viwanda na umeitambua sekta ya kilimo kuwa muhimili imara kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi za viwandani. Miongozo hiyo ya kitaifa pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015/2020 na Sera ya Kilimo ya Mwaka 2013 inatekelezwa na Wizara kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya pili *(ASDP*

II) ambayo inalenga kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa kuongeza mitaji, teknolojia na ubunifu sekta binafsi inashirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wa *ASDP II*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ASDP II* ilizinduliwa rasmi tarehe 04 Juni 2018 na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli Rais wa Jamuhiri ya MUungano wa Tanzania. Inalenga kubadilisha maisha ya mkulima kwa kufanya mageuzi makubwa kwenye kilimo kwa kuzingatia mazao ya kipaumbele kulingana na ikolojia ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchango wa Sekta ya Kilimo Katika Uchumi. Kilimo ni sekta kubwa na muhimu kwa maendeleo kutokana na mchango wake katika uchumi. Katika mwaka 2017 sekta hiyo imetoa ajira kwa watanzania kwa asilimia 65.5 ikichangia takribani asilimia 28.7 ya Pato la Taifa ambapo sekta ndogo ya mazao ilichangia asilimia 16.58. vilevile sekta ya kilimo inachangia asilimia 65 ya malighafi za viwandani. Takwimu zinaonesha kuwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2018 ukuaji wa sekta ya kilimo ulifikia asilimia 7.1. Ukuaji huu ulichangiwa na jitihada za Serikali za kuhakikisha upatikanaji na matumizi ya pembejeo bora hali nzuri ya mvua na uboreshaji wa miundombinu ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Chakula. Upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2018/2019 ulifikia tani milioni 16.89 zikiwemo tani milioni 9.53 za mazao ya nafaka na tani milioni 7.35 za mazao yasiyo ya nafaka. Kiwango hicho cha uzalishaji kimeiwezesha nchi kujitosheleza kwa mahitaji yake ya chakula ya tani milioni 13.56 na hivyo kuwa na ziada ya tani milioni 3.32 za chakula kwa kiwango cha utoshelevu wa asilimia 124. Niwahakikishie Watanzania kwamba tunacho chakula cha kutosha nchini. Hata hivyo tuendelee kuweka akiba katika kaya zetu hadi hapo tutakapovuna tena kwani inaonekana kwamba huenda tusiwe na mavuno mazuri sana msimu huu kutokana na uhaba wa mvua kwenye maeneo ya kanda ya ziwa, kanda ya kati, kanda ya kaskazini mwa nchi yetu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina yanapatikana katika ukursa wa tano wa kitabu cha hotuba ya bajeti ambayo imewasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umwagiliaji. Katika mwaka 2018/2019 wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha Mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa Mwaka 2002 ili kubaini maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kuzingatia Mpango Shirikishi wa Maendeleo ya Rasilimali Maji. Katika mpango huo hekta laki tano na sitini mia nane na themanini zimepangwa kuendelezwa kwa lengo la kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta laki nne na sabini na tano elfu na hamsini na mbili kwa mwaka 2018/2019 hadi hekta milioni moja ifikapo mwaka 2035. Maelezo ya kina yanapatikana ukurasa wa sita wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Ushirika. Kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kuimarisha sekta ya ushirika kwa kusimamia na kuhamasisha maendeleo yake. Vyama vya ushirika vimeongezeka kutoka vyama 10990 Desemba mwaka 2017 hadi vyama 11331 kufikia Desemba mwaka 2018. Vilevile idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika imeongezeka kutoka 2,617,311 mwaka 2017 hadi 3,998,193 ilipofika Februari mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 53. Hadi Desemba mwaka 2018 mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.3 imetolewa kwa wananchama ikilinganishwa na shilingi bilioni 902 iliyotolewa katika kipindi cha Desemba mwaka 2017. Aidha, akiba na amana za wanachama katika *SACCOS* zimefikia shilingi bilioni 575 na hisa za shilingi bilioni 79. Maelezo ya kina yanapatikana ukurasa wa 7 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2018/2019. Katika mwaka 2018/2019 Wizara imetekeleza maeneo ya kipaumbele ya kuongeza tija kwa kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, udhibiti wa visumbufu, matumizi ya zana bora za kilimo na huduma za ughani, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi mazao ya

kilimo na masoko, kufanya utafiti wa kilimo na kuzalisha teknolojia kwa mazao ya mahindi, mihogo, ngano, michikichi, ufuta, alizeti, pamba na mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ya kipaumbele ni kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora za mazao na kusambaza kwa wakulima. Kuboresha maarifa na ujuzi kwa watafiti, kuimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa udongo kuendana na mahitaji ya mazao ya kilimo ki-ikolojia, mafunzo na usambazaji taarifa za kilimo na sayansi shirikishi kusajili na kuandaa kazi data ya wakulima na kuimarisha ushirika. Masuala yote haya yanapatikana katika kitabu cha bajeti ambacho tumekiswasilisha kuanzia ukurawa sa 10 mpaka ukurasa wa 61 katika kitabu hicho cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza vipaumbele hivyo shilingi bilioni 102.07 ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kati ya fedha hizo fungu 43 (Wizara ya Kilimo) iliidhinishiwa shilingi bilioni 166.26 zikiwemo shilingi bilioni 68.14 za Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 98.12 za Matumizi ya Maendeleo. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu Namba Tano iliidhinishiwa shilingi bilioni 29.77 zikiwemo shilingi bilioni 3.95 za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 25.82 fedha za maendeleo; na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (Fungu 24) iliidhinishiwa bilioni 8.05 zikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuongeza Tija Katika Kilimo; Upatikanaji wa Mbegu Bora za Mazao. Katika mwaka 2018/ 2019 upatikanaji wa mbegu bora umefikia tani 49,040.66. Kati ya kiasi hicho tani 38,507.87 zimezalishwa hapa nchini na tani 8,361.46 zimeagizwa kutoka nchi za nje; na tani 2,171.33 ni bakaa ya msimu wa mwaka 2017/2018. Vilevile miche 1,507 ya miwa, vipande 121,805 vya muhogo na vikonyo 520,000 vya viazi lishe vimezalishwa. Aidha, aina mpya 13 za mbegu bora zimeidhinishwa na zitaanza kuzalishwa katika msimu wa mwaka 2019/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji na Udhibiti wa Ubora wa Mbolea/ Hadi mwezi Machi mwaka 2019

upatikanaji na usambazaji wa mbolea nchini ulikuwa tani 492,394 ikilinganishwa na mahitaji ya tani 514,138 katika msimu wa mwaka 2018/2019. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (*TFRA)* imefanya ukaguzi wa uuzaji wa mbolea 1,350 na wafanyabiashara 496 wapya wa mbolea wamesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu. Katika mwaka 2018/2019 Wizara imenunua lita 296,000 na kilo 3,000 za viwatilifu zenye thamani ya shilingi bilioni tisa kwa ajili ya kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mazao. Hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2019 ndege waharibifu wa nafaka walizidhibitiwa katika skimu za umwagiliaji za Kahe, Lekitatu na Misenyi kwa mazao ya mpunga na mtama. Aidha, lita 119,000 kwa ajili ya kudhibiti viwavijeshi vamizi zimesambazwa katika Kanda ya Ziwa, Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Mashariki na kutoa mafunzo kwa maafisa ugani na wakulima 350.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zana za Kilimo. Takwimu zinaonesha kwamba wastani wa kitaifa wa matumizi ya dhana bora za kilimo umeongezeka hadi kufikia asilimia 20 kwa matrekta na asilimia 27 kwa wanya makazi ikilinganishwa na asilimia 14 ya matrekta na asilimia 24 ya wanyamakazi kwa mwaka 2013. Kutokana na ongezeko hilo matumizi ya jembe la mkono yamepungua na kufikia asilimia 53 kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 62 kwa mwaka 2013. Aidha, kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo *(AGITF)* Wizara imeendelea kutoa mikopo na pembejeo ya zana za kilimo. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi mwezi Machi mwaka 2019 mikopo 33 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.5 imetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji. Tume ya Taifa ya Maendeleo ya Umwagiliji imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo unaofadhiliwa na Serikali ya Japan. Mradi umekarabati skimu za umwagiliaji 129 katika halmashauri 68 nchini pamoja na ununuzi wa mitambo ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utafiti wa Kilimo na Uhaulishaji wa Teknolojia. Katika mwaka 2018/2019 Wizara kupitia TARI imegundua mbegu bora mpya aina nne za mahindi. Mbegu hizo zina uwezo wa kutoa mavuno kwa wastani wa tani 5.8 kwa hekta kwenye mashamba ya wakulima katika ukanda wa chini na kati. Zinahimili ukame na zina ukinzani wa magonjwa ya majani ya mahindi na michirizi ya ukungu. Vilevile kwa kushirikiana na kampuni binafsi TARI imezalisha aina sita za miche bora ya migomba na kugundua aina 62 ya mbegu za mikunde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Mazao; Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao mbalimbali kwa kuimarisha huduma za utafiti, upatikanaji na utumiaji wa pembejeo na zana za kilimo, udhibiti wa visumbufu vya mazao, huduma za ugani, uongezaji wa thamani na upatikanaji wa masoko.

Aidha, Wizara imeandaa mkakati wa miaka minne kuanzia mwaka 2018/2019 hadi mwaka 2021/2022 wa kuendeleza zao la michikichi ili kuweza kuchangia katika upatikanaji wa mafuta ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazao Makuu ya Asili ya Biashara. Uzalishaji wa mazao makuu ya biashara uliongezeka kutoka tani 901,641 msimu wa mwaka 2016/2017 hadi tani 967,184 msimu wa mwaka 2017/2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.2. Katika msimu wa mwaka 2018/2019 Wizara ililenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara hadi kufikia tani milioni 1,356, 368. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 tani 667,631.77 sawa na asilimia 49.2 ya lengo zilikuwa zimezalishwa na uzalishaji bado unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazao ya Bustani. Katika mwaka 2017/2018 uzalishaji wa mazao ya bustani ulikuwa tani milioni 5.33 na matarajio ya uzalishaji kwa mwaka 2018/2019 ni tani milioni 5.96. hadi kufikia mwezi Machi, 2019 uzalishaji umefikia tani milioni 4.36 sawa na asilimia 73.17 ya lengo na msimu wa uzalishaji bado unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo na Masoko; Miundombinu ya Kuhifadhi mazao. Wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* inaendelea kutekeleza Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka. Hadi kufikia mwezi Machi 2019, asilimia 83 ya vifaa vilikuwa vimeingizwa nchini kwa ajili ya ujenzi wa ghala katika vituo vya Makambako, Mbozi, Songea, Shinyanga na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* inaendelea kutekeleza Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019, asilimia 83 ya vifaa vilikuwa vimeingizwa nchini kwa ajili ya ujenzi wa ghala katika vituo vya Makambako, Mbozi, Songea, Shinyanga na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masoko ya Mazao ya Kilimo, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeanzisha kitengo cha masoko ya mazao ya kilimo ambacho kinahusika na kutafuta masoko ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeingia makubaliano ya Itifaki ya usafi baina ya Tanzania na Serikali ya China kuwezesha kuuza muhogo nchini China ambapo hadi mwezi Machi 2019, kampuni tano zimesajiliwa kwa ajili ya kuuza zao hilo nchini China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi na usalama wa chakula, katika mwaka 2018/2019, *NFRA* imenunua tani 46,236.035 za mahindi kwa ajili hifadhi na imeliuzia Shirika la Mpango wa Chakula Duniani tani 36,000 za mahindi zenye thamani ya Shilingi bilioni 21. Aidha, Wizara imeanza kutekeleza miradi ya kudhibiti sumu kuvu katika mazao unaolenga kudhibiti tatizo la sumu kuvu katika mazao ya mahindi na karanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Ushauri Kuhusu Utafiti, Mafunzo na Usambazaji Taarifa za Kilimo na Sayansi Shirikishi, Huduma za Ugani. Katika mwaka 2018/2019, Wizara imeandaa rasimu ya mwongozo wa utoaji na usimamizi wa huduma za ugani utakaotumiwa na Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Aidha, elimu kuhusu kanuni bora za uzalishaji wa

mazao, kuongeza thamani mazao ya kilimo, upatikanaji wa masoko, upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuwekeza kwenye kilimo, pembejeo na zana bora za kilimo imetolewa kupitia maonesho na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo na Vituo vya Mafunzo ya Kilimo, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Vyuo vyake vya Kilimo imedahili na kufundisha wanafunzi 2,389 ambapo wanafunzi 2,051 wamefadhiliwa na Serikali na 338 wanajilipia wenyewe. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, wanafunzi 1,537 ni ngazi ya Astashahada na 852 ni ngazi ya Stashahada. Jumla ya wanafunzi 1,026 wakiwemo 263 wa Stashahada na 763 wa Astashahada watahitimu masomo yao itakapofika mwezi Juni, mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha Ushirika, katika mwaka 2018/2019, Tume ya Maendeleo ya Ushirika kupitia Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika *(COASCO)* limefanya ukaguzi wa nje kwa vyama vya ushirika 2,297. Kati ya Vyama vilivyokaguliwa, asilimia 4.6 vilipata hati inayoridhisha, asilimia 64.6 vilipata hati yenye shaka, asilimia 21.6 vilipata hati isiyoridhisha na asilimia 9.2 vilipata hati mbaya. Hali hii ya Vyama vya Ushirika siyo nzuri na hatuwezi kuifumbia macho. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yenu tuendelee kushirikiana na halmashauri zetu kuvisaidia vyama hivi ambavyo ni mkombozi wa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usajili wa Wakulima Wizara imeanza usajili wakulima wote kwa mazao ambayo yanasimamiwa na Bodi. Mazao hayo ni, kahawa, korosho, miwa, pamba, chai, mkonge, tumbaku na pareto. Hadi kufikia mwezi Machi 2019, wakulima 1,464,827 wametambuliwa na kusajiliwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usajili wa Wakulima, Wizara imeanza usajili wakulima wote kwa mazao ambayo yanasimamiwa na Bodi. Mazao hayo ni, kahawa, korosho, miwa, pamba, chai, mkonge, tumbaku na pareto. Hadi kufikia mwezi Machi 2019, wakulima 1,464,827 wametambuliwa na kusajiliwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masuala Mtambuka, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kuzingatia masuala mtambuka katika kutekeleza majukumu yake. Masuala hayo ni pamoja na ushiriki wa vijana katika kilimo, lishe, jinsia, hifadhi ya mazingira na VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2019/2020, kuongeza tija katika kilimo. Upatikanaji wa mbegu bora za mazao, katika mwaka 2019/2020, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, imejipanga kuzalisha jumla ya tani 53,608.2 za mbegu mbalimbali. Wazalishaji hao ni pamoja na *ASA*, yaani Wakala wa Mbegu wa Taifa, *ASA,* Vituo vya Utafiti, Magereza na Sekta binafsi. Vilevile, *ASA* itazalisha vipando bora vya mihogo pingili 7,000,000 na miche bora ya matunda 20,000. Ili kufikia malengo hayo, miundombinu ya umwagiliaji itaboreshwa katika mashamba yanayomilikiwa na *ASA* na eneo la uzalishaji wa mbegu litaongezwa hadi kufikia hekta 811 katika mashamba ya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji na udhibiti wa ubora wa Mbolea, katika mwaka 2019/2020, Wizara itasimamia uagizaji na usambazaji wa tani 625,000 za mbolea zinazokadiriwa kutumika nchini. Aidha, Kampuni ya Mbolea Tanzania *(TFC)* itaongeza mauzo ya mbolea kutoka tani 10,000 hadi tani 100,000. Vilevile, ghala moja lenye uwezo wa kuhifadhi tani 20,000 za mbolea, litakarabatiwa katika Wilaya ya Tabora pamoja na kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuchanganya mbolea kwa uwiano yaani *blending plant* katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu, katika mwaka 2019/2020, Wizara itanunua na kusambaza lita 300,000 na kilo 3,000 za viuatilifu kwa ajili ya kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mazao. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha kituo cha kudhibiti milipuko cha Kilimo Anga, Arusha ili kutoa huduma bora. Vilevile, Wizara itaendelea kuvijengea uwezo na kukarabati vituo 10 kati ya vituo 36 vya ukaguzi wa mazao vilivyoko mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zana za Kilimo, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaanzisha kituo kimoja cha zana za kilimo kwa ajili ya kutoa huduma za kiufundi na mafunzo kwa watoa huduma binafsi, wamiliki na watumiaji wa zana za kilimo kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wakulima katika Kanda ya Ziwa. Vilevile, Wizara kupitia *AGITF,* imepanga kutoa mikopo 250 yenye thamani ya shilingi bilioni 4.12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itafanya tathmini ya miradi ya umwagiliaji ambayo ujenzi wake haukukamilika ili miradi hiyo iweze kukamilishwa kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia Mradi wa Kuendeleza Skimu za Wamwagiliaji Wadogo, Wizara itakamilisha ujenzi wa skimu 16 za umwagiliaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utafiti wa Kilimo na Uhaulishaji wa Teknolojia. Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia TARI imepanga kutafiti, kugundua na kusambaza aina 15 za mbegu bora za mazao ya nafaka, mizizi, mbegu za mafuta, mikunde, migomba na mazao ya bustani. Vilevile, Wizara itasafisha aina tisa za mbegu ya mpunga na kuzalisha tani 10 za mbegu za awali katika Kituo cha Utafiti cha KATRINI. Aidha, kupitia kituo cha TARI Naliendele, Serikali itajenga kinu cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 1,800 kwa mwaka na kusindika tani 1,000 za mvinyo na sharubati *(juice).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Mazao, katika mwaka 2019/2020, Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa mazao ya kipaumbele kwa kuendeleza kuratibu utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao hayo ikiwemo kuimarisha utafiti, upatikanaji na utumiaji wa pembejeo na zana za bora za kilimo, udhibiti wa visumbufu, huduma za ugani, kuongeza maeneo ya uzalishaji, uongezaji wa thamani na upatikanaji wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la Korosho, Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Korosho itaendelea kutekeleza programu ya kuzalisha miche bora milioni 10 ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango itahakiki na kulipa vikundi vya wazalishaji wa miche ya mikorosho kwa msimu wa 2017/2018 ambao hawajalipwa katika mikoa saba. Vilevile, Wizara itaratibu upatikanaji na usambazaji wa tani 30,000 na lita 500,000 za salfa kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Sukari itaratibu uzalishaji wa tani 403,786 za sukari kwa kuongeza eneo la uzalishaji wa kilimo cha miwa kutoka hekta 52,000 hadi hekta 97,000. Wizara, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* itawezesha upatikanaji wa ardhi na uwekezaji wa miradi mipya ya sukari katika Wilaya za Kasulu, Kibondo, Rufiji, Geita, Kilombero, Karagwe, Pangani, Bagamoyo na Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la Kahawa, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya kahawa itaongeza uzalishaji wa kahawa kutoka tani 65,000 hadi tani 80,000. Aidha Bodi imepanga kuzalisha na kusambaza miche milioni 10 ya kahawa katika Wilaya 42 zinazolima zao la kahawa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la Mkonge, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Mkonge imepanga kuongeza uzalishaji wa mkonge kutoka tani 38,506 hadi tani 113,506 kwa kuongeza eneo la uzalishaji kutoka hekta 42,426.11 hadi 114,915.08, kusimamia uendeshaji wa mfumo wa kilimo cha wakulima wadogo cha mkataba na kuimarisha vyama vya ushirika na masoko ya mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la Pamba, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Pamba imepanga kuongeza uzalishaji wa pamba kutoka tani 222,000 hadi tani

700,000 na kuongeza tija kutoka tani 300 hadi tani 600 kwa ekari. Aidha, upatikanaji wa mbegu za pamba utaongezeka kutoka tani 22,000 hadi 40,000 na upatikanaji wa viuatilifu utaongezeka kutoka lita milioni 7 hadi milioni 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la Tumbaku, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku imepanga kuongeza uzalishaji kutoka tani 55,000 hadi tani 60,000; kuimarisha vituo 1,972 vya kufungia na kuchambulia tumbaku itaimarisha mfumo wa upatikanaji wa pembejeo za zao la tumbaku kwa kuwaunganisha watoa huduma wa pembejeo na Vyama vya Ushirika ili ziwafikie kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la Chai, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Chai imepanga kuongeza uzalishaji wa chai kavu kutoka tani 34,000 hadi tani 40,000 ambazo ni sawa na tani 182,000 za majani mabichi ya chai. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(PSSSF)* itafufua kiwanda cha chai cha Mponde ili kuimarisha upatikanaji wa soko la majani mabichi ya chai kwa wakulima na kuongeza ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miundombinu ya Hifadhi na Uongezaji Thamani Mazao ya Kilimo, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia *NFRA* itakamilisha Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi ambapo ujenzi wa maghala matano yenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000 na vihenge nane vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 190,000 za nafaka utakamilika na hivyo kuongeza uwezo wake wa kuhifadhi nafaka kutoka tani 251,000 hadi tani 501,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Utafiti huduma za Ugani na Mafunzo, Kuimarisha Vituo vya Utafiti, katika mwaka 2019/2020, Wizara itakarabati ofisi na kuvipatia vifaa muhimu vituo vya utafiti vya Ukiriguru, Ilonga na Tumbi.

Aidha, miundombinu ya umwagiliaji ya vituo vya utafiti vya Ilonga, Naliendele, Ukiliguru na miundombinu ya uhifadhi wa mbegu katika vituo vya Uyole, Ilonga na Seliani itaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Ugani, Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais -TAMISEMI na Sekta binafsi itakamilisha Mwongozo wa Utoaji na Usimamizi wa Huduma za Ugani Kilimo ili kuendana na mahitaji ya sasa ya utoaji wa huduma hizo hapa nchini kusudi maafisa ugani wale watoe huduma zinazostahili kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo na Vituo vya Mafunzo ya Kilimo, katika mwaka 2019/2020, Wizara itadahili wanafunzi 2,500 ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa ufadhili wa Serikali. Vilevile, itakarabati miundombinu ikiwa ni pamoja na madarasa 6, ofisi 12, mabweni 12, maktaba 6 na mabwalo ya chakula 6 katika vyuo vya mafunzo ya kilimo vya Mtwara, Igurusi, Horiti Tengeru, Tumbi, Mlingano na Maruku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha Ushirika, katika mwaka 2019/2020, Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaimarisha udhibiti na usimamizi wa vyama vya ushirika; itahamasisha wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Mazao kuanzisha *SACCOS* 1,500 kwenye maeneo yao, na itahuisha Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 ili kupitia upya Sheria za ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uratibu, Takwimu, na Ufuatiliaji, katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar itafanya Sensa ya kilimo kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masuala Mtambuka, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuzingatia masuala mbalimbali mtambuka yakiwemo ushiriki wa vijana katika kilimo, kuongeza lishe, jinsia, VVU na UKIMWI na kuboresha mazingira katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maeneo Maalum ya Maboresho katika Kilimo, Naomba sasa nizungumzie maeneo machache ya kimkakati ambayo kama Wizara tumeona ni

muhimu kuyafanyia maboresho ili kuimarisha usimamizi wa kilimo na kuwapatia wakulima huduma kwa urahisi zaidi. Maeneo hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Sera na Sheria, Wizara imeanza na itaendelea kuipitia Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013 na Sheria mbalimbali kwa lengo la kubaini maeneo ambayo yatapaswa kuhuishwa ili kwenda na hali halisi ya sasa na mwelekeo wa Serikali wa kubadili kilimo chetu kuwa kilimo cha kibiashara. Mtazamo wa Wizara, ni kuwa na Sheria moja itakayosimamia rasilimaliwatu, matumizi bora ya pembejeo ardhi ya kilimo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bima ya Mazao, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanza mchakato wa kuanzisha Bima ya Mazao hapa nchini ili kumwezesha mkulima kulipwa fidia pale anapopata hasara. Maandalizi yanaendelea kufanyika ili katika mwaka wa fedha 2019/2020, tuwe angalau na aina mbili za mifumo ya Bima ya mazao inayoweza kutumika hapa nchini. Hata hivyo, utaratibu huu ili uwezekane, kutahitajika takwimu sahihi za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na uzingatiaji wa kanuni bora za Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa wakulima; katika mwaka 2019/2020, Wizara itaimarisha kanzidata ya wakulima na kuendelea na usajili wa wakulima wa mazao mchanganyiko kwa kushirikiana kwa karibu sana na vyama vya ushirika na taasisi nyingine kilele za wakulima kama vile Tanganyika *Farmers Association (TFA).* Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kuhamamisha wakulima katika maeneo yenu ili watakapofikiwa na zoezi la uandikishaji watoe ushirikiano na waelewe kwamba zoezi hili ni la kuwasaidia kupata huduma bora za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko ya mazao; Wizara imeamua kuimarisha utafutaji wa masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2019/2020 Wizara itakiimarisha kitengo cha masoko kwa kukijengea uwezo wa kufanya chambuzi na utafutaji wa masoko ndani na nje ya nchi. Aidha, elimu itaendelea kutolewa kwa wakulima ili

wazalishe kulingana na mahitaji ya soko. Vile vile tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na taasisi nyingine zinazohusika na masoko nchini ikiwemo *TANTRADE* na soko la bidhaa ya *TMX.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa upatikanaji wa pembejeo za kilimo; Wizara imeanza zoezi la kupitia kwa kina mifumo iliyopo ya uzalishaji, uagizaji na usambazaji wa mbegu, mbolea na viuatilifu. Mifumo iliyopo kwa sasa inatofautiana kwani kuna baadhi ya Bodi za Mazao zinajihusisha na uagizaji na usambazaji wa pembejeo wakati mwingine Vyama vya Ushirika vinaagiza na wakati mwingine vinashiriki kusambaza pembejeo kwa wanachama wao. Wakulima pia hununua pembejeo moja kwa moja kutoka kwa wafanyabiashara na pia mbolea kwa sasa inaagizwa kwa mfumo wa pamoja *(bulk procurement).* Mfumo huu tutaupitia ili kurahisisha kuwa na mfumo mmoja ambao utakuwa unaeleweka kwa kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa pembejeo za kilimo na tofauti ya mifumo hiyo tumeamua kuipitia yote ili kuona mfumo bora unaoweza kutumika kuhakikisha pembejeo zenye ubora zinapatikana na kusambazwa kwa wakulima kwa wakati. Malengo yetu ni kukamilisha mapitio hayo na kupata majawabu ya mfumo bora ifikapo Juni, 2019 ili mwaka 2019/2020 tuwe na mfumo madhubuti utakaokuwa na tija kwetu sote. Nina uhakika kwamba mfumo mzuri wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo utawezesha uwepo wa pembejeo bora kwa bei nafuu na hivyo kuongeza matumizi kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina ya hotuba yangu hususan mpango na maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2019/2020, yanapatikana ukurasa wa 61 hadi ukurasa wa 91 katika kitabu cha hotuba cha Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2019/2020 kilichowasilishwa Bungeni hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani; kabla sijamaliza hotuba yangu naomba nitoe shukrani za dhati kwa watu, taasisi, makundi na wadau mbalimbali ambao tunashirikiana kuendeleza kilimo. Kwanza nawashukuru sana Naibu Mawaziri

Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumbae) na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu Mhandisi Mercy John Ntigumwe, Naibu Katibu Mkuu Profesa Caesar Tumbo, Wakurugenzi wa Idara na Wakuu wa Vitengo, Taasisi na Asasi zote zilizoko chini ya Wizara. Watumishi wote wa Wizara na wadau wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliotuwezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 pamoja na kuandaa hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba wataendelea kunipatia ushirikiano huo katika mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi ya Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo:-

Serikali ya Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia. Korea ya Kusini, India, Misri, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Vietnam, Canada na Poland. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo:-

Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, ILRI* na *CABI.* Nyingine ni *CFC, AVRDC, AGRA, CIP, CIAT, UNEP, WARDA,* Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani *(HELVETAS).* Wadau wengine ni Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu, *Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust, Rockfeller Foundation, Aga Khan Foundation, Unilever* na Asasi Zisizo za Kiserikali nyingi ambazo hatuwezi kuzitaja hapa ambazo zinashiriki katika kuchangia katika kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Vwawa kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, nawashukuru viongozi wangu cha Chama cha Mapinduzi kwa heshima kubwa ambapo kwa kweli wamekuwa wakiniunga mkono na kunisaidia katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, nawashukuru sana familia yangu wakiongozwa na mke wangu na watoto kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakiniombea katika kutekeleza majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwahimiza wananchi wote wa Jimbo la Vwawa kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Kwa umuhimu wa pekee, natoa shukurani za dhati kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa ujumla. Nawapa hongera sana wakulima wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2019/2020. Katika mwaka 2019/2020, Wizara inaomba idhini ya kukusanya maduhuli ya Sh.3,472,515,000 yatokanayo na vyanzo mbalimbali ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Kilimo inaomba kutumia jumla ya Sh.253,856,943,970 kupitia Fungu 43, Fungu Na.5 na Fungu 24 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 43 - Wizara ya Kilimo; jumla ya shilingi 208,044,783,140 zinaombwa. Kati ya fedha hizo shilingi 143,577,036,140 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo shilingi 82,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 61,577,036,140 ni fedha za nje. Aidha, shilingi 64,467,747,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi 13,214,159,060 ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara na shilingi 29,621,801,490 ni kwa ajili ya mishahara ya Bodi na Taasisi. Shilingi11,453,309,490 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Wizara na shilingi 10,178,479,510 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Bodi na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na.5 - Tume ya Umwagiliaji; jumla ya shilingi 37,485,090,830 zinaombwa. Kati ya fedha hizo shilingi 32,501,462,613 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo shilingi 3,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 29,501,462,613 ni fedha za nje. Aidha, shilingi 4,983,628,217 zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi 4,098,444,217 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Tume na shilingi 885,184,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 24 – Tume ya Ushirika; jumla ya shilingi 8,327,070,000 zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi 6,127,370,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 2,199,700,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya sehemu ya maombi ya fedha kwa Mwaka 2019/2020, kwa mafungu 43, Fungu Na. 5 na Fungu 24 yanapatikana ukurasa wa 93 hadi ukurasa wa 95 wa kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; pamoja na hotuba hii, vipo viambatanisho vinavyotoa ufafanuzi wa baadhi ya maeneo. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Kilimo (www.kilimo.go.tz).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kuwasilisha vizuri hoja yako.

HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

2. Mheshimiwa Spika , awali ya yoteninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa wazima wa afya njema na kuendelea kuijalia nchi yetu amani na mshikamano na kujadili bajeti hii inayolenga kusukuma mbele kasi ya maendeleo ya Sekta ya Kilimo na wakulima kwa ujumla wao.

3. Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tan- zania, kwa kuniteua kuwa Waziri wa Kilimo. Niwashukuru pia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayofanya kusukuma maendeleo ya nchi hii, ikiwemo Sekta ya Kilimo. Napenda kuwaahidi kwamba nitafanya kazi ya kuongoza Wizara ya Kilimo kwa uaminifu, juhudi na maarifa ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya maendeleo ya kilimo zinawafikia walengwa ili kuongeza tija na kuinua kipato chao.

4. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni. Hotuba hiyo iligusa maeneo mengi ikiwemo Sekta ya Kilimo na kuleta mjadala

mzuri na wenye afya kwa nchi yetu. Aidha, nimpongeze tena Mhe. Waziri Mkuu kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele kuhamasisha na kusimamia kilimo hususan mazao ya kimkakati ya michikichi, korosho, kahawa, chai, pamba na tumbaku. Vilevile, Mhe.Waziri Mkuu amekuwa mstari wa mbele kuhamasisha maendeleo ya Vyama vya Ushirika pamoja na upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo.

5. Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi, na Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.) pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa. Aidha, nitumie nafasi hii kuwapongeza Wabunge wote kwa umahiri wao mkubwa katika mijadala inayoendelea katika Bunge hili la Bajeti.

6. Mheshimiwa Spika, nina chukua fursa hii pia kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji chini ya Ue nye kiti wa Mhe . Mahmoud Mgi mwa, Mbun ge wa Muf indi Kaskazini na Makamu Mwenye kiti Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma (Mb). Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wizara na kutembelea baadhi ya maeneo kuona utekelezaji wa kazi za kilimo na kushauri namna ya kuimarisha ute ke lezaji wa majukumu ya Wizara, Bodi na Taasisi zake. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, ushauri wao umezingatiwa na tutaendeleea kushirikiana na Kamati ili kuleta mageuzi ya kilimo nchini na kufikia matarajio ya wananchi katika kufikia uchumi wa kati.

2.0 MWELEKEO WA SEKTA YA KILIMO

7. Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kubadilisha kilimo kutoka kuwa cha kujikimu na kuwa kilimo cha kibiashara. Mabadiliko haya yanafanyika kwa kuzingatia malengo ya kitaifa yaliyowekwa hususan nchi yetu kufikia kipato cha kati kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Vilevile, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo unaoweka mkazo kwenye mapinduzi ya viwanda, unaitambua Sekta ya Kilimo ka ma mhim ili imara utakaowe ze sha upatikanaji wa malighafi za viwanda.

Miongozo hiyo ya Kitaifa, pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na Sera ya Kilimo ya mwaka 2013, inatekelezwa na Wizara kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) ambayo inalenga kuleta mageuzi katika Sekta ya Kilimo (Kilimo, Mifugo na Uvuvi). Aidha, kwa kutambua umuhimu wa Sekta Binafsi kwenye kuongeza mitaji, teknolojia na ubunifu, sekta hiyo inashirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wa ASDP II.

8. Mheshimiwa Spika, ASDP II iliyozinduliwa rasmi tarehe 4 Juni, 2018 na Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inalenga kubadilisha maisha ya mkulima kwa kufanya mage uzi makubwa kwenye kilimo. Utekelezaji wa Programu hiyo utazingatia mazao ya kipaumbele kulingana na ikolojia za kilimo. Mazao yaliyopewa kipaumbele ni korosho, pamba, tumbaku, kahawa, chai, miwa, mahindi na mpunga. Mazao mengine, mikunde, viazi mviringo na vitamu, mazao ya bustani na mbegu za mafuta (alizeti, ufuta na michikichi). Mkazo umewekwa kuhakikisha kwamba pembejeo na zana za kilimo bora zinapatikana; kuimarisha utafiti, huduma za ugani na mafunzo; upatikanaji wa masoko ya mazao na miundombinu ya uzalishaji.

Utekelezaji makini wa ASDP II utaleta mapinduzi makubwa kwenye Kilimo.

3.0 MCHANGO WA KILIMO KATIKA UCHUMI

9. Mheshimiwa Spika, kilimo ni Sekta kubwa na muhimu kwa maendeleo kutokana na mchango wake katika uchumi. Katika mwaka 2017, sekta hiyo ilitoa ajira kwa Watanzania kwa asilimia 65.5, ikichangia asilimia 28.7 ya Pato la Taifa ambapo sekta ndogo ya mazao ilichangia asilimia 16.58. Vilevile, Sekta ya Kilimo inachangia asilimia 65 ya malighafi za viwanda. Takwimu zinaonesha kuwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2018, ukuaji wa Sekta ya Kilimo ulifikia asilimia 7.1. Ukuaji huu ulichangiwa na hali nzuri ya hewa na jitihada za Serikali za kuhakikisha kuwa pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati pamoja na uboreshaji wa miundombinu katika maeneo ya uzalishaji.

3.1 Upatikanaji wa Chakula

10. Mheshimiwa Spika, tathmini ya uzalishaji wa Mazao ya Chakula nchini kwa msimu wa 2017/2018 na hali ya upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2018/2019 iliyofanyika Desemba 2018 imebaini kuwa, uzalishaji wa mazao ya chakula ulifikia tani 16,891,974 zikiwemo tani 9,537,857 za mazao ya nafaka na tani 7,354,117 za mazao yasiyo nafaka. Kiwango hicho cha uzalishaji kimeiwezesha nchi kujitosheleza kwa mahitaji yake ya chakula ya tani13,569,285 katika mwaka 2018/2019 na hivyo kuwa na ziada ya tani 3,322,689 za chakula kwa kiwango cha utoshelevu cha asilimia 124.Niwahakikishie watanzania kwamba, tunacho chakula cha kutosha nchini. Hata hivyo, tuendelee kuweka akiba katika kaya zetu hadi tutakapovuna tena kwani inaonekana kwamba huenda tusiwe na mavuno mazuri sana msimu huu kutokana na uhaba wa mvua kwenye maeneo ya Kanda ya Ziwa, Kati na Kaskazini mwa nchi yetu.

3.2 Umwagiliaji

Kilimo cha umwagiliaji ni hakikisho la mavuno

11. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 ili kubaini maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kuzingatia Mipango Shirikishi ya Maendeleo ya Rasilimali za Maji (Intergrated Water Resource Development Management Plans- IWRDP). Matokeo ya mapitio hayo yametumika kuandaa Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji (Re-viewed National Irrigation Master Plan 2018) na mkakati wa utekelezaji. Katika mpango huo, hekta 560,880 zimepangwa kuendelezwa kwa lengo la kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 475,052 mwaka 2018/2019 hadi hekta 1,000,000 ifikapo mwaka 2035.

3.3 Maendeleo ya Ushirika

Ushirika ni Mkombozi wa Mkulima

12. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kuimarisha sekta ya ushirika kwa kusimamia na kuhamasisha maendeleo ya sekta. Vyama vya Ushirika vimeongezeka kutoka vyama 10,990 Desemba 2017 hadi vyama 11,331 kufikia Desemba 2018. Aidha, SACCOS 365 zimepangwa kwenye madaraja ya kupewa leseni ambapo SACCOS 32 zimeshapewa leseni na 3,245 zinabaki kwenye daraja la SACCOS zilizosajiliwa. Vilevile, idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika imeongezeka kutoka 2,619,311 mwaka 2017 hadi kufikia 3,998,193 Februari, 2019 sawa na ongezeko la asilimia 53. Kutokana na kuimarika kwa Ushirika, vyama vya ushirika vimetoa ajira 32,688 ambapo ajira 19,980 ni za mikataba na 12,708 zisizo za mikataba.

13. Mheshimiwa Spika, Tume imeendelea kuvijengea na kuimarisha uwezo wa kiuchumi kwa wanachama wa vyama vya ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS). Hadi Desemba 2018, mikopo yenye thamani ya Shilingi trilioni 1.3 imetolewa kwa wanachama ikilinganishwa na Shilingi bilioni 902 zilizotolewa kufikia Desemba 2017. Aidha, Akiba na Amana za wanachama katika SACCOS zimefikia Shilingi bilioni 575 na hisa za wanachama Shilingi bilioni 79 **(Kiambatisho Na. 1).**

14. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha wakulima wa mazao ya chai, kahawa, pamba, tumbaku, michikichi na kakao kukusanya na kuuza mazao yao kupitia vyama vya ushirika chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Matumizi ya mfumo huo yameleta mafanikio kwa wakulima, wafanyabiashara na Serikali kwa kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao, bei yenye tija, mapato ya Serikali na kupatikana kwa takwimu sahihi. Hadi kufikia Desemba 2018, tani 221,619 za pamba zenye thamani ya Shilingi 243,780,900,000 zilikusanywa na kuuzwa kupitia vyama vya ushirika. Aidha, uzalishaji wa zao la chai uliendelea kuimarika ambapo tani 34,010.65 za chai kwa msimu wa 2018/2019 zimekusanywa na kuuzwa kupitia vyama vya ushirika ikilinganishwa na tani 26,975.39 za msimu wa 2017/2018. Kwa upande wa zao la tumbaku, hadi kufikia Desemba 2018 tani 60,552.72 zenye thamani ya Shilingi 222,394,389,507 zime kusanywa na kuuzwa kupitia vyama vya ushirika.

Uzalishaji na ukoboaji wa kahawa unaimarika

15. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Desemba 2018, jumla ya tani 97,151 za kahawa ya maganda zilikuwa zimekusanywa kwenye vyama vya ushirika katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Kagera, Mara, Ruvuma, Mbeya, Songea, Kigoma, Mwanza, Iringa na Njombe. Aidha, tani 55,247.28 za kahawa iliyokobolewa yenye thamani ya Dola za Kimarekani 102,287,051 imeuzwa kupitia vyama vya ushirika katika mnada unaosimamiwa na Bodi ya Kahawa na soko la moja kwa moja. Vilevile, zao la kakao limeendelea kuuzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ambapo kufikia Februari 2019, tani 8,145 zimekusanywa na tani 4,445.57 zimeuzwa kwa bei kati ya Shilingi 3,700 na 5,011 kwa kilo kupitia minada 20 kwa mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na Shilingi 3,200 kwa kilo mwaka 2017/2018.

4.0 UTEKELEZAJI WA MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2018/2019

16. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara inatekeleza maeneo ya kipaumbele ya kuongeza tija kwenye kilimo kwa kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, udhibiti wa visumbufu, matumizi ya zana bora za kilimo na huduma za ugani; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; ujenzi w a miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo na masoko; kufanya utafiti wa kilimo na kuzalisha

teknolojia kwa mazao ya mahindi, muhogo, ngano, michikichi, ufuta, alizeti, pamba na mpunga.

17. Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ya kipaumbele ni kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora za mazao na kusambaza kwa wakulima; kuweka mfumo endelevu wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo nchini; kuboresha maarifa na ujuzi kwa watafiti kupitia mafunzo ili kuwezesha utafiti kufanyika kwa weledi na tija; kuimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa udongo kuendana na mahitaji ya mazao ya kilimo ki-ikolojia; kuimarisha vituo vya tafiti kwa kujenga miundombinu muhimu na kuongeza vitendea kazi vya utafiti; kutoa huduma za ushauri kuhusu utafiti, mafunzo na usambazaji taarifa za kilimo na sayansi shirikishi; kusajili na kuandaa kanzidata ya wakulima na kuimarisha ushirika.

18. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vipaumbele hivyo, jumla ya Shilingi 204,072,066,331.9 ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kati ya fedha hizo, Fungu 43 – Wizara ya Kilimo iliidhinishiwa Shilingi 166,255,956,331.9 zikiwemo Shilingi 68,136,440,331.9 za matumizi ya kawaida na Shilingi 98,119,516,000 za matumizi ya maendeleo; Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - Fungu 05 iliidhinishiwa Shilingi 29,767,866,000 zikiwemo Shilingi 3,947,408,000 za matumizi ya kawaida na Shilingi 25,820,458,000 fedha za maendeleo; na Tume ya Maendeleo ya Ushirika - Fungu 24 iliidhinishiwa Shilingi 8,048,244,000 zikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida.

4.1 Kuongeza Tija katika Kilimo

Upatikanaji wa mbegu bora za mazao

19. Mheshimiwa Spika, tija kwenye kilimo chetu kwa ujumla bado ni ndogo kutokana na matumizi yasiyoridhisha ya pembejeo muhimu na kutozingatia kanuni bora za kilimo. Lengo la Serikali ni kuwezesha pembejeo muhimu zikiwemo mbegu bora, mbolea na viuatilifu kuwafikia wakulima kwa wakati. Katika mwaka 2018/2019, upatikanaji wa mbegu bora zikiwemo za mahindi, ngano, maharage, mpunga, soya, alizeti,

mtama, ufuta, viazi mviringo na mbegu za mazao ya bustani umefikia tani 49,040.66 **(Kiambatisho Na. 2).** Kati ya kiasi hicho, tani 38,507.87 zimezalishwa hapa nchini, tani 8,361.46 zimeagizwa toka nje ya nchi na tani 2,171.33 ni bakaa ya msimu wa 2017/2018. Vilevile, miche 1,507 ya miwa, vipando 121,805 vya muhogo na vikonyo 520,000 vya viazi lishe vimezalishwa. Pamoja na uzalishaji huo, matumizi ya aina mpya 13 za mbegu bora zikiwemo tisa (9) za mahindi, soya tatu (3) na tumbaku moja (1) zitakazoanza kuzalishwa msimu wa 2019/2020 zimeidhinishwa **(Kiambatisho Na. 3).**

20. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwezesha upatikanaji na matumizi ya mbegu bora, suala la udhibiti wa ubora wa mbegu limeendelea kusimamiwa kupitia Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI). Hadi Machi 2019, hekta 42,999.6 za mashamba ya mbegu, maduka 713 na maghala 43 ya mbegu yamekaguliwa katika mikoa ya Mbeya, Arusha, Morogoro, Rukwa na Mwanza. Ukaguzi ulibaini tani 1,686 za mbegu zilikuwa na kiwango kidogo cha uotaji na ziliondolewa sokoni. Vilevile, kutokana na kuimarishwa kwa TOSCI kupitia ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya maabara na rasilimaliwatu, Wizara imepata ithibati ya Shirika la Kimataifa la Uthibiti wa Ubora wa Mbegu (International Seeds Testing Association – ISTA) kwa maabara ya TOSCI ambayo itaiwezesha nchi kufanya biashara ya mbegu kimataifa.

Maabara ya kisasa ya TOSCI

Upatikanaji na udhibiti wa ubora wa Mbolea

21. Mheshimiwa Spika, upatikanaji na usambazaji wa mbolea katika mikoa 26 ya Tanza- nia Bara hadi Machi 2019, ulikuwa tani 492,394 ikilinganishwa na mahitaji ya tani 514,138 katika msimu wa 2018/2019 (Kiambatisho Na. 4). Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imetoa mafunzo ya ukaguzi wa mbolea kwa maafisa kilimo 50 kutoka mikoa ya Arusha, Rukwa, Mbeya, Songwe, Njombe, Manyara, Kilimanjaro, Kagera, Iringa, Shinyanga, Ruvuma, Mara, Lindi, Morogoro, Tabora, Tanga, Geita na Katavi. Vilevile, mafunzo kwa wafanyabiashara 405 wa mbolea kuhusu uhifadhi bora wa mbolea yamefanyika katika mikoa ya Kagera (112), Mara na Simiyu (57), Tabora na Shinyanga (83), Lindi (65), Mtwara (42) na Mwanza (46).

22. Mheshimiwa Spika, TFRA imefanya ukaguzi kwa wauzaji wa mbolea 1,350 katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Vilevile, wafanyabiashara wapya wa mbolea 496 wamesajiliwa na kufikia idadi ya wafanyabiashara wa mbolea 2,784 nchi ni wanaonunua na kusambaza mbolea kwa wakulima.

Matumizi ya uhakika ya mbolea yanaongeza tija na uzalishaji

Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu

23. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara imenunua lita 296,000 na kilo 3,000 za viuatilifu vyenye thamani ya Shilingi bilioni tisa (9) kwa ajili ya kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mazao vikiwemo Viwavijeshi vamizi, Kweleakwelea, Panya, Nzige wekundu, na nzi wa matunda.

Hadi kufikia mwezi Machi 2019, ndege waharibifu wa nafaka (kweleakwelea) walidhibitiwa katika skimu za umwagiliji za Kahe (Kilimanjaro), Le kita tu (Arusha) na Mise nyi (K age r a) kwa kutumia lita 400 za sumu aina ya Fenthion kwa mazao ya mpunga na mtama. Aidha, panya waharibifu wa mazao shambani na kwe nye maghala walidhibitiwa katika Wilaya za Igunga, Nzega, Kahama, Msalala, Shinyanga, Kishapu, Nyang'wale, Chalinze, Kilwa Masoko, Iramba, Mkalama, Singida, Hanang, Misungwi,Kwimba na Maswa ambapo kilo 673 za sumu zilitumika.

Serikali imejizatiti kudhibiti visumbufu vya mimea

24. Mheshimiwa Spika, Wizara imesambaza lita 119,000 kwa ajili ya kudhibiti Viwavijeshi Vamizi katika Kanda ya Ziwa, Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Mashariki na kutoa mafunzo kwa maafisa ugani na wakulima 350 katika kanda hizo. Aidha, kwa kushirikiana na Kituo cha ICIPE Kenya, mafunzo ya udhibiti wa nzi wa matunda yametolewa kwa wakulima 100 wa mboga na maafisa ugani 25 wa Wilaya za Kibaha, Bagamoyo na Mkuranga. Wakulima waliopata mafunzo wamepewa mitego 1,000 ya kunasa nzi, chambo chenye sumu vipande 2,000 pamoja na vipeperushi 500. Pamoja na usambazaji huo, elimu kuhusu matumizi ya teknolojia ya Push – Pull ya kudhibiti funza wa mabua na gugu

aina ya kiduha pia imetolewa katika Wilaya za Morogoro, Muheza na Tari m e. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira ime baini uwepo wa wadudu rafiki (Trichogramma spp) na Te le nom us s pp w a kudhibiti Kiwavijeshi Vamizi (Fall Army Worm). Wadudu hao rafiki ambao watasaidia kudhibiti kiwavijeshi vamizi wamegunduliwa katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Kagera, Dodoma, Morogoro na Mara.

25. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Taasisi ya Kitropiki ya Utafiti wa Viuatilifu (TPRI) imekarabati maabara na kununua ma shin e mbili (2) za kucham bua viuatilifu kwa usahihi zaidi ili maabara hizo ziwezekupata ithibati za kimataifa. TPRI pia ilifanya kipimo cha kutathmini kiwango cha sumu mwilini (Ache Test) kwa watumiaji 84 wa viuatilifu ambapo asilimia 19 kati yao walibainika kuwa na kiwango kikubwa cha sumu mwilini. Elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu na vifaa kinga kwa waathirika hao imetolewa.

26. Mheshimiwa Spika, TPRI pia, imesajili viuatilifu 362 ambapo 92 vimesajiliwa kwa mara ya kwanza kwa ajili ya matumizi hapa nchini. Vilevile, maduka 245 katika Kanda za Nyanda za juu Kusini, Kati, Kaskazini, Mashariki, Magharibi na Kanda ya Ziwa yamekaguliwa. Ukaguzi ulibaini maduka 20 hayakuwa na vibali vya biashara, saba (7) yalikuwa yanauza viuatilifu vilivyokwisha muda wake na vingine vikiwa havina usajili wa kutumika hapa nchini na maduka hayo yalifungwa. Aidha, TPRI imetoa mafunzo ya udhibiti husishi (Inte- grated Pest Management) wa kisumbufu aina ya Kantangaze kwa wakulima 415 wa nyanya kutoka Singida (28), Shinyanga (15), Simiyu (22), Tabora (35), Morogoro (165) na Dar es Salaam (150). Vilevile, TPRI imetoa mafunzo kwa wadau 683 w a k i w e m o w a k u l i m a , m a a f i s a u g a n i n a wafanyabiashara kuhusu matumizi sahihi na salama ya viuatilifu.

Zana za Kilimo

27. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kwamba matumizi ya zana bora za kilimo yanaongezeka miongoni

mwa wakulima wetu. Tathmini iliyofanyika imeonesha kuwa kwa mwaka 2018, wastani wa kitaifa wa matumizi ya zana bora za kilimo umeongezeka hadi kufikia asilimia 20 kwa matrekta na asilimia 27 kwa wanyama kazi ikilinganishwa na asilimia 14 ya matrekta na asilimia 24 ya wanyama kazi mwaka 2013. Kutokana na ongezeko hilo, matumizi ya jembe la mkono yamepungua na kufikia asilimia 53 kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 62 kwa mwaka 2013.

Matumizi ya zana bora za kilimo yameongezeka nchini

28. Mheshimiwa Spika, ili matumizi ya zana bora za kilimo yaongezeke kwa kasi zaidi, Wizara inahamasisha Sekta Binafsi kuingiza matrekta na zana zake nchini. Kati ya mwaka 2016/ 2017 na 2017/2018, jumla ya matrekta makubwa 2,476 na matrekta madogo 586 yaliingizwa nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), TIB Corporate Bank na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imetoa mafunzo kwa waendesha mitambo 76 kuhusu uendeshaji na matengenezo ya matrekta aina ya URSUS. Vilevile, viongozi 108 wa Vyama vya Msingi na 53 wa Vyama vya Mazao (AMCOS) wamepatiwa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa matrekta. Kati ya AMCOS hizo, 50 ni za Mkoa wa Mwanza na 3 za Wilaya ya Bunda Mkoa wa Mara.

29. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana Shirika la Maendeleo la Japan imetoa mafunzo ya uendeshaji wa mitambo ya kuvunia na mashine za kukoboa mpunga kwa maopareta 28 na mafunzo ya usimamizi na uendeshaji mradi wa zana kwa wakulima viongozi katika skimu 14 za umwagiliaji. Skimu hizo ni Mbuyuni, Uturo, na Ipatagwa (Mbarali), Nakahuga (Songea), Magozi (Iringa), Mkindo (Mvomero), Kilangali (Kilosa), Bagamoyo BIDP (Bagamoyo), Mombo (Korogwe), Kivulini (Mwanga), Musa Mwinjanga (Hai), Lekitatu (Arumeru), na Muungano (Babati).

30. Mheshimiwa Spika, kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) Wizara inaendelea kutoa mikopo ya pembejeo na zana za kilimo. Tangu kuanzishwa kwa Mfuko mwaka 1994, jumla y a mikopo yenye thamani y a Shilingi 82,103,746,770 imetolewa na katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, mikopo 33 yenye thamani ya Shilingi 1,495,362,060 ikiwemo 22 ya mitambo ya mashambani, sita (6) ya pembejeo za kilimo na mitano (5) ya umwagiliaji imetolewa (Kiambatisho Na. 5). Vilevile, ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo ya nyuma umeendelea kufanyika ambapo katika mwaka 2018/2019, Shilingi 1,842,698,117.73 zimerejeshwa.

4.2 Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji

31. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/20219, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kutekeleza kazi za upembuzi yakinifu ambazo zilianza katika mwaka wa fedha 2017/2018. Hadi kufikia Februari 2019, kazi hizo zilikuwa zimekamilika kwa asilimia 50 katika mradi wa Luiche uliopo katika Halmashauri za Wilaya Kigoma/Ujiji we nye he kta 3,000 na Ibanda (Sengerema/Geita) wenye hekta 1,500. Aidha, Tume imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo (SSIDP) unaofadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia JICA. Mradi umekarabati skimu za umwagiliaji 129 katika Halmashauri 68 nchini pamoja na ununuzi wa mitambo ya ujenzi. Hadi Februari 2019, utekelezaji wa miradi hiyo umefikia wastani asilimia wa 37 kwa kazi zote zilizopangwa. Vilevile,Tum e kup

itia Program ya Feed the Future imeendelea kuboresha miundombinu mbalimbali katika skimu ya umwagiliaji ya Dakawa (Mvomero) yenye hekta 2,000.

4.3 Utafiti wa Kilimo na Uhaulishaji wa Teknolojia

32. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia TARI imegundua mbegu bora mpya aina nne (4) za mahindi ambazo ni WE5135, WE5141, WE7118 na WE7133. Mbegu hizo zina uwezo wa kutoa mavuno kwa wastani wa tani 5.8 kwa hekta kwenye mashamba ya wakulima katika ukanda wa chini na kati, zinahimili ukame na zina ukinzani wa magonjwa ya majani ya mahindi (maize leaf necrosis) na michirizi na ukungu. Mbegu hizo zitatumika kuzalisha mbegu za msingi (basic seeds) na zilizothibitishwa (certified seeds) kuanzia msimu wa 2019/2020. Vilevile, TARI inatekeleza mradi wa kuzalisha taarifa za udongo nchi nzima kwa ajili ya matumizi ya wadau wa kilimo ili kuwezesha kufanya uamuzi sahihi wa matumizi bora ya ardhi. Hadi Januari 2019, sampuli za udongo 4,604 katika mikoa ya Mara, Simiyu na Shinyanga zimekusanywa kwa ajili ya uchunguzi.

33. Mheshimiwa Spika, ili kupeleka taarifa sahihi kwa wakulima, TARI imeandaa nyenzo tatu za kumsaidia mkulima kufanya uamuzi wa kuboresha uzalishaji wa zao la muhogo kwa kutumia simu janja za mkononi. Nyenzo hizo zitamsaidia mkulima kujua aina, viwango na muda sahihi wa kutumia mbolea, idadi sahihi ya mimea ya kuchanganya katika shamba na kung'amua muda wa kupanda, kujua gharama za uzalishaji na faida. Nyenzo hizo zimeanza kutumika katika wilaya za Biharamulo, Sengerema, Buchosa, Bunda, Serengeti, Butiama, Kisarawe, Mkuranga, Rufiji, Mtwara vijijini, Newala, Nachingwea, Masasi na Lindi Vijijini. TARI pia imechapisha vipeperushi 72,000 vya matumizi ya teknolojia zilizovumbuliwa na watafiti; makala za watafiti zimechapishwa kwenye majarida 22 maarufu ya utafiti duniani na kutoa nakala 10,000 za vitabu vinavyofafanua kwa kina matumizi ya teknolojia na ubunifu unaofanywa na watafiti wa kilimo nchini.

4.4 Maendeleo ya Mazao

34. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao kwa kuimarisha huduma za utafiti, upatikanaji na utumiaji wa pembejeo na zana za kilimo, udhibiti wa visumbufu vya mazao, huduma za ugani, uongezaji wa thamani na upatikanaji wa masoko.

Zao la Mahindi

35. Mheshimiwa Spika, Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la mahindi kufikia tani 8,000,000 mwaka 2019/2020 ikilinganishwa na tani 6,300,000 zinazozalishwa sasa. Ili kufikia lengo hilo, katika msimu wa 2018/2019, elimu kuhusu udhibiti wa viwavijeshi vamizi imetolewa kwa wakulima 2,080 wa mahindi kutoka mikoa ya Singida (385), Shinyanga (425), Simiyu (495), Tabora (530) na Morogoro (245).

36. Aidha, Wizara imesimamia upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima, ambapo jumla ya tani 17,525.65 za mbegu bora za mahindi zimepatikana kwa ajili ya msimu wa 2018/2019.

Zao la Mpunga

37. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa zao la mpunga kwa lengo la kufikia tani 5,000,000 ifikapo 2021/2022 ikilinganishwa

na tani 3,400,000 zinazozalishwa sasa. Ili kufikia lengo hilo, Wizara imesimamia uendeshaji wa mashamba darasa 1,331 ya mpunga pamoja na kuanzisha mashamba ya mfano 1,120 ya kilimo shadidi katika skimu 40 za umwagiliaji katika Halmashauri za Ulanga, Mvomero, Kilombero, Morogoro Vijijini, Kilosa na Malinyi.

38. Mafunzo hayo yamechangia kuongezeka kwa tija kutoka tani 2.5 hadi kufikia tani 6 kwa hekta katika skimu za umwagiliaji. Ili kuongeza matumizi ya mbegu bora, Wizara imetambulisha kwa wakulima aina 11 za Mbegu bora za mpunga kupitia mashamba ya mfano ambapo wakulima walichagua aina 2 za TXD 306 (SARO 5) na NERICA 7.

Kilimo bora cha mpunga kuimarisha usalama wa chakula

39. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mradi wa ERPP imetoa mafunzo kwa wakulima 5,647, Maafisa Ugani na Mafundi Sanifu wa Umwagiliaji 109 kutoka skimu 40 za umwagiliaji kuhusu kilimo bora cha mpunga ikiwemo kilimo shadidi. Vilevile, mafunzo yametolewa kwa wakulima viongozi 40 wa skimu nne (4) za Mkindo, Kigugu, Dihombo na Mb ogok omtonga kuhusu te knolojia bora za uvunaji, hifadhi na usindikaji wa mpunga. Vilevile, kupitia mradi wa ERPP, Wizara imetoa mafunzo kuhusu umuhimu wa ushirika, uongozi wa ushirika, utunzaji wa mpunga baada ya kuvuna, usi ndi ka ji, kupa nga m a da r aja i li kuong e z a thamani, ujuzi wa masoko na ujasiriamali kwa wakulima viongozi 250 katika skimu 40 za umwagiliaji.

Zao la Muhogo

40. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara ilipanga kuzalisha pingili milioni 25 za muhogo kupitia vituo vya utafiti kwa kushirikiana na Sekta binafsi. Hadi Machi 2019, jumla ya pingili milioni 13 zimezalishwa katika mikoa 14 ya Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Mara, Kigoma, Morogoro, Mwanza, Kagera, Geita, Simiyu, Dodoma na Dar es Salaam. Aidha, tija ya zao la muhogo mbichi imeongezeka kutoka tani 3.35 kwa hekta mwaka 2016/2017 hadi tani 8.4 kwa hekta msimu wa 2017/2018. Hadi kufikia Desemba 2018, TOSCI imesajili mashamba ya mbegu hekta 349.05 yenye uwezo wa kuzalisha pingili 34,906,500.

Zao la Migomba

41. Mheshimiwa Spika, Zao la migomba huzalishwa kwa wingi katika mikoa ya Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Arusha, Songwe, Mara, Kigoma, Tanga, Morogoro na Pwani ambapo inakadiriwa kuwa zaidi ya kaya 900,000 za wakulima wadogo hujihusisha na uzalishaji wa ndizi kwa ajili ya chakula na biashara. Eneo linalolimwa migomba ni takribani hekta 700,000 na wastani wa tani millioni 3.7 kwa mwaka huzalishwa. Asilimia 80 ya ndizi zinazozalishwa hutumika kama chakula, ambapo 5% ni kwa ajili ya kuchoma/ kukaanga, 10% huliwa kama ndizi mbivu na 5% hutumika kwa ajili ya kutengeneza juisi na mvinyo.

42. Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa zao la migomba, tija kwa zao hilo ni wastani wa tani 10 kwa hekta ambayo ni ndogo ikilinganishwa na fursa ya kuzalisha tani 40 kwa hekta. Hii huchangiwa na matumizi ya mbegu zisizo bora, magojwa na kutofuata kanuni bora za kilimo cha migomba. Aidha, TARI kwa kwa kushirikiana na wadau wengine ilingiza na kusambaza mbegu bora za migomba aina ya FHIA 17, FHIA 23 na Yangambi (Km 5) zenye uzalishaji mkubwa, kustahimili magonjwa na wadudu.

43. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, TARI kwa kushirikiana na kampuni binafsi imeendelea kutafiti na kuzalisha miche ya mbegu bora za migomba. Kupitia ushirikiano huo, zaidi ya miche milioni 6 za mbegu bora

ilizalishwa katika vituo vya TARI (Maruku), TARI (Uyole), TARI (Tengeru), kampuni binafsi ya Crop Bioscience (Arusha) na Kilimorgano (Dar es Salaam) na kusambazwa kwa wakulima.

Mazao ya jamii ya Mikunde

44. Mheshimiwa Spika, mazao jamii ya mikunde hujumuisha maharagwe, mbaazi, kunde, choroko, njugu mawe, ngwara (Fiwi), soya, njegere na dengu na huzalishwa katika mikoa yote hapa nchini na takribani hekta 2,067,230 hutumika. Kiasi cha tani milioni 2 huzalishwa kwa mwaka, ambapo tija ni wastani wa tani moja kwa hekta ikilinganishwa na fursa ya tani 2.5 hadi 3.5 kwa hekta. Kiwango kidogo cha matumizi ya mbegu bora huchangia kushusha tija miongoni mwa wakulima.

45. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TARI na kwa kushirikia na wadau wengine imeendelea kuimarisha utafiti wa mazao hayo ambapo jumla ya aina 62 za mbegu bora zimegunduliwa zikiwemo soya (5), Mbaazi (7), Kunde (8), Choroko (2), Dengu (4), Njugumawe (6) na maharagwe (29). Aidha,TARI imezalisha mbegu za jamii ya mikunde tani 87.5 za daraja la awali, tani 756.4 za daraja la msingi, tani 1,877.5 za daraja la kuthibitishwa na tani 299.2 za kuazimiwa ubora. Takribani wakulima 10,160,577 wakiwemo wanawake 4,062,861 na wanaume 6,097,716 wamenufaika. Vilevile, TARI imetoa mafunzo ya kilimo bora cha maharage kwa wakulima 1,908, kati ya hao, wanawake ni 827 na wanaume 1,081.

Zao la Alizeti

Uendelezaji wa zao la alizeti utasaidia kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula nchini

46. Mheshimiwa Spika, Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la alizeti ili kujitosheleza kwa mafuta ya kula nchini na kukuza ajira na kipato. Lengo hili litafikiwa kwa kuongeza upatikanaji na matumizi ya mbegu bora, kutoa mafunzo ya kilimo bora na kuimarisha utafiti wa zao hilo. Katika mwaka 2018/2019, TARI imesafisha (purify) mbegu ya alizeti aina ya Record ili kurejesha uwezo wake wa kuongeza mavuno. Hadi Februari 2019, eneo la ekari 90 zimeandaliwa kwa matarajio ya kuzalisha tani 60 za mbegu ya alizeti zitakazosambazwa kwa wakulima.

Aidha, ekari 20 zimeandaliwa kwa ajili ya kuzalisha tani 7.5 za mbegu za alizeti za awali (pre basic) zitakazosambazwa kwa kampuni za mbe gu. Vilevile, Wizara kupitia TARI imeagiza germplasm 20 kutoka Romania zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na viwango vikubwa vya mafuta kwa ajili ya utafiti na ugunduzi wa mbegu mpya za alizeti. ASA pia, imeongeza eneo la uzalishaji wa mbegu bora za alizeti kutoka hekta 110 mwaka 2017/2018 hadi kufikia hekta 835 mwaka 2018/2019.

Zao la Mchikichi

47.Mheshimiwa Spika, Wizara imepanga kuendeleza zao la mchikichi ambalo ni miongoni mwa mazao sita yak imkakati yaliyopewa kipaumbele Kitaifa. Katika kutekeleza azma hiyo, mkoa wa Kigoma ni kitovu cha kuendeleza zao hilo na tayari kimeanzishwa kituo cha utafiti cha TARI Kihinga. Wizara imeandaa mkakati wa kuendeleza zao la michikichi unaolenga kutosheleza mahitaji ya mafuta ya kula nchini kwa kuzalisha mbegu bora za michikichi kwa kipindi cha miaka minne (2018/2019 hadi 2021/2022). Mkakati huo unalenga kuzalisha miche ya michikichi milioni tano (5) kila mwaka kwa ajili ya kusambaza kwa wakulima kwa kushirikiana na wadau wakiwemo Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Jeshi la Kujenga Taifa, Magereza, Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na Sekta binafsi.

Uendelezaji wa zao la mchikichi utasaidia kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula nchini

48.Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mbegu bora za zao la mchikichi katika Kituo cha TARI Kihinga ulianza Agosti 2018 ambapo hadi mwezi Machi, 2019 kituo kimezalisha mbegu 4,747 ambazo zimefanyiwa uoteshwaji wa awali (pre-germination). Wizara pia imeingia makubaliano na kampuni za FELISA Co. Ltd na Yangu Macho Group kuzalisha jumla ya mbegu milioni tatu ifikapo Juni 2020. Aidha, kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Kigoma uhamasishaji wakulima kujiunga na vyama vya ushirika umeanza. Hadi mwezi Machi 2019, wakulima 2,752 wamehamasishwa na vyama vya ushirika vya msingi vipatavyo 12 vimesajiliwa.

Mazao Makuu ya Asili ya Biashara

49. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya kimkakati umeongezeka kutoka tani 901,641 msimu 2016/2017 hadi tani 967,184 msimu wa 2017/2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.2. Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya Pamba, Chai, Pareto, Korosho, Kahawa na Mkonge kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya pembejeo na maeneo ya uzalishaji hususan katika zao la Chai na Pamba. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa zao la tumbaku ulishuka kutokana na kupungua kwa mahitaji ya tumbaku katika soko la dunia uliosababisha kampuni za

ununuzi wa tumbaku nchini kupunguza kiasi cha uzalishaji wa tumbaku kwa wakulima kupitia mikataba iliyopo kati ya wakulima na wanunuzi.

50. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2018/2019, Wizara ililenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara hadi kufikia tani 1,356,368 ambapo hadi kufikia Machi 2019, takribani tani 667,631.77 ikiwa ni sawa na asilimia 49.2 ya lengo zimezalishwa na uzalishaji unaendelea. Uzalishaji huo umechangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa sukari na kahawa kwa asilimia 36.9 na 7.9 mtawalia na msimu unaendelea. Takwimu za uzalishaji wa mazao ya biashara umeoneshwa katika (Kiambatisho Na. 6). Aidha, mikakati ya kuendeleza mazao ya asili ya biashara imeelezwa kwa zao mojamoja kama ifuatavyo:

Zao la Korosho

51. Mheshimiwa Spika , Wizara katika kuendeleza zao la korosho imesambaza miche bora 12,252,197 katika mikoa 17 inayolima zao hilo kati ya miche 13,661,433 iliyozalishwa kupitia mikataba iliyoingiwa msimu wa 2017/2018 kati ya Bodi ya Korosho na wazalishaji 678. Vilevile, katika mwaka 2018/ 2019, mbegu za korosho kilo 47,484 (Kiambatisho Na. 7) ambazo zitazalisha miche 6,647,760 ya kutoshele za ekari 391,045.19 zimezalishwa na Kituo cha Utafiti cha Naliendele. Mbegu hizo zimesambazwa katika mikoa 20 na uzalishaji wa miche unaendelea. Hadi Machi 2019, miche bora ya korosho 52,839 imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima **(Kiambatisho Na. 8).**

Kituo cha Utafiti Naliendele kinaendelea kuzalisha miche bora ya korosho

52. Mheshimiwa Spika, mwaka 2018/2019, Wizara imesimamia ununuzi wa pembejeo za zao la korosho kwa utaratibu wa pamoja kupitia zabuni na Vyama vya Ushirika ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu. Kupitia utaratibu huo, jumla ya tani 31,500 na lita 520,000 za salfa zimenunuliwa ambapo wakulima wamenunua jumla ya tani 1,994.175 na lita 14,283. Bakaa ya viuatilifu vilivyonunuliwa kwa njia ya za buni ni tani 29,505.825 na lita 505,717 za salfa ambavyo vinaendelea kuuzwa kwa wakulima kwa ajili ya msimu wa 2019/2020.

53. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi ya Korosho inaendelea na usajili wa wakulima wakorosho ambapo hadi kufika Machi 2019, wakulima 200,000 wamesajiliwa. Aidha, Bodi imeandaa mfumo endelevu ambao utawawezesha maafisa katika kila Halmashauri kukusanya na kuhuisha taarifa kwa kutumia simu za mkononi. Vilevile, mafunzo kuhusu udhibiti wa ubora wa korosho ghafi yametolewa kwa wataalam 63 katika Halmashauri za Mkuranga, Kibiti, Masasi, Ruangwa, Nachingwea na Tunduru. Mafunzo hayo yalijumuisha wataalamu kutoka Bodi ya Usimamizi ya Stakabadhi za Ghala, waendesha ghala na wanunuzi.

Usindikaji wa korosho kwa ajili ya kuongeza kipato

54. Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu litakumbuka kwamba, Serikali ilifanya uamuzi wa kununua korosho zote zilizozalishwa katika msimu wa 2018/2019 kutokana na

wanunuzi na wakulima kutokuafikiana bei elekezi na kusababisha wakulima kukataa kuuza korosho zao. Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imeratibu zoezi la ununuzi na malipo kwa wakulima. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2019, tani 222,825 zimekusanywa kutoka kwa wakulima. Kati ya hizo, tani 211,184 zimehakikiwa ambapo tani 177,357 zenye thamani ya Shilingi 578,487,470,664 zimelipwa kwa wakulima 379,283. Korosho hizo zimeuzwa kwa bei ya Shilingi 3,300 kwa kilo ya korosho ghafi daraja la kwanza na Shilingi 2,640 kwa kilo ya korosho ghafi daraja la pili bila makato

Zao la Pareto

55. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi ya Pareto imeendelea kuhamasisha kilimo cha pareto katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Songwe, Iringa, Arusha, Manyara na Kilimanjaro. Hadi Machi 2019, uzalishaji wa pareto kwa msimu wa 2018/2019, umefikia tani 1,800 sawa na asilimia 69.23 ya lengo la kuzalisha tani 2,600 na uzalishaji unaendelea. Aidha, Kituo cha Utafiti wa Kilimo TARI Uyole kimezalisha miche bora ya pareto 6,037 na kusambaza kwa wakulima 735 katika Halmashuri za Mbeya, Ileje, Mufindi, Makete, Babati, Mbulu, Njombe, Ludewa na Siha.

56. Mheshimiwa Spika, katika msimu 2018/2019, bei ya kuuza maua ya pareto imefikia wastani wa Shilingi 3,700 kwa kilo ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 2,800 kwa kilo msimu wa 2017/2018 kutokana na ubora wa maua. Kutokana na kupanda kwa bei ya maua ya pareto, wakulima wamehamasika kuongeza uzalishaji na kupanua maeneo ya kilimo hicho katika Wilaya za Arusha, Meru, Siha, Babati, Mbulu, Hanang, Iringa, Mufindi, Kilolo na Hai. Aidha, Bodi ya Pareto inaendelea kusajili wakulima wa pareto ambapo hadi mwezi Machi 2019, wakulima 4,500 kutoka mikoa ya Mbeya, Iringa, Manyara na Njombe wamesajiliwa.

Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari

57. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi ya Sukari inaendelea kusimamia kilimo cha miwa kwe nye mashamba ya wakulima wadogo na mashamba

makubwa yanayomilikiwa na wenye viwanda vya sukari ili kuongeza uzalishaji wa sukari nchini. Katika msimu wa 2018/2019, Wizara ilipanga kuzalisha sukari tani 353,900 ikilinganishwa na mahitaji ya tani 515,000 za sukari kwa ajili ya matumizi ya kawaida nchini. Hadi kufikia Machi 2019, tani 345,879.25 zimezalishwa, sawa na asilimia 98 ya lengo.

58. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na usajili wa wakulima wa miwa kupitia mfumo wa usajili wa kielektroniki ambapo hadi kufikia Machi, 2019 wakulima 6,125 wamesajili wa katika mashamba ya Kilombero (5,899) na Mtibwa (226). Usajili unaendelea katika mashamba ya TPC, Kagera, Manyara, Mkulazi I na Mkulazi II. Katika kuimarisha upatikanaji wa huduma ya pamoja mashambani na mitaji ya kuboresha kilimo cha miwa, Wizara imehamasisha uanzishwaji na uimarishaji wa Vyama vya Ushirika vya wakulima. Hadi kufikia mwezi Machi 2019, vyama vya ushirika 19 vimeanzishwa katika kiwanda cha Kilombero; chama cha ushirika na umoja wa wakulima katika kiwanda cha Mtibwa; na umoja wa wakulima katika kiwanda cha sukari cha Kagera.

59. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Bodi ya Sukari Tanzania imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Kuongeza Tija kwa Wakulima Wadogo wa Miwa Awamu ya Tatu unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya. Kupitia mradi huo, Kilometa 33.5 za barabara za mashamba ya wakulima wa miwa katika wilaya za Kilombero na Misenyi zimekarabatiwa; miundombinu ya umwagiliaji katika kijiji cha Msolwa Ujamaa kwa ajili ya wakulima wadogo 146 wanaomiliki ekari 250 imejengwa; na ujenzi wa tuta la kukinga maji lenye urefu wa kilometa 10.6 katika bonde la Ruembe (Kilosa) umekamilika. Vilevile, ekari 750 za mashamba ya bega kwa bega ya wakulima wadogo katika Wilaya ya Misenyi na ekari 200 za mashamba ya pamoja ya wakulima wadogo katika vijiji vya Nyameza, Nyamamba na Nyarubungo katika Wilaya ya Kilombero yameanzishwa. Aidha, wakulima wa miwa 316 kutoka katika mashamba ya Kilombero, Mtibwa na Kagera wamepatiwa mafunzo ya mbinu bora za biashara, uongozi, ushawishi na utetezi.

Zao la Kahawa

60. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi ya Kahawa inaendelea kutekeleza mkakati wa uendelezaji wa zao la kahawa unaolenga kuzalisha tani 100,000 za kahawa safi ifikapo mwaka 2021/2022. Mkakati unatekelezwa kwa kuhamasisha upandaji wa miche bora ya kahawa, kukarabati miti iliyopo, kuhamasisha matumizi ya mbolea na viuatilifu bora, kuongeza matumizi ya mashine na mitambo ya kuongeza thamani na kuboresha masoko. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Bodi ya Kahawa imepanga kuzalisha miche bora ya kahawa 12,000,000. Hadi kufikia mwezi Machi 2019, miche 6,494,930 imezalishwa ambapo miche 1,780,430 imezalishwa na Bodi ya Kahawa na miche 4,714,500 imezalishwa na TaCRI.

61. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi, 2019 tani 61,925 za kahawa safi zimezalishwa sawa na asilimia 95.27 ya lengo la kuzalisha tani 65,000. Uzalishaji kwa msimu huu umeongezeka kutokana na Wizara kuimarisha usimamizi wa zao la kahawa kuanzia ngazi ya uzalishaji hadi masoko, kuimarisha vyama vya ushirika vya msingi ambapo vyama vya msingi 288 na vyama vikuu vya ushirika 10 vimeshiriki katika ununuzi wa kahawa. Usimamizi huu umeongeza ubora wa kahawa, udhibiti wa utoroshaji wa kahawa na upatikanaji wa takwimu za mauzo ya kahawa kupitia masoko ya ndani na nje ya nchi.

62. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Kahawa imekagua ubora wa viwanda 23 na maghala 23 na kutoa leseni za kuendesha biashara ya kahawa. Pia, wataalam 89 wa viwanda vya kuchakata kahawa kutoka Wilaya ya Mbinga wamepewa mafunzo ya kanuni bora za uchakataji kahawa. Aidha, mafunzo kuhusu kilimo bora cha kahawa yametolewa kwa maafisa ugani 92, wakulima viongozi 18 na wakulima 408 na usajili wa wakulima wa kahawa kote nchini unaendelea ambapo hadi mwezi Februari 2019, jumla ya wakulima 254,202 wamesajiliwa.

Zao la Mkonge

63. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi ya Mkonge imeendelea kuhamasisha kilimo cha zao la Mkonge kwa

kutoa elimu ya kilimo bora, kuimarisha mfumo wa masoko na ushirika kwa kute ke le za mkakati wa kue ndele za zao hilo unaolenga kuongeza uzalishaji kutoka tani 34,589 hadi tani 100,000 ifikapo 2020/2021. Mavuno ya mkonge yameongezeka kutoka tani 36,533 msimu wa 2016/2017 hadi tani 43,533.25 msimu wa 2017/2018 na uzalishaji wa bidhaa za mkonge kwa maana ya kamba, mazulia na magunia) ulifikia tani 7,825.64 kwa mwaka 2017/2018. Katika msimu wa 2018/ 2019, tani 15,480.54 zimezalishwa sawa na asilimia 34.4 ya lengo la kuzalisha tani 45,000 na m simu unaendelea. Katika kuimarisha uzalishaji na masoko ya zao la mkonge, Bodi imepitia upya mikataba ya wakulima wadogo wa mkonge na kampuni ya Katani Limited ili kuondoa migogoro ya malipo kwa wakulima ambapo kuanzia Januari 2019, mkonge wa wakulima unauzwa chini ya usimamizi wa vyama vya ushirika kwa njia ya ushindani kupitia minada.

Zao la Pamba

Pamba kwa ajili ya viwanda vya nguo

64.Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi ya Pamba inatekeleza mkakati wa kuendeleza zao la pamba ili kuongeza uzalishaji kutoka tani 133,000 hadi tani 700,000 ifikapo mwaka 2020/2021. Katika msimu wa kilimo wa 2018/ 2019, makadirio ya mahitaji ya mbegu bora za pamba yalikuwa tani 20,083.94. Hata hivyo, kutokana na uhamasishaji wa

matumizi ya mbegu bora uliofanyika, mahitaji yaliongezeka. Hadi Januari 2019, tani 21,535.62 za zilikuwa UKM08 zimesambazwa kwa wakulima (Kiambatisho Na. 9). Vilevile, ekapaki 7,000,000 za viuatilifu vya zao la pamba zilipangwa kusambazwa kwa wakulima. Kutokana na uhamasisha ji uliofanyika wa kuongeza uzalishaji kwenye zao la pamba, mahitaji ya viuatilifu yanakadiriwa kufikia ekapaki 10,000,000. Hadi kufikia Machi 2019, ekapaki 3,326,990 za viuatilifu zimesambazwa katika Halmashauri 41 za mikoa ya Kigoma, Katavi, Singida, Dodoma, Kagera, Mara, Tabora, Geita, Mwanza, Shinyanga na Simiyu.

65. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, mafunzo ya kanuni za kilimo bora cha pamba, ikiwemo utambuzi wa visumbufu, viuatilifu na matumizi sahihi ya viuatilifu yametolewa kwa washiriki 2,036 wakiwemo maafisa ugani kutoka ngazi ya Wilaya, Kata na vijiji; wakulima viongozi na maafisa ushirika. Washiriki hao walitoka katika mikoa ya Tabora, Mwanza, Mara, Shinyanga, Katavi, Kigoma, Singida, Kagera, Geita, Simiyu, Iringa, Dodoma, Manyara, Kilimanjaro, Morogoro, Pwani na Tanga.

66. Mheshimiwa Spika, Mavuno ya Pamba kwa msimu wa 2017/2018, yalifikia tani 222,039 na msimu wa ununuzi ulianza Mei 2018. Kampuni 32 zilipatiwa leseni za ununuzi wa Pamba ambapo tani zote 222,039 sawa na marobota 380,000 yenye wastani wa kilo 181 kilamoja zilinunuliwa kupitia AMCOS.

Zao la Tumbaku

67. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku ilipanga kusambaza kilo 594 za mbegu za tumbaku kwa wakulima. Hadi kufikia mwezi Machi 2019, kilo 588 za mbegu zinazotosheleza hekta 39,191 zimesambazwa kwa wakulima 53,903 kwenye vyama vya ushirika 258 katika mikoa ya Kigoma, Katavi, Ruvuma, Mbeya, Tabora, Shinyanga, Geita na Iringa. Mbegu hizo zinatarajiwa kuzalisha tani 54,868 za tumbaku.

68. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2017/2018, uzalishaji wa tumbaku ulifikia tani 50,522 zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.83. Uzalishaji kwa mwaka 2017/2018 ulishuka ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 58,639 kwa mwaka 2016/2017 kutokana na kupungua kwa mahitaji ya tumbaku katika soko la dunia na kusababisha kampuni za ununuzi wa tumbaku kupunguza kiasi cha ununuzi wa zao hilo. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara inaendelea kutafuta wanunuzi wengine kupitia Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi, maonesho ya biashara, makongamano ya uwekezaji na biashara ya ndani na nje. Kutokana na jitihada hizo, katika msimu wa 2018/2019, kampuni nne (4) zimeingia mikataba ya ununuzi wa tumbaku na kampuni ya British American Tobacco kwa mara ya kwanza imeonesha nia ya kununua tumbaku nchini.

69. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/ 2019, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku ilipanga kuzalisha tani 54,868 za tumbaku ambapo hadi Machi, 2019 tani 16,460.4 sawa na asilimia 30 ya lengo zimezalishwa na uzalishaji unaendelea. Aidha, Bodi ilipanga kuboresha mabani 56,398 ya kukaushia tumbaku ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2019, mabani 23,960 sawa na asilimia 42.5 yameboreshwa na kazi inaendelea. Vilevile, miche ya miti 13,657,493 imeoteshwa kwa ajili ya kutunza mazingira na vituo 60,000 vya kufungia na kuchambua tumbaku vimesajiliwa.

Zao la Chai

70. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi ya Chai kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutekeleza mkakati wa miaka 10 wa kuongeza uzalishaji wa zao la chai kutoka tani 35,000 hadi tani 50,000 ifikapo 2022/2023. Katika msimu wa 2018/2019, Wizara ilipanga kuzalisha miche 10,000,000 ya chai ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2019, miche bora 7,130,000 imezalishwa kupitia sekta ya umma na binafsi. Kati ya miche hiyo, miche 3,100,000 imesambazwa kwa wakulima katika Wilaya za Njombe, Ludewa, Tarime, Rungwe na Mufindi kwa ajili ya kujaza mapengo na kufungua mashamba mapya.

71. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tan- zania (TSHTDA) kwa kushirikiana na Njombe Outgrowers Services Company (NOSC), Mufindi Outgrowers na Chai Project imetoa mafunzo kupitia mashamba darasa kwa wakulima wadogo wa chai 15,000 na maafisa ugani saba (7) Mafunzo hayo yalihusu uanzishaji na utunzaji wa bustani za miche bora ya chai, upandaji chai mashambani, uchumaji wa majani mabichi ya chai, matumizi sahihi ya pembejeo na upandaji wa miti kwa ajili ya hifadhi ya mazingira. Vilevile, TSHTDA kwa kushirikiana na vyama vya wakulima wa chai imeanza kutekeleza agizo la Serikali la kuvibadilisha vyama vya wakulima na kuwa ushirika wa wakulima wadogo wa chai kwa lengo la kuwawezesha wakulima kuuza majani mabichi ya chai kupitia ushirika. Hadi kufikia mwezi Desemba 2018, vyama vya Luwika (Njombe) na Kagera Tea Association - KATEA (Kagera) vimebadilishwa kuwa vyama vya ushirika.

72. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2018/2019, tani 37,000 za chai kuvu zilipangwa kuzalishwa na kufikia Machi 2019, tani 19,412.16 sawa na asilimia 52.5 zimezalishwa na uzalishaji unaendelea. Aidha, tani 32,000 za chai kavu zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 62.4 zinatarajiwa kuuzwa kwenye soko la nje ya nchi ikilinganishwa na tani 29,160 zenye thamani ya Dola za Marekani 62,167,167 zilizouzwa mwaka 2017/2018 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1 hapo chini.

Jedwali Na. 1: Mauzo ya chai kavu Soko la Nje

Mwaka	**2016/2017**	**2017/2018**	**2018/2019***
Mauzo (Kg)	23,315,000	29,160,000	32,000,000
Thamani (US$)	41,267,550	62,110,800	62,400,000
Wastani wa bei kwa kilo (US$/kg)	1.77	2.13	1.95

Usindikazji wa chai kwa ajili ya kuongeza kipato

73. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa soko la ndani, mauzo ya chai kavu yanatarajiwa kufikia tani 5,500 ikilinganishwa na tani 5,434 za mwaka 2017/2018. Ongezeko hilo litatokana na kuanza uzalishaji katika kiwanda kipya cha Chai Tanzania Collection kilichopo Dar es Salaam na kuimarishwa kwa viwanda vya Rift Valley (DSM) na BK Tea Blenders – Kagera.

Mazao ya Bustani

74. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na sekta binafsi kuendeleza mazao ya bustani kwa kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kuendeleza Mazao ya Bustani. Katika mwaka 2017/2018, uzalishaji wa mazao ya bustani ulikuwa tani 5,333, 297 na matarajio ya uzalishaji kwa mwaka 2018/2019 ni tani 5,965,027.

Mazao ya bustani ni fursa kubwa kiuchumi

Hadi Machi 2019, uzalishaji umefikia tani 4,364,485 sawa na asilimia 73.17 ya lengo na msimu wa uzalishaji unaendelea. Mwenendo wa hali ya uzalishaji wa mazao ya bustani ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani)

Chanzo: *Wizara ya Kilimo, 2019*

4.5 Ujenzi wa Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo na Masoko

Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo

75. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) inaendelea kutekeleza Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka. Hadi kufikia mwezi Machi 2019, asilimia 83 ya vifaa vilikuwa vimeingizwa nchini kwa ajili ya ujenzi wa ghala katika vituo vya Makambako, Mbozi, Songea, Shinyanga na Dodoma **(Kiambatisho Na.10)**

Vihenge vya kuhifadhia nafaka huongeza ubora wa nafaka

76. Ujenzi wa misingi ya kusimika vihenge pamoja na kazi nyinginezo katika vituo hivyo imefikia asilimia 48. Aidha, ujenzi wa vihenge katika Wilaya za Babati, Mpanda na Sumbawanga umefikia asilimia 14.5. Vilevile, Wizara kupitia Mfuko Kichocheo (SAGCOT Catalytic Trust Fund) imefadhili ujenzi wa ghala la kuhifadhi mpunga lenye uwezo wa tani 7,500 na ukarabati na ujenzi wa barabara zinazounganisha ghala na skimu ya umwagiliaji ya Mwendamtitu katika kijiji cha Mwakanga (Mbarali).

Masoko ya Mazao ya Kilimo

77. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara imeendelea kutekeleza mipango na mikakati ya kupata masoko na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Ili kuongeza juhudi zaidi za utafutaji wa masoko ya mazao ya kilimo, Wizara katika mwaka 2018/2019, imeanzisha kitengo cha masoko ya mazao ya kilimo ambacho kitahusika na kutafuta masoko ndani na nje ya nchi na kufanya utafiti na uchambuzi wa kina wa mahitaji ya mazao na bidhaa za kilimo kwa masoko mbalimbali duniani. Wizara pia iliboresha mifumo ya masoko ya mazao ya kimkakati kwa kufanya utafiti wa mahitaji ya masoko na kuimarisha vyama vya ushirika, kusimamia mikataba baina ya wanunuzi na wakulima. Matokeo ya awali ya utekelezaji ya mifumo hiyo, yameonesha kuwepo kwa tija kwa mkulima, bei nzuri, takwimu na ubora wa mazao. Bei kwa mazao ya

kahawa, korosho na kakao kwa soko la ndani ziliimarika ikilinganishwa na masoko ya nje. Kwa mfano, bei ya kahawa ya Arabika katika soko la dunia ilikuwa ni Dola za Marekani 107.04 ikilinganishwa na Dola 112 katika soko la ndani kwa gunia la kilo 50. Aidha, bei ya kahawa ya Robusta katika soko la dunia ilikuwa Dola 73.90 ikilinganishwa na Dola 87.13 katika soko la ndani kwa gunia la kilo 50.

78. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeendelea kutafuta masoko ya zao la muhogo ikiwemo kuingia Makubalino ya Itifaki ya Usafi baina ya Tanzania na Serikali ya China kuwezesha kuuza zao hilo nchini China. Hadi mwezi Machi 2019, kampuni tano za Dar Canton Investment, Jielong Holdings (T) Company, EPOCH Agriculture Development, Gelimesha Company na Tanzania Export Processing Zone (TAEPZ) zimesajiliwa kwa ajili ya kuuza muhogo nchini China. Kampuni hizo zimeanza ununuzi wa muhogo katika mikoa ya Pwani na Tanga.

79. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kusindika muhogo kwa lengo la kuongeza thamani. Kampuni ya Cassava Starch of Tanzania Corporation (CSTC) inaendelea kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata unga bora wa muhogo (High Quality Cassava Flour) katika mkoa wa Lindi. Ujenzi huo umefikia asilimia 90 na kitakuwa na uwezo wa kuchakata muhogo mbichi tani 60 sawa na tani 25 za unga bora wa muhogo kwa siku. Aidha, ujenzi wa viwanda vingine unaendelea vikiwemo viwanda vya Kampuni ya KIRARE (Kwedizungwa-Tanga) na Maiga Family Farm (Chanika-Dar es Salaam).

80. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilipanga kununua tani 14,000 za mahindi na tani 6,000 za mbegu za alizeti. Hadi kufikia Machi, 2019, Bodi imenunua mahindi tani 7,230 na alizeti tani 621 na kusaga tani 1,003.0 za mahindi ambazo zimetoa tani 802.4 za unga wa mahindi na tani 208.9 za pumba. Tani 1,003.0 za unga wa mahindi zenye thamani ya Shilingi 561,680,000 na tani 208.9 za pumba ze nye thamani ya Shilingi 45,570,000 ziliuzwa katika mikoa ya Iringa, Mwanza,

Dodoma na Dar es Salaam. Aidha, ili kujiimarisha zaidi, Bodi imefunga mashine za kukamua mafuta ya alizeti na kusaga mahindi katika eneo la Kizota Jijini Dodoma hadi Machi, 2019 ufungaji wa mashine za kusaga mahindi umefikia asilimia 90 na alizeti asilimia 65. Mashine hizo zina uwezo wa kusaga tani 60 za mahindi kwa siku na kukamua tani 20 za mbegu za alizeti kwa siku.

Hifadhi na Usalama wa Chakula

Serikali inaendelea kuimarisha hifadhi ya chakula

81. Mheshimiwa Spika, NFRA ilipanga kununua tani 28,200 za mahindi kutoka kwa wakulima kwa ajili ya hifadhi. Hadi kufikia Machi 2019, NFRA imenunua tani 46,236.035. Vilevile, NFRA imetekeleza makubaliano ya kuliuzia Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) tani 36,000 za mahindi yenye thamani ya Shilingi bilioni 21. Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi, ununuzi na uuzaji wa mahindi ili kuimarisha hifadhi ya Taifa ya Chakula na kuuza chakula kwa utaratibu wa kuziunganisha.

82. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara imekamilisha maandalizi ya Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu katika Mazao (Tanzania Initiatives for Preventing Aflatoxin Contamination – TANIPAC). Mradi huo uliozinduliwa tarehe 12 Machi, 2019 unalenga kudhibiti tatizo la sumukuvu katika mifumo ya uzalishaji wa mazao ya chakula

hususan mahindi na karanga. Mradi utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Mtwara, Ruvuma, Tabora, Kigoma, Mwanza, Manyara, Simiyu, Geita na Zanzibar. Aidha, maeneo ambapo ujenzi wa miundombinu ya maabara Kuu ya kilimo nchini, kituo cha mfano cha usimamizi wa mazao baada mavuno na ghala 14 yametambuliwa. Udhibiti wa sumukuvu utaimarisha masoko ya mazao hayo kwani usalama wa mazao ni jambo la msingi katika upatikanaji wa masoko ya uhakika.

4.6 Huduma za Ushauri Kuhus u Utafiti, Mafunzo na Usambazaji Taarifa za Kilimo na Sayansi Shirikishi

Huduma za Ugani

Elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo ni muhimu kwa wadau

83. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/ 2019, Wizara imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Utoa ji na Usim a miz i w a Hud uma za Ugani utakaotumiwa na Sekta ya Umma na Binafsi kulingana na mahitaji ya sasa ya utoaji wa huduma za ugani hapa nchini. Mwongozo huo upo tayari kwa ajili ya kupitiwa na kuridhiwa na watoa huduma za ugani. Aidha, Wizara imeendelea kusambaza teknolojia za kilimo kupitia huduma za ugani kwa kuratibu maonesho ya Nanenane kitaifa yaliyofanyika mkoani Simiyu katika Uwanja wa Nyakabindi pamoja na viwanja vingine katika Kanda saba (7). Viwanja hivyo ni Mwl. J.K. Nyerere (Morogoro), Themi (Arusha), Ngongo (Lindi), John Mwakangale (Mbeya), Nzuguni (Dodoma), Fatma Mwasa (Tabora) na Nyamhongolo (Mwanza). Maonesho hayo yalihusisha utoaji wa elimu kwa

wadau kuhusu upatikanaji wa mtaji kwa ajili ya kuwekeza kwenye kilimo, kanuni bora za uzalishaji wa mazao, pembejeo na zana bora za kilimo, kuongeza thamani mazao ya kilimo na upatikanaji wa masoko.

84. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mradi wa ERPP imetoa mafunzo ya teknolojia ya kilimo shadidi cha mpunga (System of Rice Intensification- SRI) kwa wakulima viongozi 168, Maafisa Ugani na Mafundi Sanifu Umwagiliaji 70 kutoka skimu 40 za umwagiliaji, Maafisa Ugani 20 kutoka Halmashauri sita (6) na Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro. Aidha, mashamba ya mfano 1,120 ya kilimo shadidi kwa zao la mpunga yameanzishwa kwenye skimu 40 za umwagiliaji katika Halmashauri sita (6) za Mkoa wa Morogoro. Pia, mafunzo hayo yametolewa kwa wakulima 250 wa skimu za Kasela, Kazunzu, Luchili na Sukuma zilizopo katika Halmashauri ya Buchosa.

Vyuo na Vituo vya Mafunzo ya Kilimo

85. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha vyuo na vituo vya mafunzo ya kilimo ili kukidhi mahitaji ya wataalam wa ugani kilimo katika ngazi ya kijiji na kata. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia vyuo vyake 14 vya kilimo imedahili na kufundisha wanafunzi 2,389 ambapo wanafunzi 2,051 wamefadhiliwa na Serikali na 338 wanajilipia wenyewe. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, 1,537 ni ngazi ya Astashahada na 852 ni ngazi ya Stashahada. Jumla ya wanafunzi 1,026 wakiwemo 263 wa Stashahada na 763 wa Astashahada watahitimu masomo yao mwezi Juni, 2019. Vyuo hivyo vinatoa Astashahada na Stashahada za Kilimo Mseto, Stashahada ya Umwagiliaji, Matumizi Bora ya Ardhi, Uzalishaji Chakula na Lishe, Matumizi ya Zana za Kilimo, Uzalishaji wa Mazao, Mboga, Maua na Matunda.

86. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Lutheran World Relief (LWR) kupitia mradi wa Invest imehuisha mtaala wa Kilimo Mseto (Agriculture General) na kuzalisha mtaala mpya wa kilimo (Agriculture Production) ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira na kutimiza masharti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Aidha, mradi wa Invest

umejenga kitalu nyumba katika Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu ili kutoa mafunzo bora kwa wagani tarajali na wakulima. Vilevile, mradi umewajengea uwezo wakufunzi 20 kutoka vyuo vya Kilimo Ilonga (Kilosa), KATRIN (Ifakara) na Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu ili wafundishe kwa kufuata mwongozo wa mfumo wa moduli.

87. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wakufunzi wa kilimo 22 ambapo wakufunzi 10 wapo katika mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) na 12 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi nchini India na China. Vilevile, Wizara kupitia vyuo vyake vya Kilimo kwa kushirikiana na Taasisi Binafsi imeandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya kuwajengea uwezo wakulima kuhusu teknolojia mbalimbali za kilimo. Mafunzo hayo yalihusu Kilimo cha Korosho-MATI Mtwara (wakulima 67); Kilimo cha Mahindi na Maharage-MATI Ukiriguru (wakulima 51); Usindikaji wa mazao-MATI Uyole (wakulima vijana 56); na Kilimo bora cha soya (wakulima 31); Kilimo shadidi cha mpunga (wagani 33); kilimo bora cha alizeti (wakulima 25 na wagani 5); na kilimo bora cha mpunga (wakulima 20)-MATI Ilonga.

88. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na JICA kupitia mradi wa TANRICE2 imetoa mafunzo kwa wakulima wa mpunga 1,964. Kati ya hao, wakulima 923 wametoka katika skimu za umwagiliaji za Kimbande Nyasa (Ruvuma), Magoma (Korogwe) Wamiluhindo (Mvomero), Tulokongwa (Morogoro), Solola Nkanga (Sumbawanga) na Legezamwe ndo (Tunduru), Litumbadyosi (Mbinga), Njomulole (Namtumbo), Msanjesi (Namtumbo) na Kyamyorwa (Muleba). Aidha, wakulima 1,041 wametoka katika Wilaya za Babati, Bukoba Vijijni, Namtumbo, Kisarawe, Ulanga, Bariadi, Momba na Kyela ambao wanalima kwa kutegemea mvua.

4.7 Kuimarisha Ushirika

Ushirika imara husaidia wakulima kupata bei nzuri ya pembejeoza mazao yao

89. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kusimamia na kudhibiti Vyama vya Ushirika kwa kukagua na kuchunguza, kupitia mikataba, kusimamia chaguzi za Bodi, kusajili masharti ya SACCOS, kutatua migogoro na kushughulikia malalamiko pamoja na kuviunganisha Vyama vya Ushirika moja kwa moja na masoko. Katika mwaka 2018/2019, Tume ya Maendeleo ya Ushirika kupitia Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) limefanya ukaguzi wa nje kwa vyama vya ushirika 2,297. Kati ya Vyama vilivyokaguliwa, asilimia 4.6 vilipata hati inayoridhisha, asilimia 64.6 vilipata hati yenye shaka, asilimia 21.6 vilipata hati isiyoridhisha na asilimia 9.2 vilipata hati mbaya. Hali hiyo ya Vyama vya Ushirika siyo nzuri na hatuwe zi kufumbia macho. Tayari Tume ya Ushirika ina programu ya kuvijengea uwezo Vyama vya Ushirika na inaendelea kutekelezwa. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yetu tuendelee kushirkiana na Halmashauri zetu kuvisaidia vyama hivi ambavyo ni mkombozi wa mkulima.

4.8 Usajili wa Wakulima

90. Mheshimiwa Spika, Wizara imeamua kuanza zoezi maalum na endelevu la kusajili wakulima wote nchini na kuwapa vitambulisho. Lengo la zoezi hilo ni kuwatambua wakulima mahali walipo, mazao wanayolima na ukubwa wa

mashamba yao. Zoezi hilo linafanyika kitaalam kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kuwa na kanzidata ya uhakika ya kila zao na baadaye kuwa na kanzidata moja iliyounganishwa kwa mazao yote.

91. Mheshimiwa Spika, tumeanza na usajili wa wakulima wa mazao ambayo yanasimamiwa na Bodi za Mazao. Mazao hayo ni, kahawa, korosho, miwa, pamba, chai, mkonge, tumbaku na pareto. Tangu zoe zi hilo lianze , jumla ya wakulima 1,464,827 wametambuliwa na kusajiliwa katika maeneo mbalimbali nchini. Zoezi hilo siyo tu litatusaidia kuwatambua wakulima walipo na kuwafikishia huduma muhimu, bali pia litaisaidia Serikali kujua mahitaji halisi ya pembejeo ikiwemo mbegu, mbolea, viuatilifu na kuweza kukadiria mavuno kwa mwaka husika. Uzoefu utakaopatikana kwenye uandikishaji wa wakulima wa mazao hayo utasaidia kuandikisha wakulima wa mazao mengine mchanganyiko siku zijazo. Tumejiwekea lengo la kukamilisha usajili wa wakulima wa mazao hayo ya biashara ifikapo Juni 30, 2019.

4.9 Kuunda na Kupitia Sera na Sheria zake

92. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha Sera, Sheria, Kanuni na Mikakati ya kilimo ili kuwa na mazingira wezeshi ya uwekezaji katika Sekta ya Kilimo. Katika mwaka 2018/2019, Wizara imefuta ushuru, tozo na ada 80 ambazo katika mwaka 2017/2018 zilionekana kuwa kero kwa wakulima na vikwazo kwa maendeleo ya Sekta ya Kilimo.

93. Mheshimiwa Spika, vilevile, katika mwaka 2018/2019, Wizara imefuatilia na kutathmini maendeleo ya uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Sekta ya Kilimo kwa lengo la kubaini changamoto za kisera na kisheria zinazoathiri mazingira ya uwekezaji na biashara. Ufuatiliaji huo ulihusisha mazao ya bustani, mazao ya mbegu za mafuta, chai na pareto katika Mikoa ya Njombe, Iringa, Singida, Manyara, Arusha na Kilimanjaro. Katika ufuatiliaji huo, changamoto za kisera zikiwemo kero za kodi, tozo, ada na ushuru ambazo zinaathiri uwekezaji zaidi katika Sekta ya Kilimo zimebainika. Changamoto hizo zimewasilishwa katika Kamati ya Ushauri wa

Sera za Kodi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kujadiliwa na kutoa mapendekezo ya marekebisho. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa usimamizi wa Mazao baada ya Mavuno. Mkakati huo unalenga kupunguza upotevu wa mazao ya chakula katika mnyororo wa thamani, kuongeza upatikanaji wa chakula na kipato.

4.10 Uratibu, Takwimu, Ufuatiliaji na Tathmini

94. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kukusanya takwimu za uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kutumia mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za kilimo (Agriculture Routine Data System - ARDS) kwa ajili ya matumizi mbalimbali katika mipango ya kilimo. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Maafisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Wilaya na wasimamizi kuhusu mfumo wa takwimu za kilimo katika Halmashauri 185.

4.11 Matumizi Endelevu ya Ardhi ya Kilimo

95. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Matumizi Endelevu ya Ardhi katika Lindimaji za Mito ya Ruvu na Zigi katika mikoa ya Morogoro na Tanga. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa maafisa ugani 40 kuhusu hifadhi ya udongo na maji mashambani kutoka wilaya za Muheza, Korogwe na Mkinga. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Viwanda na Biashara na Sekta Binafsi imefuatilia mashamba yaliyobatilishwa umiliki na Serikali kuona kama yatafaa kwa kilimo cha Alizeti. Hadi Machi, 2019 mashamba 15 yenye ekari 17,646.65 katika wilaya za Mvomero na Kilosa yaliyobatilishwa yamebainika yanafaa kwa kilimo cha alizeti na yanatakiwa yabadilishwe umiliki.

4.12 Masuala Mtambuka

Ushiriki wa Vijana katika kilimo

96. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Vijana Kushiriki katika Kilimo na Kuongeza Ajira kwa kushirikiana na Sekta binafsi, washirika

wa maendeleo na Wizara za Kisekta. Katika mwaka 2018/ 2019, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), SUGECO na Farm Africa imewezesha vijana 560 kutoka mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Morogoro, Singida, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Mtwara na Kigoma kujiajiri katika mnyororo wa thamani wa mazao ya bustani, ufugaji kuku na nyuki. Aidha, mafunzo ya vitendo kuhusu kilimo biashara yametolewa kwa vijana 60 katika Kambi ya Vijana ya Kilimo ya Mkongo, Rufiji. Vilevile kupitia mradi wa East Africa Youth Inclusion Program (EAYIP) imetoa mafunzo kwa vijana 6,584 kuhusu kilimo cha biashara katika mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa na Njombe. Vilevile, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania kupitia SUGECO imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 200,000,000 kwa vijana watatu (3) waliopata mafunzo ya kilimo nchini Israel na sasa wanaendesha kilimo cha Bustani katika wilaya ya Rufiji.

97. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imetoa mafunzo kwa vijana 8,700 kuhusu ujenzi wa vitalu nyumba katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Simiyu, Iringa, Kagera, Geita, Mwanza, Manyara, Kilimanjaro, Lindi, Ruvuma na Mbeya. Aidha, Taasisi ya International Trade Centre imejenga vitalu nyumba (Green Houses) 15 kwa ajili ya vijana. Kati ya hivyo, vitalu saba (7) vimejengwa katika mkoa wa Dodoma, saba (7) mkoa wa Pwani na kimoja (1) katika mkoa wa Morogoro kwa ajili ya kuzalisha mazao na kufundishia vijana.

Lishe

98. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, OR- TAMISEMI, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, na Taasisi nyingine zinazotekeleza masuala ya lishe inatekeleza Mpango wa Kitaifa wa Lishe Nchini - National Multisectoral Nutrition Action Plan (NMNAP). Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Chakula na Lishe nchini pamoja na shirika la Lishe la Kimataifa (Nutrition International) imekamilisha Mwongozo wa Kitaifa wa Uzalishaji na Matumizi ya Mazao yaliyoongezwa Virutubisho. Vilevile,

Wizara imebainisha maeneo ya kipaumbele kuhusu lishe yaliyo kwenye ASDP II na NMNAP na kuyaoanisha kwa ajili ya kuongeza ufanisi kwenye utekelezaji.

Jinsia

99. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhusisha masuala ya jinsia katika kilimo kupitia mradi wa "Sambaza mbegu za viazi vitamu fasta". Wizara imetoa mwongozo wa masuala ya jinsia kwa ajili ya kufundishia maafisa ugani, wahamasishaji jamii, walimu, viongozi wa Kata na Vijiji ambapo nakala 5,760 zimesambazwa kwa wadau. Vilevile, kitabu cha vikaragosi cha watoto wa shule za msingi darasa la IV-VI cha Kilimo na Jinsia kimeandaliwa na kufanyiwa tathmini na Taasisi ya Elimu Tanzania ili kisambazwe kwenye mashule.

Mazingira

100. Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa mafunzo kwa wataalam 98 wa Kilimo, Mifugo, Mazingira, Mipango na Ugani kuhusu kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi. Mafunzo hayo yametolewa katika Halmashauri za Wilaya za Mbinga, Songea, Madaba, Mvomero, Kilombero, Kilosa, Chunya, Mbeya, Mbarali, Pangani, Handeni, Korogwe, Lushoto, Muheza, Siha, Hai, Same, Rombo na Mwanga. Aidha, nakala 101 za Mwongozo wa Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi, nakala 101 za Kitabu cha Mbinu na Teknolojia za Kilimo zinazohimili Mabadiliko ya Tabianchi na nakala 101 za kitabu cha Kiongozi cha Mwalimu zimesambazwa.

101. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Mazingira Duniani (UNEP) na Taasisi ya Kuendeleza Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT Centre Ltd.) kupitia Halmashauri ya Iringa, katika Mkoa wa Iringa, imeanzisha shamba darasa la umwagiliaji kwa njia ya matone (drip irrigation) lenye ukubwa wa ekari tatu (3) katika kijiji cha Wangama. Lengo la shamba darasa hilo ni pamoja na kuhamasisha kilimo bora cha mazao ya bustani hususan,

maharage na njegere changa, na kusambaza teknolojia ya matumizi bora ya maji kama njia ya kukabiliana na upungufu wa maji kutokana na ukame. Shamba hilo litatumika kuelimisha wakulima ndani na nje ya kijiji cha Wangama juu ya matumizi bora ya maji na kwa tija zaidi. Kwa sasa mashirikiano hayo yananufaisha wakulima 50 kati yao wanawake 36 na wanaume 14 ambao wanajishughulisha na kilimo cha maharage mabichi.

102. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza kilimo hifadhi, Wizara kwa kushirikiana na Conservation Farming Unit (CFU), Diocese of Central Tanganyika (DCT) na TAMISEMI imetoa mafunzo ya matumizi ya kilimo hifadhi kwa wakulima viongozi 365. Mafunzo hayo yametolewa katika wilaya za Babati, Kiteto, Same, Monduli, Chamwino, kwa lengo la kuongeza uzalishaji katika maeneo yanayokabiliwa na changamoto za mabidiliko ya tabianchi.
VVU na UKIMWI

103. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI mahali pa kazi, Wizara imeendelea kuwahamasisha watumishi kupima afya ili kutambua hali zao. Katika mwaka 2018/2019, watumishi 15 waliojitambulisha kwa mwajiri kuwa wanaishi na VVU wameendelea kupatiwa fedha kila mwezi kwa ajili ya kuwawezesha kupata lishe bora. Aidha, Wizara imeendelea kutoa vifaa kinga kwa watumishi na kuwekwa katika maeneo yanayofikiwa na watumishi wengi. Vilevile, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao ambapo watumishi wa Wizara waliopo Dodoma walipima ili kujua hali za afya zao.

5.0 MPANGO NA MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2019/2020

5.1 Kuongeza Tija katika Kilimo Upatikanaji wa mbegu bora za mazao

104. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020 , Wizara itaendelea kuhamasisha na kuimarisha uzalishaji wa mbegu

bora kwa kutumia rasilimali za Serikali pamoja na kuishirikisha Sekta Binafsi na kuongeza udhibiti wa ubora wa mbegu.

Mbegu bora kwa tija zaidi

105. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mbegu za Kilimo kwa kushirikiana na Sekta Binafsi katika mwaka ujao wa fedha, umejipanga kuzalisha jumla ya tani 3,673.6 kutoka katika mashamba yake. Aidha, Wakala kwa kushirikiana na wakulima wa mkataba pamoja na taasisi za serikali kama vile magereza na vituo vya utafiti unategemea kuzalisha mbegu kiasi cha tani 1,246.6. Vilevile, wakala kwa kutumia mashamba yake yanayotumiwa na makampuni binafsi unatarajia kuzalisha kiasi cha tani 8,688. Hivyo, ASA kwakutumia rasilimali ardhi yake itazalisha takribani tani 13,608.2 za mbegu nchini kwa msimu wa 2019/2020. Pia, ASA itazalisha vipando bora vya muhogo pingili 7,000,000 na miche bora ya matunda 20,000.

106. Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo hayo, miundombinu ya umwagiliaji itaboreshwa na eneo la uzalishaji wa mbegu litaongezwa hadi kufikia hekta 811 katika mashamba ya Dabaga hekta 200 (Iringa), Mwele hekta 160 (Tanga), Mbozi hekta 62 (Mbeya) na Msimba hekta 389 (Morogoro). Aidha, maghala mawili ya Msimba na Kilangali yenye uwezo wa kuhifadhi mbegu tani 1,300 yatafanyiwa ukarabati.

107. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TARI itaanza kuzalisha mbegu za msingi na zilizothibitishwa na kuzisambaza kwa wakulima ili kupunguza pengo la upatikanaji wa mbegu bora. TARI itazalisha Mbegu bora za awali tani 200, za msingi tani 1,000 na mbegu zilizothibitishwa tani 3,000 za mazao ya aina ya nafaka, mikunde, mboga mboga, mafuta na miche/ vikonyo milioni 20 za mazao ya mizizi na migomba na kusambaza kwenye maeneo yanayolima mazao hayo.

108. Mheshimiwa Spika, Wizara pia kupitia TOSCI itakagua hekta 50,000 za mashamba ya mbegu; itafanya majaribio ya uhalisia (DUS test) wa mbegu mpya 120; itahakiki majaribio ya uhalisia (control plots tests) kwa sampuli 500 za mbegu; itaandaa kanuni na miongozo ya kufanya majaribio ya utambuzi na umahiri wa mazao ya biashara; itachukua sampuli 3,000 za mbegu na kupima ubora wake; itakagua maduka 1,000 na maghala 20 ya mbegu; itafanya majaribio 70 ya sampuli za viazi na muhogo ili kuchunguza uwepo wa magonjwa; na itatoa mafunzo ya ukaguzi wa mbegu kwa wakaguzi 50 walioidhinishwa na TOSCI katika Wilaya 50.

Upatikanaji na udhibiti wa ubora wa Mbolea

109. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara itasimamia uagizaji na usambazaji wa tani 625,000 za mbolea zinazokadiriwa kutumika nchini. Aidha, kupitia Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) itaongeza mauzo ya mbolea kutoka tani 10,000 hadi tani 100,000. Vilevile, ghala moja (1) lenye uwezo wa kuhifadhi tani 20,000 za mbolea litakarabatiwa katika wilaya ya Tabora pamoja na kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuchanganya mbolea kwa uwiano (blending plant) katika mkoa wa Dar es salaam. Pia, Wizara kupitia TFRA itawakagua wafanyabiashara 1,000 wa mbolea; itawajengea uwezo wakaguzi 100 wa mbolea. Aidha, TFRA itafanya tathmini ya kubaini mahitaji sahihi ya mbolea nchini na kuanzisha maabara ya uchunguzi wa ubora wa mbolea eneo la Kurasini Dar es Salaam.

Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu

110. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara itanunua na kusambaza lita 300,000 na kilo 3,000 za viuatilifu

kwa ajili ya kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mazao. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha kituo cha kudhibiti milipuko cha Kilimo Anga (Arusha) ili kutoa huduma bora. Vilevile, Wizara itaendelea kuvijengea uwezo na kukarabati vituo 10 kati ya 36 vya ukaguzi wa mazao mipakani.

111. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TPRI, itakarabati na kununua vifaa kwa Maabara mbili (2) za kupima viuatilifu ili zipate ithibati ya kimaifa; itatoa mafunzo yanayohusu matumizi sahihi ya viuatilifu na uhifadhi wa taka zake kwa wakulima na maafisa 1,200 katika kanda za Mashariki, Kaskazini, Kati na Magharibi; itakagua maduka ya wafanya bi ashara 2,000, wafuk izaji 800 na watengenezaji nane (8) wa viuatilifu; itasajili viuatilifu vipya 150 na kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara 2,000 wapya wa viuatilifu. Ili kukidhi ubora wa mazao kwa soko la ndani na nje, TPRI itakusanya sampuli 1,600 za mazao ya chai, kahawa, mboga na maua ili kupima masalia ya viuatilifu kwenye mazao hayo.

Zana za Kilimo

112. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaanzisha kituo kimoja (1) cha zana za kilimo kwa ajili ya kutoa huduma za kiufundi na mafunzo kwa watoa huduma binafsi wamiliki na watumiaji wa zana za kilimo kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wakulima katika Kanda ya Ziwa. Kituo hicho kitakuwa na matrekta, zana za kukatua, kupandia, kupalilia, kuvunifa, kunyunyizia dawa, kilimo hifadhi na mashine za usindikaji zitakazokuwa zinakodishwa kwa wakulima. Wizara pia, itahuisha Mkakati wa Matumizi ya Zana Bora za Kilimo wa mwaka 2006 ili kuongeza matumizi ya zana bora za kilimo.

113. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia AGITF, imepanga kutoa mikopo 250 yenye thamani ya Shilingi 4,119,000,000 inayojumuisha mitambo ya mashambani; pembejeo za kilimo, mifugo na samaki; matrekta ya mikono; ukarabati wa zana za kilimo; miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi; fedha za kuendeshea shughuli za shamba; kununua ardhi kwa

ajili ya kilimo, mifugo na ufugaji wa samaki; zana unganishi; zana za kusindika na vifunganishio (Kiambatisho Na. 11). Vilevile Mfuko utatambua skimu 100 za umwagiliaji kwa ajili ya kupewa mikopo.

5.2 Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji

114. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itafanya tathmini ya miradi ya umwagiliaji ambayo ujenzi wake haujakamilika ili miradi hiyo iweze kukamilishwa kwa awamu. Wizara pia, itakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu katika skimu mbili (2) za Luiche (Kigoma Ujiji) na Ibanda (Sengerema/Geita); itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika skimu mpya nne (4) za Mwamkulu (Mpanda), Mkombozi (Iringa), Msia (Mbozi) na Luhafwe (Tanganyika) na kupitia usanifu na maandalizi ya zabuni katika skimu tano (5) za Lupiro iliyopo kwenye halmashauri ya Ulanga, Endagaw (Hanang') Bugwema (Musoma), Rudewa (Kilosa) na Nyamitita (Serengeti).

115. Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa Kuendeleza Skimu za Wamwagiliaji Wadogo (Small Scheme Irrigation Development Project – SSIDP) Wizara itakamilisha ujenzi wa skimu 16 za kilimo cha umwagiliaji za Mwisa (Karagwe), Nyida (Shinyanga), Katela Ntaba na Mbaka (Busekelo), Mgambalenga (Kilolo), Mwalunili (Igunga), Ngongowele (Liwale), Nanganga (Ruangwa), Ngage (Simanjiro), Orumwi (Siha), Soko (Moshi), Nyatwali na Maliwanda (Bunda), Kutuani Mwenzae na Kwemgiriti (Lushoto) **(Kiambatisho Na. 12).** Aidha, Wizara kupitia Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Zao la Mpunga (Expanded Rice Production Project - ERPP) itajenga na kukarabati skimu tano (5) za Kigugu (Mvomero), Msolwa Ujamaa na Njage (Kilombero), Mvumi na Kilangali Seed farm (Kilosa).

116. Mheshimiwa Spika, Wizara itavijengea uwezo Vyama vya Wamwagiliaji kwa kuwezesha uanzishwaji wa Kilele cha Vyama vya Wamwagiliaji (IOs APEX); kuanzisha Vyama vya Wamwagiliaji 200 na kuimarisha Vyama 300 kuhusu usimamizi

na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji; kusaidia Halmashauri 80 na Vyama vya Wamwagiliaji 240 kuandaa kanuni ndogondogo kulingana na Sheria Na. 5 ya Umwagiliaji (2013) pamoja na Kanuni zake za mwaka 2015; na kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa uanzishwaji wa Vyama vya Wamwagiliaji na kusambaza kwa wadau.

5.3 Utafiti wa Kilimo na Uhaulishaji wa Teknolojia

117. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/ 2020, Wizara kupitia TARI imepanga kutafiti, kugundua na kusambaza aina 15 za mbegu bora za mazao ya nafaka, mizizi, mbegu za mafuta, mikunde na mazao ya bustani. Pia, TARI imepanga kukamilisha majaribio ya mbegu mpya za NARITAs Hybrid zenye ukinzani mkubwa wa wadudu na magonjwa katika mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya na Kagera. Aidha, TARI itatafiti, kugundua na kusambaza teknolojia bora 20 za agronomia, teknolojia tano (5) za kupunguza harubu katika kilimo na usindikaji na teknolojia 15 za kuzuia upotevu wa mazao baada ya kuvuna na uhifadhi wa mazao kwa ajili ya kuimarisha usalama wa chakula na lishe.

118. Mheshimiwa Spika, Wizara itasafisha aina tisa (9) za mbegu ya mpunga na kuzalisha tani 10 za mbegu za awali katika Kituo cha Utafiti cha KATRINI. Kupitia kituo cha TARI Naliendele Serikali itajenga kinu cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 1,800 kwa mwaka na kusindika tani 1,000 za mvinyo na sharubati (juice). Usindikaji huo utaenda sanjari na kutoa teknolojia za usindikaji ili kuongeza ubora wa korosho-karanga na mazao yake.

5.4 Maendeleo ya Mazao

119. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao kwa kuimarisha utafiti, upatikanaji na utumiaji wa pembejeo na zana za kilimo, udhibiti wa visumbufu vya mazao, huduma za ugani, uongezaji wa thamani na upatikanaji wa masoko.

Zao la Mahindi

120. Mheshimiwa Spika, Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la mahindi kufikia tani 8,000,000 mwaka 2019/2020 ikilinganishwa na tani 6,300,000 zinazozalishwa sasa.

Zao la Mpunga

121. Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa Mpunga kutoka tani milioni 3.385 mwaka 2017/2018 hadi tani milioni 4.36 mwaka 2019/2020. Lengo hilo litafikiwa kwa kuongeza ene o la uzalishaji, matumizi ya mbe gu bora, kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga ikiwemo ya kilimo shadidi katika skimu za umwagiliaji. Aidha, Wizara kwa kushirikana na wadau itaboresha mkakati wa kuendeleza zao la mpunga nchini ili uendane na mahitaji ya sasa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Se kta binafsi na taasisi za k i m a t a i f a i t a j e n g a u w e z o k w a w a k u l i m a , wasindikaji, wafanyabiashara na wasafirishaji wa mpunga/mchele nchini.

Zao la Ngano

122. Mheshimiwa Spika, mahitaji ya ngano nchini ni tani 250,000 ambapo uzalishaji kwa mwaka 2017/2018 ni wastani wa tani 56,651. Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa ngano hadi kufikia tani 100,000 ifikapo mwaka 2021/2022. Katika kuhakikisha lengo hilo linafikiwa, Wizara itahamasisha kilimo cha ngano katika Ukanda wa Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini. Kwa mwaka 2018/2019 matarajio ni kuzalisha tani 76,400 na kwa msimu wa 2019/2020 imepanga kuzalisha tani 85,000 za ngano kwa kuongeza matumizi ya mbegu bora, kutoa mafunzo ya kanuni za kilimo bora, kuimarisha upatikanaji wa masoko na utafiti wa zao hilo.

Zao la Muhogo

123. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2019/2020, Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa muhogo mbichi kutoka tani milioni 8 mwaka 2017/2018 hadi tani milioni 10. Ili kufikia lengo hilo, Wizara kupitia vituo vya utafiti na Sekta binafsi

itazalisha mbegu bora za muhogo pingili milioni 40, kupanua maeneo ya uzalishaji kwa kushirikana na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuongeza thamani na kuimarisha masoko.

Zao la Alizeti

124. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendendelea kutekeleza mkakati wa kuendeleza zao la alizeti ili kutosheleza mafuta ya kula kwa kuongeza uzalishaji wa alizeti kutoka tani 768,188 mwaka 2017/2018 hadi tani 1,500,000 kufikia 2020/2022 ambapo matarajio ni kuzalisha tani 820,905 msimu wa 2019/2020. Lengo hilo litafikiwa kwa kuimarisha ugunduzi wa mbegu bora, kuongeza upatikanaji wa pembejeo, kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya usindikaji, kutoa mafunzo ya kanuni za kilimo bora cha alizeti na kuwaunganisha wakulima na wasindikaji ili kuwa na masoko ya uhakika. Mikakati hii itasaidia kupunguza kiasi cha mafuta kinachoagizwa toka nje nchi na kufikia mahitaji ya tani 570,000 za mafuta zinazohitajika nchi kwa mwaka.

Zao la Mchikichi

125. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia TARI, ASA, Jeshi la Kujenga Taifa, Magereza, Sekretarieti za Mikoa na Sekta Binafsi itazalisha miche ya mchikichi 5,000,000 kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo. Vilevile, Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) itatoa mikopo ya kuendele za zao hilo kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu na uongezaji wa thamani. Aidha, Wizara itashirikiana na SIDO, CARMATEC, NDC na FAO/UNIDO kuwapatia wakulima zana bora za uzalishaji na uongezaji thamani zao la michikichi.

Zao la Korosho

126. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Korosho itaendelea kutekeleza programu ya kuzalisha miche bora 10,000,000 ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango itahakiki na kulipa vikundi vya wazalisha

miche ya mikorosho kwa msimu wa 2017/2018 ambao hawajalipwa kutoka katika mikoa ya Mtwara, Lindi , Ruvuma, Pwani, Tanga, Dodoma, na Singida. Vilevile, Wizara itaratibu upatikanaji na usambazaji wa tani 30,000 na lita 500,000 za salfa kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao la korosho.

Zao la Pareto

127. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Pareto imepanga kuongeza uzalishaji wa pareto kufikia tani 2,600 kutoka tani 2,400 za mwaka 2018/ 2019. Aidha, katika kipindi hicho, tija ya zao hilo inatarajia kuongezeka kutoka kilo 300 hadi 350 kwa ekari. Vilevile, ubora wa maua unatarajiwa kuongezeka kutoka wastani wa asilimia 1.2 mwaka 2018/2019 hadi asilimia 1.5 mwaka 2019/2020. Wizara kupitia Bodi ya Pareto itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika mitambo ya kuchuja sumu ya pareto, kuwezesha upatikanaji wa aina moja ya mbegu ya pareto kupitia utafiti wa aina saba za pareto na kujenga maabara ya kupima sumu ya pareto.

Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari

128. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/ 2020, Wizara kupitia Bodi ya S uka ri imepanga kuzalisha sukari tani 403,786 kwa kuongeza eneo la uzalishaji wa kilimo cha miwa kutoka hekta 52,000 hadi hekta 97,000. Aidha, tija ya uzalishaji wa miwa kwa wakulima wadogo itaongezeka kutoka tani 50 hadi tani 70 kwa hekta kwa kutumia teknolojia za kilimo bora. Wizara, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) itawezesha upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji wa miradi mipya ya sukari katika Wilaya za Kasulu, Kibondo, Rufiji, Ge ita, Kilombe ro, Karagwe , Pangani, Bagamoyo na Morogoro. Vilevile, Wizara kupitia kituo cha utafiti wa miwa TARI Kibaha, itafanya majaribio ya aina mpya za mbegu za miwa katika Ukanda wa Afrika Mashariki na kukamilisha uhakiki wa mwisho (National Performance Trial) wa ubora wa aina tatu za mbegu bora za miwa ambazo zimeonesha kuwa na ukinzani na ugonjwa wa smut disease na kustahimili ukame.

Zao la Kahawa

129. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya kahawa itaongeza uzalishaji wa kahawa kutoka tani 65,000 hadi tani 80,000. Vilevile, itashirikiana na wadau kuongeza matumizi ya mitambo ya awali ya kuchakata kahawa Central Pulpery Unity (CPU) kutoka asilimia 35 ya sasa hadi 50. Bodi itakamilisha usajili wa wakulima wa kahawa na kuwapatia vitambulisho, itaimarisha mifumo ya masoko ya kahawa ikiwa ni pamoja na kuanzisha minada katika kanda za uzalishaji wa kahawa na kuimarisha vyama vya ushirika. Pamoja na hayo miche 10,000,000 ya kahawa itazalishwa na kusambazwa kwenye Wilaya 42 zinazolima kahawa na kutoa mafunzo kwa wakulima wa kahawa 4,000; maafisa ugani 500 na wakulima viongozi 300.

Zao la Mkonge

130. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Mkonge imepanga kuongeza uzalishaji wa mkonge kutoka tani 38,506 hadi tani 113,506 kwa kuongeza eneo la uzalishaji kutoka hekta 42,426.11 hadi 114, 915.08. Kutokana na uzalishaji huo, mauzo ya bidhaa za mkonge kwenye soko la nje yanatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 24.5 hadi asilimia 35.5 na kuongezeka kwa matumizi ya mkonge kutoka asilimia 2 hadi asilimia 20. Bodi pia itasimamia uendeshaji wa mfumo wa kilimo cha wakulima wadogo cha mkataba kwa kuimarisha vyama vya ushirika na masoko ya mkonge kupitia minada itakayomwezesha mkulima kuuza kwa bei ya ushindani. Aidha, Wizara itatafuta wawekezaji wapya wa mashamba makubwa mawili ya Mabogo na Kwalukonge yaliyofutiwa hati za umiliki na Serikali ili mashamba hayo yazalishe kwa tija na kuongeza ajira.

Zao la Pamba

131. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Pamba imepanga kuongeza uzalishaji wa pamba kutoka tani 222,000 hadi tani 700,000 na tija kutoka

300 hadi 600 kwa ekari. Bodi pia, imepanga kuongeza ubora wa pamba kutoka asilimia 43 hadi 75. Aidha, upatikanaji wa mbegu za pamba utaongezeka kutoka tani 22,000 hadi 40,000 na upatikanaji wa viuatilifu utaongezeka kutoka lita 7,000,000 hadi 10,000,000. Ili kuongeza ukuaji wa tasnia ya pamba, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara itahamasisha uwekezaji katika viwanda vya kuchambua pamba, kusokota nyuzi, kuseketa na kufuma vitambaa, utengenezaji na ushonaji wa mavazi pamoja na viwanda vya mafuta ya kula na vyakula vya mifugo.

Zao la Tumbaku

132. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku imepanga kuongeza uzalishaji kutoka tani 55,000 hadi tani 60,000; kukamilisha usajili wa wakulima wa zao la tumbaku kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuimarisha vituo 1,972 vya kufungia na kuchambulia tumbaku; na kusajili na kukagua vituo 790 vya kuuzia tumbaku. Aidha, Bodi itasimamia masoko na kutoa mafunzo ili kuongeza ubora wa tumbaku kutoka asilimia 87 hadi 92. Bodi itaimarisha mfumo wa upatikanaji wa pembejeo za zao la tumbaku kwa kuwaunganisha watoa huduma wa pembejeo na vyama vya ushirika ili ziwafikie kwa wakati. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau itahamasisha uanzishwaji wa kiwanda cha kuchakata, kutafuta masoko mapya ya tumbaku na kuwezesha kufanyika kwa majaribio ya aina mbili (2) za mbegu bora za tumbaku.

Zao la Chai

133. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Chai imepanga kuongeza uzalishaji wa chai kavu kutoka tani 34,000 hadi tani 40,000 ambazo ni sawa na tani 182,000 za majani mabichi ya chai. Vilevile, tija ya majani mabichi kwa mkulima mdogo kuongezeka kutoka kilo 1,000 hadi 1,300 kwa ekari na mkulima mkubwa kutoka kilo 2,000 hadi 2,500 kwa ekari; ubora wa majani mabichi ya

chai kuongezeka kutoka asilimia 50 hadi asilimia 70; kuhamasisha unywaji wa chai kutoka gramu 110 kwa mtu hadi 250 kwa mtu kwa mwaka na kuhakiki na kusajili maeneo yaliyopandwa chai ili kuboresha daftari la wakulima wa chai.

134. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF) itafufua kiwanda cha chai cha Mponde ili kuimarisha upatikanaji wa soko la majani mabichi ya chai kwa wakulima na kuongeza ajira. Vilevile, miundombinu ya mashamba ya chai yanayomilikiwa na vijiji vya Tarafa ya Lupembe Wilaya ya Njombe itakarabatiwa, shamba la chai la Mlangali lililopo katika Tarafa ya Lupembe lenye ukubwa wa hekta 200 litafufuliwa na mfumo wa malipo kwa wakulima wadogo wa chai wa Bukoba na Muleba katika Mkoa wa Kagera utaboreshwa. Sanjari na juhudi hizo, minada ya chai itaanzishwa katika maeneo yanayozalisha chai ili kuimarisha
masoko ya ndani badala ya kutazama minada ya nje ya nchi.

5.5 Miundombinu ya Hifadhi na Uongezaji Thamani Mazao ya Kilimo

135. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia NFRA itakamilisha awamu ya kwanza ya Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi ambapo ujenzi wa maghala matano (5) yenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000 na vihenge nane (8) vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 190,000 za nafaka utakamilika na hivyo kuongeza uwezo wake wa kuhifadhi nafaka kutoka tani 251,000 hadi tani 501,000. Aidha, Wizara itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa ghala tano (5) kwa ajili ya hifadhi ya zao la mahindi katika Halmashauri za Wilaya za Buchosa (1), Mkalama (1), Kasulu (1); Itilima (1); na Ileje (1). Vilevile, kupitia Mradi wa ERPP, ghala tano (5) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 6,700 za zao la mpunga katika skimu tano (5) za umwagiliaji za Njage (1,700), Msolwa Ujamaa (1,700), Kigugu (1,000), Mvumi (1,300) na Mbogokomtonga (1,000) katika mkoa wa Morogoro zitajengwa.

136. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko itasindika

tani 29,000 za mahindi ili kuzalisha tani 17,400 za unga wa mahindi na tani 4,350 za pumba za mahindi kwa ajili ya chakula cha mifugo; itasindika tani 15,000 ili kuzalisha lita 3,461,000 za mafuta ya alizeti na tani 10,350 za mashudu ya alizeti. Vilevile, Bodi itakoboa tani 27,000 za mpunga zitakazozalisha tani 8,100 za mchele na tani 4,000 za pumba za mpunga; na itanunua na kuuza mazao ghafi baada ya kusafishwa na kufungashwa. Wizara pia, itakamilisha ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati katika Mikoa ya Kagera, Mara na Shinyanga (Kahama).

137. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Mradi wa TANIPAC itajenga kituo cha mfano cha kusambaza teknolojia za usimamizi wa mazao baada ya mavuno (Post-harvest Center of Excellence) na Maabara Kuu ya Kilimo (Central Agriculture Reference Laboratory). Aidha, mradi huo utakarabati na kukipatia vifaa Kituo cha Udhibiti wa Magonjwa ya Kibaolojia cha Kibaha (NBCU) na ujenzi wa ghala 14. Mradi pia utazijengea uwezo Taasisi za TFDA, TBS, ZBS na vituo vya utafiti wa Kilimo vya Ilonga, Naliendele na Zanzibar kuhusu udhibiti wa sumukuvu kwa kununua vifaa vya maabara na kutoa mafunzo na teknolojia kuhusu udhibiti wa sumukuvu.

5.6 Vituo vya Utafiti huduma za Ugani na Mafunzo

Kuimarisha Vituo vya Utafiti

138. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaboresha na kuimarisha miundombinu ya utafiti kwa kukarabati ofisi na kuvipatia vifaa muhimu vituo vinne (4) vya utafiti vya Ukiriguru, Ilonga na Tumbi. Wizara pia, itaboresha miundombinu ya mashambaya uzalishaji wa mbegu kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora. Aidha, miundombinu ya umwagiliaji ya vituo vya utafiti vya Ilonga, Naliendele, Ukiriguru na miundombinu ya uhifadhi wa mbegu katika vituo vya Uyole, Ilonga na Seliani itaboreshwa. Vilevile TARI itaimarishwa ili iweze kujikita zaidi kwenye utafiti na uzalishaji wa mbegu za michikichi.

Huduma za Ugani

139. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Sekta binafsi itakamilisha Mwongozo wa Utoaji na Usimamizi wa Huduma za Ugani Kilimo ili kuendana na mahitaji ya sasa ya utoaji wa huduma za ugani nchini. Aidha, Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata na Vituo vya Mafunzo kwa Wakulima vitaedelea kutoa mafunzo kwa wakulima kulingana na mazao yanayolimwa kwenye kanda husika. Vilevile, Wizara itaendelea kuratibu maonesho ya kilimo (Nane Nane) yatakayofanyika katika Kanda nane (8) za maonesho. Pia, Wizara itatoa mafunzo kwa wakulima viongozi katika skimu 20 kuhusu masoko na watunzaji wa mghala kuhusu usimamizi wa mazao ghalani. Vilevile, wakulima viongozi kutoka katika skimu 35 watapewa mafunzo kuhusu uvunaji, uhifadhi na usindikaji wa mpunga.

140. Mheshimiwa Spika, Wizara pia kwa kushirikiana na TAMISEMI pamoja na Wadau wengine itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima katika Halmashauri zote nchini kwa kutumia mbinu shirikishi ikiwa ni pamoja na mashamba darasa, ziara za mafunzo, vipeperushi, Mifumo ya TEHAMA, vipindi vya televisheni, redio na majukwaa ya watoa huduma za ugani. Vile vile , Wizara kupitia Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji katika zao la mpunga (ERPP), itaandaa siku ya wakuli ma kwa kushirikisha wakulima 280 kutoka katika skimu 10 za umwagiliaji za Mkoa wa Morogoro katika Halmashauri sita (6) zinazotekeleza kilimo shadidi na itaendesha mafunzo ya kilimo shadidi kwa wakulima viongozi 320 kutoka katika skimu 40 za umwagiliaji.

Vyuo na Vituo vya Mafunzo ya Kilimo

141. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara itadahili wanafunzi 2,500 ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa ufadhili wa Serikali. Vilevile, itakarabati miundombinu ikiwa ni pamoja na madarasa sita (6), ofisi (12), mabweni (12), maktaba sita (6) na mabwalo ya chakula sita

(6) katika vyuo vya mafunzo ya kilimo vya Mtwara, Igurusi, HORTI Tengeru, Tumbi, Mlingano na Maruku. Wizara pia itawezesha mafunzo ngazi ya Shahada ya Uzamili kwa watumishi 11 na ngazi ya Shahada ya Kwanza kwa watumishi wawili (2) katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA).

5.7 Kuimarisha Ushirika

142. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaimarisha udhibiti na usimamizi wa vyama vya ushirika; kuhamasisha wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Mazao kuanzisha SACCOS 1,500 kwenye maeneo yao; kuimarisha masoko, uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi; na Kuhuisha Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 na kuipitia upya Sheria za ushirika.

5.8 Uratibu, Takwimu, Ufuatiliaji na Tathmini

143. Mheshimiwa Spika, Wizara katika mwaka 2019/2020, itakusanya takwimu za gharama za uzalishaji wa mazao ya kilimo, pembejeo na zana za kilimo, uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta na mazao ya bustani. Wizara pia, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar itafanya Sensa ya kilimo. Vilevile, itaendelea kutoa taarifa za hali ya uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini kwa kufanya tathmini mbili (2) za hali ya chakula nchini na kuwajengea uwezo wataalam wa kilimo ngazi ya wilaya katika Halmashauri zote nchini kuhusu ukusanyaji wa takwimu na taarifa hizo muhimu za kilimo kuunganishwa.

5.9 Upimaji wa Matabaka na Ubora wa Udongo

144. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuhimiza na kusimamia matumizi bora ya ardhi ya kilimo kwa kutathmini mashamba yenye hati ambayo yametelekezwa katika mikoa ya Morogoro, Mtwara, Lindi, Pwani, Tanga, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro, Arusha na Manyara kwa lengo la kushauri namna ya kuyaendeleza

. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya za mikoa ya Rukwa, Katavi, Lindi, Kigoma, Mtwara, Morogoro, Songwe, Mbeya na Kagera Wizara itafanya utambuzi wa maeneo mapya ya kilimo kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha kibiashara na kuwezesha Vijana kujiajiri katika kilimo.

145. Mheshimiwa Spika, Wizara pia kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, itapima na kuwezesha upatikanaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila pamoja na kufanya tathmini ya ubora wa udongo na kuandaa ramani za udongo kwenye maeneo ambayo ardhi ya kilimo imetambuliwa kwa ajili ya vijana katika Halmashauri za wilaya za Singida na Morogoro. Vilevile, tathmini hiyo itafanyika katika vijiji vinavyozunguka mashamba ya uwekezaji katika Bonde la Mto Rufiji (Lukulilo, Muhoro na Tawi), Mkulazi, Pangani, Kitengule na Bagamoyo. Taarifa na ramani hizo zitasaidia kuchagua mazao yatakayolimwa pamoja na matumizi sahihi ya mbolea. Vilevile, tathmini ya uharibifu wa ardhi unaotokana na shughuli za Kilimo utafanyika katika Halmashauri za Wilaya za Mpwapwa, Kongwa, Chamwino, Bahi na Kondoa.

5.10 Masuala Mtambuka

Ushiriki wa Vijana na makundi mengine katika kilimo

146. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara itafuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mkakati wa Vijana wa Kushiriki katika Kilimo. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta na wadau wa maendeleo kutoa mafunzo na kuwaunganisha vijana na taasisi za fedha ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu na hivyo vijana kuwekeza kwenye kilimo kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa chakula na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira. Wizara pia itayashirikisha katika kilimo makundi mengine muhimu ya jamii wakiwemo wastaafu wenye weledi mkubwa katika kilimo ili uzoefu na elimu yao katika kilimo uweze kutumika vizuri na kusaidia katika mapinduzi makubwa ya kilimo yanayoendelea nchini.

Lishe

147. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Kilimo itaendelea kushirikiana na Wizara, Taasisi na Washirika wa Maendeleo wa lishe kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Lishe (NMNAP). Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuhamasisha uzalishaji, usindikaji na kuhimiza matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ili kuimarisha hali ya lishe katika ngazi ya kaya kwa mikoa ya Ruvuma, Kagera, Iringa, Mbeya, Songwe, Njombe, Dodoma, Morogoro, Mtwara, Rukwa na Tanga.

Jinsia

148. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020 Wizara itaboresha utafiti unaozingatia masuala mtambuka ya kijinsia (gender mainstreaming) kwa kuelimisha wataalamu na wakulima umuhimu wake katika miradi kwa manufaa ya wakulima wa jinsia zote na kuongeza upokeaji wa teknolojia kwa mazao 8 ya kipaumbele kwa ASDP II.

Mazingira

149. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuwajenge a uwezo wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo kinachohifadhi mazingira katika vijiji 31vinavyozunguka Ziwa Manyara. Vilevile, itasambaza nakala 420 za Mwongozo wa Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Halmashauri za Wilaya za Mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Mara Manyara, Geita, Simiyu, Kagera, Kigoma, Njombe, Songwe, Rukwa na Katavi. Pia itafuatilia ujumuishwaji wa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya Kilimo katika Halmashauri za Wilaya za mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Kilimanjaro, Tanga, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Mara, Manyara, Geita, Simiyu na Kagera.

VVU na UKIMWI

150. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuwahudumia watumishi walioathirika na kutoa

elimu kuhusu VVU na UKIMWI ili kupunguza maambukizi mapya kwa watumishi 1,000 wa Wizara.

5.11 Maeneo Maalum ya Maboresho katika Kilimo

151. Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie maeneo machache ambayo kama Wizara tumeona ni muhimu kuyafanyia maboresho ili kuuimarisha usimamizi wa kilimo na kuwapatia wakulima huduma kwa urahisi zaidi. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

Mapitio ya Sera na Sheria

152. Mheshimiwa Spika, Wizara imeanza kazi ya kuipitia Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013 kwa lengo la kubaini maeneo ambayo yatapaswa kuhuishwa ili kwenda na hali halisi ya sasa na mwelekeo wa Serikali wa kubadili kilimo chetu kuwa kilimo cha kibiashara kwa kasi zaidi. Sanjari na mapitio hayo ya sera, sheria mbalimbali zimeanza kupitiwa ili kubaini namna zinavyotekelezeka na kama baadhi zinawe za kuunganishwa. Mapitio hayo pia yataiwezesha Wizara kuangalia uwezekano wa Kutunga Sheria moja yenye nguvu itakayosimamia Kilimo kwa upana wake. Mtazamo wa Wizara ni kuwa na Sheria itakayotoa mwelekeo wa usimamizi wa rasilimali watu katika Sekta ya Kilimo, usimamizi wa matumizi bora ya pembejeo, usimamizi wa ardhi ya kilimo, pamoja na masuala mengine muhimu.

153. Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya mapitio ya sheria zilizopo, Wizara itaandaa mapendekezo ya muswada wa kutunga Sheria ya Kilimo na kuiwasilisha katika Bunge lako Tukufu. Vilevile, Wizara itaendelea kufanya uchambuzi wa ada na kodi hususan kwenye vifungashio na vifaa vinavyotumika katika uhifadhi wa mazao ili kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tutaendelea kushirikiana kwa karibu sana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji pamoja na Bunge zima katika safari hii ya kuboresha Sera na Sheria zetu za Kilimo.

Bima ya Mazao

154. Mheshimiwa Spika, Kilimo ni moja ya maeneo yenye changamoto kubwa ya kupata hasara katika uwekezaji kutokana na masuala mbalimbali ikiwemo ukame, mafuriko, magonjwa na wadudu waharibifu wanaoweza kuharibu mazao. Changamoto hizo zinasababisha taasisi za fedha kutotoa kipaumbele cha kutosha kutoa mikopo kwenye Kilimo. Katika kukabiliana na changamoto hizo, nchi nyingi duniani zimeanzisha na kutekeleza mfumo wa Bima ya Mazao. Mfumo huo humwezesha mkulima kulipwa fidia pale anapopata hasara na pia kumwezesha kupata mkopo kutoka vyombo vya fedha kwa urahisi. Kutokana na ukweli huo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanza mchakato wa kuanzisha Bima ya Mazao hapa nchini.

155. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kuanzia imefanya vikao na wadau mbalimbali ili kufanya maandalizi ya awali ya kuanzisha utaratibu wa Bima ya mazao kwa kuanza na baadhi za mazao na maeneo machache. Maandalizi hayo yanaendelea kufanyika ili katika mwaka 2019/2020 tuwe angalau na aina mbili za mifumo ya Bima ya mazao (Products) inayoweza kutumika nchini. Hata hivyo, ili utaratibu huu uwezekane, kutahitajika takwimu sahihi za hali ya hewa pamoja na uzingatiaji wa kanuni bora za kilimo. Hivyo, kunahitajika ushirikiano wa karibu na Mamlaka ya Hali ya Hewa pamoja na maafisa ugani kutimiza wajibu wao kikamilifu.

Usajili wa wakulima

156. Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema hapo awali, tulianza zoezi la kuwatambua, kuwasajili na kuwapatia vitambulisho wakulima wetu. Tumeanza zoezi hilo kupitia mazao makuu ya biashara yanayosimamiwa na Bodi za Mazao ambapo zoezi hilo litakamilika Juni, 2019. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaimarisha kanzidata ya wakulima na kuendelea na usajili wa wakulima wa mazao mchanganyiko kwa kushirikiana kwa karibu sana na Vyama vya Ushirika na Taasisi nyingine za wakulima kama vile Tanganyika Farmers Association (TFA). Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kuhamasisha wakulima katika maeneo yetu ili watakapofikiwa na zoezi la uandikishaji watoe ushirikiano na waelewe kwamba zoezi hili ni la kuwasaidia kupata huduma bora za Kilimo.

Masoko ya Mazao ya Kilimo

157. Mheshimiwa Spika, Wahe shimiwa wabunge watakubaliana na mimi kwamba, upatikanaji wa masoko ya uhakika wa mazao ya kilimo ni moja ya kichocheo kikubwa kwa mkulima kuzalisha zaidi. Pale soko la uhakika linapopatikana na bei kuwa ya kuridhisha, uzalishaji huongezeka. Kwa upande mwingine, wakulima wanapokosa masoko ya uhakika au bei inapokuwa ya chini huwakatisha tamaa na hivyo kupunguza uzalishaji katika misimu inayofuata. Hata hivyo, tunaelewa kwamba soko la uhakika linategemea pia uhakika wa upatikanaji wa mazao wanayohitaji wanunuzi na yenye ubora wa kutosha

158. Kwa kutambua umuhimu wa masoko, Wizara imeamua kuimarisha utafutaji wa masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itakiimarisha kitengo cha masoko kwa kukijengea uwezo wa kufanya uchambuzi na utafutaji wa masoko ndani na nje ya nchi. Aidha, elimu itaendelea kutolewa kwa wakulima ili wawe ze kuzalisha mazao bora yanayohitajiwa sokoni pamoja na kuwaunganisha wakulima moja kwa moja na masoko. Vilevile, tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na taasisi

nyingine zinazohusika na masoko nchini ikiwemo TANTRADE na Soko la Bidhaa (TMX).

Mfumo wa upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo

159. Mheshimiwa Spika, Wizara imeanza zoezi la kupitia kwa kina mifumo iliyopo ya uzalishaji, uagizaji na usambazaji wa mbegu, mbolea na viuatilifu. Mifumo iliyopo kwa sasa inatofautiana kwani kuna baadhi ya Bodi za Mazao zinazojihusisha na uagizaji na usambazaji wa pembejeo, wakati mwingine Vyama vya Ushirika vinaagiza na kusambaza pembejeo kwa wanachama wao, wakulima pia hununua pembejeo moja kwa moja kutoka kwa wafanyabishara na pia mbolea kwa sasa inaagizwa kwa mfumo wa pamoja (Bulk Procurement).

160. Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa pembejeo na kilimo na tofuati ya mifumo hiyo, tumeamua kuipitia yote ili kuona mfumo bora unaoweza kutumika kuhakikisha pembejeo zenye ubora zinapatikana na kusambazwa kwa wakulima kwa wakati. Malengo yetu ni kukamilisha mapitio hayo na kupata majawabu ya mfumo bora ifikapo Juni 2019, ili mwaka 2019/2020 tuwe na mfumo madhubuti utakaokuwa na tija kwetu sote. Nina uhakika kwamba, mfumo mzuri wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo utawezesha uwepo wa pembejeo bora kwa bei nafuu na hivyo kuongeza matumizi kwa wakulima wetu.

6.0 SHUKRANI

161. Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu naomba nitoe shukrani za dhati kwa taasisi, makundi, na wadau mbalimbali tunaoshirikiana kuendeleza kilimo cha Tanzania. Kwanza, ninawashukuru sana, Naibu Mawaziri wa Kilimo, Mhe. Omary Tebweta Mgumba (Mb.) na Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb.) kwa ushirikiano wanaonipatia katika kuteke le za majukumu yangu. Napenda pia, kuwashukuru Katibu Mkuu, Mhandisi Mathew John Mtigumwe; Naibu Katibu Mkuu Prof. Siza D. Tumbo; Wakurugenzi wa Idara na Wakuu wa Vitengo; Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote wa Wizara; na

wadau wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowe ze sha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 pamoja na kuandaa Hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba, nitaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2019/2020.

162. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuz ishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Vietnam, Canada na Poland.
Ninayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, ILRI na CABI. Nyingine ni AVRDC, AGRA, CIP, CIAT/ PABRA, UNEP, WARDA, Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO-EA) na HELVETAS. Wadau wengine ni Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu (IRLCO-CSA), Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust, Rockfeller Foundation, Aga Khan Foundation, Unilever na Asasi zisizo za kiserikali nyingi ambazo hatuwezi kuzitaja zote hapa.

163. Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Vwawa kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, napenda kuwahimiza kufanya kazi kwa bidii ili kuleta maendeleo ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Kwa umuhimu wa kipekee ninatoa shukrani za dhati, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

7.0 MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2019/2020

164. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara inaomba idhini ya kukusanya maduhuli ya Shilingi **3,472,515,000** yatokanayo na vyanzo mbalimbali vya mapato.

165. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Kilimo inaomba kutumia jumla ya Shilingi **253,856,943,970** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 kama ifuatavyo:-

FUNGU 43 – Wizara ya Kilimo

166. Mheshimiwa Spika, jumla ya Shilingi 208,044,783,140 zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **143,577,036,140** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo Shilingi **82,000,000,000** ni fedha za ndani na Shilingi **61,577,036,140** ni fedha za nje. Aidha, Shilingi **64,467,747,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi **13,214,159,060** ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara, Shilingi **29,621,801,490** ni kwa ajili ya mishahara ya Bodi na Taasisi, Shilingi **11,453,309,490** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Wizara na Shilingi **10,178,476,510** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Bodi na Taasisi.

FUNGU 05 – Tume ya Umwagiliaji

167. Mheshimiwa Spika, jumla ya Shilingi **37,485,090,830** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **32,501,462,613** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi **3,000,000,000** ni fedha za ndani na Shilingi **29,501,462,613** ni fedha za nje. Aidha, Shilingi **4,983,628,217** zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi **4,098,444,217** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Tume na Shilingi **885,184,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

FUNGU 24 – TUME YA USHIRIKA

168. Mheshimiwa Spika, jumla ya Shilingi **8,327,070,000** zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi **6,127,370,000** kwa ajili ya mishahara na Shilingi 2,199,700,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

8.0 HITIMISHO

169. Mheshimiwa Spika, Pamoja na hotuba vipo viambatisho vinavyotoa ufafanuzi wa baadhi ya maeneo.

Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Kilimo, www.kilimo.go.tz. Ninaomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

***170. Mheshimiwa Spika,* NAOMBA KUTOA HOJA**

MWENYEKITI: Tunaendelea. Tumsikilize Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Sawa, namwona Makamu wake Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, una muda usiozidi dakika 30. Karibu.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwasilishe Taarifa na Maoni ya Kamati ya Wizara ya Kilimo. Naomba Taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo kwenye vitabu vyenu vya Taarifa ya Kamati mlivyogawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa maana ya Fungu 43 - Wizara ya Kilimo; Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika; na Fungu 05 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia maelezo hayo ya utangulizi, Taarifa hii inafafanua mambo matano yafuatayo:-

(1) Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

(2) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

(3) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

(4) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020; na

(5) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipochambua maombi ya fedha kwa Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, ilitoa ushauri kwenye maeneo takribani 18.

Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Kamati haijaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kutekeleza baadhi ya ushauri wa Kamati kutokana na ukweli kwamba majibu ya Serikali kuhusu hoja zilizotolewa na Kamati yamekuwa yakijirudia kila mara bila ya kuonesha hatua mahsusi zinazochukuliwa kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa tatu hadi wa nne kwenye kitabu cha Taarifa ya Kamati mliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya majibu yaliyotolewa na Wizara ni kuwa Mipango iliyopangwa na Wizara ni mizuri, wataalam wa kutekeleza mipango hiyo wapo, tatizo ni ukomo wa Bajeti inayopewa Wizara. Bajeti inayotengewa ni ndogo kuweza kutekeleza mipango iliyoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, umeainishwa kwa kirefu kuanzia ukurasa wa sita hadi 12 kwenye kitabu cha Taarifa ya Kamati mliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara kupitia mafungu yake matatu, Kamati imebaini yafuatayo:

(i) Wizara ya Kilimo - Fungu 43; Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa kwa Sekta ya Kilimo ni ya muda mrefu na haijakamilika;

(ii) Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - Fungu Na.5; miradi ya maendeleo kwa Fungu Na.5 imetekelezwa kwa fedha za wadau wa maendeleo ambao wametoa asilimia 26 ya fedha zilizotengwa na Bunge na hakuna fedha yoyote ya ndani iliyotolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo; na

(iii) Tume ya Maendeleo ya Ushirika - Fungu 24; hakukuwa na fedha za miradi ya maendeleo iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo ya ushirika nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Bajeti ya Uchambuzi wa Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2019/2020, umeandaliwa kwa kuzingatia masuala mbalimbali yaliyoainishwa kuanzia kipengele (a) hadi (g) kama yalivyoainishwa kwenye ukurasa wa 13 hadi 14 na ufafanuzi wa baadhi ya vipengele vya mpango yamefafanuliwa kwenye ukurasa wa 14 hadi 15 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo unajumuisha mafungu matatu ambayo yatatekeleza malengo na mikakati 13 ambapo kipaumbele kimewekwa katika maeneo yaliyoko kwenye kipengele namba moja hadi 13 kama yalivyoainishwa kwenye Taarifa ya Kamati katika ukurasa wa 16 hadi 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza maeneo hayo ya vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Kilimo, kupitia Fungu 43 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 208,044,783,140, Fungu 24 linaomba kuidhinishiwa shilingi 8,327,070,000 na Fungu 05 linaomba kuidhinishiwa shilingi

37,485,090,830. Kwa ujumla Wizara ya Kilimo, kupitia Mafungu yote Matatu Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 253,856,943,970. Aidha, Wizara kupitia Fungu 43 na Fungu 05 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 inatarajia kukusanya jumla ya maduhuli kiasi cha shilingi 3,487,515,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, kamato imebaini yafuatayo:-

Kuongezeka kwa Bajeti ya Wizara ya Kilimo (Fungu 43) kwa asilimia 28, ongezeko hili linadhihirisha adhima ya Serikali ya kuendelea kukuza kilimo na kukifanya Kilimo cha Tanzania kuwa kilimo cha biashara badala ya kilimo cha kujikimu na hivyo kuongeza tija. Hata hivyo, juhudi zaidi zinahitajika katika kuongeza bajei ya Wizara ya Kilimo ili kufikia na kutekeleza Azimio la Maputo na Malabo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhamishwa kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwenye Wizara ya Kilimo kuanzia mwaka huu wa fedha ni utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati, kwani itarahisisha uratibu, usimamizi na kuhuisha shughuli za Umwagiliaji na Kilimo na hivyo Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itapewa kipaumbele tofauti na ilivyokuwa chini ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Mpango wa Bajeti ya Wizara utajielekeza kwenye kilimo kitakachohakikisha usalama wa chakula ili kukabiliana na tatizo la njaa na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda. Kamati katika tathmini yake imebaini changamoto mbalimbali zinazoweza kukwamisha utekelezaji wa malengo ya Wizara. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i. Upungufu wa akiba ya chakula kutokana fedha ndogo zilizotengwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Chakula.

ii. Serikali kutotoa kiuatilifu aina ya *Sulphur* pamoja na vifungashio vya korosho (magunia) kwa njia ya ruzuku kama ilivyokuwa kwa Msimu wa Kilimo wa mwaka 2017/2018.

iii. Kukosekana kwa uhakika wa upatikanaji wa masoko ya mazao ya jamii ya mikunde (mbaazi, choroko, dengu) pamoja na nafaka (mahidni, mtama, ulezi na uwele), pamoja na mazao ya mizizi (mihogo).

iv. Kuchelewa kupatikana kwa mbolea kwa wakati na isiyo na ubora, kuwepo kwa viuatilifu bandia na vilivyokwisha muda wake pamoja na mbegu zisizo na ubora.

v. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati (Pamba, Tumbaku, Chai, Kahawa, Pareto, Miwa, na Mkonge).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati. Naomba sasa kuwasilisha maoni na mapendekezo 10 ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usambazaji wa Pembejeo Aina ya *Sulphur* Isiyo na Ubora Kwenye Mikoa Inayolima Korosho. Katika kutekeleza majukumu yake Kamati imebaini kuwepo kwa Pembejeo zisizo na ubora zaidi ya tani 400,000 zilizogunduliwa na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu *(TOSCI)* na Ofisi ya Mkemia Mkuu. Kamati inazipongeza Taasisi hizo kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kubainika kwa Pembejeo hizo, Kamati inaishauri Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu na za kisheria wote waliohusika kuingiza nchini pembejeo zisizo na ubora na kupelekea madhara kwenye uzalishaji wa mazao, kwa mfano korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja ya kazi nzuri inayofanywa na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu *(TOSCI)* bado kuna changamoto ya uwepo wa mbegu feki, yaani zisizokuwa na ubora inayochangiwa pamoja na mambo mengine na upungufu wa Watumishi hasa Wakaguzi wa mbegu ikilinganishwa na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuipatia Taasisi hii wafanyakazi wa kutosha watakaosaidia kufanya ukaguzi wa

mbegu kwa wakati na hivyo kuzuia mianya ya uingizaji wa mbegu zisivyo na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tathimini ya Msimu wa Ununuzi wa Korosho wa Mwaka 2018/2019. Kama tunavyofahamu Msimu wa Korosho wa Mwaka 2018/2019 ulikuwa wa kusuasua kulikofanywa na wafanyabiashara au wanunuzi wa korosho ghafi na kupelekea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuagiza korosho zote za msimu wa mwaka 2018/ 2019 kununuliwa na Serikali kupitia uratibu wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza uamuzi huo wa Serikali kununua korosho kwani maamuzi hayo yalisaidia kuongeza bei ya korosho kutoka bei elekezi ya shilingi 1,650 kwa kilo hadi shilingi 3,300 na hivyo kuwawezesha wakulima wa korosho kunufaika na kazi za mikono yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya Serikali kuwasaidia wakulima wa korosho, Kamati imebaini kuwa zoezi zima la ununuzi wa korosho limekabiliwa na changamoto zifuatazo: -

Zoezi la uhakiki kuwagawa wakulima sehemu mbili na kupelekea baadhi ya wakulima kuchelewa kulipwa fedha zao na wengine kutolipwa kabisa hadi leo. (Makofi)

Uhaba wa wataalam wa uhakiki na wasio na uzoefu kwenye sekta ndogo ya korosho na hivyo kupelekea uhakiki wa wakulima kuchukua muda mrefu na hasa wakulima wenye kilo zaidi ya 1,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imejiridhisha kuwa Mfumo wa Kangomba unasababishwa na changamoto za wakulima zinazoambatana na gharama kubwa za kuandaa mashamba, kupalilia pamoja na bei kubwa za viuatilifu na mbolea. Gharama ambazo wakulima wa kawaida hawawezi

kuzimudu hivyo kuingia mikataba ya kupata fedha zitakazosaidia kuhudumia mashamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuvunjwa kwa Bodi ya Korosho. Kukosekana kwa Bodi ya Korosho kumepelekea wakulima kukosa namna ya kukutana na kujadili matatizo yao yanayohusu sekta ndogo ya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tano, Kukwama kwa Juhudi za Serikali Kutafuta Wanunuzi wa Korosho Zilizorundikana Kwenye Maghala Mbalimbali Nchini. Kushindwa kwa Serikali kuuza korosho iliyoinunua kumepelekea kujaa kwa maghala ya kuhifadhia korosho na hivyo inatarajiwa kukosekana kwa maghala ya kuhifadhia korosho zitakazozalishwa kwenye Msimu mpya wa Korosho unaotegemea kuanza hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la sita ni kuchelewa kukamilika kwa zoezi la uhakiki ambako kumetokana pia na Wizara kutotekeleza wajibu wake ipasavyo kwa kutokuwa na Mfumo wa Usajili wa Wakulima na hivyo kupelekea mashamba kuhakikiwa wakati korosho zimeshavunwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Namba Saba ni Uwezo Mdogo wa Viwanda vya Ndani Kubangua Korosho Inayozalishwa Nchini. Kufuatia changamoto zilizobainika, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba moja, Serikali kufanyia kazi changamoto zilizobainika kwenye Msimu wa Ununuzi wa korosho wa mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kuboresha Sekta ndogo ya Korosho kwa manufaa ya wakulima wa zao hilo na Taifa kwa ujumla.

Serikali kuunda Bodi ya Korosho mapema iwezekanavyo ili iweze kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Sheria iliyotungwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwa na Mfumo Rasmi wa kuwatambua Wakulima wa mazao yote nchini, hatua itakayosaidia kuwa na takwimu sahihi na idadi kamili ya wakulima kulingana na mazao wanayolima.

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) na Wizara ya Viwanda na Biashara kuharakisha mchakato wa kuwapata wawekezaji watakaojenga viwanda vya kubangua korosho nchini ili nchi iweze kunufaika na mnyororo wa thamani kwa zao hili. *(Makofi)*

Serikali kuwa na Mipango ya muda mfupi na muda mrefu ya kujenga maghala ya kuhifadhia korosho.

Serikali kutafakari upya uamuzi wake wa kuondoa kiuatilifu aina ya *sulphur* kilichokuwa kinatolewa bure kwa wakulima wa korosho kupitia fedha za *Export Levy* na hivyo kusaidia kuongeza uzalishaji wa korosho.

Serikali kuharakisha mchakato wa kuwapata wanunuzi wa korosho ili kuuza korosho zilizoko kwenye maghala mbalimbali ili kupata fedha na kukamilisha zoezi la kuwalipa wakulima ambao hawajalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wake wa busara kwa agizo alilolitoa hivi karibuni alipokuwa kwenye ziara ya kikazi mikoa ya Kusini kwa kuitaka Wizara kuhakikisha wananchi waliohusika na Kangomba wanalipwa fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto zinazovikabili vituo vya utafiti wa Kilimo. Vituo vya utafiti wa kilimo vinakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Changamoto za kibajeti ambapo asilimia 78 ya fedha za utafiti wa vituo zinatokana na fedha za wadau wa maendeleo ambazo huambatana na masharti ya aina ya utafiti unaotakiwa kufanyika, wakati mchango wa Serikali ni

asilimia 22 tu; Ukosefu wa motisha kwa watafiti na wagunduzi; vituo vya utafiti wa kilimo vinafanya kazi nzuri za utafiti, hata hivyo matokeo ya utafiti hayawafikii Wakulima. Utaratibu wa manunuzi ya vichochea (*reagentss*) unachukuwa muda mrefu kwenye upatikanaji wa vibali *(clearance*); Kuchelewa kupatikana kwa Sheria ya Kulinda Haki za Wagunduzi; na uhaba wa watumishi au watafiti ambao wengi wao wamestaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

Kutekeleza uamuzi uliokwishapitishwa ambao unaitaka Serikali kutenga asilimia moja ya Pato Ghafi la Taifa kwa ajili ya utafiti. Kwa kufanya hivyo kutawezesha vituo vya utafiti wa Kilimo kuboresha miundombinu, kununua vifaa vya kisasa vya utafiti pamoja na fedha za kufanyia tafiti mbalimbali. Fedha zinazozalishwa na mazao ya utafiti zisipelekwe kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina badala yake zirudishwe kwenye vituo vya utafiti wa kilimo ili zisaidie kufanya utafiti kwa ajili ya maendeleo ya Sekta ya Kilimo na viweze kujiendesha ikiwezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuharakisha mapema iwezekanavyo mchakato wa Utungwaji wa Sheria ya kulinda Haki za Wagunduzi.

Kuwa na Mpango wa uendelezaji Watumishi/Watafiti ili kuwa na muendelezo wa utumishi mara wengine wanapostaafu. *(Makofi)*

Kuanzisha programu mbalimbali kwenye vipindi vya redio, televisioni, na mitandao ya kijamii kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu matokeo ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Deni la Mawakala wa Pembejeo kwa Msimu wa mwaka 2015/2016. Kamati imepokea malalamiko kutoka kwa mawakala wa pembejeo kuwa tangu wasambaze pembejeo za kilimo kwa msimu wa mwaka 2015/2016 bado Serikali haijawalipa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matokeo ya uhakiki yameonesha kuwa kuna baadhi ya mawakala hawakufanya udanganyifu, Kamati inashauri wale wachache ambao uhakiki umekamilika na hakuna udanganyifu waliofanya walipwe fedha zao na kwa wale ambao uhakiki wao una walakini ndiyo uchunguzi uendelee. Kamati inashauri kuwa ni vyema uchunguzi huo ukakamilika haraka ili kuwawezesha Mawakala kujua hatima yao na kwa wale watakaobainika walifanya udanganyifu hatua za kisheria zichukuliwe ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Umwagiliaji. Wakati wa uchambuzi wa bajeti Kamati ilibaini kuanzia Mwaka wa Fedha 2019/2020 Miradi ya Umwagiliaji itatekelezwa kupitia manispaa na halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kiasi kikubwa cha fedha kinachohitaji, utaalamu na rasilimali watu inayohitajika katika kutekeleza miradi ya umwagiliaji Kamati inashauri Serikali kuwa ni vyema miradi ya umwagiliaji ikaendelea kutekelezwa na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na halmashauri na manispaa ambazo wananchi wake ndio watakuwa watumiaji wa skimu za umwagiliaji ili kuwa na usimamizi wa karibu na kuifanya miradi kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati imebaini kuwa kwa miaka mitatu mfululizo Tume ya Maendeleo ya Ushirika haijawahi kutengewa fedha yoyote ya maendeleo. Maelezo yanayotolewa na Serikali ni kuwa fedha ya maendeleo ya Tume hii inakasimiwa kupitia Fungu 43 ambalo linahusu Wizara ya Kilimo ilhali Tume ya Maendeleo ya Ushirika inafungu lake ambalo ni Fungu 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri fedha za fungu hili zinazohusu miradi ya maendeleo zitengwe kwenye fungu lake ili Tume ya Maendeleo ya Ushirika iweze kupanga na kutekeleza mipango yake pamoja na kuwajibika moja kwa moja kwa fedha iliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti Ndogo Iliyotengwa kwa ajili ya Hifadhi ya Chakula Nchini. Wakati wa uchambuzi wa bajeti Kamati imebaini kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Chakula Nchini *(NFRA)* iliomba shilingi bilioni 66 kwa ajili ya ununuzi wa tani 110,000. Hata hivyo Serikali imetenga shilingi bilioni 15 ambazo zitaelekezwa kwenye ununuzi wa nafaka. Kiasi kilichotengwa ni asilimia 22 ya fedha zilizoombwa ambazo zitawezesha upatikanaji wa tani 28,000 tu. Maelekezo ya Wizara yanaitaka Mamlaka ya Hifadhi ya Chakula Nchini kuuza mahindi ya akiba na kupata fedha kwa ajili ya kufidia mahitaji ya tani zinazohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maboresho ya Sera ya Kilimo na Kuanzishwa kwa Sheria ya Kilimo. Kwa muda mrefu sasa uratibu na usimamizi wa sekta ya kilimo umekuwa wa kusuasua kutokana na kukosekana kwa mwelekeo sahihi unaoendana na hali halisi ya mazingira ya sasa kwenye kilimo. Kwa kutambua changamoto hizo Wizara imeanza mchakato wa kukusanya maoni kuhusu maboresho ya Sera ya Kilimo ya Mwaka 2013 ambayo kwa kiasi kikubwa imeshindwa kutatua matatizo mbalimbali yaliyoikabili sekta ya kilimo. Sambamba na hilo, Wizara iko kwenye mchakato wa kukusanya maoni kwa ajili ya kuanzisha Sheria ya Kilimo ambayo haikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza uamuzi huo kwani maboresho ya Sera ya Kilimo ya Mwaka 2013 itasaidia kuendana na mabadiliko mbalimbali ya kisera na wakati. Aidha, kuanzishwa kwa Sheria ya Kilimo itatoa usimamizi madhubuti na kuwa suluhisho la changamoto zinazomkabili mkulima na sekta ya kilimo kwa ujumla wake. Hivyo Kamati inapongeza uamuzi huo wa Wizara na kusisitiza kuwa mchakato huo ni lazima ukamilike mapema iwezekanavyo na ushirikishe wadau wote muhimu; hatua ambayo itasaidia kupata Sera na Sheria ya Kilimo inayokidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhakika wa Upatikanaji wa Masoko ya Uhakika wa Mazao ya Kibiashara Yanayolimwa Nchini. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati imebaini

kuwa ipo changamoto kubwa ya upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya kimkakati kama vile chai, tumbaku, pamba, kahawa, mkonge, alizeti, muhogo na mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa masoko ya uhakika kumepelekea wakulima wengi kuvunjika moyo kwenye shughuli za kilimo na kusababisha kushuka kwa tija. Kufuatia changamoto hiyo Kamati inaishauri Serikali kuimarisha Vitengo vya Masoko vilivyopo Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara ili viweze kutafuta masoko ya uhakika sehemu yoyote ile ili kuhusu mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dhana ya Uchumi wa Viwanda na Utekelezaji wake, tafiti zinaonesha kuwa asilimia 60 ya malighafi ya viwanda vilivyopo nchini vinategemea malighafi zitokanazo na mazao ya kilimo. Ili Serikali iweze kutekeleza.. ya uchumi wa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, muda wetu ndiyo huo.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho napenda kushukuru kwa kunipa nafasi na napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Naibu Waziri Omari, Mheshimiwa nipende pia kumpongeza kumshukuru Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Japhet Hasunga Mbunge, Naibu Waziri Mheshimiwa Omari Mgumba na Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Mwandisi Mathew Mtigumwe na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati wakiongozwa na Mheshimiwa Mwenyekiti Mheshimiwa Mgimwa pamoja na Wajumbe wengine wote kwa kupitia taarifa hii na kuiweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kumshukuru Katibu wa Bunge ndugu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ya Bunge ndugu Athuman Hussein na Mkurugenzi Msaidizi, Kamati ya sehemu ya Huduma ya Jamii ndugu Dickson Bisile, kwa kusaidia ushauri wa kitaalam na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili, na kuidhinisha makadilio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru.

MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

1.1 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya

Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa maana ya Fungu 43 (Wizara ya Kilimo), Fungu 24 (Tume ya Maendeleo ya Ushirika) na Fungu 05 (Tume ya Taifa ya Umwagiliaji).

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, kufuatia maelezo hayo ya utangulizi, Taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo: -

a) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

b) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

c) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; na

e) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

SEHEMU YA PILI

2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipochambua maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo takribani kumi na nane (18). Sehemu hii itabainisha baadhi ya hoja za Kamati na majibu ya Serikali kama ifuatavyo: -

i) Hoja ya Kamati: Utekelezaji usioridhisha wa Azimio la MAPUTO la mwaka 2003 na badae MALABO, 2004 ambalo linazitaka nchi za Afrika kutenga asilimia 10 ya Pato la Taifa ili kukuza Sekta ya Kilimo kwa asilimia sita ifikapo mwaka 2025.
Majibu ya Serikali: Serikali itaendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Kilimo katika mgao wa fedha kwa kadri fedha itakavyoruhusu.

ii) Hoja ya Kamati: Umuhimu wa upatikanaji wa ubora wa mbolea kupitia Mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja (*fertilizer bulk procurement).*
Majibu ya Serikali: Serikali ipo katika mazungumzo na wawekezaji wanaokuja na mitaji ili wawekeze katika Viwanda vya Mbolea.

iii) Hoja ya Kamati: Mpango wa uzalishaji mbegu za kilimo.
Majibu ya Serikali: Serikali imeendelea kuweka mazingira bora ili kuvutia wawekezaji wakiwemo wazalishaji wa mbegu bora ili kuzalisha mbegu kwa wingi na kwa gharama nafuu.

iv) **Hoja ya Kamati:** Mikakati ya kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa sukari ya uhakika wakati wote na kwa bei nafuu.
Majibu ya Serikali: Serikali inaangalia uwezekano wa kuwa na Mikataba inayofunga na kuwabana wenye Viwanda vya Sukari ili waongeze uzalishaji na kupunguza uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi.

v) Hoja ya Kamati: Mikakati ya Serikali ili kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa Masoko ya Mazao kama mbaazi, korosho, chai, kahawa, pamba na mahindi.
Majibu ya Serikali: Serikali imeandaa mikakati mbalimbali ya kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mbaazi na mazao mengine, mkakati mmojawapo ni kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini ambayo yamewezesha Kampuni kutoka China ijenge Kiwanda cha Kusindika aina zote za jamii ya kunde, korosho, na ufuta.

vi) Hoja ya Kamati: Hatima ya madeni ya wakala wa mbolea za ruzuku.

Majibu ya Serikali: Vyombo vya Ulinzi na Usalama vipo katika uchunguzi. Uchunguzi utakapokamilika taarifa kuhusu malipo ya mawakala zitatolewa.

vii) Hoja ya Kamati: Umuhimu wa uharakishwaji wa mchakato wa ujenzi wa Viwanda vya Mbolea hapa nchini.
Majibu ya Serikali: Serikali ipo katika mazungumzo na wawekezaji wanaokuja na mitaji ili wawekeze katika viwanda vya mbolea.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati haijaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kutekeleza ushauri wa Kamati, Aidha, majibu ya Serikali kuhusu hoja hizo yamekuwa yakijirudia kila mara bila ya kuonyesha hatua mahususi zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, hayo ni baadhi ya majibu ya Wizara kuhusu ushauri uliotolewa na Kamati katika maeneo mbalimbali, tafsiri ya majibu haya ni kuwa Mipango iliyopangwa na Wizara ni mizuri, wataalamu wa kutekeleza mipango hiyo wapo, tatizo ni ukomo wa Bajeti inayopewa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Bajeti inayotengwa ni ndogo kuweza kutekeleza Mipango iliyoainishwa na hii inadhihirishwa na jinsi bajeti ya Serikali inavyofanya vizuri kwenye eneo la mishahara na matumizi ya kawaida. Jambo la kujiuliza ni kuwa hawa Watumishi wa Serikali wanaolipwa mishahara kila mwezi wanatekeleza majukumu gani kama fedha za kutekeleza mipango na mikakati ni kidogo na hazitolewi kwa wakati.

2.1. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019 kwa Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 5 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha na makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi mwezi Aprili, 2019.

2.1.1. WIZARA YA KILIMO - FUNGU 43

a) Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ya Kilimo - **Fungu 43**, liliidhinishiwa jumla ya shilingi **162,224,814,000:00** kati ya fedha hizo shilingi **68,136,440,331.90** ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi **98,119,516,000:00** ni Fedha za Maendeleo, ambapo shilingi **82,000,000,000:00** zilikuwa ni Fedha za Ndani na **16,119,516,000:00** ni Fedha za Nje.

b) Mwenendo wa utoaji Fedha zilizoidhinishwa

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2019 fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa ni shilingi **45,408,960,307.00** ambazo ni sawa na **asilimilia 67 %** ya kiasi kilichoidhinishwa. Kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa zilikuwa shilingi **41,222,224,778.00** sawa na **asilimia 42%** ya fedha zilizoidhinishwa**.** Kati ya Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa shilingi **39,964,621,000.00** ni Fedha za Ndani na shilingi **1,310,923,278.00** ni Fedha za Nje. Aidha, Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa ni sawa na **asilimia 49** ya fedha iliyoidhinishwa na Fedha za Nje zilizotolewa ni sawa na **asilimia 9** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, japokuwa Fedha za Miradi ya Maendeleo za Ndani zilizotolewa ni chini ya **asilimia 50** hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kutoa **asilimia 49** ya Fedha za Ndani kwenye Miradi ya Maendeleo ikilinganishwa na **asilimia 9** zilizotolewa kutoka vyanzo vya nje. Mwenendo huu unaonyesha utayari wa Serikali kujitegemea katika kupeleka maendeleo kwa wananchi wake. Aidha, Kamati inasisitiza umuhimu wa fedha zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge kutolewa kama zilivyoidhinishwa na kwa wakati.

c) Makusanyo ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ya Kilimo Fungu 43 ilikadiria kukusanya Mapato ya shilingi **2,315,010,000**. Hadi kufikia Aprili, 2019 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **1,689,815,058.47** ambayo ni sawa na **asilimia 73%** ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaamini

malengo yaliyowekwa yatafikiwa ifikapo mwisho wa Mwaka wa Fedha mwezi Juni, 2019.

2.1.2. TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA - FUNGU 24

a) Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa na kutolewa

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Tume ya Maendeleo ya Ushirika - **Fungu 24** awali liliidhinishwa jumla ya shilingi **8,048,244,000:00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida tu, kati ya fedha hizo, shilingi **2,199,7000:00** ni Fedha za Matumizi Mengineyo na shilingi **5,848,544:00** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Tume na Watumishi wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO).

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi **608,662,620.00** ziliongezwa kwa ajili ya kulipia madeni ya Watumishi na wazabuni mbalimbali na hivyo kufanya jumla ya pesa iliyoidhinishwa kwa ajili ya Tume ya Ushirika kufikia shilingi **8,656,906,620:00,** Fungu 24 halikutengewa Fedha yoyote ya Maendeleo kwa maelezo kuwa Fedha za Miradi ya Maendeleo zinakasimiwa kupitia Fungu 43. Hadi kufikia Aprili, 2019 kiasi cha shilingi **4,334,854,768.57** zilitolewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo ni sawa na **asilimia 53.86%** ya kiasi kilichoidhinishwa.

2.1.3. TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI - FUNGU 05

a) Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa na kutolewa

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji **- Fungu 05**, liliidhinishiwa jumla ya shilingi **29,767,866,000.00** kati ya fedha hizo shilingi **3,947,408,000.00** ni Fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **25,820,458,000** fedha za maendeleo, ambapo shilingi **6,000,000,000.00** ni Fedha Ndani na **19,820,458,000.00** ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **5,265,635,000.00** Fedha za Nje kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambayo ni sawa na **asilimia 26** na hakuna Fedha yoyote ya Ndani iliyotolewa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Kilimo cha Mvua kimeathiriwa na mabadiliko ya Tabianchi, na kwamba Kilimo cha Umwagiliaji ndio njia pekee na mbadala kwa ajili ya kilimo kitakachosaidia kuchochea malighafi ya viwanda na usalama wa chakula, bado Serikali inashindwa kupeleke fedha yoyote kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Umwagiliaji iliyoainishwa katika Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango Kambambe wa Taifa wa Umwagiliaji ulikuwa ukamilike mwaka 2025 hata hivyo kutokana na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kupewa pesa kidogo za kutekeleza Miradi hiyo na mara nyingine kutopewa fedha kabisa imepelekea kuongezwa kwa muda wa kutekeleza mpango huu hadi mwaka 2035.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa Serikali kutopeleka Fedha za Miradi ya Maendeleo kama zilivyopangwa na kuidhinishwa na Bunge na badala yeke Serikali inaongeza muda wa utekelezaji hauna tija kwa Taifa kwani Tanzania ni nchi inayotegemea kilimo na Sekta ya Kilimo ni muhimu katika kuinua uchumi na kutoa malighafi ya viwanda. Hasa ikizingatiwa kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi yameathiri uzalishaji kwenye kilimo ambacho kwa kiasi kikubwa kinategemea hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, njia pekee ya kuongeza uzalishaji kwenye kilimo ili kuhakikisha usalama wa chakula na malighafi ya viwanda ni Kilimo cha Umwagiliaji ambacho hakipelekewi Fedha ya Miradi ya Maendeleo. Kwa muktadha huu, Kamati ina maoni kuwa uzalishaji wenye tija katika kilimo ni lazima uendane sambamba na kutenga na kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Umwagiliaji.

b) Makusanyo ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - **Fungu 05** ilikadiria kukusanya Mapato ya shilingi **15,000,000.00** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Aprili, 2019 Tume ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **10,440,000.00** ambayo ni sawa na **asilimia 69.*60%*** ya

malengo ya ukusanyaji. Kamati inaamini hadi kufikia tarehe 30 mwezi Juni Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itafikisha malengo ya ukusanyaji wa maduhuli iliyokiwekea.

2.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 98(1) inaitaka Kamati kufanya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. Msingi wa Kamati kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha ni kufanya ukaguzi wa tathimini halisi ya fedha iliyotumika (*Value for Money*) na namna miradi iliyotekelezwa inavyonufaisha wananchi.

Mheshimwia Spika, ili kutekeleza ipasavyo matakwa ya Kanuni ya kanuni hiyo, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Pwani, Mtwara, Lindi, Mwanza na Arusha. Katika ziara hizo Kamati ilibaini Miradi mingi inayotekelezwa kwa Sekta ya Kilimo ni ya muda mrefu na haijakamilika. Kutokamilika kwa Miradi hiyo kunapelekea Miradi hiyo kutofikia malengo na kucheleweshwa kwa matarajio yaliyokusudiwa na hivyo kupelekea thamani ya Fedha katika Miradi hiyo kutofikiwa.
Mheshimiwa Spika, kufuatia maelezo hayo iliilazimu Kamati kutembelea Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Naliendele mkoani Mtwara, Kituo cha Utafiti wa Kilimo Kibaha mkoani Pwani, Kituo cha Utafiti wa Kilimo Ukirigulu - Mwanza na Kituo cha Utafiti Serian – Arusha. Aidha, Kamati pia ilitembelea Viwanda vya kubangua korosho vilivyoko Lindi na Mtwara na kuzungumza na baadhi ya Wakulima wa korosho wa Mikoa hiyo. Ushauri wa Kamati kuhusu maeneo yaliyotembelewa umeambatanishwa kwenye sehemu ya tatu inayohusu maoni na ushauri wa Kamati kwa ujumla wake.

2.4. MPANGO WA BAJETI NA UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 tarehe 25 - 26 Machi, 2019. Mpango ambao umeandaliwa kwa kuzingatia: -

a) Maelekezo yaliyoko kwenye Mwongozo wa Mpango wa Bajeti ya Serikali wa Mwaka 2019/2020;

b) Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025) Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (*Five Year Development Plan Phase* II – FYDP II);

c) Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustanable Development Goals* – SDGs);

d) Mpango wa Uwekezaji katika Kilimo na Usalama wa Chakula Tanzania (*Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan* – TAFSIP);

e) Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013;

f) Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili na;

g) Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2015-2020.

2.4.1 Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/2020

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/2020 vinatokana na maeneo manne ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17- 2020/21 ambapo katika eneo la ukuzaji uchumi pamoja na sekta zingine msisitizo umewekwa katika Viwanda vya Uzalishaji wa bidhaa kwa kutumia malighafi kutoka nchini ambazo kwa kiasi kikubwa zinatokana na kilimo.

2.4.2 Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

Mheshimiwa Spika, Kamati imechambua Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa vipengele saba (7) vilivyoanishwa hapo juu na hususan Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo lengo lake kuu ni kuiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi zenye kipato cha kati na kuondokana na umaskini uliokithiri ifikapo 2025.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine inatazamiwa ifikapo mwaka 2025 nchi yetu itakuwa imepitia katika marekebisho ya kiuchumi kwa kujenga viwanda vya

kisasa zaidi ambavyo vitatumia malighafi zinazopatikana ndani na zinazotokana na mazao ya kilimo na hivyo kuondoa umasikini kwa kuongeza ajira, masoko ya thamani ya mazao ambayo yanalimwa hapa nchini na wananchi wengi waishio vijijini. Aidha, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/2020 ambao umezingatiwa katika uandaaji wa Bajeti umebeba dhima ya **"Kujenga Uchumi wa Viwanda ili kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu ".**[1]

2.4.3 Lengo Namba Mbili la Maendeleo Endelevu ya Dunia

Mheshimiwa Spika, vilevile Bajeti ya Wizara ya Kilimo imeandaliwa kwa kuzingatia lengo namba mbili ambalo ni miongoni mwa Malengo 17 ya Malengo Endelevu ya Dunia, lengo hili limeridhiwa na nchi wanachama za Jumuiya ya Umoja wa Mataifa ambayo Tanzania pia ni mwanachama na linalenga kutokomeza njaa, kuwa na uhakika wa chakula, lishe bora na kukuza kilimo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Lengo Namba MbIli la Maendeleo Endelevu ya Dunia linabainisha kwamba njaa ni tatizo linalotakiwa kuondolewa kwa kushughulikiwa kikamilifu ili kuhakikisha kila kaya au binadamu anafurahia maisha kwa kuwa na uhakika wa kupata chakula cha kutosha, salama na chenye virutubishi sahihi hasa kwa watu maskini. Ili kufanikisha lengo hili ni lazima Kilimo kiboreshwe, kikuzwe na kiwe endelevu ili ifikapo 2030 tatizo la njaa liwe limemalizika.[2]

2.5. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo, unajumuisha Mafungu Matatu ambayo ni: -

(a) Fungu 43 – Wizara ya Kilimo;
(b) Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika; na
(c) Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

---

[1] Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025
[2] Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, kwa Mafungu yote Matatu Wizara imepanga kutekeleza Malengo yenye Mikakati kumi na tatu (13) ambapo kipaumbele kimewekwa katika:-

(i) Kuongeza tija kwenye Kilimo kwa kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo, udhibiti wa visumbufu, matumizi ya zana bora za kilimo na huduma za ugani;

(ii) Ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji;

(iii) Ujenzi wa maghala, masoko na miundombinu ya kuhifadhia mazao ya kilimo**;**

(iv) Kufanya utafiti wa kilimo na kuzalisha teknolojia kwa mazao ya mahindi, muhogo, ngano, michikichi, ufuta, alizeti, pamba na mpunga;

(v) Kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za mazao na kuzisambaza kwa wakulima;

(vi) Kuweka mfumo endelevu wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo nchini;

(vii) Kuboresha maarifa na ujuzi kwa watafiti kupitia mafunzo mbalimbali ili kuwezesha kufanya utafiti kwa weledi na tija;
(viii) Kuanzisha utaratibu wa Bima za Mazao;

(ix) Kuimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa ardhi kuendana na mahitaji ya mazao ya kilimo ki- ikolojia;

(x) Kuimarisha vituo vya tafiti kwa kujenga miundombinu ikiwemo Ofisi ya Makao Makuu ya TARI na kuongeza vitendea kazi vya utafiti;

(xi) Kutoa huduma za ushauri kuhusu utafiti, mafunzo na usambazaji taarifa za kilimo na sayansi shirikishi;

(xii) Kusajili na kuandaa kanzidata ya wakulima na

(xiii) Kuimarisha ushirika.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza maeneo hayo ya vipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2019/ 2020, Wizara ya Kilimo, kupitia **Fungu 43** inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **208,044,783,140:00, Fungu 24** linaomba kuidhinishiwa shilingi **8,327,070,000:00** na **Fungu 05** linaomba kuidhinishiwa shilingi **37,485,090,830:00** Kwa ujumla Wizara ya Kilimo, kupitia Mafungu yote Matatu Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **253,856,943,970:00.** Aidha, Wizara kupitia Fungu 43 na Fungu 05 kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 inatarajia kukusanya jumla ya maduhuli kiasi cha shilingi **3,487,515,000:00.**

2.5.1. Wizara ya Kilimo- Fungu 43

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 **Fungu 43** linaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **208,044,783,140:00** Kati ya Fedha hizo, shilingi **64,105,298,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **143,577,036,140:00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, shilingi **82,000,000,000:00** ni Fedha za Ndani na shilingi **61,577,036,140:00** ni Fedha za Nje. Aidha, Fedha inayoombwa kutekeleza Mipango mbalimbali ya Wizara ni ongezeko la Bajeti la shilingi **45,819,969,140:00** ambalo ni ongezeko la **asilimia 28** ya Bajeti ya Sekta ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

2.5.2. Tume ya Maendeleo ya Ushirika- Fungu 24

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara kupitia **Fungu 24** inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **8,327,070,000:00.** Kiasi kinachoombwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili Miradi ya Maendeleo, Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Fungu 24 zinakasimiwa kupitia Fungu 43 ambalo linahusu Wizara ya Kilimo.

2.5.3. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji- Fungu 05

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara kupitia Tume ya Umwagiliaji - **Fungu 05** inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **37,485,090,830:00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi **4,983,628,217:00** sawa na **asilimia 13.29** ni kwa

ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **32,501,462,613:00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi **3,000,000,000:00** sawa na **asilimia 9.23** ni Fedha za Ndani na shilingi **24,501, 462,613:00** sawa na **asilimia 90.77** ni Fedha za Nje.

2.6. TATHIMINI YA MALENGO KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini Malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020 na kuridhishwa nayo kwa kuwa Mpango huu wa Bajeti umeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele na miongozo ya kitaifa ili kuhakikisha kuwa kilimo kinachangia kutoa malighafi za viwanda ili kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

2.6.1. Kuongezeka kwa Bajeti ya Wizara ya Kilimo - Fungu 43

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Bajeti ya Wizara ya Kilimo imeongezeka kwa kiasi cha shilingi **45,819,969,140:00** ongezeko hili ni sawa na **asilimia 28** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 ya shilingi **162,224,814,000:00** hadi kufikia shilingi **208,044,783,140:00.** Ongezeko hili linadhihirisha adhima ya Serikali ya kuendelea kukuza kilimo na kukifanya Kilimo cha Tanzania kuwa kilimo cha biashara badala ya kilimo cha kujikimu na hivyo kuongeza tija.

2.6.2. Kuhamishwa kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kutoka Wizara ya Maji na kuhamia Wizara ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, Sera ya Umwagiliaji ya Taifa ya mwaka 2010 ilianzishwa kwa lengo la kuhakikisha sekta ya umwagiliaji inatoa mchango unaofaa katika kuongeza tija na uzalishaji katika Sekta ya Kilimo. Tangu kuanzishwa kwa Sera hii ni takribani miaka 9 sasa kilimo cha Tanzania kimeendelea kutokuwa cha uhakika na chenye tija ndogo kutokana na utegemezi mkubwa wa mvua pekee ambayo imeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea duniani kote na kuathiri upatikanaji wa rasilimali maji inayotakiwa kwa uzalishaji wa mazao.

Mheshimiwa Spika, kuhuisha shughuli za Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwenye Wizara ya Kilimo kuanzia mwaka huu wa fedha ni utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati na itarahisisha uratibu, usimamizi na kuhuisha shughuli za Umwagiliaji na Kilimo na hivyo Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itapewa kipaumbele tofauti na ilivyokuwa chini ya Wizara ya Maji.

2.6.3. Tathimini ya Jumla ya Malengo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 Mpango wa Bajeti ya Wizara utajielekeza kwenye kilimo kitakacho hakikisha usalama wa chakula ili kukabiliana na tatizo la njaa na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda. Kamati katika tathimini yake imebaini changamoto mbalimbali zinazoweza kukwamisha utekelezaji wa malengo ya Wizara. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Upungufu wa akiba ya chakula kutokana fedha ndogo zilizotengwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Chakula

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula uliomba kuidhinishiwa shilingi **bilioni 67** kwa ajili ya ununuzi wa **tani 124,000** za nafaka kwa ajili ya Hifadhi ya Akiba ya Chakula kwa ajili ya kukabiliana na dharura zinazoweza kujitokeza kutokana na utabiri wa hali ya hewa unaonyesha upungufu wa mvua na kuchelewa kwa mvua za masika kunaweza kusababisha upungufu wa chakula. Hata hivyo, Serikali imetenga shilingi **bilioni 15** tu, kiasi ambacho ni **asilimia 22** tu ya fedha zilizoombwa ambazo zitawezesha upatikanaji wa **tani 28,000** tu.

Mheshimiwa Spika, ukomo wa Bajeti uliotolewa na Serikali kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula unaweza kusababisha upungufu wa chakula na kuleta athari ya moja kwa moja kwenye Akiba ya Chakula ya Taifa kwani utapunguza uwezo wa Serikali kukabiliana na dharura iwapo itajitokeza.

(b) Serikali kutotoa kiuatilifu aina ya *Sulphur* pamoja na vifungashio vya korosho (magunia) kwa njia ya ruzuku kama ilivyokuwa kwa Msimu wa Kilimo wa Mwaka 2017/2018

Mheshimiwa Spika, kipindi cha Msimu wa Kilimo wa Mwaka 2017/2018 kiuatilifu aina ya *Sulphu*r ambacho ni muhimu kwenye kilimo cha korosho kilitolewa bure kupitia fedha za *Export Levy* na hivyo kusaidia kuongeza uzalishaji wa korosho kwa kiwango kikubwa. Tangu Msimu wa Kilimo wa Mwaka 2018/2019 na 2019/2020 kiuatilifu aina ya *Sulphur* na vifungashio vya korosho ambavyo ni moja ya mahitaji makubwa na muhimu kwa wakulima wa korosho kimekuwa kikipatikana kwa mkulima kujigharamia mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa ruzuku ya Serikali kwenye kiuatilifu aina ya *Sulphur* kumepelekea wakulima wa korosho kununua kiuatilifu hicho kwa bei juu na hivyo kuathiri uzalishaji na kuongezeka kwa gharama kwa wakulima na hivyo kuchochea ulanguzi na kupelekea kuongezeka kwa utaratibu wa "Mfumo wa Kangomba".

(c) Kukosekana kwa uhakika wa upatikanaji wa masoko ya mazao ya jamii ya kunde (mbaazi, choroko, dengu, ufuta, nafaka (mtama, ulezi na uwele), mizizi (mihogo) na mahindi

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa Wizara imefanikiwa kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao hayo kwa kudhibiti visumbufu vya mazao ya mimea, kusambaza teknolojia bora za kilimo, kutoa elimu kuhusu kanuni bora za kilimo, kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo bora za kilimo kwa wakati zikiwemo mbegu bora. Uzalishaji wa mazao hayo umeongezeka kwa kuwa wananchi waliitikia mwito wa Serikali, hata hivyo changamoto kubwa ni kukosekana kwa masoko ya uhakika kwa ajili ya kufanikisha kilimo cha biashara.

(d) Kuchelewa kupatikana kwa mbolea kwa wakati na isiyo na ubora, kuwepo kwa viuatilifu bandia na vilivyokwisha muda wake pamoja na mbegu zisizo na ubora.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kufanya uamuzi wa ununuzi wa mbolea wa pamoja kwa lengo la kuongeza matumizi na upatikanaji wa mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu kwa wakulima wadogo ili kuongeza uzalishaji wenye tija, hata hivyo mfumo huu haujaweza kufikia malengo yaliyokusudiwa kutokana na ukweli kwamba bado mbolea inawafikia wakulima wengi kwa kuchelewa na kwa bei ya juu. Aidha, bado kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa viuatilifu na mbegu bora kwa wakulima na hivyo kuathiri uzalishaji.

(e) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati ya Pamba, Tumbaku, Chai, Kahawa, Pareto, Miwa, na Mkonge.

Mheshimiwa Spika, mipango ya Wizara inaonyesha mikakati ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati kwa kuzalisha miche bora, kuongeza maeneo ya uzalishaji, kufanya majaribio ya aina mpya za mbegu, kuongeza utafiti wa mazao hayo sambamba na kushirikisha Sekta Binafsi katika kuwajengea uwezo wakulima, wasindikaji na kujenga miundombinu ya masoko na hususan ujenzi wa maghala kwa lengo la kupata bei nzuri na kuongeza thamani. Pamoja na mikakati hiyo ya Wizara bado hakuna tija kwenye mazao hayo kutokana na gharama kubwa za uzalishaji, ukosefu wa pembejeo pamoja na kukosekana kwa uhakika wa masoko.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya Fedha kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020. Naomba sasa kuwasilisha maoni na mapendekezo Kumi (10) ya Kamati ambayo ni:

1. Usambazaji wa Pembejeo aina ya *SULPHUR* isiyo na ubora kwenye Mikoa inayolima Korosho

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba zao la Korosho ni miongoni mwa mazao yanaloliingizia Taifa Fedha nyingi za Kigeni, bado Pembejeo muhimu inayotumika kustawisha korosho inaingizwa nchini ikiwa haina ubora unaostahili na hivyo kuhatarisha ustawi wa zao hilo. Katika kutekeleza majukumu yake Kamati imebaini kuwepo kwa Pembejeo zisizo na ubora zaidi ya **tani 400,000**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuhakiki kudhibiti ubora wa pembejeo kwa kuweza kubaini tani hizo **400,000** za Pembejeo zisizo na ubora.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kubainika kwa Pembejeo hizo, Kamati inaishauri Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu na za kisheria wote waliohusika kuingiza nchini Pembejeo zisizo na ubora na kupelekea madhara kwenye uzalishaji wa korosho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kugundulika kwa Pembejeo aina ya *sulphur* kukosa ubora, bado bei ya Pembejeo hiyo imepanda kwa kasi kutoka shilingi **28,000:00** ya Msimu wa korosho wa mwaka **2017/2018** hadi kufikia shilingi **60,000:00** kwa msimu wa korosho wa mwaka **2018/2019.** Kwa ongezeko hili la bei na kwa kuzingatia kuwa Msimu wa mwaka 2017/ 2018 kiuatilifu aina ya *sulphur* kilitolewa bure kupitia fedha za *export levy* inatazamiwa uzalishaji wa korosho utashuka kwa kasi kwa kipindi cha Msimu wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, aidha, kufuatia ongezeko hilo kubwa la bei ya kiuatilifu aina ya *sulphur*, Kamati inashauri Serikali kushirikiana na wadau mbalimbali kuweka mkakati wa kuhakikisha kiuatilifu aina ya *sulphur* inapatikana kwa wakati na kwa bei elekezi. Vile vile ni muhimu kwa Serikali kuimarisha usimamizi wa upatikanaji wa *sulphur* bora na kwa bei nafuu ili kuwa na uhakika wa uzalishaji wa zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, pamoja ya kazi nzuri inayofanywa na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI), bado kuna changamoto ya uwepo wa mbegu bandia (mbegu feki) inayochangiwa pamoja na mambo mengine upungufu wa Watumishi hasa Wakaguzi wa mbegu ikilinganishwa na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuipatia Taasisi hii wafanyakazi wa kutosha watakaosaidia kufanya ukaguzi wa mbegu bora kwa wakati na hivyo kuzuia mianya ya uingizaji wa viuatilifu visivyo na ubora vinavyoingizwa kwa njia za panya.

2. Tathimini ya Msimu wa Ununuzi wa Korosho wa mwaka 2018/2019

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu Msimu wa Korosho wa Mwaka 2018/2019 ulikuwa wa kusuasua kulikofanywa na Wafanyabiashara/ Wanunuzi wa korosho ghafi na kupelekea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuagiza korosho zote za Msimu wa Mwaka 2018/2019 kununuliwa na Serikali kupitia uratibu wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa kushirikiana na Taasisi zingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza uamuzi huo wa Serikali kununua korosho kwani maamuzi hayo yalisaidia kuongeza bei ya korosho kutoka bei elekezi ya shilingi **1,650:00** kwa kilo hadi shilingi **3,300:00** na hivyo kuwawezesha wakulima wa korosho kunufaika na kazi za mikono yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali kuwasaidia wakulima wa korosho, Kamati imebaini kuwa zoezi zima la ununuzi wa korosho limekabiliwa na changamoto zifuatazo: -

a) Zoezi la uhakiki kuwagawa wakulima sehemu mbili zilizohusisha uhakiki wa wakulima wenye korosho za hadi kilo 1,500 na wenye korosho zaidi ya kilo 1,500. Uhakiki wa wakulima wa koshoro zaidi ya kilo 1,500 ambao ndio

wazalishaji wakubwa na wameajiri makundi makubwa ya wananchi umechukua muda mrefu na kupelekea baadhi ya wakulima kuchelewa kulipwa pesa zao na wengine kutolipwa kabisa hadi leo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeshangazwa na utekelezaji wa zoezi hili kwani wakati Serikali inaagiza kununua korosho, Serikali haikutenga madaraja kwenye malipo ya korosho bali iliagiza Watendaji kuhakikisha korosho zote za wakulima zinanunuliwa na Serikali.

b) Uhaba wa Wataalam wa uhakiki na wasio na uzoefu kwenye Sekta ndogo ya korosho na hivyo kupelekea uhakiki wa wakulima kuchukua muda mrefu na hasa wakulima wenye kilo zaidi ya 1,500.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango mkubwa walionao wakulima wakubwa, kwenye uhakiki wakulima waliokutwa na korosho nyingi wameonekana kama watuhumiwa na hivyo kuhitajiwa na Kamati za Ulinzi na usalama za Wilaya kuonyesha mashamba yao na kuthibitisha kuwa wao ni wamiliki halali wa mashamba hayo.

c) Kamati imejiridhisha pasipo shaka kuwa Mfumo wa Kangomba unasababishwa na changamoto za wakulima zinazoambatana na gharama kubwa kuandaa mashamba, kupalilia pamoja na bei kubwa za viuatilifu na mbolea. Gharama ambazo wakulima wa kawaida hawawezi kuzimudu hivyo kuingia mikataba ya kupata fedha zitakazosaidia kuhudumia mashamba yao. Hali hii inatokana na wakulima kukosa usaidizi wa Serikali wakati wa kuandaa msimu mpya wa mazao.

d) Kuvunjwa kwa Bodi ya Korosho, kukosekana kwa Bodi ya Korosho kumepelekea wakulima kukosa namna ya kukutana na kujadili matatizo yanayohusu Sekta ndogo ya Korosho.

e) Kukwama kwa juhudi za Serikali kutafuta wanunuzi wa korosho zilizorundikana kwenye maghala mbalimbali nchini. Kushindwa kwa Serikali kuuza korosho iliyoinunua

kumepelekea kujaa kwa maghala ya kuhifadhia korosho na hivyo inatarajiwa kukosekana kwa maghala ya kuhifadhia korosho zitakazozalishwa kwenye Msimu mpya wa Korosho unaotegemea kuanza hivi karibuni.

f) Kuchelewa kukamilika kwa zoezi la uhakiki kumetokana pia na Wizara kutotekeleza wajibu wake ipasavyo kwa kutokuwa na Mfumo wa Usajili wa Wakulima na hivyo kupelekea mashamba kuhakikiwa wakati korosho zimeshavunwa.

g) Uwezo mdogo wa viwanda vya ndani kubangua korosho inayozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto zilizobainika, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-
(a) Serikali kufanyia kazi changamoto zilizobainika kwenye Msimu wa Ununuzi wa korosho wa mwaka 2018/2019 kuwa funzo kwa ajili ya kuboresha Sekta ndogo ya Korosho kwa manufaa ya wakulima wa zao hilo na Taifa kwa ujumla.

(b) Serikali kuunda Bodi ya Korosho mapema iwezekanavyo ili iweze kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Sheria iliyotungwa na Bunge lako Tukufu.

(c) Kamati inaishauri Serikali kuwa na Mfumo Rasmi wa kuwatambua Wakulima wa mazao yote nchini, hatua itakayosaidia kuwa na takwimu sahihi na idadi kamili ya Wakulima kulingana na mazao wanayolima.

(d) Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu- Uwekezaji na Wizara ya Viwanda na Biashara kuharakisha mchakato wa kuwapata wawekezaji watakaojenga viwanda vya kubangua korosho nchini ili nchi iweze kunufaika na mnyororo wa thamani kwa zao hili.

(e) Serikali kuwa na Mipango ya muda mfupi na muda mrefu ya kujenga maghala ya kuhifadhia korosho.

(f) Serikali kutafakari upya uamuzi wake wa kuondoa kiuatilifu aina ya *sulphur* kilichokuwa kinatolewa bure kwa wakulima

wa korosho kupitia fedha za *Export Levy* na hivyo kusaidia kuongeza uzalishaji wa korosho.

(g) Serikali kuharakisha mchakato wa kuwapata wanunuzi wa korosho ili kuuza korosho zilizoko kwenye maghala mbalimbali ili kupata fedha na kukamilisha zoezi la kuwalipa wakulima ambao hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inampongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wake wa busara kwa agizo alilolitoa hivi karibuni alipokuwa kwenye ziara ya kikazi mikoa ya Kusini kwa kuitaka Wizara kuhakikisha Kangomba wote wanalipwa pesa zao.

3. Changamoto zinazokabili Vituo vya Utafiti wa Kilimo

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati ilitembelea Vituo vya Utafiti vya Naliendele - Mtwara, Kituo cha Utafiti wa Kilimo, Kibaha, Serian - Arusha na Ukirigulu-Mwanza kwa ajili ya kujifunza na kujionea shughuli zinazotekelezwa na Vituo vya Utafiti wa Kilimo nchini na kubaini changamoto mbalimbali zifuatazo:

(a) Changamoto za kibajeti ambapo **asilimia 78** ya Fedha za Utafiti wa vituo zinatokana na pesa za Wadau wa Maendeleo ambazo huambatana na masharti ya aina ya utafiti unaotakiwa kufanyika, wakati mchango wa Serikali ni **asilimia 22** tu;

(b) Ukosefu wa motisha kwa watafiti na wagunduzi wa mbegu;

(c) Vituo vya Utafiti wa Kilimo vinafanya kazi nzuri za utafiti, hata hivyo matokeo ya utafiti hayawafikii Wakulima;

(d) Utaratibu wa manunuzi ya vichochea (*reagentss*) unachukuwa muda mrefu kwenye upatikanaji wa vibali (*clearance*) wakati hizi ni dawa zinazozuia maambukizi ya magonjwa kwa zaidi ya asilimia 50. Kuchelewa kwake kunapelekea kukosekana kwa wakati kwa dawa za kuzuia

maambukizi ya magonjwa na hivyo kuathiri uaandaaji wa mashamba wakati wa Msimu wa Kilimo;

(e) Kuchelewa kupatikana kwa Sheria ya kulinda Haki za Wagunduzi; na

(f) Uhaba wa Watumishi/Watafiti ambao wengi wao wamestaafu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

i) Kutekeleza uamuzi uliokwishapitishwa ambao unaitaka Serikali kutenga asilimia moja ya Pato Ghafi la Taifa (GDP) kwa ajili ya Utafiti kwa kufanya hivyo kutawezesha vituo vya Utafiti wa Kilimo kuboresha miundombinu, kununua vifaa vya kisasa vya utafiti pamoja na fedha za kufanyia tafiti mbalimbali;

ii) Fedha zinazozalishwa na mazao ya utafiti zisipelekwe kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, badala yake zirudishwe kwenye Vituo vya Utafiti wa Kilimo ili zisaidie kufanya utafiti kwa ajili ya maendeleo ya Sekta ya Kilimo;

iii) Kuharakisha mapema iwezekanavyo mchakato wa Utungwaji wa Sheria ya kulinda Haki za Wagunduzi.

iv) Kuwa na Mpango wa uendelezaji Watumishi/Watafiti (*succession plan*), ili kuwa na muendelezo wa utumishi mara wengine wanapostaafu; na

v) Kuanzisha programu mbalimbali kwenye vipindi vya redio, televisioni, na mitandao ya kijamii kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu matokeo ya utafiti.

4. Deni la Mawakala wa Pembejeo kwa Msimu wa Mwaka 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Kamati imepokea malalamiko kutoka kwa Mawakala wa pembejeo kuwa tangu wasambaze

pembejeo za kilimo kwa Msimu wa mwaka 2015/2016 bado Serikali haijawalipa pesa zao.

Mheshimiwa Spika ni takribani miaka minne sasa maelezo yanayotolewa na Serikali ni kuwa madeni ya Mawakala wa Msimu huo yamepelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uhakiki. Aidha, uhakiki unaofanywa unahusisha pia Vyombo vya Dola kwa ajili ya uchunguzi kwa kuwa imethibitika kuna udanganyifu mkubwa kwa baadhi ya Mawakala na bado uhakiki haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matokeo ya uhakiki yameonyesha kuna baadhi ya Mawakala hawakufanya udanganyifu, Kamati inashauri wale wachache ambao uhakiki umekamilika na hakuna udanganyifu waliofanya walipwe pesa zao na kwa wale ambao uhakiki wao una walakini ndio uchunguzi uendelee. Kamati inashauri ni vyema uchunguzi huo ukakamilika haraka ili kuwawezesha Mawakala kujua hatima yao na kwa wale watakaobainika walifanya udanganyifu hatua za kisheria zichukuliwe ili iwe fundisho kwa wengine.

5. Miradi ya Umwagiliaji

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Umwagiliaji inatekelezwa kupitia Fungu 05 lililoko chini ya Wizara ya Kilimo ambapo hapo awali lilikuwa chini ya Wizara ya Maji. Kutokana na umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji katika kuchangia ukuaji wa Sekta ya Kilimo, Kamati ilipendekeza Tume ya Umwagiliaji ihamishiwe Wizara ya Kilimo uamuzi ambao umetekelezwa na Serikali. Pamoja na kutekelezwa kwa ushauri wa Kamati, wakati wa uchambuzi wa Bajeti Kamati ilibaini kuanzia Mwaka wa Fedha 2019/2020 Miradi ya Umwagiliaji itatekelezwa kupitia Manispaa na Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kiasi kikubwa cha Fedha kinachohitaji, Utaalamu na Rasilimali Watu inayohitajika katika kutekeleza Miradi ya Umwagiliaji. Kamati inashauri Serikali kuwa, ni vyema Miradi ya Umwagiliaji ikaendelea kutekelezwa na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na

Halmashauri na Manispaa ambazo wananchi wake ndio watakuwa watumiaji wa skimu za umwagiliaji ili kuwa na usimamizi wa karibu na kuifanya miradi kuwa endelevu.

6. Tume ya Maendeleo ya Ushirika

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati, imebaini kwa miaka mitatu mfululizo Tume ya Maendeleo ya Ushirika japo inawajibu wa kuhakikisha Ushirika unaendelea, haijawahi kutengewa fedha yoyote ya Maendeleo. Maelezo yanayotolewa na Serikali ni kuwa Fedha ya Maendeleo ya Tume hii inakasimiwa kupitia Fungu 43 ambalo linahusu Wizara ya Kilimo, wakati Tume ya Maendeleo ya Ushirika inafungu lake ambalo ni Fungu 24.

Mheshimiwa Spika Kamati inashangazwa na uamuzi huu na inahoji kama kuna ulazima wa Fedha za Maendeleo ya Tume kupitia Fungu 43 wakati inafungu lake, hivyo Kamati inashauri Fedha za fungu hili zinazohusu miradi ya maendeleo itengwe kwenye fungu lake ili Tume ya Maendeleo ya Ushirika iweze kupanga na kutekeleza Mipango yake pamoja na kuwajibika moja kwa moja kwa fedha itakayotengewa**.**

7. Bajeti ndogo iliyotengwa kwa ajili ya Hifadhi ya Chakula Nchini

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa Bajeti, Kamati imebaini Mamlaka ya Hifadhi ya Chakula Nchini (NFRA) iliomba shilingi **bilioni 67** kwa ajili ya ununuzi wa **tani 110,000** hata hivyo Serikali imetenga shilingi **bilioni 15** ambazo zitaelekezwa kwenye ununuzi wa nafaka, kiasi kilichotengwa ni **asilimia 22** ya fedha zilizoombwa ambazo zitawezesha upatikanaji wa **tani 28,000** tu. Maelekezo ya Wizara yanaitaka *Mamlaka ya Hifadhi ya Chakula Nchini (NFRA)*kuuza mahindi ya akiba na kupata fedha kwa ajili ya kufidia mahitaji ya tani zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelekezo hayo ya Wizara, Kamati inatahadharisha juu ya hali halisi ya mwenendo wa soko la mahindi nchini ambapo bei iko chini kiasi cha

kutowezesha Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula kuweza kuzungusha shehena ya mahindi iliyopo kwa tija. Ni vyema Serikali ikaipa **NFRA** kiasi cha fedha ilichoomba kwa ajili ya kununua na kuhifadhi akiba ya kutosha ya mahindi kwa ajili ya kukabiliana na majanga yoyote yatakayojitokeza.

8. Kukamilisha maboresho ya Sera ya Kilimo na kuanzishwa kwa Sheria ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa uratibu na usimamizi wa Sekta ya Kilimo umekuwa wa kusuasua kutokana na kukosekana kwa mwelekeo sahihi unaoendana na hali halisi ya mazingira ya sasa kwenye kilimo. Kwa kutambua changamoto hii Wizara imeanza mchakato wa kukusanya maoni kuhusu maboresho ya Sera ya Kilimo ya mwaka 2013 ambayo kwa kiasi kikubwa imeshindwa kutatua matatizo mbalimbali yanayoikabili Sekta ya Kilimo. Sambamba na hilo, Wizara iko kwenye mchakato wa kukusanya maoni kwa ajili ya kuanzisha Sheria ya Kilimo ambayo haikuwepo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza uamuzi huo kwani maboresho ya Sera ya Kilimo ya Mwaka 2013 itasaidia kuendana na mabadiliko mbalimbali ya kisera na wakati. Aidha, kuanzishwa kwa Sheria ya Kilimo itatoa usimamizi madhubuti na kuwa suluhisho la changamoto zinazomkabili mkulima na Sekta ya Kilimo kwa ujumla wake. Hivyo Kamati inapongeza uamuzi huo wa Wizara na kusisitiza kuwa mchakato huo ni lazima ukamilike mapema iwezekanavyo na ushirikishe Wadau wote muhimu hatua ambayo itasaidia kupata Sera na Sheria ya Kilimo inayokidhi mahitaji ya sasa.

9. Uhakika wa Upatikanaji wa Masoko ya Uhakika wa Mazao ya Kibiashara yanayolimwa nchini

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati imebaini kuwa ipo changamoto kubwa ya upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya kimkakati kama vile Chai, Tumbaku, Pamba, Kahawa, Mkonge, Alizeti, Muhogo na Mahindi.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa masoko ya uhakika kumepelekea wakulima wengi kuvunjika moyo kwenye shughuli za kilimo na kusababisha kushuka kwa tija. Aidha, baadhi ya mazao kama tumbaku yamewekewa ukomo wa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha vitengo vya masoko vilivyoko Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara ili viweze kutafuta masoko ya uhakika sehemu mbalimbali duniani.

10. Dhana ya Uchumi wa Viwanda na Utekelezaji wake

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonyesha kuwa asilimi 60 ya malighafi za viwanda vilivyopo nchini vinategemea malighafi zitokanazo na mazao ya kilimo. Ili Serikali iweze kutekeleza vyema kauli mbiu ya Uchumi wa Viwanda ni vyema ikaongeza Bajeti ya Wizara ya Kilimo na hususan kwenye eneo la uzalishaji wa mbegu na Vituo vya Utafiti wa Kilimo. Aidha, ni muhimu Serikali ikahakikisha kuwa fedha zinatotengwa zinapatikana kwa wakati. Kwa kufanya hivi Kamati inaamini dhana ya Uchumi wa Viwanda itafikiwa na kilimo kitaimarika

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo, Mhe. Japhet Hasunga (Mb), Manaibu Waziri Mhe. Omary Mgumba (Mb) na Mhe. Innocent Bashungwa (Mb), Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Mhandisi Mathew Mtigumwe pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ikichambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara

pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb Mjumbe
4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb "
5. Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani, Mb "
6. Mhe. Katani Ahmad Katani Mb "
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb "
8. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb "
9. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb "
10. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb "
11. Mhe. Lucy Simon Magereli, "
12. Mhe. Justine Joseph Monko "
13. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb "
14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb "
15. Mhe. Pascal Yohana Haonga "
16. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb "
17. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb "
18. Mhe. Devotha Methew Minja, Mb "
19. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb "
20. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb "
21. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb "
22. Mhe. Juma Ali Juma, Mb "
23. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb "
24. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb "
25. Mhe. Anthony Calist Komu, Mb "
26. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb "

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein na Mkurugenzi Msaidizi – Kamati za Sehemu ya Huduma za Jamii, Ndg. Dickson Bisile kwa kuisaidia ushauri wa kitaalam na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kwa namna ya kipekee naishukuru Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Rachel Nyega pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John na

Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa katika hoja ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga Mkono Hoja iliyowasilishwa na Mtoa Hoja muda mfupi uliopita na naomba kuwasilisha.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)
MWENYEKITI,
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,
MIFUGO NA MAJI
17 Mei, 2019

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, tupokee sasa taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Haonga. *(Makofi)*

MHE. PASCAL Y. HAONGA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba hotuba yangu yote iweze kuingia kwenye *Hansard*. kwa heshima kubwa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na afya kuweza kusimama mbele ya adhira hii ili kutoa maoni kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Kilimo, kwa mwaka 2018/ 2019 na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2019/2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Mbozi kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono mimi na chama changu wakati wote ninapoendelea kuwatumikia licha ya changamoto mbalimbali za kisiasa ninazopitia. Kikubwa waelewe kwamba ili dhahabu ing'ae lazima ipitie kwenye moto. Pia waamini kwamba siyo kila

changamoto ninayoipitia lengo lake ni kunidhoofisha bali nyingine zinanijenga au kuniimarisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pole na pongezi kwa Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Esther Matiko na wapiganaji wengine kwa magumu wanayopitia, kitu kikubwa ni kuwa waelewe kwamba gereza au mahabusu siyo kaburi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Chakula Kwa Msimu Ujao Wa Kilimo, takwimu zinaonesha kuwa hali ya upatikanaji wa chakula kwa misimu miwili ya 2017/2018 ilikuwa ni yenye kutia matumiani sana kwani uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2017/2018 ulifikia tani 16,981,974. Na mahitaji ya chakula kwa msimu 2018/19 yalikuwa ni tani 13,569,285 na hivyo kuwa na ziada ya tani 3,322,689. Kwa msimu huu wa 2018/2019 ni dhahiri dalili zimeanza kuonekana mapema kuwa kutakuwa na upungufu mkubwa wa chakula kutokana na kwamba; mbali na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameikumba mikoa ya Kanda ya Kati yenye mikoa ya Morogoro, Dodoma na Singida, na Kanda ya Magharibi kwa maana ya Mikoa ya (Tabora, Katavi na Kigoma) Kanda ya Kaskazini Mikoa ya (Tanga, Kilimanjaro, Manyara na Arusha). Lakini kanda ambayo ni mzalishaji mkubwa wa nafaka hasa mahindi kwa maana ya Mikoa ya (Songea, Njombe, Iringa, Mbeya, Rukwa na Katavi) mvua haikuwa tatizo ila tatizo ni upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na kukosekana kwa soko la kutoa bei nzuri ya mahindi na hivyo kusababisha hasara kubwa kwa wakulima katika msimu uliopita. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo litasababisha kupungua kwa uzalishaji wa mahindi kwa msimu huu wa kilimo. Kimsingi bei nzuri ya soko la bidhaa za mkulima na wepesi wa kuuza bidhaa zao nikichocheo kikubwa kwa wakulima kuendelea kuwekeza kuzalisha bidhaa kwaajili ya jamii ya watanzania na kuuza nje ya nchi ili Tanzania iweze kupata fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameikumba mikoa mingi

hapa nchini na hivyo majira ya mvua kubadilika sana na hivyo kusababisha mimea mingi kuharibika kabla ya kufika wakati wa kuvunwa, ni wazi kuwa mkakati tofauti unahitajika ili kuendelea kukidhi mahitaji ya chakula, na zaidi kufikia soko la bidhaa za kilimo kwenye ukanda wa Afrika Mashariki yaani *(Eastern Africa)* na Ukanda wa Kusini mwa Afrika *(Southern Africa).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitahadharisha Serikali kuchukua hatua madhubuti katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na akiba ya chakula ya kutosha na inachukua hatua stahiki kupunguza madhara yanayoweza kutokana na hali hii ya ukame ambayo imekikumba kilimo kwa msimu 2018/19. Ninaomba kurudia eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitahadharisha Serikali kuchukua hatua madhubuti katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na akiba ya chakula ya kutosha na inachukua hatua stahiki kupunguza madhara yanayoweza kutokana na hali ya ukame ambayo imekikumba kilimo kwa msimu 2018/2019

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Sekta ya Kilimo Uwezo wa kilimo na biashara ya kilimo ni mkubwa sana kwa Tanzania, lakini matarajio lazima yawekwe inavyostahili. Sehemu kubwa ya sekta hii kwa sasa haina uwezo wa kushindana kwa sababu ya gharama kubwa za uzalishaji, hamasa ndogo miongoni mwa wazalishaji kutokana na muingiliano wa serikali hasa kwenye soko, ubora hafifu wa pembejeo, pamoja na ukosefu wa wagani wa kutosha wenye hamasa,ari ya kazi, weledi na kiunganifu hafifu kati ya watafiti na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa kilimo ndiyo sekta kiongozi au ndio muhimili mkuu katika uchumi wa nchi yetu. Sekta hii inachangia takriban asilimia 25.3 ya Pato la Taifa, asilimia 30 ya mauzo ya nje; na asilimia 65 malighafi ya viwanda vyetu vya ndani. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa sekta ya kilimo kilitoa ajira kwa takriban

wastani wa 85%, 75% na 65.5% kwa mwaka 2001, 2006 na 2016 mtawalia yaani *(Consecutively)* wakati huo viwanda na sekta za utoaji wa huduma kwa kipindi hicho ajira zilikuwa ni 3%, 5%, 6%; na 15%, 20%, na 27% kwa mtawalia. Pia kwa asilimia hizo za waajiriwa katika sekta ya kilimo, kati yao asilimia 53 ya nguvu kazi yote ni wanawake. Aidha takwimu zinaonesha zaidi kuwa asilimia 80 ya watu masikini wanategemea kuedesha maisha yao kupitia kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Japokuwa Kilimo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu kwa ushahidi huo, lakini Serikali bado haijaweka juhudi kuhakikisha kuwa kilimo kinachangia zaidi na zaidi katika uchumi. Hoja hii inajionesha wazi kutokana na takwimu za ukuaji wa Sekta ya Kilimo zinavyozidi kushuka kila mwaka ambapo wastani wa ukuaji kwa mwaka 2014 ilikuwa ni asilimia 3.4; na asilimia 2.3 kwa mwaka 2015 na kwa mwaka 2017 wastani wa ukuaji ukawa asilimia 3.1, wastani wa ukuaji huu ni wa chini zaidi kulinganisha na wastani wa kiwango cha azimio la Malabo wa 6%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo uwekezaji katika Sekta ya Kilimo umekuwa ukishuka vile vile, Bajeti iliyotengwa kwa kilimo kwa kulinganisha na Bajeti nzima ya Serikali kwa mwaka 2012 ambayo ilikuwa ni asilimia 7.2 ikashuka hadi asilimia 4.7 kwa mwaka 2017, kiwango ambacho ni chini ya asilimia 10 ya makubaliano ya Malabo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinaonesha kuwa kama Serikali itaamua kwa dhati kuwekeza katika Sekta ya Kilimo ni dhahiri mabadiliko makubwa ya uchumi Tanzania sambamba na watanzania tutaondokana na umaskini wa kipato uliokithiri kwa miaka nenda rudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukuaji wa uchumi wetu umejikita katika wastani wa asilimia 6 kwa mwaka, ambapo ukuaji wa pato la nchi ni asilimia 7 toka mwaka 2013. Wachumi wabobezi wanasema kuwa ukuaji wa uchumi ungekuwa zaidi ya hapo kama Sekta ya kilimo ingekuwa kwa wastani wa asilimia 6 kama kiwango cha uwekezaji wa asilimia 10 cha

azimio la Malabo kingezingatiwa, na hivyo uchumi ungekuwa kwa asilimia 8 hadi 10 kwa mwaka na nchi ingefikia lengo lake la kuwa nchi ya uchumi wa kati kwa mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji kwenye kilimo unajikita kwenye asilimia 4.7 ya jumla ya bajeti kuu ya Taifa kwa mwaka 2017/2018 kwa kulinganisha na asilimia 7.8 kwa mwaka 2010/2011 kiwango cha chini pia kwa kulinganisha na makubaliano ya asilimia 10 ya wakuu wa nchi za *SADC* kule Malabo. Pia Tanzania ilitoa asilimia 0.29% mwaka 2014 na 0.19% kwa mwaka 2016 kama sehemu ya mchango wa kilimo kwenye *GDP* katika kuwekeza kwenye utafiti na maendeleo ya kilimo kulinganisha na makubaliano ya asilimia 1 kwa kila nchi za *NEPAD* na *UN* kwa nchi zinazoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na azimio hilo, Tanzania bado imeshindwa kutekeleza. Takwimu zinaonyesha kwamba; kwa miaka miwili 2015 na 2016 ukuaji wa kilimo nchini Tanzania ulikuwa ni 2.3% na 1.7% mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017, sehemu ya Kilimo kifungu cha 3.2.3.3 kinaonesha kuwa; “Lengo ni kuhakikisha uwepo wa chakula cha kutosha na upatikanaji wa uhakika wa malighafi za uzalishaji katika viwanda vya mazao ya kilimo,mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti ya maendeleo inayoenda kwenye kilimo Fungu 43 ni dhahiri kwamba dhamira ya mpango wa maendeleo wa miaka mitano kama ilivyonukuliwa hapa juu haiwezi kufikiwa hata kwa robo yake. Hii ni kutokana na mwenendo wa utoaji wa fedha za maendeleo kwa ajili ya miradi ya kilimo kulingana na bajeti zinazokuwa zimeidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwa Serikali kuheshimu ahadi yake ya kutenga walau asilimia 10 ya bajeti yake kwa sekta ya kilimo kama inavyoonekana katika Azimio la Maputo. Kwa mgawo huu

wa sasa ambapo chini ya asilimia 10 ya fedha za serikali zinatengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo tuna wasiwasi kwamba malengo yaliyopangwa hayatafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia ni kwamba mikopo kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta umezidi kushuka, kwa mfano mwaka 2013 ilikuwa ni 8.7%, na 7.7% kwa mwaka 2015, na 6.9% mwaka 2017 hii ni kutokana na ukweli kwamba benki za biashara zinaamini kuwa uwekezaji kwenye sekta hii ni *"high risk investments"***.** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema jambo hili litamalizika na kuleta imani kwa taasisi za fedha kuhusu kuwekeza au kukopesha wawekezaji kwenye sekta ya kilimo kama kutakuwepo na uchumi wa soko jamii, ambapo mzalishaji atazalisha ikiwa anafahamu atapata nini kwenye mazao yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa hatujachelewa katika kufikia lengo hilo la mwaka 2025, kama tu tutawekeza kwenye sekta ya kilimo ambayo inatoa ajira kwa watu wengi zaidi kuliko sekta nyingine za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upotevu Wa Mazao ya Mavuno yaani *(Post Harvest Losses),* ukiangalia Randama ya mwaka 2018/2019 Fungu 43 ukurasa wa 28 aya 6.1.3 na pia mwaka 2019/2020 katika Randama ukurasa wa 17 aya 6.3 kuhusu kuimarisha usimamizi wa mazao kabla na baada ya mavuno na kuongeza thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko kwa mazao yote ya wakulima. Mradi wa kudhibiti Sumukuvu katika mazao, uliozinduliwa rasmi tarehe 12 Machi, 2019 ili kudhibiti tatizo la uchafuzi wa sumukuvu katika mfumo wa uzalishaji wa mazao ya chakula hususan mahindi na karanga. Mradi huo wenye thamani ya jumla ya dola za Kimarekani milioni 35.32 sawa na shilingi bilioni 80. Lakini kwa mwaka 2019/2020 zimetengwa fedha za ndani shilingi 1,080,000,000.00 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza huu mradi ni wa miaka mingapi? Kwanini fedha

zilizotengwa kwa mwaka huu kulinganisha na thamani ya mradi itahitajika miaka takriban 80 ili mradi huo ukamilike. Je, kwa hili kweli tuko makini na maendeleo ya kilimo chetu? Naomba nirudie kwenye eneo hili Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza huu mradi ni wa miaka mingapi? Kwanini fedha zilizotengwa kwa mwaka huu kulinganisha na thamani ya mradi ni kwamba itahitajika miaka takriban 80 ili mradi huo ukamilike. Je, kwa hili kweli tuko makini na maendeleo ya kilimo chetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli kwamba wakulima wengi wanapata hasara sana kutokana na kutokuwa na njia bora za uhifadhi wa mazao yao baada ya mavuno, inakadiriwa kwamba kati ya asilimia 30-40 ya jumla ya mazao hupotea kila mwaka. Upotevu mkubwa kutoka kwenye matunda, mihogo na mboga, kama karoti na vitunguu nakadhalika Tanzania hutumia zaidi ya dola milioni 200 sawa na bilioni 400 kulingana na ripoti ya Mtungi na Affognon ya 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuagiza chakula kutoka nje ya nchi, wakulima wadogo wadogo wanalazimika kuuza mazao yao kwa bei ya chini kwa sababu ya uwezo mdogo kwenye usimamizi wa mazao baada ya mavuno. Katika Afrika Mashariki, ni asilimia 5 tu huwekezwa kwenye usimamizi wa mazao baada ya mavuno ambayo asilimia 95 hutumika katika uzalishaji. Inakadiriwa kwamba kila mwaka hasara inayotokana na kuharibika kwa mazao ya nafaka Barani Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, inafikia dola za Kimarekani bilioni 4 na hii ni sawa na asilimia 15 ya thamani ya mavuno hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kumbukumbu zinazotaja sera inayohusu suala la kudhibiti upotevu wa mazao baada ya kuvunwa, takwimu zilizopo zinaonesha kwamba kwa miaka 12 Tanzania ina maghala 1,260. Idadi hii ni ndogo mno ukiilinganisha na mahitaji halisi ya takribani vijiji zaidi ya 11,000 vilivyokuwepo, sasa hivi Tanzania ina vijiji vipatavyo 15,082. Hii ni kwa mujibu wa Tanzania *Market Plan* chini ya utafiti uliofanywa na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha licha ya ongezeko la uzalishaji wa nafaka Kitaifa ambapo uzalishaji ulifikia takribani tani milioni 9,388,772 kwa mwaka, teknolojia zinazotumiwa wakati wa kuvuna na kusindika ni duni sana. Hali hii husababisha upotevu wa mavuno unaokisiwa tani milioni 1,877,754.4 kila mwaka. Tafsiri ya takwimu hizi ni uwepo wa upotevu wa takribani asilimia 20 baada ya mavuno. Tukichukulia uzalishaji wa jumla wa mazao yote ya chakula, matunda na mbogamboga wa tani 22,476,504 upotevu wa asilimia 20 ni sawa na tani 4,495,300.8

Mheshimiwa Mwenyekiti, upotevu huu unachangiwa na matatizo mbalimbali kama vile; maghala mengi hayawafai wakulima kwa sababu ya kuwa mbali, baadhi ya maghala ni mabovu kwa kuachwa kwa muda mrefu bila kukarabatiwa, maghala mengine hayakidhi viwango kwa kukosa vifaa muhimu, maghala mengine ama yamekodishwa kwa wafanyabiashara binafsi, au yanatumiwa kwa shughuli nyingine tofauti na kuhifadhi mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilianzishwa mnamo Septemba, 2011 chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Kazi kuu ya benki hii ni uhamasishaji utoaji wa huduma za fedha na huduma zisizo za kifedha kwa sekta ya kilimo Tanzania ikiwa ni pamoja na:-
(i) Kutoa vifaa vya muda mfupi, vya kati na vya muda mrefu kwenye sekta ya kilimo;

(ii) Kuchochea utoaji wa mikopo kwa sekta ya kilimo, hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta hiyo;

(iii) Kuwa Benki Kuu inayofadhili sekta ya kilimo yenye mikakati ya kujenga uwezo, na mipango ya kuimarisha mnyororo wa thamani kwenye sekta hiyo;

(iv) Kufadhili shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji nyuki na shughuli za mifugo; na

(v) Kuimarisha mnyororo wa thamani kwa njia ya mafunzo, utafiti na ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo Septemba, 2014, Serikali ilitoa mtaji wa shilingi bilioni 60 kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania, lakini taarifa za ukaguzi zinaonesha kuwa; Benki hiyo badala ya kutoa mikopo kwa sekta ya kilimo ambayo ndiyo shughuli kuu, benki imekuwa ikiwekeza sehemu kubwa ya fedha zake katika amana za kudumu. Kufikia tarehe 31 Desemba, 2016, jumla ya Shilingi bilioni 54.70 zilikuwa zimewekezwa kwenye amana za kudumu, ambapo ni karibu asilimia 91 ya mtaji. Aidha, ilibainika kuwa, kati ya jumla ya Shilingi bilioni 3.95 ya mikopo iliyotolewa, Shilingi bilioni 1.71 ni mikopo kwa watumishi na Shilingi bilioni 2.23 ndio zimetolewa mikopo kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ukurasa wa 100 aya ya 5.5.2 unasema kwamba, Serikali imeji-*commit* kuiongezea mtaji benki hiyo hadi kufikia shilingi trilioni tatu kwa kipindi cha miaka mitano cha uhai wa Mpango wa Pili wa Maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kufahamu hadi sasa Benki hiyo imeongezewa fedha kiasi gani kati ya hizo shilingi trilioni tatu zilizoahidiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba uwepo wa Benki hii ulitarajiwa kuwa ni mkombozi katika uwekezaji kwenye kilimo pamoja na viwanda vya kuongeza thamani bidhaa za kilimo. Hata hivyo, jambo hilo limekuwa ni kinyume sana kutokana na benki kutokuwa na mtaji wa kutosha kuweza kufanyakazi zake kama yalivyo malengo ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2019/2020 ukurasa wa 57 inaonesha kuwa Benki ilitoa mikopo kwa wakulima 1,049,370 wa mahindi, mpunga, shayiri, kahawa, korosho, karafuu, miwa, mbogamboga, ufugaji wa samaki na kadhalika yenye thamani ya shilingi bilioni 95.1 tu. Hapa tunataka kujenga Tanzania ya viwanda lakini hatuoni ni kwa jinsi gani benki hii inaenda kujenga Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni kwamba; kutoa mikopo kwa wakulima bila ya kuwa na utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa bei za mazao zitaweza kurudisha mkopo na kumfanya mkopaji kuendelea kwenye kilimo ni njia mojawapo ya kumfukarisha mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hatari sana kwa mkulima kukopa fedha kwa ajili ya uzalishaji na baadaye akawekewa vikwazo katika uuzaji wa mazao yake, hii ni kinyume na misingi ya biashara. Jambo hili ndilo lililllotokea kwa wakulima wa mahindi, kahawa, korosho na pamba kwa kuwalazimisha kuuza kwenye ushirika badala ya kuuza kwa makampuni binafsi kulingana na ushindani wa bei inayotolewa baina ya makampuni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie eneo hili; ni hatari sana kwa mkulima kukopa fedha kwa ajili ya uzalishaji na baadaye akapewa vikwazo katika uuzaji wa mazao yake, hii ni kinyume na misingi ya biashara. Jambo hili ndilo lililllotokea kwa wakulima wa mahindi, kahawa, korosho na pamba kwa kuwalazimisha kuuza kwenye ushirika badala ya kuuza kwa makampuni binafsi kulingana na ushindani wa bei inayotolewa baina ya makampuni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2019/2020 ukurasa wa 56 kuhusu Benki ya Uwekezaji *(TIB)* kuwa imetoa mikopo kwa sekta ya kilimo yenye thamani ya shilingi bilioni 698.6, lakini kwa taarifa ya benki hiyo iliyotolewa kwenye Kamati ya *PAC* inaonesha kuwa; Benki inadai mikopo chefuchefu kiasi cha Sh.230,669,526,932.24 yenye dhamana zenye thamani ya Sh.550,832,170,833 na hivyo kuifanya benki hiyo kuwa na mikopo chechefu ya asilimia 35 kwa Desemba, 2016 na 2015 asilimia 14 ikiwa ni ongezeko la kama asilimia 150. Kiwango hiki ni kikubwa sana kulinganisha na kiwango kilichotolewa na *BOT* kuwa mikopo chefuchefu cha asilimia 24. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kipengele hiki hapa; ukiangalia Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/2020 ukurasa wa 56 kuhusu Benki ya Uwekezaji *(TIB)* kuwa

imetoa mikopo kwa sekta ya kilimo yenye thamani ya shilingi bilioni 698.6, lakini kwa taarifa ya Benki hiyo iliyotolewa kwenye Kamati ya *PAC* inaonesha kuwa; benki inadai mikopo chechefu kiasi cha shilingi bilioni 230,669,526,932.24 yenye dhamana zenye thamani ya shilingi 550.8

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie baadhi ya mazao, nianze na zao la pamba; zao hili ni zao ambalo limelimwa na wakulima wadogo kati ya 350 na 500,000 katika wilaya 49 za mikoa 17 ya Tanzania Bara japokuwa asilimia 80 ya pamba yote inalimwa katika Mikoa minne ya Simiyu, Shinyanga, Singida na Mwanza. Hii ni kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba Ndugu Marco Mtunga, wakati akitoa taarifa kwa wadau wa pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto mbalimbali za zao la pamba zimekuwepo kwa kipindi kirefu na Serikali imeshindwa kuzitafutia ufumbuzi. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa, mustakabali wa kilimo biashara upo katika soko la mazao na bidhaa za kilimo, ambapo wakulima na wanunuzi wataendesha shughuli zao za kibiashara katika mazingira yanayotabirika na kwamba wakulima wanaweza kupata bei nzuri kwa mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu zao la kahawa; kahawa ni zao la biashara linalolimwa hapa nchini katika Mikoa ya Songwe, Njombe, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Ruvuma, Kagera, Tanga, Iringa, Morogoro, Kigoma, Manyara, Mwanza, Rukwa na Mara. Inakadiriwa kuwa jumla ya eneo la hekta 265,000 ndilo linatumika kwa ajili ya kilimo cha kahawa aina ya *Arabica* na *Robusta* ambazo ndizo zinalimwa sana hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya nne kwa uzalishaji wa kahawa Afrika baada ya Ethiopia, Ivory Coast na Uganda ambapo kila mwaka huzalisha wastani wa tani 46,000 hadi 60,000 huku Mkoa wa Kagera ukizalisha takribani tani 12,131.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea nyaraka za watatifi wanasema kuwa, sekta ndogo ya kahawa imekuwa na matatizo mengi miongoni mwake ni hali ya hewa kubadilika sana, kukosekana kwa miundombinu imara ya umwagiliaji wa mashamba. Hili ni kwa mashamba makubwa na mibuni kuzeeka na hivyo uzalishaji kuwa chini. Aidha kukosekana kwa uwekezaji wa kutosha katika ufafiti wa magonjwa ya kahawa na huduma duni za ugani kumeathiri uzalishaji wa zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kuwa changamoto za soko zilikuwepo hata miaka iliyopita, lakini kwa sasa tatizo limekuwa kubwa zaidi kwa sababu limeibuka suala la *AMCOS* kuhodhi tena soko la kahawa kwa wakulima na hivyo kuminya fursa ya wao kuchagua bei kulingana na gharama za uzalishaji. Kambi Rasmi bado inasisitiza katika uwepo wa mfumo huru wa soko ambapo mkulima na mnunuzi watakutana na kupanga bei ili kukidhi gharama za uzalishaji na kila upande unufaike na biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu korosho; kwa mujibu wa takwimu za Randama ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2018/19 zinaonesha kwamba, mwenendo wa uzalishaji wa zao la korosho kwa miaka mitatu kuanzia msimu wa mwaka 2015/ 2016 hadi msimu wa 2018/2019 umekuwa unapanda ambapo mwaka 2015/2016 uzalishaji ulikuwa tani 155,416; 2016/2017 tani 265,238; na 2017/2018 uzalishaji ulifikia tani 311,889. Aidha, matarajio kwa mwaka 2018/2019 yalikuwa ni kuzalisha tani 350,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizo zinaonesha kwamba, wakulima wadogo wadogo takribani 280,000 wanaendesha maisha yao na familia zao kutegemea moja kwa moja zao la korosho kwa kulima kati ya eka moja hadi mbili na kufanya eneo linalolimwa zao hilo kufikia ekari 400,000 na kwa sasa eneo hilo litakuwa limeongezeka kutokana na mwamko wa wananchi kulima zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Korosho, inasema kuwa asilimia 65 ya kodi ya mauzo nje

irudishwe kwa wakulima kupitia Bodi ya Korosho na Serikali ibakie na asilimia 35. Mgawo wa hizo asilimia 65 wa *export levy,* matumizi yake makubwa ni ununuzi wa pembejeo za kilimo cha korosho na kuendeleza utafiti kwenye zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ambayo mpaka sasa haieleweki; Serikali ilivunja Bodi ya Korosho na kutaifisha ile asilimia 65 ya kodi ya mauzo ya korosho nje; na pia kuingilia biashara ya korosho kwa kuwazuia wanunuzi binafsi kununua korosho. Matokeo yake ni kwamba hakuna mauzo ya korosho nje ya nchi yaliyofanyika mpaka sasa. Serikali ilichofanya ni kununua korosho kwa wananchi tena kwa mkopo kwa ahadi ya shilingi 3,300 kwa kilo lakini wakati wa kulipa bei hiyo ikapungua kwa madai kwamba korosho hazina ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Serikali kununua korosho toka kwa wakulima badala ya kuhusisha Makampuni binafsi umeligharimu Taifa letu kwa kukosa fedha za kigeni. Mfano kwa mwaka wa fedha 2017/2018, fedha za kigeni zilizotokana na korosho zilikuwa ni dola za Kimarekani milioni 965. Kwa mwaka huu 2018/2019 unaoishia hadi sasa ni Zero. Kodi ya mauzo nje kwa maana ya *export levy* kwa mwaka 2017/2018 ilikuwa ni dola za Kimarekani milioni 200; kwa mwaka 2018/2019 hakuna chochote...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa taarifa yako.

(Hapa Mhe. Pascal Y. Haonga aliendelea kuzungumza)

MWENYEKITI: Hapana, muda umekwisha bwana, muda umekwisha.

(Hapa Mhe. Pascal Y. Haonga aliendelea kuzungumza)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga muda umekwisha. *(Makofi)*

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA PASCAL YOHANA HAONGA (MB) WIZARA YA KILIMO, KUHUSU UTEKELEZAJI MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Inatolewa chini ya Kanuni 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2016)

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na afya kuweza kusimama mbele ya adhira hii ili kutoa maoni kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Kilimo, kwa mwaka 2018/19 na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2019/20.

2. Mheshimiwa Spika, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Mbozi kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono mimi na chama changu wakati wote ninapoendelea kuwatumikia licha ya changamoto mbalimbali za kisiasa ninazopitia. Kikubwa waelewe kwamba ili dhahabu ing'ae lazima ipitie kwenye moto. Pia waamini kwamba siyo kila changamoto ninayoipitia lengo lake ni kunidhoofisha bali nyingine zinanijenga /kuniimarisha zaidi.

3. Mheshimiwa Spika, nitoe pole na pongezi kwa Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Esther Matiko na wapiganaji wengine kwa magumu wanayopitia, kitu kikubwa ni kuwa waelewe kwamba gereza au mahabusu siyo kaburi.

B. HALI YA CHAKULA KWA MSIMU UJAO WA KILIMO

4. Mheshimimwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa hali ya upatikanaji wa chakula kwa misimu miwili ya 2017/18 ilikuwa ni yenye kutia matumiani sana kwani uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2017/18 ulifikia tani 16,981,974 na

mahitaji ya chakula kwa msimu 2018/19 yalikuwa ni tani 13,569,285 na hivyo kuwa na ziada ya tani 3,322,689. Kwa msimu huu wa 2018/19 ni dhahiri dalili zimeanza kuonekana mapema kuwa kutakuwa na upungufu mkubwa wa chakula kutokana na kwamba; mbali na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameikumba mikoa ya Kanda ya Kati yenye mikoa ya Morogoro, Dodoma na Singida, Kanda ya Magharibi(Tabora, Katavi na Kigoma) Kanda ya Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro, Manyara na Arusha). Lakini kanda ambayo ni mzalishaji mkubwa wa nafaka hasa mahindi (Songea, Njombe, Iringa, Mbeya, Rukwa na Katavi) mvua haikuwa tatizo ila tatizo ni upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na kukosekana kwa soko la kutoa bei nzuri ya mahindi na hivyo kusababisha hasara kubwa kwa wakulima katika msimu uliopita, jambo hilo litasababisha kupungua kwa uzalishaji wa mahindi kwa msimu huu wa kilimo. Kimsingi bei nzuri ya soko la bidhaa za mkulima na wepesi wa kuuza bidhaa zao nikichocheo kikubwa kwa wakulima kuendelea kuwekeza kuzalisha bidhaa kwaajili ya jamii ya watanzania na kuuza nje ya nchi ili Tanzania iweze kupata fedha za kigeni.

5. Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameikumba mikoa mingi hapa nchini na hivyo majira ya mvua kubadilika sana na hivyo kusababisha mimea mingi kuharibika kabla ya kufika wakati wa kuvunwa, ni wazi kuwa mkakati tofauti unahitajika ili kuendelea kukidhi mahitaji ya chakula, na zaidi kufikia soko la bidhaa za kilimo kwenye ukanda wa Afrika Mashariki (Eastern Africa) na Ukanda wa Kusini mwa Afrika (Southern Africa).

6. Mheshimiwa Spika, hivyo basi kwa mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi ambayo inategemea sana kilimo cha mahindi, karanga, mpunga, muhogo, maharage, kunde, choroko na ufuta. Mkoa huu huzalisha mihogo, maharage, mahindi na mpunga kama mazao ya chakula pia michikichi na pamba kama mazao ya biashara.

7. Mheshimiwa Spika, Kwa kawaida katika ukanda wa kati mvua huanza mwezi Novemba hadi mwezi Machi/Aprili. Hali ni tofauti sana kwa mwaka huu kwa kuwa mvua zilianza

kunyesha mwezi Desemba haikuchukua muda kukoma hivyo kuwaacha wakulima wakiwa wamepanda kidogo mno. Hali ya ukame iliindelea katika mwezi Januari, Februari hadi mwezi Machi na hivyo kusababisha kukauka kwa mazao yaliyokuwa yamekwisha kupandwa mashambani pia ikumbukwe kuwa mikoa hiyo huzalisha malisho kwa ajili ya mifugo.

8. Mheshimiwa Spika,Kutokana na ukame wa mvua hadi mwezi Machi, 2019 umepelekea maeneo ya Wilaya za Mkoa wa Tabora kwa upande wa mpunga, majaruba ya mpunga kubaki yakiwa hayajapandwa kutokana na kukosekana kwa maji. Vivyo hivyo kwa mikoa mingine ya nchi, hivyo uzalishaji hafifu kutokana na hali ya hewa ya kutoridhisha, kunaleta tishio kubwa la upungufu wa chakula katika maeneo mengi ya nchi hii.

9. Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitahadharisha Serikali kuchukua hatua madhubuti katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na akiba ya chakula ya kutosha na inachukua hatua stahiki kupunguza madhara yanayoweza kutokana na hali hii ya ukame ambayo imekikumba kilimo kwa msimu 2018/19.

C. UMUHIMU WA SEKTA YA KILIMO-(MAZAO)

10. Mheshimiwa Spika, Uwezo wa kilimo na biashara ya kilimo ni mkubwa sana kwa Tanzania, lakini matarajio lazima yawekwe inavyostahili. Sehemu kubwa ya sekta hii kwa sasa haina uwezo wa kushindana kwa sababu ya gharama kubwa za uzalishaji, hamasa ndogo miongoni mwa wazalishaji kutokana na muingiliano wa serikali hasa kwenye soko, ubora hafifu wa pembejeo, pamoja na ukosefu wa wagani wa kutosha wenye hamasa,ari ya kazi, weledi na kiunganifu hafifu kati ya watafiti na wakulima.

11. Mheshimiwa Spika, Uzalishaji wa mboga na matunda yenye thamani kubwa, hata hivyo, inaonekana kama ni fursa halisi, kwani iko juu katika orodha iliyoandaliwa na zana zote za uchambuzi zilizotumika katika utafiti wakutambua fura

zilizopo na ambazo hazijatumika. Sekta ndogo hii ya uzalishaji wa mboga na matunda imefanya vizuri katika miaka ya karibuni kwa kuzingatia mahitaji yanayokua katika masoko ya ndani, nchi jirani na kimataifa[1].

12. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa kilimo ndiyo sekta kiongozi au ndio muhimili mkuu katika uchumi wa nchi yetu. Sekta hii inachangia takriban asilimia 25.3 ya Pato la Taifa (GDP), asilimia 30 ya mauzo ya nje; na asilimia 65 malighafi ya viwanda vyetu vya ndani. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa sekta ya kilimo kilitoa ajira kwa takriban wastani wa 85%, 75% na 65.5% kwa mwaka 2001, 2006 na 2016 mtawalia[2], wakati huo viwanda na sekta za utoaji wa huduma kwa kipindi hicho hicho ajira zilikuwa ni 3%, 5%, 6%; na 15%, 20%, 27% kwa mtawalia. Pia kwa asilimia hizo za waajiriwa katika sekta ya kilimo, kati yao asilimia 53 ya nguvu kazi yote ni wanawake. Aidha takwimu zinaonesha zaidi kuwa asilimia 80 ya watu masikini wanategemea kuedesha maisha yao kupitia kilimo.

13. Mheshimiwa Spika, Japokuwa Kilimo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu kwa ushahidi huo, lakini serikali bado haijaweka juhudi kuhakikisha kuwa kilimo kinachangia zaidi na zaidi katika uchumi. Hoja hii inajionesha wazi kutokana na takwimu za ukuaji wa sekta ya kilimo zinavyozidi kushuka kila mwaka ambapo wastani wa ukuaji kwa mwaka 2014 ilikuwa ni asilimia 3.4; 2.3 kwa mwaka 2015 na kwa mwaka 2017 wastani wa ukuaji ukawa 3.1, wastani wa ukuaji huu ni wa chini zaidi kulinganisha na wastani wa kiwango cha azimio la Malabo/CAADP wa 6%. Sambamba na hilo uwekezaji katika sekta ya kilimo umekuwa ukishuka vile vile, Bajeti iliyotengwa kwa kilimo kwa kulinganisha na Bajeti nzima ya Serikali kwa mwaka 2012 ilikuwa ni asilimia 7.2 ikashuka hadi asilimia 4.7 kwa mwaka 2017, kiwango ambacho ni chini ya asilimia 10 ya makubaliano ya Malabo/CAADP.

---

[1] www.worldbank.org/tanzania - Tanzania: Tunahitaji Ajira Zenye Tija, 2014

[2] Bajeti ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi-2017/18

14. Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonesha kuwa kama Serikali itaamua kwa dhati kuwekeza katika sekta ya kilimo ni dhahiri mabadiliko makubwa ya uchumi wa Tanzania sambamba na watanzania tutaondokana na umasikini wa kipato uliokithiri kwa miaka nenda rudi.

15. Mheshimiwa Spika,Ukuaji wa uchumi wetu umejikita katika wastani wa asilimia 6 kwa mwaka, ambapo ukuaji wa pato la nchi ni asilimia 7 toka mwaka 2013. Wachumi wabobezi wanasema kuwa ukuaji wa uchumi ungekuwa ni zaidi ya hapo kama Sekta ya kilimo ingekuwa kwa wastani wa asilimia 6 kama kiwango cha uwekezaji wa asilimia 10 cha azimio la Malabo/CAADP kingezingatiwa, na hivyo uchumi ungekuwa kwa asilimia 8 – 10 kwa mwaka na nchi ingefikia lengo lake la kuwa nchi ya uchumi wa kati kwa mwaka 2025.

16. Mheshimiwa Spika, uwekezaji kwenye kilimo unajikita kwenye asilimia 4.7 ya jumla ya bajeti kuu ya taifa kwa mwaka 2017/18 kwa kulinganisha na asilimia 7.8 kwa mwaka 2010/ 11 kiwango cha chini pia kwa kulinganisha na makubaliano ya asilimia 10 ya wakuu wa nchi za SADC kule Malabo. Pia Tanzania ilitoa asilimia 0.29% mwaka 2014 na 0.19% mwaka 2016 kama sehemu ya mchango wa kilimo kwenye GDP katika kuwekeza kwenye utafiti na maendeleo (R&D) ya kilimo kulinganisha na makubaliano ya asilimia 1 kwa kila nchi za NEPAD na UN kwa nchi zinazoendelea.

17. Mheshimiwa Spika, pamoja na azimio hilo, Tanzania bado imeshindwa kutekeleza. Takwimu zinaonyesha kwamba; kwa miaka miwili 2015 na 2016 ukuaji wa kilimo nchini Tanzania ulikuwa ni 2.3% na 1.7% mtawalia.

18. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka **2007/2008 – 2016/2017 Kilimo na Ushirika (*Fungu 43*)** imepata wastani wa shilingi bilioni 250 ambayo ni sawa na 1.8% tu ya bajeti ya taifa. Kati ya wastani huo, bajeti ya maendeleo ilipata wastani wa **shilingi bilioni 80.3** ambayo ni **sawa na 32% tu ya bajeti ya kilimo na ushirika** na **1.6% ya bajeti ya maendeleo taifa**.

19. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa Wizara ya Kilimo kupitia **fungu 43** kwa mwaka wa fedha 2015/16 ilitengewa jumla ya Shilingi **206,816,421,000/-**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **174,103,348,000/-** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi **32,713,073,000/-** ni fedha za maendeleo. Hadi mwaka huo wa fedha unamalizika Wizara ilipokea shilingi **2,663,428,542/-** kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikiwa ni fedha za ndani na shilingi **5,035,062,321/-** zikiwa ni fedha za nje, na hivyo kufanya jumla ya fedha za maendeleo kwa fungu 43 zilizopokelewa kwa mwaka 2015/16 kuwa shilingi **7,698,490,863/-** sawa na asilimia **23.53** ya fedha za maendeleo zilizopitishwa na Bunge.

20. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/17 **Fungu 43** lilitengewa jumla ya Shilingi **210,359,133,000** ziliombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **100,527,497,000** zilikuwa ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Fedha za ndani zilikuwa shilingi **23,000,000,000/-** na fedha za nje shilingi **78,527,497,000/-** Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi **2,251,881,250/**- sawa na **asilimia 2.22** tu na kati ya fedha hizo fedha za ndani zilikuwa shilingi **1,382,191,924/-** na fedha za nje shilingi **349,081,000/-**

21. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2017/18 Wizara **Fungu 43** iliombakuidhinishiwa jumla ya shilingi **214,815,759,000/-** kati ya fedha hizo shilingi **150,253,000,000/-** ni fedha za maendeleo, lakini hadi mwezi Machi 1, 2018; shilingi **16,520,540,444/-** zimetolewa ambazo ni sawa na **asilimia 11** ya fedha zilizoidhinishwa.

22. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2018/19 wizara **fungu 43** iliombewa jumla ya shilingi **162,224,814,000/-** kati ya fedha hizo shilingi **64,105,298,000/-** ni fedha za miradi ya maendeleo.

23. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/17,

sehemu ya Kilimo kifungu cha 3.2.3.3 kinaonesha kuwa; *"Lengo ni kuhakikisha uwepo wa chakula cha kutosha na upatikanaji wa uhakika wa malighafi za uzalishaji katika viwanda vya mazao ya kilimo,mifugo na uvuvi.*

24. Mheshimiwa Spika, ufinyu wa bajeti ya maendeleo inayoenda kwenye kilimo Fungu 43 ni dhahiri kwamba dhamira ya mpango wa maendeleo wa miaka mitano kama ilivyonukuliwa hapa juu haiwezi kufikiwa hata kwa robo yake. Hii ni kutokana na mwenendo wa utoaji wa fedha za maendeleo kwa ajili ya miradi ya kilimo kulingana na bajeti zinazokuwa zimeidhinishwa na Bunge.

25. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwa Serikali kuheshimu ahadi yake ya kutenga walau asilimia 10 ya bajeti yake kwa sekta ya kilimo kama inavyoonekana katika Azimio la Maputo. Kwa mgawo huu wa sasa ambapo chini ya asilimia 10 ya fedha za serikali zinatengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo tuna wasiwasi kwamba malengo yaliyopangwa hayatafikiwa.

26. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia ni kwamba mikopo kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta umezidi kushuka, kwa mfano mwaka 2013 ilikuwa ni 8.7%, 7.7% mwaka 2015, na 6.9% mwaka 2017 hii ni kutokana na ukweli kwamba benki za biashara zinaamini kuwa uwekezaji kwenye sekta hii ni ***"high risk investments".*** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema jambo hili litamalizika na kuleta imani kwa taasisi za fedha kuhusu kuwekeza/kukopesha wawekezaji kwenye sekta ya kilimo kama kutakuwepo na uchumi wa soko jamii, ambapo mzalishaji atazalisha ikiwa anafahamu atapata nini kwenye mazao yake.

27. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa hatujachelewa katika kufikia lengo hilo la mwaka 2025, kama tu tutawekeza kwenye sekta ya kilimo ambayo inatoa ajira kwa watu wengi zaidi kuliko sekta nyingine za uchumi.

D. UPOTEVU WA MAZAO BAADA YA MAVUNO (POST HARVEST LOSSES)

28. Mheshimiwa Spika, ukiangalia Randama ya mwaka 2018/19 Fungu 43 uk. 28 aya 6.1.3 na pia mwaka 2019/20 katika Randama uk.17 aya 6.3 kuhusu kuimarisha usimamizi wa mazao kabla na baada ya mavuno na kuongeza thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko kwa mazao yote ya wakulima. Mradi wa kudhibiti Sumukuvu katika mazao, uliozinduliwa rasmi tarehe 12 Machi, 2019 ili kudhibiti tatizo la uchafuzi wa sumukuvu katika mfumo wa uzalishaji wa mazao ya chakula hususan mahindi na karanga. Mradi huo wenye thamani ya jumla ya dola za Kimarekani milioni 35.32 sawa na shilingi bilioni 80. Lakini kwa mwaka 2019/20 zimetengwa fedha za ndani shilingi 1,080,000,000.00

29. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza huu mradi ni wa miaka mingapi? Kwani kwa fedha zilizotengwa kwa mwaka huu kulinganisha na thamani ya mradi ni kwamba itahitajika miaka takriban 80 ili mradi huo ukamilike. Je, kwa hili kweli tuko makini na maendeleo ya kilimo chetu?

30. Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba wakulima wengi wanapata hasara sana kutokana na kutokuwa na njia bora za uhifadhi wa mazao yao baada ya mavuno, inakadiriwa kwamba kati ya asilimia 30-40 ya jumla ya mazao hupotea kila mwaka. Upotevu mkubwa kutoka kwenye matunda, mihogo na mboga, kama karoti na vitunguu n.k. Tanzania hutumia zaidi ya dola milioni 200 sawa na bilioni 400 (Mutungi and Affognon 2013) kuagiza chakula kutoka nje ya nchi.

31. Mheshimiwa Spika, Wakulima wadogo wadogo wanalazimika kuuza mazao yao kwa bei ya chini kwa sababu ya uwezo mdogo kwenye usimamizi wa mazao baada ya mavuno. Katika Afrika Mashariki, ni asilimia 5 huwekezwa kwenye usimamizi wa mazao baada ya mavuno ambayo asilimia 95 hutumika katika uzalishaji. Inakadiriwa kwamba kila mwaka hasara inayotokana na kuharibika kwa mazao ya nafaka Barani Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, inafikia

dola za Kimarekani bilioni 4 na hii ni sawa na asilimia 15 ya thamani ya mavuno hayo.

32. Mheshimiwa Spika, hakuna kumbukumbu zinazotaja sera inayohusu suala la kudhibiti upotevu wa mazao baada ya kuvunwa, takwimu zilizopo zinaonesha kwamba kwa miaka 12 Tanzania ina maghala 1,260. Idadi hii ni ndogo mno ukiilinganisha na mahitaji halisi ya takribani vijiji 11,000 vilivyokuwepo, sasa hivi Tanzania ina vijiji vipatavyo 15,082. Hii ni kwa mujibu wa Tanzania Market Plan chini ya utafiti uliofanywa na taasisi zifuatazo[3]

33. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha licha ya ongezeko la uzalishaji wa nafaka kitaifa (uzalishaji ukifikia takriban tani 9,388,772 kwa mwaka) teknolojia zinazotumiwa wakati wa kuvuna na kusindika ni duni sana. Hali hii husababisha upotevu wa mavuno unaokisiwa kuwa tani 1,877,754.4 kila mwaka. Tafsiri ya takwimu hizi ni uwepo wa upotevu wa takribani asilimia 20 baada ya mavuno. Na tukichukulia uzalishaji wa jumla wa mazao yote ya chakula, matunda na mboga wa tani 22,476,504 upotevu wa asilimia 20 ni sawa na tani 4,495,300.8

34. Mheshimiwa Spika, upotevu huu unachangiwa na matatizo mbalimbali kama vile; maghala mengi hayawafai wakulima kwa sababu ya kuwa mbali, baadhi ya maghala ni mabovu kwa kuachwa kwa muda mrefu bila kukarabatiwa, maghala mengine hayakidhi viwango kwa kukosa vifaa muhimu, maghala mengine ama yamekodishwa kwa wafanya-biashara binafsi, au yanatumiwa kwa shughuli nyingine tofauti na kuhifadhi mazao.

---

[3] *1. Tafiti elekezi – Daima, 2. Chanzo: PMC, SUA, Usaili – Julai 2012; 3. Benki ya Maendeleo ya Afrika - ADB (Framework Paper: Programme for Post – harvest Losses Reduction in Africa, 2010 – 2014) FAO/WB Workshop on Reducing PHL in grain supply chains in Africa: lessons learned and practical guidelines, FAO Hqrts. Rome, Italy, March 2010, 4.Uzoefu wa Tanzania wa kuelimisha wakulima wadogo jinsi ya kuhifadhi mazao baada ya kuvunwa, Idara ya Uchumi na Biashara ya Kilimo – SUA, Oktoba 2012*

Maghala mengi kutokutumika

35. Mheshimiwa Spika, Maghala mengi katika Mkoa wa Songwe haya fanyikazi kutokana na kujengwa kwa maelekezo au uamuzi wa watendaji Wizarani,au Wakala za Serikali na wanasiasa bila ushirikishwaji wa wadau katika Wilaya wakiwemo wananchi na mwisho wa siku yamekuwa ni "white elephants". Kwa Wilaya ya Mbozi kuna maghala mengi katika vijiji lakini hayatumiki kuhifadhi nafaka ambazo upotevu ni mkubwa sana.

36. Mheshimiwa Spika, Jambo hili la kutoshirikisha wadau linaleta ugumu kwa watendaji wa Serikali za Mitaa katika kutekeleza sera za nchi kwani wanakutana na ugumu toka kwa wadau mbalimbali kutokuona umuhimu wa kile kinachotakiwa kutekelezwa na Serikali kwa wakati huo.

37. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge, idadi halisi ya Maghala iliyopo kwa sasa kulingana na ongezeko la vijiji pamoja na ongezeko la uzalishaji hasa kwa mazao ya nafaka.

38. Mheshimiwa Spika, Serikali haisemi jinsi ya kukabiliana na tatizo ambalo linawakabili wakulima wengi hasa wadogo na badala yake inatoa suluhu ya uongezaji thamani kwa mazao jambo ambalo ni hatua inayofuata baada ya uhifadhi katika ngazi za familia. Tukumbuke wakulima inawalazimu kuuza mazao yao kwa bei ya chini kutokana na kutokuwa na sehemu muafaka za kuhifadhia mazao yao.

E. BENKI YA MAENDELEO YA KILIMO

39. Mheshimiwa Spika, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilianzishwa mnamo Septemba 2011 chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Kazi kuu ya Benki ni uhamasishaji utoaji wa huduma za fedha na huduma zisizo za kifedha kwa sekta ya kilimo Tanzania ikiwa ni pamoja na:

i. Kutoa vifaa vya muda mfupi, vya kati na vya muda mrefu kwenye sekta ya kilimo.

ii. Kuchochea utoaji wa mikopo kwa sekta ya kilimo, hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta hiyo.

iii. Kuwa Benki Kuu inayofadhili sekta ya kilimo,yenye mikakati ya kujenga uwezo, na mipango ya kuimarisha mnyororo wa thamani kwenye sekta hiyo.

iv. Kufadhili shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji nyuki na shughuli za mifugo.

v. Kuimarisha mnyororo wa thamani kwa njia ya mafunzo, utafiti na ushauri.

40. Mheshimiwa Spika, Mnamo Septemba 2014, Serikali ilitoa mtaji wa shilingi bilioni 60 kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania**,** lakini taarifa za ukaguzi zinaonesha kuwa; benki hiyo badala ya kutoa mikopo kwa sekta ya kilimo ambayo ndiyo shughuli kuu, Benki imekuwa ikiwekeza sehemu kubwa ya fedha zake katika amana za kudumu. Kufikia tarehe 31 Desemba 2016, jumla ya Shilingi bilioni 54.70 zilikuwa zimewekezwa kwenye amana za kudumu, ambayo ni karibu asilimia 91 ya mtaji. Aidha ilibainika kuwa, kati ya jumla ya Shilingi bilioni 3.95 ya mikopo iliyotolewa, Shilingi bilioni 1.71 ni mikopo kwa watumishi na Shilingi bilioni 2.23 tu ndio zimetolewa mikopo kwenye sekta ya kilimo.

41. Mheshimiwa Spika, mpango wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano uk. 100 aya ya 5.5.2 unasema kwamba; Serikali imeji-commit kuiongezea mtaji benki hiyo hadi kufikia shilingi trilioni 3 kwa kipindi cha miaka mitano cha uhai wa mpango wa pili wa maendeleo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kufahamu hadi sasa Benki hiyo imeongezewa fedha kiasi gani kati ya hizo shilingi trilioni 3 zilizoahidiwa na Serikali?

42. Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba uwepo wa benki hii ilitarajiwa kuwa ni mkombozi katika uwekezaji kwenye kilimo pamoja na viwanda vya kuongeza thamani bidhaa za kilimo. Lakini jambo hilo limekuwa ni kinyume sana kutokana na Benki kutokuwa na mtaji wa kutosha kuweza kufanyakazi zake kama yalivyo malengo ya uanzishwaji wake.

43. Mheshimiwa Spika,ukiangalia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2019/20 uk. 57 inaonesha kuwa benki ilitoa mikopo kwa wakulima 1,049,370 wa mahindi, mpunga, shayiri, kahawa, korosho, karafuu, miwa, mbogamboga, ufugaji wa samaki n.k. yenye thamani ya shilingi bilioni 95.1 tu, hapa tunataka kujenga Tanzania ya viwanda lakini hatuoni ni kwa jinsi gani benki hii inaenda kujenga Tanzania ya viwanda.

44. Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni kwamba; kutoa mikopo kwa wakulima bila ya kuwa na utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa bei za mazao zitaweza kurudisha mkopo na kumfanya mkopaji kuendelea kwenye kilimo ni njia moja wapo ya kumfukarisha mkulima.

45. Mheshimiwa Spika, ni hatari sana kwa mkulima kukopa fedha kwa ajili ya uzalishaji na baadae akawekewa vikwazo katika uuzaji wa mazao yake, hii ni kinyume na misingi ya biashara. Jambo hili ndilo lililllotokea kwa wakulima wa mahindi, kahawa, korosho na pamba kwa kuwalazimisha kuuza kwenye ushirika badala ya kuuza kwa makampuni binafsi kulingana na ushindani wa bei inayotolewa baina ya makampuni hayo.

46. Mheshimiwa Spika, ukiangalia Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/20 uk 56 kuhusu Benki ya Uwekezaji (TIB) kuwa imetoa mikopo kwa sekta ya kilimo yenye thamani ya shilingi bilioni 698.6, lakini kwa taarifa ya Benki hiyo iliyotolewa kwenye Kamati ya PAC inaonesha kuwa; Benki inadai (mikopo chechefu) kiasi cha shilingi 230,669,526,932.24 yenye dhamana zenye thamani ya shilingi 550,832,170,833 na hivyo kuifanya benki hiyo kuwa na mikopo chechefu ya 35% kwa Desemba 2016 (2015: 14%) ikiwa ni ongezeko la kama 150%. Kiwango hiki ni kikubwa sana kulinganisha na kiwango kilichotolewa na BOT kuwa mikopo chechefu cha 24% kwa Benki hiyo.

47. Mheshimiwa Spika, taarifa hii ya benki kutoa fedha hizo zote kwenye sekta ya kilimo ni vyema ikaonekana kama imetolewa kwa miradi inayotekelezwa na Serikali na pia ni

miradi gani na iko wapi, au ni kwa sekta binafsi na ni miradi ya aina gani? Jambo hili linasaidia hata Waheshimiwa Wabunge kufanyakazi yetu ya tathimni na ufuatiliaji kwa karibu jambo ambalo litaleta tija zaidi.

48. Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba kilimo kama nguzo kuu katika uchumi wa Tanzania ni lazima kiendeshwe kwa kuzingatia misingi ya uendeshwaji wa uchumi wa soko jamii; ambapo msingi wa mfumo huu ni kujenga na kuruhusu ushindani, soko huria, kuruhusu watu na sekta binafsi kumiliki mali na kuendesha uchumi wa nchi. Kwa msingi huo wa ushiriki wa sekta binafsi uwekezaji wa ndani na nje utazinufaisha pande zote katika makubaliano ya kibiashara. Rejea Sera ya CHADEMA uk.15, 79 & 80

F. UHUSIANO KATI YA VIWANDA NA KILIMO

49. Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ina uhusiano wa moja kwa moja na viwanda na kila kimoja kinategemea kingine ili kukua, kwani malighafi za sekta zote zinategemeana. Kilimo cha miwa ni malighafi ya viwanda vya sukari; viwanda vya ngozi vinategemea mifugo; viwanda vya maziwa vinategemea mifugo (ng'ombe, mbuzi na kondoo), viwanda vya mafuta ya kula vinategemea kilimo cha alizeti, ufuta, soybeans n.k.; viwanda vya nguo vinategemea kilimo cha pamba; uzalishaji wa sigara unategemea kilimo cha tumbaku. Ni ukweli kwamba viwanda haviwezi kushamiri bila ya kilimo kushamiri, kwani hizi sekta zina mahusiano ya moja kwa moja.

50. Mheshimiwa Spika, ukweli uliopo kwa upande wa Tanzania ni kuwa mahusiano hayo ya moja kwa moja hayapo, kutokana na kwamba mazao karibu yote yanauzwa nje yakiwa ghafi kutokana na kutokuwepo kwa viwanda vya kuchakata mazao hayo. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema huu ni udhaifu kwa Serikali kwa kutokuwa na vipaumbele na kusimamia vipaumbele hivyo, kwa kuona ni sekta gani inatoa ajira nyingi na ni watu wangapi wanaitegemea ili kuendesha maisha yao.

51. Mheshimiwa Spika, mahusiano hayo ya kilimo na viwanda hayawezi kufanikiwa na kuwa na tija kama sekta binafsi haikupewa nafasi yake katika kuhakikisha biashara baina ya pande zote mbili zinanufaika, kwanza kwa mkulima kupewa uhakika wa soko na bei ya kumwezesha kuzalisha kwa faida na hivyo ubora wa mazao yake utakuwa wenye uhakika.

52. Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, CHADEMA katika sera yetu ukurasa wa 55 & 56 pamoja na 59& 60 tumeeleza ni kwa jinsi gani tutakifanya kilimo kuwa cha kisasa zaidi ili pande zote washirika kunufaika, kwa maendeleo ya Tanzania tunayoitaka.

G. PEMBEJEO- (Agricultural inputs)

53. Mheshimiwa Spika, Ili Tanzania tufanikiwe, tunahitaji kuboresha tija katika mashamba yetu, mashamba yetu mengi yana tija ndogo (kwa mfano, mavuno ya mahindi kwa wastani ni mara tano chini ya yale ya nchi zilizoendelea) ilihali kuna nafasi kubwa ya kufanya maboresho. Iwapo katika kipindi cha muda mrefu ujao sekta ya kilimo yenye tija itatumia wafanyakazi wachache zaidi, basi uwiano kati ya nguvu kazi na teknolojia mpya unaweza kukuzwa wakati wa kipindi cha mpito. Uzalishaji bora wa chakula pia utasaidia kukuza maendeleo ya viwanda vya usindikaji na biashara za bidhaa za kilimo – sekta inayoweza kutoa ajira nyingi nchini Tanzania. Ili kilimo kiwe na tija tunahitaji kuwa na matumizi sahihi ya teknolojia kwa kiwango kikubwa na matumizi ya Pembejeo za kilimo.

54. Mheshimiwa Spika, tunapoongelea pembejeo (Agricultural Inputs) katika mustakabali wa kilimo bora na cha kisasa hapa nchini tunajikita katika mambo makuu matatu ambayo ni; ***upatikanaji wa pembejeo, usambazaji wa pembejeo na matumizi yake***. Pembejeo zinazohitajika kwa wakulima ni mbegu bora, mbolea na madawa.

55. Mheshimiwa Spika, pembejeo hizo kwa Tanzania kimekuwa ni kilio kikubwa kwa wakulima kiasi kwamba watu wametumia mwanya huo kujinufaisha binafsi kwa kupeleka

kwa wakulima pembejeo feki na mwisho wa siku ni wakulima kupata hasara na umasikini kwa wakulima kuzidi kuimarika.

56. Mheshimiwa Spika, Historia inatuonesha kuwa sekta ndogo hii ya pembejeo imekuwa ikifanyiwa majaribio mengi na Serikali kuona ni mfumo upi utafaa, kwa kuanzia uwepo wa viwanda vya mbolea vya Serikali, Serikali kuhodhi ununuzi wa mbolea nje, lakini yote imeshindikana na matatizo yanabakia **pale pale.**

57. Aidha, Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa Serikali kwenye pembejeo umekuwa ukishuka kwani kwa msimu wa 2008/9 ulikuwa ni asilimia 33.9 ya bajeti ya kilimo (mazao) na mwaka 2013/14 ukawa ni asilimia 8.4; matatizo mengine ya sekta hii ndogo ya pembejeo ni; kukosekana na uhakika wa upatikanaji wa pembejeo; kucheleweshwa kwa pembejeo za ruzuku ambazo wengi wanazitegemea ***(Japokuwa siku hizi hakuna pembejeo za ruzuku);*** ulanguzi na mbolea zisizo na ubora kupelekwa kwa wakulima.

58. Mheshimiwa Spika, imebainika kuwa matatizo hayo pia yanachangiwa na kutokuwepo kwa watendaji wa kutosha na mazingira magumu ya watendaji yanayochangiwa na ufinyu wa bajeti inayotolewa. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema matatizo hayo hayawezi kumalizika bila ya uhusishwaji kikamilifu kwa sekta binafsi, hivyo basi ni muhimu sana sekta binafsi ikawa ni kiungo kikuu katika kukibadilisha kilimo chetu kuwa cha kisasa na cha kibiashara na endelevu.

H. HUDUMA ZA UGHANI-(Extension Services)

59. Mheshimiwa Spika, sera ya kilimo ya mwaka 2013 na mwongozo vinaeleza bayana kwamba kila kijiji kinahitajika kuwa na afisa ugani mmoja. Aidha, uwiano unaohitajika kati ya afisa ugani na idadi ya wakulima ni 1:600; Utafiti uliyofanyika katika maeneo ya Singida na Chamwino unaonyesha kwamba afisa ugani mmoja huhudumia kijiji zaidi ya kimoja au kata.

60. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa rasilimali watu inayotakiwa kwa sekta ya kilimo, watumishi wenye sifa mbalimbali katika kilimo wanaohitajika ni 19,228 lakini waliopo ni 8,756 sawa na 45.4%. Hii ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Jukwaa la Wadau wa Kilimo wasio wa Kiserikali (Agricultural Non – State Actors Forum – ANSAF)mwaka 2017. Utafiti huo unaonyesha kwamba; watumishi wenye taaluma kuanzia ngazi ya shahada na kuendelea mahitaji halisi ni 2,746 lakini waliopo ni 1,530 ambao ni sawa na 55.7%. Wakati wenye taaluma ngazi ya Cheti na Diploma mahitaji ni 16,542 lakini waliopo ni 7,226 sawa na 43.7%

61. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maafisa ugani kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2013 waliokuwepo ni 7,974 wakati Tanzania ina vijiji vilivyosajiliwa 15,082. Wakati kuna upungufu huo; Muongozo wa Serikali kwa maafisa ugani ni kila kijiji kimoja kuwa na afisa ugani mmoja.

62. Mheshimiwa Spika, Changamoto zilizopo mbali ya uchache/upungufu huo zinazokabili huduma ya ugani ni pamoja na kufanya kazi katika mazingira magumu, mfano: ukosefu wa vitendea kazi (mfano; pikipiki, vifaa vya kupimia udongo na mafunzo ili kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia na mabadiliko ya tabianchi.

63. Mheshimiwa Spika, maafisa ugani kupangiwa majukumu ambayo ni nje na ueledi wao, mfano kuwa watendaji wa vijiji/kata.Hata hivyo, utafiti unaonyesha kwamba maafisa ugani hawatimizi wajibu na majukumu yao vizuri, muda mwingi wanafanya kazi ofisini au shughuli binafsi. Hali hii husababisha njia zisizo bora kwenye kilimo na kuchangia kushuka kwa maendeleo ya sekta ya kilimo nchini

I. MAZAO MAKUU HAPA NCHINI

64. Mheshimiwa Spika, kwa sasa mazao yote yanayolimwa hapa nchini tunaweza kuyaita kuwa ni mazao ya biashara, japokuwa kuna mazao makuu ya biashara(traditional cash crops) ambayo ni Pamba; Korosho; Kahawa; Mkonge; Chai; na Tumbaku.

65. Mheshimiwa Spika, kwa muktadha wa hotuba hii tutajikita katika baadhi ya mazao ambayo ni kichocheo kikubwa cha kukua au kudumaa kwa uchumi wa nchi yetu.

i. Pamba;

66. Mheshimiwa Spika, zao la Pamba ni zao ambalo linalimwa na wakulima wadogo kati ya 350 na 500,000 katika Wilaya 49 za Mikoa 17 ya Tanzania Bara, japokuwa asilimia 80 ya Pamba yote inalimwa katika mikoa minne ya Simiyu, Shinyanga, Singida na Mwanza. Hii ni kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba Ndg. Marco Mtunga, wakati akitoa taarifa kwa wadau wa Pamba.

67. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa Pamba unaathiriwa kwa kiwango kikubwa na changamoto zifuatazo:- kucheleweshwa kwa pembejeo; ubora hafifu wa pembejeo (mbegu na madawa); kutokutabirika kwa bei kwenye soko la dunia na bei elekezi kupangwa bila wakulima kushirikishwa; huduma za ugani kuwa duni na hivyo wakulima kutokufuata mahitaji sahihi ya kilimo cha Pamba; matumizi hafifu ya teknolojia katika kilimo cha Pamba (Use of Agricultural mechanization); Kutokuwepo kwa vyama vya ushirika vilivyo imara; Mauzo ya Pamba ghafi kwenda nje inanyima fursa ya ajira kwa watanzania wengi na hivyo kuongeza kipato chao.

68. Mheshimiwa Spika, changamoto hizo kwenye zao la Pamba zimekuwepo kwa kipindi kirefu na Serikali imeshindwa kuzitafutia ufumbuzi. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa mustakabali wa kilimo biashara upo katika soko la mazao na bidhaa za kilimo, ambapo wakulima na wanunuzi wataendesha shughuli zao za kibiashara katika mazingira yanayotabirika, na kwamba wakulima wanaweza kupata bei nzuri kwa mazao yao.

69. Mheshimiwa Spika,Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa katika soko kama hilo litasaidia matumizi ya teknolojia katika kuboresha shughuli za kilimo ili kukidhi viwango vya ubora vya kimataifa na hivyo kuhakikisha kwamba walaji wanapata bidhaa bora.

ii. Kahawa

70. Mheshimiwa Spika, Kahawa ni zao la biashara linalolimwa hapa nchini katika mikoa ya Songwe, Njombe-(Ludewa), Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Ruvuma- (Mbinga), Kagera, Tanga, Iringa, Morogoro, Kigoma, Manyara, Mwanza, Rukwa na Mara. Inakadiriwa kuwa jumla ya eneo la hekta 265,000 ndilo linatumika kwa ajili ya kilimo cha Kahawa aina ya ARABICA NA ROBUSTA ambazo ndizo zinalimwa sana hapa Tanzania.

71. Mheshimiwa Spika, Kahawa aina ya Arabica inachukua asilimia 70 ya uzalishaji wote wa Kahawa hapa nchini. Aina hii ya Kahawa inalimwa kwa wingi katika Mikoa ya Songwe, Mbeya, Ruvuma na Kilimanjaro. Robusta inazalishwa kwa asilimia 30 na inalimwa zaidi katika Mkoa wa Kagera.

72. Mheshimiwa Spika, Kahawa inalimwa na takriban familia 450,000 kwa Mikoa ambayo imeainishwa hapo awali na familia hizo zinachangia takriban asilimia 90 ya uzalishaji wote wa Kahawa hapa nchini. Asilimia 10 iliyobaki katika uzalishaji inachangiwa na mashamba makubwa yanayomilikiwa na watu au Kampuni binafsi. Kwa ujumla asilimia 6 ya idadi ya watu wote Tanzania (ambayo kwa sasa ni takriban watu milioni 55) wanategemea uchumi wa Kilimo cha Kahawa kuendesha maisha yao.

73. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya nne kwa uzalishaji wa Kahawa Afrika baada ya Ethiopia, Ivory Coast na Uganda ambapo kila mwaka huzalisha wastani wa tani 46,000 hadi 60,000 huku mkoa wa Kagera ukizalisha takribani tani 12,131.

74. Mheshimiwa Spika, uzalishaji Kahawa Duniani kwa msimu wa 2016/17 ulifikia magunia milioni 158.93. sawa na tani milioni 9.535 hili ni ongezeko la asilimia 0.8 ikilinganishwa na msimu uliopita wa mwaka 2015/16. Arabika ilizalishwa magunia milioni 98.84 (62%) na Robusta magunia milioni 60.10 (38%).

75. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania uzalishaji kwa mwaka 2014/15 jumla zilizalishwa tani 42,768; mwaka

2015/16 tani 60,188; mwaka 2016/17 tani 47,591.5; mwaka 2017/18 tani 41,679.4

76. Mheshimiwa Spika, Kwa takwimu hizo za uzalishaji wa Kahawa hapa nchini ni dhahiri kuwa kuna tatizo sehemu katika sekta ndogo ya Kahawa, na hivyo ni jukumu letu kama wawakilishi wa wananchi kulipatia ufumbuzi tatizo hilo.

77. Mheshimiwa Spika, Ukirejea nyaraka za watatifi wanasema kuwa sekta ndogo ya Kahawa imekuwa na matatizo mengi miongoni mwake ni hali ya hewa kubadilika sana, kukosekana kwa miundombinu imara ya umwagiliaji wa mashamba (Hili ni kwa mashamba makubwa) na mibuni kuzeeka na hivyo uzalishaji kuwa chini. Aidha kukosekana kwa uwekezaji wa kutosha katika ufafiti wa magonjwa ya kahawa na huduma duni za ugani kumeathiri uzalishaji wa zao hili.

78. Mheshimiwa Spika, mbali ya changamoto ya utafiti kwenye zao la kahawa lakini tatizo kubwa zaidi linalowakumba wakulima ni kutokuwepo kwa soko la uhakika la kuweza kununua kahawa kwa bei ambayo italifanya zao hilo kuendelea kulimwa kitaalam zaidi.

79. Mheshimiwa Spika, ukweli ni kuwa changamoto za soko zilikuwepo hata miaka iliyopita, lakini kwa sasa tatizo limekuwa kubwa zaidi kwa sababu limeibuka suala la AMCOS kuhodhi tena soko la kahawa kwa wakulima na hivyo kuminya fursa ya wao kuchagua bei kulingana na gharama za uzalishaji. Kambi Rasmi bado inasisitiza katika uwepo wa mfumo huru wa soko ambapo mkulima na mnunuzi watakutana na kupanga bei ili kukidha gharama za uzalishaji na kila upande unufaike na biashara hiyo.

iii. Korosho

80. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa takwimu za Randama ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2018/19 zinaonesha kwamba, mwenendo wa uzalishaji wa zao la korosho kwa miaka mitatu kuanzia msimu wa mwaka 2015/ 16 hadi msimu wa 2018/19 umekuwa unapanda ambapo

mwaka 2015/16 uzalishaji ulikuwa tani 155,416; 2016/17 tani 265,238 na 2017/18 uzalishaji ulifikia tani 311,899. Aidha, matarajio kwa mwaka 2018/19 yalikuwa ni kuzalisha tani 350,000.

81. Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinaonesha kwamba, wakulima wadogo wadogo takribani 280,000 wanaendesha maisha yao na familia zao kutegemea moja kwa moja zao la korosho kwa kulima kati ya eka moja hadi mbili na kufanya eneo linalolimwa zao hilo kufikia ekari 400,000. Na kwa sasa eneo hilo litakuwa limeongezeka kutokana na mwamko wa wananchi kulima zao hilo.

82. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Korosho (***Cashewnut Industry Act (Cap, 203),*** inasema kuwa asilimia 65 ya kodi ya mauzo nje yarudishwe kwa wakulima kupitia Bodi ya Korosho (CBT) na Serikali ibakie na asilimia 35. Mgawo wa hizo asilimia 65 wa export levy, matumizi yake makubwa ni ununuzi wa pembejeo za kilimo cha Korosho na kuendeleza utafiti kwenye zao la Korosho.

83. Mheshimiwa Spika, katika hali ambayo mpaka sasa haieleweki; Serikali ilivunja Bodi ya Korosho; na kutaifisha ile asilimia 65 ya kodi ya mauzo ya korosho nje; na pia kuingilia biashara ya korosho kwa kuwazuia wanunuzi binafsi kununua korosho. Matokeo yake ni kwamba hakuna mauzo ya korosho nje ya nchi yaliyofanyika mpaka sasa; Serikali ilichofanya ni kununua korosho kwa wananchi– tena kwa mkopo kwa ahadi ya shilingi 3,300 kwa kilo lakini wakati wa kulipa bei hiyo ikapungua kwa madai kwamba korosho hazina ubora.

84. Mheshimiwa Spika,uamuzi wa Serikali kununua korosho toka kwa wakulima badala ya kuhusisha makampuni binafsi umeligharimu taifa letu kwa kukosa fedha za kigeni, mfano kwa mwaka wa fedha 2017/18 fedha za kigeni zilizotokana na korosho zilikuwa ni dola za kimarekani milioni 965, kwa mwaka huu 2018/19 unaoishia hadi sasa ni Zero. Kodi ya mauzo nje **(export levy)** kwa mwaka 2017/18 ilikuwa ni dola za kimarekani milioni 200; kwa mwaka 2018/19 hakuna chochote.

85. Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya utatanishi Serikali ilisaini mkataba wa kuuza korosho tani laki moja na kampuni ya Indo Power ya Kenya, mkataba ambao haukutekelezeka licha ya kupigiwa debe na Waziri wa Katiba na Sheria wa wakati huo Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi(Mb) na Gavana wa Benki Kuu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwawajibisha wahusika wote kwa kulipotosha Taifa na kuliingizia hasara kubwa kutokana na mkataba ambao haukufanyiwa upembuzi yakinifu.

86. Mheshimiwa Spika,kitendo cha kuvunja Bodi ya Korosho – chombo ambacho kiliundwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge bila kuleta Bungeni muswada wa sheria wa kuifuta sheria hiyo mosi ni ukiukwaji wa katiba, pili ni dharau kwa Bunge; lakini mbaya zaidi ni hujuma kwa wakulima wa zao la korosho ambao mpaka sasa haijulikani zao lao linaratibiwa na chombo gani. Kwa maneno mengine zao la korosho ni kama vile halina mwenyewe na wakulima wa korosho wamekuwa kama kondoo wasio na mchungaji.

87. Mheshimiwa Spika, kutokana na mchanganyiko huo wa mambo kumekuwa pia na sintofahamu ya biashara ya korosho katika msimu huu ambapo wakulima wengi wameshindwa kupata fedha kulingana na mauzo ya korosho zao. Jambo la ajabu ni kwamba korosho ambazo zilikuwa zimechukuliwa na Serikali na kwa maana kwamba kilichokuwa kikisubiriwa ni wananchi kulipwa fedha zao zimeanza kurejeshwa kwa wenyewe kwa madai kuwa hazina ubora unaostahili. Na pia wakulima wenye korosho nyingi kukataliwa kulipwa kwa kigezo cha uhakiki wa mashamba.

88. Mheshimiwa Spika, ni ajabu kwamba; kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania tunakwenda kuhakiki shamba la mkulima kisa tu ana mazao mengi**.** Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa uzalishaji mkubwa ni neema kwa nchi kwa kuwa wingi wa korosho ndani ya nchi maana yake ni kupata fedha za kigeni kwa wingi tutakapouza nje na hivyo kukuza uchumi wetu. Inashangaza sana kwa Serikali imeendelea kuweka vikwazo vingi sana katika biashara nzima ya zao la korosho.

89. Mheshimiwa Spika, katika muendelezo wa mauzo na malipo ya korosho, wakulima katika Wilaya za Ruangwa, Kitangali-Newala Vijijini na Mjini wakulima walikwishauza korosho zao lakini kutokana na wasombaji kutokujua jinsi korosho zinavyotakiwa kutunzwa kwenye maghala, zilinyeshewa na mvua na kuharibika. Hivyo iliwalazimu wapokee korosho toka kwa mnunuzi (Serikali) ili wakulima wachambue upya na kuuza upya. Katika kadhia hiyo wakulima wamepata hasara kubwa sana, kwani mkulima aliyekuwa ameuza kilo 500 baada ya kurudishiwa mzigo wa kilo hizo ili kuchambua upya anajikuta anauza upya kilo 300 na hivyo kufanya kilo 200 kuwa ni hasara.

90. Mheshimiwa Spika, mbali ya hasara iliyotokana na uzembe wa utunzaji, lakini wakulima wengi wakienda kudai fedha zao wanawekwa ndani, na hilo limekuwa ni kero kubwa sana kwa wakulima kwa maeneo mengi ya mikoa inayolima korosho.

91. Mheshimiwa Spika,kwa kuwa lengo la nchi ni kuwa na Tanzania ya viwanda, ni muda mwafaka sasa kuhakikisha viwanda vinakuwa na uhakika wa malighafi, na malighafi itapatikana ndani au nje ya mipaka ya nchi yetu.

92. Mheshimiwa Spika, Uchumi wa Viwanda kwa nchi hii utafikiwa tu, pale bei za mazao ya kilimo zitakapokuwa nzuri na hivyo kumfanya mkulima kuongeza uzalishaji kwa kutumia teknolojia bora na kisasa. Kambi Rasmi tunaamini ***kwamba mustakabali wa kilimo cha kisasa, endelevu na cha kibiashara upo katika soko la mazao ya bidhaa za kilimo, ambapo wakulima na wanunuzi wataendesha shughuli zao za kibiashara katika mazingira yanayotabirika***,na kwamba wakulima wanaweza kupata bei nzuri kwa mazao yao. Rejea Sera ya Chadema uk.55 sura ya 9.3 Biashara ya Mazao na Bidhaa za Kilimo.

iv. MIWA

93. Mheshimiwa Spika, Kilimo cha miwa ni kilimo chenye tija kwa mkulima, kilimo hiki kinaweza kufanywa na mtu yeyote yule aidha awe ameajiriwa au laaa! Jambo la msingi ni

kuhakikisha anajitoa kikamilifu katika kuhakikisha anawekeza akili yake katika kulima kilimo hiki.

94. Mheshimiwa Spika, Wazalishaji wakubwa wa sukari nchini ni: Kilombero Sugar Co. Ltd.; TPC Ltd.; Kagera Sugar Ltd. na Mtibwa Sugar Estates Ltd. Na katika maeneo hayo yote kuna wazalishaji wa nje. Kwa Kampuni ya Sukari ya Kilombero - wakulima wa nje 8,500 wanazalisha 43% ya miwa inayokamuliwa na viwanda vya K1 na K2.

95. Mheshimiwa Spika, Uzalishaji wa sukari ya matumizi ya nyumbani (consumption sugar) umeongezeka mara nne kutoka tani 80,000 (1997/98) kabla ya ubinafsishaji na kufikia tani 330,000 kwa msimu wa 2016/17. Uzalishaji wa sukari nchini huchangia 72% ya mahitaji ya sukari ya matumizi ya nyumbani. Kuna wakulima wa miwa wa nje (Outgrowers) 15,000 waliosajiliwa wanaochangia asilimia thelathini (30%) ya miwa inayosagwa kwa uzalishaji sukari. Hutoa ajira 18,000 kwa wafanyakazi walioajiriwa viwandani na katika mashamba ya miwa. Mapato ya shilingi bilioni 45 kwa wakulima wa nje kila mwaka. Malipo ya zaidi ya shilingi bilioni 100 ya kodi za Serikali kila mwaka.

96. Mheshimiwa Spika, Katika programu iliyokuwa inajulikana kama Matokeo Makubwa Sasa ("Big Results Now"), serikali ilitaka kuongeza uzalishaji wa sukari. Serikali iliahidi kushirikiana na wawekezaji binafsi kuongeza mashamba makubwa ya miwa. Katika program maalum nyingine iitwayo "Southern Agricultural Growth Corridor", au SAGCOT, serikali ilikuwa na mpango kwa ajili ya wawekezaji binafsi kuanzisha na kupanua mashamba ya miwa na mpango wa wakulima wa nje katika Kijiji cha Ruipa, karibu na Ifakara. Sheria ya Sukari, hairuhusu kwa makampuni mengine kujenga kiwanda cha miwa ndani ya eneo la km 40 za eneo la Kampuni ya Sukari Kilombero iliyopo Kidatu.

97. Mheshimiwa Spika, Makadirio ya mahitaji ya Sukari: Mahitaji ya Sukari kwa matumizi ya nyumbani na viwandani yataongezeka kutoka tani 580,000 mwaka 2016/17 hadi tani 695,000 - 755,000 mwaka 2020/21. **Sukari kwa matumizi ya**

nyumbani: Mahitaji yataongezeka kutoka tani 445,000 mwaka 2016/17 na kufikia tani 535,000 – 580,000 ifikapo mwaka 2020/21. Sukari kwa matumizi ya viwandani: Mahitaji yataongezeka kutoka tani 135,000 hadi tani 160,000 – 175,000 ifikapo mwaka 2020/21[4].

98. Mheshimiwa Spika, Sukari ni bidhaa nyeti na yenye changamoto nyingi sehemu nyingi duniani. Ni muhimu mno kuanisha uzalishaji sukari hapa nchini kwa siku za usoni kwa kutathmini mustakabali wa masoko ya sukari ya EAC, SADC, na EU. Ieleweke kwamba karibu nchi zote zinazozalisha sukari duniani, serikali zake hulinda wazalishaji wa ndani kwa njia mbalibali, hasa, kiwango cha sukari inayoingizwa nchini na kwa ushuru wa forodha (import duty).

99. Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumesikia kuwa Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema kwamba; *"baada ya kufanya mazungumzo na viwanda vinavyozalisha sukari nchini, serikali inatoa ruhusa kwa viwanda vya sukari nchini kuagiza nje sukari pungufu ambayo ni tani 30,000 pekee na viwanda hivyo kufanya biashara na wafanyabiashara wengine nje ya nchi kutokana na viwanda hivyo kuonyesha juhudi katika uzalishaji"[5].*

100. Mheshimiwa Spika, Mahitaji ya sukari mwaka mzima ni tani 670,000 ambapo viwanda hutumia tani 155,000 na matumizi ya kawaida huwa ni tani 515,000. Kwa mujibu wa Waziri huyo, Bodi ya Sukari imetoa ripoti Februari mwaka huu na kubaini kuwa jumla ya sukari iliyopo kwa wafanyabiashara na kwenye hifadhi ni tani 129,228. Mheshimiwa Hasunga amevitaja viwanda vitano vinavyozalisha sukari nchini kuwa ni TPC Moshi, Kagera Sugar, Mtibwa, Kilombero na kiwanda kidogo cha Manyara. Viwanda hivyo havizalishi sukari ya viwandani.

---

[4] Wasilisho la **Katibu Mtendaji -Chama cha Wazalishaji Sukari Tanzania (TSPA), 06 Desemba 2017**

[5] https://pesatu.com/viwanda/uzalishaji/ruksa-viwanda-vya-sukari-kuagiza-nje/

101. Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kuna changamoto nyingi kwenye kilimo cha miwa na sukari yenyewe, lakini kitendo cha Serikali kutoa vibali kwa viwanda kuagiza sukari toka nje bila kuweka utaratibu madhubuti na wawazi wa kudhibiti kiasi kinachoagizwa, maana yake ni kuua kilimo cha miwa hapa nchini hasa wakulima wa nje. Tukumbuke kwamba sukari toka nje inazalishwa kwa gharama za chini kulinganishwa na uzalishaji wa sukari yetu, hivyo kutoa upenyo wa viwanda kuagiza ni dhahiri kuwa mahitaji ya miwa toka kwa wakulima yatapungua sana na mipango na uhamasishaji kwa wananchi kulima miwa itakuwa ni kuwaingiza kwenye shimo la hasara kubwa na hivyo kuwaletea umasikini.

J. FURSA ZILIZOPOTEA

102. MheshimiwaSpika,takwimu za kutisha zinaonesha nchi yetu inaendelea kuagiza bidhaa za maziwa, nyama, samaki, mafuta ya kura, ngano, mchele na matufa ya kula, hasa mawese pamoja na sukari. Inakadiriwa kwa mwaka, nchi yetu huagiza bidhaa za chakula zenye gharama ya takribani Tzs. 1,345 bilioni. Kiwango hiki ni karibia mara tano ya bajeti ya mwaka ya Wizara ya Kilimo. Bidhaa za mafuta ya kula inagharimu zaidi ya dola za Kimarekani 250 milioni, wakati bidhaa za sukari, ngano, maziwa na nyinginezo hugharimu kiwango kikubwa pia cha fedha za kigeni. Wakati ambapo serikali ya Awamu ya Tano inajipambanua na suala la viwanda, ni lazima Wizara ya Viwanda na Kilimo zilete mkakati wenye kuonesha uratibu halisi wa sekta/minyororo ya thamani ya kimkakati yenye uwezo wa kuleta mabadiliko kwa wazalishaji, wafanyabiashara, wachakataji na uchumi wa nchi kwa ujumla.

K. MABADILIKO YA TABIANCHI NA KILIMO

103. Mheshimiwa Spika,Takwimu zilizotolewa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa, FAO, Jumatano tarehe 11 Julai 2018 zinaonesha kwamba kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi, hadi kufikia mwaka 2050, shughuli za uvuvi baharini hasa katika nchi maskini zaidi duniani,

zitaathirika sana, sanjari na kupungua kwa kiwango cha maji baridi duniani. Hali hii itakuwa na madhara makubwa sana kwa mamilioni ya watu wanaotegemea kwa kiasi kikubwa kupata mahitaji yao msingi kutoka katika sekta ya uvuvi baharini. FAO inasema, waathirika wakuu wa athari za mabadiliko ya tabianchi daima wataendelea kuwa ni maskini.

104. Mheshimiwa Spika,Nchi tatu za Afrika ya Mashariki za Tanzania, Kenya na Uganda pamoja na mataifa ya Pwani ya Pembe yataendelea kuwa na upungufu wa mvua kwa kipindi chote cha mwezi wa nne na hali inatarajia kuwa mbaya kutokana na kipindi cha ukame kuendelea na hali isiyo yakawaida ya joto kuwa juu sana

105. Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ilitolewa baada ya kufanyika kwa kikao cha mamlaka ya maendeleo ya mataifa ya ***IGAD on Climate Prediction and Application Centre (ICPAC)*** kuwa uwezekano mkubwa wa ukame ambao hautakuwa wa kawaida kwa mikoa yote ya mwambao wa Tanzania, Magharibi ya Kenya, Kusini na Kusini Mashariki mwa Ethiopia, Ukanda wa Kati na Kaskazini Mashariki mwa Somalia, Uganda na Sudani ya Kusini. Maeneo hayo yaliyotajwa kwenye mataifa hayo yatakuwa na kipindi cha ukame na joto kuwa la juu kuliko kawaida na hivyo kuwa na athari kwenye malisho, upatikanaji wa maji kwa matumizi ya binadamu, mifugo na wanyamapori.

106. Mheshimiwa Spika, hili limejitokeza pia kutokana na kukosekana kwa mvua za vuli za Oktoba hadi Desemba, na kufuatiwa na kipindi kisicho cha kawaida cha joto kuwa kali kuanzia mwezi Januari 2019, jambo ambalo limeathiri sana rasilimali za malisho na hivyo kuanza kuathiri maisha ya wananchi ambao kwa kiwango kikubwa mifugo ndio maisha yao.

107. Mheshimiwa Spika, Hii sio kuwa inaathiri jamii za wafugaji tu bali inaathiri pia wakulima waishio kwenye maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi na pia waishio kwenye ukanda wa kati wa nchi yetu ya Tanzania. Jambo hili linaleta madhara makubwa hasa kwa wakulima wa maeneo ya Wilaya za

Mkoa wa Morogoro, Singida, Dodoma; Pia kwa ukanda wa Magharibi kwa Mikoa ya Tabora na Kigoma hali ya upatikanaji wa mvua imekuwa mbaya sana kiasi kwamba hasara kubwa imewakumba wakulima ambao tayari walishafanya maadalizi ya msimu huu wa kilimo.

108. Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, ni kuwa usalama wa chakula ambao pia ni usalama wa nchi kwa mwaka ujao uko mashakani, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuanza kuiona hali hiyo na kuiwekea mkakati wa utekelezaji mapema na sio kusubiri hadi janga litokee.

L. TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI (Fungu 05)

109. Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 25.82 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 6 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 19.82 ni fedha za nje.

110. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari 2019 shilingi bilioni 5.27 zilikuwa zimetolewa sawa na asilimia 20.4 ya fedha zote za maendeleo zilizokuwa zimeidhinishwa. Licha ya utekelezaji mdogo wa bajeti katika eneo hili la umwagiliaji, bado Serikali imeendelea kuwa tegemezi kwa wahisani wa maendeleo kutoka nje.

111. Mheshimiwa Spika, kutokana na fedha kidogo zilizotolewa kwa Tume, miradi mingi ya umwagiliaji imeshindwa kutekelezwa na mingine kuchukua muda mrefu kukamilika hivyo kuondoa maana halisi ya kupunguza utegemezi wa mvua katika kilimo. Hivyo basi; **Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuboresha zaidi mazingira ya utendaji kwa Tume ili eneo hili la umwagiliaji liweze kuokoa zaidi ya dola za Kimarekani milioni 800 (Shilingi trilioni 1.84) zinazotumika kuagiza chakula kutoka nje ya nchi kila mwaka.**

M. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2018/19 NA MPANGO WA MWAKA 2019/20

112. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/19 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 98,119,516,000.00 kama fedha za miradi ya maendeleo kwa Fungu 43, kati ya fedha hizo

shilingi 82,000,000,000.00 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi 16,119,516,000.00 zilikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019, shilingi 41,222,448,778.00, sawa na asilimia 42 ya fedha zote za bajeti ya maendeleo kwa fungu 43 zilizokuwa zimeidhinishwa ndizo zilikuwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo fedha za ndani zilikuwa shilingi 39,964,621,000.00 na fedha za nje ni shilingi 1,257,827,778.00. Fedha za ndani zilizotolewa zikiwa sawa na asilimia 48.74 ya bajeti ya fedha za ndani na asilimia 7.8 ya fedha za nje.

113. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/20 Wizara Fungu 43 inaomba jumla ya shilingi 208,115,500,575.00 Kati ya fedha hizo shilingi 143,577,033,140 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na shilingi 64,538,467,435.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 17,992,293,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara.

114. Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo zinaoombwa mwaka 2019/20 ni ongezeko la shilingi 45,457,517,140.00 sawa na asilimia 31.66 kwa kulinganisha na zile zilizoombwa mwaka wa fedha 2018/19.

115. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 05 iliidhinishiwa jumla ya shilingi **53,626,690,195.** Kati ya fedha hizo shilingi **232,116,195** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **53,394,574,000** ni fedha kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31, Machi, 2016 fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha shilingi **96,884,227** zilitolewa ambayo ni sawa na asilimia 42 ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge. Fedha za maendeleo kiasi cha shilingi **5,131,032,985** zilitolewa ambazo ni sawa na asilimia 10 ya fedha zilizoidhinishwa. (Fedha hizo ni za nje tu na hakuna fedha za ndani zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo).

116. Aidha, Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/ 2016, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliidhinishiwa kiasi cha shilingi **53, 394, 574,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo wakati mahitaji halisi yanakadiriwa kufikia shilingi **400,000,000,000.** Uwiano huu hauonyeshi dhamira ya dhati ya Serikali ya kutambua na kutumia ipasavyo fursa zinazotokana na kilimo cha umwagiliaji. Aidha,Fungu 05

lilitengewa jumla ya shilingi **63,412,358,800.** Kati ya fedha hizo, shilingi **58,905,747,200** zilikuwa ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. *Rejea taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo ya mwaka 2016/17*

N. HITIMISHO

117. Mheshimiwa Spika,

Kwa kuwa; Kambi Rasmi ya Upinzani inakichukulia kilimo cha kisasa kama matumizi ya mbinu za kisasa za kilimo ambazo zinahusisha matumizi ya madawa ya kilimo, na teknolojia ya kisasa katika mchakato mzima wa uzalishaji shambani;

Na kwa kuwa; Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba kilimo cha kisasa kinatumia zaidi pembejeo kutoka kwa wasambazaji binafsi ili kukuza uzalishaji uendelevu;

Na kwa kuwa; Kambi Rasmi ya Upinzani inatazama Tanzania kama Taifa ambalo sekta binafsi inatakiwa kuendesha viwanda vya mazao (Agro Processing Industries) ili kuongeza ubora wa mazao yanayozalishwa na wakulima mashambani;

118. Mheshimiwa Spika, Hivyo basi; Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa mustakabali wa kilimo cha Tanzania upo katika soko la mazao ya bidhaa na bidhaa za kilimo ambapo wakulima na wanununuzi wataendesha shughuli za kibiashara katika mazingira yanayotabirika, na kwamba wakulima wanaweza kupata bei nzuri kwa mazao yao. Soko kama hilo pia litasaidia matumizi ya teknolojia kama kuboresha shughuli za kilimo ili kukidhi viwango vya ubora vya kimataifa na hivyo kuhakikisha kwamba walaji wanapata bidhaa bora. **Kwa ufafanuzi zaidi rejea Sera ya Chadema Kuhusu Kilimo**.

119. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

……

Pascal Yohana Haonga (Mb)

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI - WIZARA YA KILIMO

17.05.2019

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge nina orodha ya wachangiaji hapa kama nilivyoletewa na Kambi zetu. Mchangiaji wetu wa kwanza, wa pili na wa tatu watakuwa ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Deo Ngalawa, Mheshimiwa Neema Mgaya na Mheshimiwa Njalu Silanga ajiandae.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Wizara hi ya Kilimo. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Hasunga na Manaibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Bashungwa pamoja na Mheshimiwa Mgumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi sasa ime-*target* kwenda kwenye uchumi wa viwanda na uchumi wa viwanda hautaweza kuja kama kilimo chetu hakijawa ni kilimo cha ufanisi kwa sababu naamini kwamba viwanda hivi malighafi zake zitatoka kwenye kilimo. Sasa nipende tu kujua mpango mkakati wa Wizara wa ku-*boost up* hivi viwanda ili viweze kuimarika ukoje, kwa sababu naamini asilimia zaidi ya 75 ya wananchi wa Tanzania ni wakulima, sasa mpango upoje wa kuwainua hawa wakulima ili waweze kuhakikisha wkamba wanatengeneza malighafi za kutosha kwa ajili ya ku-*boost up* hivi viwanda, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba viwanda vyetu vinasimama na kujitegemea bila kutegemea kwa kiasi kikubwa malighafi kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu wana uwezo wa kuhakikisha kwamba kilimo kinakuwa endelevu, lakini kitu kikubwa ambacho kinazuia hiyo, ni miundombinu ya maeneo ya uzalishaji. Maeneo ya uzalishaji miundombinu yake kufikika ni migumu sana na hii ndiyo inayopelekea wakulima wetu kupata faida kidogo. Sasa ifike mahali maeneo ya uzalishaji miundombinu yake iwe ya uhakika. Mfano, kule kwetu Ludewa; Ludewa ina uwezo wa kuilisha hii nchi kupitia mahindi lakini miundombinu yake siyo mizuri sana, barabara zetu siyo nzuri sana. Kwa hiyo niiombe sasa Serikali iboreshe miundombinu ya barabara ili iweze kuwafikia wale wakulima na tuweze kuilisha hii nchi na tuweze kutoa malighafi ya

kutosha ku-*support* hivi viwanda ambavyo sasa tunategemea viwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kilimo kupewa kipaumbele kwa kiasi kikubwa, hivi viwanda ambavyo tunavitegemea kwamba ndiyo iwe *engine* ya uchumi wa hii nchi tutakuwa tunapoteza muda. Kwa hiyo, napende kusema kwamba hii miundombinu ambayo ipo lazima iboreshwe hususan barabara wakulima wetu wanapata shida sana. Mfano, katika kipindi hiki cha masika, kuna mazao ambayo yanavunwa kipindi cha masika lakini yanashindwa kutoka kwenye eneo la uzalishaji kuja sokoni. Kwa hiyo tukiweza kuhakikisha kwamba tunatengeneza miundombinu vizuri hasa ya barabara, naamini kwamba kilimo kina uwezo mkubwa wa ku-*support* viwanda ambavyo sisi tumejielekeza kama nchi kwenye uchumi wa hivyo viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza kilimo, tunazungumza mbegu. Mbegu zetu nyingi siyo bora, lakini nauona mpango wa Serikali sasa wa kuhakikisha kwamba tunawaletea wakulima wetu mbegu bora ili tuweze kufanya uzalishaji mkubwa na ambao ni wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kitu kingine ambacho wakulima wetu wanapata nacho shida ni suala la mbolea. Mbolea kwa kweli haziendi kwa *target*, hazi-*meet target* za wakulima. Kipindi cha ukulima mbolea hazipo, lakini wakati unaelekea kwenye maeneo ya mavuno ndiyo zinakuja mbolea za kupandia. Kwa hiyo kuna haja sasa Serikali ikajipanga mbolea ziende katika kipindi husika. Kama ni mbolea ya kupandia basi iende katika kipindi cha kupandia, kama ni mbolea ya kukuzia iende kwenye kipindi cha kukuzia. Hilo litaleta tija kwa wakulima na pia Serikali itapata faida kwa kupitia kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu wana tatizo kubwa la soko. Tumeona mwaka jana wakulima wetu walikuwa na mazao mengi, walizalisha kwa kilimo kikubwa hususani mahindi. Mahindi kwetu kule Ludewa ni zao la biashara si zao la kilimo, kwa hiyo tunapozungumza mahindi

kama zao la biashara kulikuwa na kuna haja sasa ya Serikali kuja na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba tunapata soko la kutosha ili kuwahamasisha wakulima wetu kulima kwa bidii na kwa tija, la sivyo tukitegemea tu soko moja la *NFRA* halitoshi. Kwa hiyo nchi ijipange sasa kutafuta masoko ya mazao ya mahindi na mazao mengine yote ya chakula ili wakulima wetu walime kwa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia kama nchi tunalo *gap* kubwa, tunalo *gap* la mafuta ya kula, sasa sijajua kama nchi tumejipangaje. Ifike mahali sasa tuweke kilimo kwa *zone* kwa sababu tunategemea mafuta kutoka nje wakati wakulima wetu wana uwezo wa kufanya hivyo vitu. Sasa ni nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba tunaliziba hilo pengo kuhakikisha kwamba mafuta tutayotegemea yatoke hapa nchini na ikiwezekana mafuta hayo tuweze kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna tatizo la mbolea. Kama nchi tumejipangaje kuwa na viwanda vyetu wenyewe vya mbolea badala kutegemea mbolea kutoka nje. Kwa hiyo mimi niseme tu, uchumi wetu wa viwanda utategemea kwa kiasi kikubwa kilimo na kilimo ni lazima tukipe kipaumbele kikubwa. Tukizungumzia viwanda usisahau kiwanda cha chuma kule Liganga na usisisahau makaa ya mawe Mchuchuma. Viwanda hivi ndivyo viwanda *flagship* ambavyo vina uwezo wa kuzaa viwanda vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna kila haja ya kuhakikisha kwamba kilimo chetu kiwe ni kilimo cha uhakika, tuondoke kwenye kilimo cha kutegemea mvua twende kwenye kilimo cha umwagiliaji. Hii nchi ina mabwawa mengi, hii nchi ina mito mingi, kwa hiyo twende kwenye kilimo cha uhakika ili hatimaye wakulima wetu walime kwa tija na waone faida ya wao kuwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Benki ya Kilimo, iko Dar es Salaam. Mimi ningependekeza kuwa hii Benki ya Kilimo ije Ludewa ambako wakulima ndipo wapo. Benki ya Kilimo kukaa Dar es Salaam mtu wa Ludewa aende Dar es Salaam

kwenda kukopa mkopo; kwanza hata hiyo elimu ya mkopo hana. Kwa hiyo Benki hizi ambazo zinawa-*target* wazalishaji ziende kwa wazalishaji wenyewe ili hatimaye tuione hiyo tija. Kwa sababu leo hii unaponzungumza hapa kwenye taarifa unaiona kabisa Benki ni ya kilimo sawa lakini wakopaji wakubwa si wakulima. Kwa hiyo ifike mahali sasa kila kitu ambacho tunakilenga basi tukipe kipaumbele ili hatimaye tuone kwamba wakulima wetu wanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo bado niendelee kusisitiza kwa Serikali kuhusu masoko ya mazao, bado ni machache. Na pia tuzungumzie suala la wale walio *supply* mbolea. Lipo hili ombi ambalo linaonekana kwamba walio *supply* mbolea walio wengi walighushi; lakini mimi ninaamini kwamba wapo walio *supply* mbolea hawakuwa na shida yoyote. Kwa hiyo wale ambao hawakuwa na shida yoyote walipwe sasa, kwa sababu tunasumbuliwa sana, kwa sababu hatusemi sasa ni nani ambaye ameghushi, ni nani ambaye amekuwa ni fisadi kwenye huo mfumo. Wale ambao wanaonekana wapo *clean* walipwe fedha zao, kwa sababu tunao watu wengi wako *stranded* sasa hivi huu ni mwaka wa tatu wanasubiri malipo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri hebu jaribu kuliona hilo ili mwisho wa siku hawa watu waweze kukopa.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ngalawa.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mgaya.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuweza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu kuweza kuchangia mjadala huu wa bajeti ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya na ambayo wanaendelea kuifanya ya usajili wa wakulima. Kwa sababu naamini kwa kufanya usajili wa wakulima kutatupelekea tuwe na takwimu sahihi ambayo itatusaidia kujua mahitaji sahihi ya wakulima katika masuala ya pembejeo, masuala ya masoko, lakini vilevile na miundombinu ya kilimo kwa maana ya maghala. Kwa kuwa tutakuwa na takwimu sahihi itatusaidia kupanga mipango sahihi ya kutatua changamoto mbalimbali za wakulima pamoja na wadau wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze kwa kuanza kufanya tathmini ya afya ya udongo, kwa sababu kwa kufanya tathimini ya afya ya udongo itawasaidia wakulima wetu kulima mazao sahihi, sehemu sahihi na vilevile kutumia pembejeo sahihi katika maeneo yao ambayo itawezesha kuongeza uzalishaji na vilevile kuongezeka kwa kipato cha mkulima mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nilikuwa napenda sasa niishauri Serikali katika maeneo mbalimbali, nitaanza na kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kubadilika ni lazima kabisa tuachane na kilimo cha jembe la mkono tujikite kwenye *commercial farming.* Niseme tu, isiwe *large scale* tuwekeze kwenye *small scale* ili kuweza kuwalenga kundi kubwa la wakulima wadogo nao waweze kutumia nyenzo za kisasa wakati wanafanya shughuli za kilimo kwa maana ya kutumia matrekta, lakini vilevile waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji ambacho wataweza kuvuna na kulima zaidi ya mara mbili kwa mwaka. Hivyo basi Serikali ione umuhimu wa kuweza kuchimba malambo maeneo mbalimbali ya nchi yetu ili wakulima hawa waweze kupata fursa ya kuweza kufanya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la kilimo chenye tija; na utakubaliana na mimi kabisa kwamba

wakulima wetu wanatumia gharama kubwa sana katika uzalishaji kuliko kile kivuno wanachokipata. Wakulima wengi wanapata mavuno machache hivyo basi inawapelekea pia hata faida ile ya kilimo chao kuwa faida ndogo. Ningependa niishauri Serikali; kwanza kabisa muhakikishe kwamba hili zoezi la tathimini ya afya ya udongo linakamilika mapema ili kuweza kusaidia kilimo chetu kiweze kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niiombe Wizara hii ya Kilimo ikae na Wizara ya Viwanda ione namna bora ya kutengeneza vivutio kwa wawekezaji ambao wanawekeza katika viwanda vya pembejeo, kwa maana ya viwanda vya mbolea, ili kusudi wakiwekeza kwa wingi, wakifungua viwanda vingi vya mbolea ndani ya nchi yetu hii itapelekea wakulima wetu kupata mbolea kwa bei nafuu lakini vilevile itawasaidia wakulima wetu kuwa na uhakika wa mbolea pindi wanapokuwa wanahitaji na vilevile itakuwa kichocheo cha wakulima wengi kutumia mbolea na matokeo yake kilimo chetu kitaenda kuwa na tija, uzalishaji utaongezeka kipato cha mtu mmoja mmoja kitaongezeka na taifa kwa ujumla. Vilevile tukumbuke pia uanzishwaji wa viwanda hivyo vya mbolea italeta ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende pia kuishauri Serikali katika suala zima la ushuru wa pembejeo za kilimo. Niishauri Serikali itoe ushuru katika pembejeo za kilimo, kwa maana ya mbolea na viuwadudu, ili kumpa nafuu mkulima aweze kununua pembejeo hizi kwa gharama nafuu na kuweza kuzalisha kwa gharama nafuu na kuweza kupata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mbegu, naendelea kuishauri Serikali itumie vituo vya utafiti vya mbegu na kuviimarishavituo ili kuhakikisha kwamba wanazalisha mbegu bora ili wakulima wetu waweze kupata mbegu bora na kuweza kuzalisha mazao bora na kuweza kupata faida. Vilevile waangalie mbegu hizo zinaenda mahali gani, kwa mfano kwenye sehemu ambazo zina ukame wahakikishe kwamba mbegu wanazozipeleka kule ziwe zinakubaliana na hali halisi ya ukame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumzia zao la parachichi ndani ya Mkoa wa Njombe. Kwanza kabisa nimpongeza Mheshimiwa Rais, alipokuja Mkoa wa Njombe kwenye ziara yake ailituhakikishia kwamba tutapata ndege ya mizigo ambayo itakuwa inatua Songwe na kuweza kubeba parachichi zetu sisi wakazi wa Mkoa wa Njombe, lakini vilevile na wa Songwe na wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii fursa ya zao la parachichi sisi wananchi wa Mkoa wa Njombe tumeipokea vizuri, tunalima kwa wingi, hivyo basi nilipenda kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Kilimo akae pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi waone namna bora ya kuweza kutumia reli ya *TAZARA* kwenye, yale mabehewa ya mizigo baadhi yao watengenezewe mfumo wa ubaridi na upoozwaji, kwa maana ya *cold room,* ili wakulima wengi watumie njia ya reli ya usafirishaji ambayo ni rahisi zaidi uki-*compare* na njia zingine. Hivyo basi nawashauri Wizara hii ikae na Wizara ya ujenzi ione namna bora ya kutumia ile reli ya *TAZARA* ili tuweze kusafirisha mazao yetu ya parachichi na yaweze kufika kwa mlaji wa ndani na wa nje yakiwa na ubora ili tuweze kuuza kwa bei nzuri na kuweza kulipa kodi na kuchangia Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri; hii fursa ya parachichi; maana kila mtu sasa hivi anajua kwamba parachichi sasa hivi ulimwenguni inaitwa *green gold* kwa sababu ina thamani kubwa sana na kila mtu sasa hivi amehamasika kulima parachichi. Lakini ningependa kumwambia Mheshimiwa Waziri, tukumbuke kwamba hii fursa ambayo sisi Watanzania hususani Mkoa wa Njombe tumeiona na Nyanda za Juu Kusini kwa maana ya Iringa na Mbeya tumeiona ya kulima parachichi na nchi zingine nayo wanaiona fursa hii, hivyo nilikuwa napenda kuishauri Serikali muhakikishe kwamba mnaingia mkataba mzuri na nchi walaji katika masuala ya masoko ili kuweza kulinda soko la mkulima wa parachichi ndani ya Tanzania yetu. Kwa sababu mnaona kwamba *demand* ya parachichi ni kubwa lakini kadri muda unavyozidi kuendelea kwa sababu fursa hii imeonwa na nchi nyingi

baadaye *supply* ya parachichi itakuja kuwa kubwa na *demand* itakuwa iko pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi kumsaidia mkulima wa parachichi wa Mkoa wa Njombe na mikoa mingine ambayo inalima parachichi ndani ya Tanzania ni vyema basi mkaweka mikataba mizuri kwa nchi walaji ili kuweza kulinda soko la parachichi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Njalu Silanga.

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Kilimo, hotuba nzuri. Nimpongeze Katibu Mkuu pamoja na timu yake ya Wakurugenzi, Wenyeviti wa Bodi zinazoshughulikia mazao yetu. Nitaanza na kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoingilia masuala ya mazao ya biashara, Kahawa, Pamba, Tumbaku nakadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri mwaka huu tulikutana na wewe ukasema mambo ya pembejeo ulikuwa na mashaka lakini nafurahi sana katika kitabu chako ukurasa wa 37 jinsi viuatilifu vilivyopatikana katika maeneo yetu, nasema ahsante sana. Naiomba Serikali; mwaka jana tuliazimia katika Bunge kuwa ifikapo tarehe moja Mei kila mwaka lazima msimu wa zao la pamba uwe umefunguliwa ili wananchi waweze kupata fedha katika kipindi hicho. Tulileta hiyo hoja binafsi kwa makusudi kwa kutambua maeneo tunayotoka na wananchi wetu adha wanayoipata; kuanzia mwezi wanne kunakuwa na changamoto ya uhitaji wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anisaidie, kuna baadhi ya maeneo hadi sasa makampuni hayajapata vibali kwa ajili ya kuingia kununua. Lakini ieleweke kwamba sisi kama nchi na kama taifa tunategemea wakubwa wetu walioko nje Duniani kule kwa ajili ya mazao yetu haya. Bila kuwa na mipango na mikakati na utaratibu litakuwa Bunge na itakuwa nchi ya kulalamika kila kukicha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini tukisimama vizuri tukashirikiana kwa pamoja Waheshimiwa Wabunge, wenyeviti wa Bodi zile husika, wafanyabiashara, tutatatua changamoto tuliyonayo hii. Haya mengine Mheshimiwa Waziri mnapita katika kipindi kigumu lakini mimi ninaamini tukiweka mazingira ambayo yatakuwa rafiki tutaondokana na zana nzima ya kila mwaka lazima zao la pamba wakae wakutane kupiga kelele, tumbaku wapige kelele, kahawa wapige kelele ilhali waamuzi tuko ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo naamini tukisimama kwa pamoja na kuweka utaratibu na tukatumia taaluma za wataalam naamini tutafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia miaka mitatu katika Bunge lako Tukufu lakini nimeshuhudia katika mikutano ya wadau hakuna jambo lolote la maana tunaloondoka kwa kuzungumza isipokuwa ni kutimiza wajibu tu. Naiomba Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, hebu lisimamie hili jambo ukae nalo kwa makini tuondokane na mambo ambayo hayana maana. Kinachotuletea matatizo ni kuchelewesha utekelezaji lakini dhana ni nzuri. Leo ukisoma kuhusu zao la pamba zao linaendelea kuteremka lakini hatujui hatima yake ni nini, tutaanza tena kulalamika lakini majibu tunayo sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanaojua dhamana ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ningeomba sana suala hili hasa kwenye pamba; nazungumzia sana kwenye pamba kwa sababu natoka kwenye pamba na nita-*declare interest* kwamba mimi ni mnunuzi wa pamba, najua changamoto wanazozipata wananchi. Siku mbili hizi pale Kishaku kuna watu wamekamatwa wananunua pamba

shilingi 500 kwa kilo. Kwa hiyo utaona ni adha gani wananchi walivyo na shida. Ana mali yake anahitaji hela, hiyo ulichukue na ulifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, nilimsikiliza kwenye hotuba yake kwenye kipindi akielezea habari ya ushirika. Ushirika umeleta tija katika maeneo yetu kuwa na ubora wa pamba ambao ni mzuri na tunahangaika sasa, navyoona kadri tunavyokwenda tunaweza tukaanza kupata *premium* ambayo ilikuwa imepotea kama senti tatu na kuendelea kwa ubora tunaoendelea nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini changamoto iliyopo lazima ushirika muendelee kuuimarisha si maneno ya kukutana kusema tumekubaliana, hapana; na Mheshimiwa Waziri nikushauri, mwaka jana tuliingia kwenye ushirika na wengine tulikuwa tuna wasiwasi nao lakini tunaanza kuona inakokwenda. Ta hivyo bado kuna vitu vinakuwa vinaongezeka kila mwaka. Ningeshauri Serikali tuwe na mfumo tunaoanza nao wa kwanza tunapata na majibu yake, si leo tukianza mwaka huu baada ya miezi mitatu unasema wakulima wote wafungue *account*, baada ya miezi miwili tena unakuja na ajenda nyingine; ningeomba kwa jambo hili tuwape muda watu tusiwe tukijiaribia hili tunakuja na jingine inatutia mashakani na tunaleta wasiwasi kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ieleweke kwamba benki tulizonazo zina uwezo mdogo kuwafikia wananchi vijijini. Tulikuwa na benki *NBC* ikabadilishwa kuwa *NMB* kwa maana ya *Rabobank* ndio watakuwa washughulikiaji wakati wa kusaidia wakulima wetu; lakini maeneo mbalimbali na wilaya nyingine zilizoko humu ndani hazina benki za hizo *NMB*. Kwa hiyo utawezaje kupeleka fedha kijijini zaidi ya makampuni labda 10 halafu waingize kwenye *account* halafu yule mwananchi atoke kilomita 150 kwenda benki; mtaona hata walimu wanapoitapa ile adha ya hela zao kwenye mabenki. Kwa hiyo kutakuwa na changamoto nyingine ambayo sio

rafiki kwa wakulima na kutuletea maswali yasiyokuwa na maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali mifumo hii iendelee kusimamiwa vizuri. Pia tusimamie kupata viongozi wa ushirika wenye weledi na wenye uchungu na watu. Yako malalamiko, baadhi ya wahasibu waliochaguliwa fedha wanazolipwa hazitoshi, mtu hawezi kulipwa shilingi 80,000 na huku anasimamia mamilioni ya watu. Maana yake ni kwamba unakaribisha wizi mwingine kwenye ushirika huo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningeomba hao watu wanaosimamia fedha wapewe angalau posho kubwa ainayoweza kulingana na hadhi yao kama wasimamizi wa fedha za umma au za wafanyabiashara itatusaidia kuliko mtu anashinda njaa analipwa 80,000 mshahara na huku anapokea mamilioni ya fedha; unatengeneza ushawishi moja kwa moja kuibiwa fedha hizo na matokeo yake tunaanza kusema ushirika haufai; kwa hiyo niombe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho nimpongeze Mwenyekiti wa Tume ya Ushirika kaka yangu Titus Mlengea Kamani kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya sasa aendelee zaidi kule chini kuhakikisha anasimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwneyekiti, niwapongeza sana Bodi ya Pamba nimpongeze Dkt. Kabisa alistaafu lakini amerudi na pamba sasa imeanza kuongezeka muendelee...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge hapo ndipo tunafikia mwisho kwa mchango wetu kwa asubuhi hii.

Watakaoanza mchana saa 10 ni wafuatao. Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Daniel Nzanzugwanko, Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Jitu Soni; na wengine watafuata baada ya hapo. Ninyi muwahi tu; Waheshimiwa Wabunge sina matangazo, kwa hiyo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 10: 00 jioni.

(Saa 7:00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10:00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Niliwataja wachangiaji wetu wa kwanza, wawili wana udhuru. Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Lupembe.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia kwenye hii hoja yetu ya Kilimo. Kwanza kabisa niunge hoja mkono kwa asilimia mia moja na nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sana katika taarifa au hoja aliyoisoma Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba, kuna matatizo ya *climate change* kwenye maeneo mbalimbali ya Tanzania ambayo yanaweza yakasababisha upungufu wa mazao au chakula hasa katika Mkoa wetu wa Shinyanga. Mimi naongelea Mkoa wetu wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha mikoa ambayo hali ya hewa ikibadilika kidogo tu mambo yanakuwa tofauti kabisa na watu walivyotarajia katika suala zima la kilimo. Ukilinganisha Mikoa ya Shinyanga na mikoa ya Kusini, mikoa ya Kusini ukiongelea masuala mazima ya umwagiliaji wanakushangaa. Mikoa ile imeneemeka na mvua ni nyingi na watu wanalima vizuri sana, lakini Mkoa kama wa Shinyanga hivi ninavyozungumza hali ya mazao katika Jimbo la Solwa *per se*, Jimbo la Solwa sasahivi mazao mengi yamekauka. Ukienda Bariadi, ukienda Mkoa wa Simiyu,

ukienda kote mambo ni hivyohivyo yanakauka halafu baadaye kidogo tena mvua inanyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili nataka tu nimshauri Mheshimiwa Waziri kwenye maeneo ambayo ni muhimu sana ya kimkakati katika kuyaokoa, sisi katika Mkoa wa Shinyanga tunalima vizuri sana na hatupendi kuomba chakula, kinachohitajika pale ni kutengenezewa miundombinu itakayokwenda kuondoa tatizo hili la tatizo la njaa. Sasa eneo pekee, nimweleze Mheshimiwa Waziri, angechukua Mkoa wa Shinyanga na mikoa mingine ambayo anaiona yeye inafaa kwa kuanzia hizi fedha kwa ajili ya umwagiliaji skimu za umwagiliaji ziende maeneo hayo kwa sababu, hakuna eneo linaweza likatusaidia au kuwasaidia wakulima wa Jimbo la Solwa kama skimu ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Solwa tuna skimu sita, lakini skimu ambazo ziko vizuri ni skimu tatu ambazo hata hivyo upembuzi yakinifu ulishafanyika na tumeshaomba fedha kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa kwenye maeneo hayo. Hizo skimu zipo kweli, tunashukuru sana kwanza Serikali ka kufanya kazi kubwa ya kutuletea skimu hizo, lakini skimu ni mifereji ina maana kwamba, mvua ikikauka na yenyewe haina kazi kwa hiyo, ili mifereji ifanye kazi vizuri lazima ujenge bwawa, lile bwawa ndio linanywesha, ndio linamwaga pale kwenye skimu ya umwagiliaji kwenye mifereji, wakulima wanalima hata kama mvua haipo. Hivi ninavyoongea sasa hivi kuna tatizo kubwa sana la njaa, yaani njaa ipo, baada ya miezi miwili mitatu itakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina skimu ya umwagiliaji ya Nyida ambayo kwenye taarifa hapa kampuni au Shirika la Maendeleo la *JICA* ndio sasahivi linafanya kazi pale katika kutengeneza ile mifereji. Tunawashukuru sana na tunashukuru sana Serikali kwa kuliona hilo. Gharama inayotumika pale ni milioni 466, urefu wa mita 1,325 itakuwa ni skimu ya umwagiliaji nzuri sana. Kinachotakiwa pale ni kujenga bwawa tu, upembuzi wa bwawa na usanifu ulishamalizika na tulishaomba maombi maalum kabisa ya *2.5 billion* ili sasa

skimu ile iweze kukamilika, Skimu ya Umwagiliaji ya Nyida katika Jimbo la Solwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Umwagiliaji katika Kata ya Masengwa, Skimu ya Umwagiliaji katika Bwawa la Isololo, wote huu ni umwagiliaji ambao sasa hivi nataka Serikali kwa jicho la huruma sana, kama ni fedha kwa ajili ya kuwasaidia wakulima, kama ni fedha kwa ajili ya kuondokana na matatizo haya ya njaa katika Mkoa wa Shinyanga, eneo muhimu sana, mimi binafsi namshauri sana Mheshimiwa Waziri tujikite sana kwenye skimu ya umwagiliaji. Kwa hiyo, naomba sana na tayari tulishaomba fedha hizo na tayari iko Wizarani kwako, sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kujibu hoja zetu Mheshimiwa ni matarajio yangu ataniambia kwamba, fedha zote tulizoomba ameshatupa, ili twende sasa tukawaambie wananchi waende wachimbe mabwawa na Mungu atambariki sana na tunaunga hoja mkono vizuri na Serikali ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Masengo ni skimu ya muda mrefu sana. Kuna wakati tuliwahi kupata fedha milioni 900, lakini kutokana na *committment* nyingi za Serikali fedha hizi hatukuletewa, tukasema haina shida, lakini sasa hivi tunaomba. Bahati nzuri sana usanifu, narudia tena, usanifu ulishafanyika kwa skimu zote tatu hizi, kwa hiyo, suala hapa ni kutafuta fedha tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye Bwawa la Isololo ambalo nalo ni muhimu sana kwenye Kata ya Usule, bwawa hili lilianza mradi mwaka 2013. Mkandarasi aliyepewa bwawa hili alifikia asilimia 30 na muda wake wa mkataba ukawa umekwisha kwa hiyo, fedha tulizopewa na *Bank of Africa* wakasitisha wakaondoka. Kwa hiyo, mradi umefika asilimia 30 na umesimama mpaka hivi ninaongea leo. Tumerudia tena usanifu, tumeomba fedha kwa mara ya pili ni *1.2 billion.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninayoongea haya ni miradi ambayo inafanyika, iko njiani tunakwenda

kukamilisha, siongelei miradi mipya. Katika hoja yake Mheshimiwa Waziri amesema atajikita zaidi kwenye miradi ambayo haikukamilika, iko kati ya asilimia 30, 50 mpaka mwisho, kwa hiyo, miradi hii ninayomweleza ya Skimu ya Umwagiliaji ya Nyida, skimu ya Umwagiliaji ya Masengwa, Bwawa la Isholo ni miradi ambayo ipo katika asilimia 30 au 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea hii Wizara ya Kilimo ina Waziri ambaye namwaminia sana. Mheshimiwa Waziri namwamini sana, najua kabisa atayachukua haya, atakwenda kuyafanyia kazi. Sisi Waheshimiwa Wabunge katika Mkoa wa Shinyanga hakuna kitu kinatusumbua sisi kama mabadiliko ya hali ya hewa. Yaani hali ya hewa ikikataa mvua kidogo tu mazao yanakauka na mambo yote yanakuwa yameharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu wa Maafisa Ugani 56. Maafisa Ugani ni watu muhimu sana, bila kuwa na Maafisa Ugani kwenda kuwaeleza wakulima, wakulima bado wanalima kilimo kilekile cha zamani, kilimo kisichokuwa na tija, kilimo ambacho kwa kweli, wanatumia nguvu kubwa, lakini mafanikio yao yanakuwa ni madogo. Kwa hiyo, pamoja na kuwa tuna upungufu wa Maafisa 56 ni kweli inawezekana kabisa akatuletea 10, 20, ninachoomba atuongezee pale ambapo anaona inampendeza, ili sasa Jimbo la Solwa tuweze kuongeza Maafisa Ugani wazuri waweze kutoa elimu vizuri, hii ni pamoja na usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani wanapata shida sana kwenda kwa wakulima. Mheshimiwa Waziri atuletee mwongozo tu kwamba, katika bajeti ya mwaka huu tunahitaji, Halmashauri ninyi katika mwongozo wa kilimo kwamba, mpange pikipiki kwa ajili ya Maafisa Ugani hata kwa ngazi ya kata. Tunaweza tukaanzia kwa ngazi ya kata peke yake. Mimi nina kata 26 nikipata pikipiki 26 maana yake tayari tumeshajenga *network* ya Maafisa Ugani na wakulima, tutakuwa tayari tumewajengea uwezo mzuri mno wakulima kulima kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sana katika Jimbo la Solwa tuna zao moja la dengu ambalo linatumika kama zao la biashara, lakini zao la dengu wanalima kata kama nne au tano tu. Ukichukua Kata ya Salawe, Kata ya Bhukande, Kata ya Mwakitolyo na Kata ya Solwa ndio wanaolima dengu na hiyo dengu kwa mfano hivi sasa hivi kama kuna matatizo ya mazao, kutokuwepo na mazao hawavuni vizuri wanategemea mazao hayo ya dengu, lakini kata zilizobaki zote wanategemea zaidi mahindi pamoja na mpunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi zaidi ya hapa. Nilikuwa nataka tu kujikita zaidi kwenye masuala mazima ya umwagiliaji na hili suala la umwagiliaji hatuna namna yoyote kabisa katika kuokoa wakulima wa Jimbo la Solwa au Mkoa wa Shinyanga...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Chikota wajiandae.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia muda huu. Naomba nimshukuru Mungu kwa kutulinda mchana kutwa na ametupa fursa tena kwa mara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wote wawili kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Kusema kweli Mheshimiwa Hasunga hongera sana, tunamwona jinsi anavyokimbizana. Nafikiri mafanikio kupitia kilimo kwa Watanzania yatawezekana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi tunalima zao la tumbaku. Zao hili sasa hivi limeweza kuyumba kwa sababu, makampuni ambayo yanakuja kuchukua zao hili katika Mkoa wetu wa Katavi wameleta makisio kwa wakulima, kila mwaka wanaweka makisio, sasa kila siku wananchi wa Katavi wanavyopewa yale makisio sio ya kupanda ila makisio yale ya kushuka. Sasa kutokana na hiyo uchumi kidogo wa Mkoa wetu wa Katavi umepungua kwa sababu zao hili kupitia halmashauri zetu zilikuwa tunapata manufaa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kwa sababu, zao hili ni zao la kibiashara. Najua Waziri ana mikakati mingi mikubwa, mipana, naomba hili zao lifufuliwe upya, tutafute wadau ambao watakuja kununua zao letu la tumbaku kwa sababu, sasa hivi Mkoa wetu wa Katavi kupitia halmashauri zetu mapato yamepungua sana. Sasa sio kwenye halmashauri zetu tu hata Taifa mapato yameshuka, naomba tukazie mkazo kupitia tumbaku zao hili liweze kutafutiwa wadau ili waweze kununua katika msimu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali, katika Mkoa wetu wa Katavi msimu huu na msimu uliopita tulilima pamba. Pamba imeitikiwa sana hususan katika Wilaya yetu ya Tanganyika wamelima takribani kilo milioni 16 wananchi wameweza kufanikiwa kupata. Naomba sasa Bodi ya Pamba iweze kuja kuchukua kwa sababu, wananchi wetu wa Katavi pamba hiyo wameivuna wameweka majumbani. Sasa ili tuweze kupata manufaa makubwa na wale tuweze kuwapa hamasa kubwa wananchi wa Mkoa wa Katavi tunaomba basi hii Bodi iweze kuja kununua ili sasa wananchi hawa waweze kutafuta mbegu nyingine kwa ajili ya msimu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika mbolea. Pembejeo ni kitu muhimu sana, naomba, ndani ya nchi yetu tuna mazingira tofauti ya hali ya hewa. Ukiangalia Mkoa wa Katavi, Rukwa, Kigoma mvua zinaanza kunyesha mwezi wa Kumi, Kigoma mwezi wa Tisa katikati mvua zinaanza kunyesha.

Sasa pembejeo zinakuja Mkoa wa Katavi Januari, je, Januari huyu mkulima atapata manufaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima hawezi kupata manufaa hata kidogo. Vilevile sasa hivi kuna matapeli wengi wanawaletea wakulima wetu pembejeo feki ambazo hazina tija kwa sababu, wanajua kabisa huku mjini watu wanaelewa; wanajua kuwa wakipeleka vijijini kule watu hawaelewi wanawapelekea pembejeo, wanawapelekea viatilifu ambavyo ni vya bandia, *fake,* sasa tija inakosekana. Mkulima analima akiweka ile mbolea, vile viatilifu havina manufaa katika ule mmea, sasa wananchi wetu wanapata hasara. Naomba kwa sababu tuna Shirika la *ASA,* shirika hili ni zuri sana, sasa hivi shirika hili linafanya kazi nzuri na ukizingatia sasa hivi wanajiendesha wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wanalima mbegu na mbegu yao ni bora halafu wanauza bei rahisi. Kwa kilo ya alizeti wanauza Sh.3,500 lakini tukienda madukani mbegu ileile inaizwa Sh.35,000 mpaka Sh.70,000, sasa tuimarishe Shirika hili la *ASA* ili sasa Watanzania waweze kupata tija kwa sababu, shirika hili litafanya kazi nzuri zaidi. Vilevile shirika hili halipati pesa miaka mitano sasahivi hawajapeleka pesa kwenye Shirika la ASA. Naomba tuliimarishe Shirika hili la *ASA* litakuja kuwaletea tija Watanzania kwa sababu ni shirika la wazalendo, sasa sidhani kama wanaweza wakafanya vitu tofauti, vilevile hizi mbegu *fake,* viatilifu *fake,* vitapotea shirika hili tukiliimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye umwagiliaji. Kwetu Mpanda, Wilaya ya Tanganyika, Kata ya Kalema tulipeleka pesa kwa ajili ya umwagiliaji, ile skimu haijamalizika mpaka leo. Wanajua kama hizi skimu zinatumia pesa, wakandarasi, siku hadi siku *value for money* inabadilika, ina maana hii skimu sasa hivi haiwezi kufaa tena na wananchi wa Kalema hawawezi kupata tija. Sio Kalema tu katika Mkoa wetu wa Katavi kuna Kata ya Ugala, skimu yake mpaka leo ilimalizika, lakini haifanyi kazi, ina maana kuwa inaharibika haitaendelea kufanya kazi vizuri. Tuna Kata ya Urwila skimu yake haijakaa vizuri, tuna Kata ya Mbede skimu yake nayo

haijakaa vizuri, naomba katika kata hizi ambazo tumeweka umwagiliaji, umwagiliaji ndio mkombozi wa Watanzania. Tukiweka skimu hizi vizuri, hawa wananchi wakilima mara mbili mara tatu tutapata faida kubwa na mazao mengi yataweza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya nchi yetu ya Tanzania kuna Kanda ambayo Iringa, Njombe, Ruvuma, Songwe, Rukwa, Katavi, katika *zone* hii ni wakulima sana wa mahindi. Sasa hivi ukiangalia katika nchi ya Zaire kuna uhaba sana wa chakula wananchi wengi wanapeleka mazao yao Zaire na sisi ndani ya Mkoa wetu wa Katavi kupitia Kata yetu ya Kalema inajengwa bandari pamoja na Rukwa inaweza kujengwa bandari, ili kanda hizi zote wakapeleka mazao yao katika Bandari ya Kalema pamoja na Kasanga, mazao haya yakapelekwa Zaire Watanzania hawa wakapata kipato kupitia bandari hizo mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwa sababu, nchi ya Zaire hakuna chakula, Burundi wanategemea sana Tanzania, tukiweka mazingira mazuri nafikiri tutapata mafanikio makubwa sana. Naomba sana kupitia Waziri Mheshimiwa Hasunga, najua alikuwa anafanya ziara sana wakati ule alivyokuwa maliasili...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lupembe kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Chikota na Mheshimiwa Aida, dakika tano.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kuweza kupata fursa ya kuchangia. Pia nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri na kubwa na kwa nia ya dhati ya kuonesha kwamba,

kutakuwa na mabadiliko katika sekta nzima ya kilimo. Nimshukuru Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ambayo iko Wizarani kwa kazi kubwa na nzuri na taasisi zote zilizoko chini yao kwa kazi kubwa wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote tunaendelea kushauri na ningeomba Wabunge wengi badala ya sehemu kubwa kutumia muda wetu kuelezea changamoto, changamoto kila mtu anazijua. Tuendelee kutoa ushauri mbalimbali ili kwenye dakika 10 kama dakika nane kila mtu atatoa ushauri, kwa Wabunge 300 angalau moja au mbili ikichukuliwa hapo tayari tutakuwa na mageuzi makubwa kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza ningeendelea kuomba kwamba bajeti ya Serikali tuendelee kuiongeza. Najua wataalam wanaweza kusema kwamba bajeti hii kwa kilimo peke yake inajitosheleza kwa sababu bado kuna mengi huko kwa sababu ni mtambuka, bajeti inaenda kubwa yaani inaenda kwa Wizara nyingine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa utafiti wangu binafsi, naweza kuwa nimekosea, nikiangalia bajeti ya mwaka jana na mwaka huu ya kilimo utaona imepanda kidogo lakini ukiirudisha *(convert)* kwenye bei ya *USD* bado imeteremka haijapanda. Lakini ukiichukulia kwa ujumla wake, kwamba trilioni 33, ukichukulia *10 percent* yake ambayo ilikuwa ndiyo makubaliano kwamba iende kwenye kilimo, inatakiwa angalau kwenye trilioni tatu au zaidi. Hivi nikichukulia Wizara zote ambazo zinaenda vijijini ambako kilimo kwa sehemu kubwa kinapofanyika hiyo trilioni tatu sikuiona; yaani mimi nilivyojumlisha jumlisha tu sioni hiyo trilioni tatu. Kwa hiyo, bado bajeti ya kilimo inazidi kushuka na mchango wake katika Pato la Taifa bado nao unaendelea kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwamba sekta nyingine zinaendelea kukua, lakini asilimia kubwa ya Watanzania walipo ndipo huko kwenye Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kwa ujumla tunasema kilimo; kwa hiyo ni

vizuri tukaangalia namna ya kuboresha bajeti yake. Serikali isiangalie tu namna ya kuongeza bajeti kwa kupitia Serikali yenyewe, iweke mazingira wezeshi ili na sekta binafsi pia iweze kuchangia kwa sehemu kubwa na kama ilivyokuwa kwenye *ASDP II,* asilimia 65 inatakiwa fedha zitoke kwa sekta binafsi; lakini pasipokuwa na mazingira wezeshi, Serikali isipoweza kufanya kama timu moja, pakawa na uratibu, bado haya mambo yote hayatawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusitegemee Wizara ya Kilimo, wanafanya kazi nzuri na wana mpango mzuri ila Wizara nyingine zote zisiposhirikiana bado tutaendelea kupata changamoto hiyo. Kwa hiyo, naomba mfanye kazi kama timu na wote mkae mezani mnapojadili kilimo basi kama ni kodi, tozo na ada mbalimbali mshirikiane namna ya kuzipunguza au kuziondoa. Huku kukiwa na tija huko kwingine utaendelea kupata kodi kwa njia nyingine ambayo ni *indirect tax. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuomba; tunaendelea kutegemea umwagiliaji, bila umwagiliaji hatutaweza kusogeza kilimo mbele. Sasa kwenye umwagiliaji tulikuja hapa na wazo kubwa tukaanzisha sheria na ikaanzishwa Tume ya Umwagiliaji; lakini tangu imeanzishwa bado haijawahi kupewa fedha yoyote, yaani ni sifuri, kwenda kushughulika na umwagiliaji. Sasa nilikuwa naomba tuiwezeshe Tume ya Umwagiliaji ili kwenda kushughulika kwenye umwagiliaji. Sasa nilikuwa naomba tuiwezeshe Tume ya Umwagiliaji ili iweze kufanya kazi yake. Pamoja na hiyo ningeomba kwamba Benki ya Kilimo na Mfuko wa Pembejeo nao wawezeshwe vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila kwenye hiyo pesa ambayo wamepata pawe na mkakati maalum, kwamba asilimia 20 ya fedha wanayopewa kukopeshwa kwenye sekta ya kilimo basi 20 iweze kutumika kwenye umwagiliaji tu, hapo pia utaiona sekta binafsi kwa sababu ni pesa ambayo watakopa watarudisha. Kwa hiyo, Benki ya Kilimo na Mfuko wa Pembejeo watenge asilimia 20 ambazo zitaenda kwenye umwagiliaji tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye umwagiliaji bado kuna changamoto nyingi. Kwa mfano ukitaka leo kuchimba visima, ukitaka kuleta mitambo ya kuchimba visima, kutengeneza mabwawa, *solar pump* za *irrigation* zote zina kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukishirikiana, kama Serikali mkikaa pamoja, ondoeni hizo kodi, wekeni mazingira wezeshi ili watu waweze kuchimba visima, kutengeneza mabwawa, na *private sector* itafanya. Kwa hiyo Serikali iweke tu mazingira mtaona kwenye kilimo jambo hilo la umwagiliaji litaendelea kukua. Pia mboreshe na kuandaa wataalam wa kutosha kwa upande wa umwagiliaji ili wao wakiweza kufanya kazi vizuri kwenye umwagiliaji ndiyo tutakuwa tunaweza kuokoa Watanzania badala ya kutegemea mvua, tuweze kufanya kilimo cha uhakika zaidi, na badala ya kufanya msimu mmoja, tufanye misimu miwili au mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishukuru kwamba kuna wazo la kuwa na Sera na Sheria mpya ya Kilimo ambayo tunaamini itakuja kulinda ardhi za kilimo. Leo hii maeneo mengi ya kilimo yanachukuliwa kuwa makazi na kubadilishwa matumizi; na hayo sisi si kama wenzetu, uwezo wetu ni mdogo. Leo Mji wa Dodoma tu kila mahali itakuwa makazi, hii zabibu na mvinyo wa Dodoma utapotea. Vivyo hivyo, maeneo ya makazi yamechukua hayo maeneo ya kilimo. Kwa hiyo, sheria ije ya dhati, tunaweza kwenda kujenga milimani, tukajenga maeneo ambayo hakuna rutuba na ardhi ambayo siyo nzuri kwa uzalishaji, tukapeleka tu maji, barabara na nishati makazi yatakuwa mazuri, lakini maeneo ya kilimo yalindwe kwa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija pia kwenye sekta ya mbogamboga *(horticultural)* inafanya vizuri. Huko pia tulikuwa tunaomba *cold storage* ili wakulima waweze kuhifadhi mazao yao kabla ya kwenda kusafirisha, hasa kwenye maeneo ambayo Serikali itawekeza. Vilevile sekta binafsi iweze kuwekeza kwenye *cold storage* na kwenye

mambo ya *chillers* pia muangalie namna ya kusaidia kupunguza na kuondoa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Upande wa Ushirika. Tulishakubaliana kwamba leo tunaweka nguvu kubwa kwenye shirika, na ndiyo njia pekee ya kwenda mbele kwenye kilimo. Kwenye ushirika bado ile Sheria ya 2013 tulipobadilisha kuliwa na dhana kwamba pale lazima tuhakikishe kwamba fedha ambayo ushirika itakuwa inachukua hakutakuwa na makato ya wakulima, tulisema ushirika kazi yao ni kuhudumia wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanapotafuta masoko, wanapoleta pembejeo tofauti ya kwenye bei na nini wanaponunua kwa wingi ile tofauti ya bei ndiyo iwe inaendesha ushirika. Ushirika usimkate mkulima hata shilingi moja, ndiyo maana wakulima hawapendi kupeleka mazao yao kwenye ushirika. watu wapendelee kwenda kwenye ushirika badala ya kukwepa kwenda kwenye ushirika. Kwa hiyo, ni jambo ambalo naamini tukikaa tukaelezea vizuri, tutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, luna jambo linguine. Leo hii tunaagiza vitu vitano; mbegu, asilimia kubwa ya mbegu zetu hasa mahindi, asilimia 65 ya mbegu inatoka nje ya nchi, usalama wa chakula na mbegu haupo. Kwenye mbegu kuna alizeti na mbegu hizi ambazo zinazalisha mafuta, tunaangiza sisi, baada ya mafuta ya magari mafuta haya ya kula ndiyo sehemu kubwa ya fedha yetu inakotumika. Kwa hiyo mbegu, sukari, mafuta, mchele, mbogamboga, matunda na hivi vyote ambavyo tunaagiza kutoka nje tuwekeza. Muwe na *timeframe,* kwamba ndani ya miaka mitatu hakuna kitu kitakachoagizwa nje, tutazalisha ndani ya nchi na sisi ndio tutapeleka nchi nyingine. Hayo yanashindikana kutokana na mazingira wezeshi kwenye sekta hii ya kilimo na Wizara zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie mfano, *juice* zote tunazokunywa hapa Tanzania asilimia 99.5 ni *concentrates* kutoka nje, ni asilimia 0.5 ndiyo inazalishwa hapa nchini, kwa

nini? Tukizalisha hapa nchini kwanza tutapata lishe bora, fedha kwenye uchumi wetu na tutapata mazingira bora kwa ajili ya miti hiyo mingi. Kwa hiyo itakuwa na *trickling effect* kwenye Wizara nyingine zote. Kwa hiyo, naomba tuifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni muhimu ni kwamba bajeti ya *TARI* ni ndogo sana, na tunapanga wakati mwingine tunaweza kupitisha hapa lakini fedha zinazokwenda ni ndogo. Bila utafiti kwenye kilimo hakuna uwezekano kwa kwenda popote kwa sababu kilimo ni sayansi, kilimo ni biashara kama biashara yoyote nyingine. Wekezeni kwenye *TARI* ili vituo vya utafiti vizalishe mbegu, viangalie namna ya kudhibiti magonjwa lakini pia tuangalia namna ya kuboresha *ASA. ASA* ina mashamba mazuri sana, wanahitaji uwekezaji wa kwenye umwagiliaji na uwekezaji kwenye zana za kilimo (matrekta na zana zake). Mkiwawezesha wale wala siyo kwa kuwapa bajeti, wakopesheni wataweza kulipa kwa sababu wanafanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *TPRI* na...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JITU V. SONI: Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni kwa ushauri wako mzuri, Mheshimiwa Abdallah Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza viongozi wa Wizara hii, Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Hasunga, Manaibu wake Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Mgumba; kwa kweli wote tumejionea ni jinsi gani

wanavyohangaika kusukuma sekta ya kilimo. Wamekuwa wakihangaika usiku na mchana kuhakikisha yale mazao yetu ya kimkakati yanapata ufumbuzi wa changamoto zilizopo, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unajikita katika maeneo matatu; kwanza zao la korosho, umwagiliaji na sekta ya ushirika. Nikianza na korosho, nichukue nafasi hii kipekee kumpongeza Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa maamuzi ya kijasiri ambayo aliyafanya mwaka jana kwa kuamua kununua korosho baada ya soko la korosho kuanza kuyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayeitakia mema sekta hii ya korosho hawezi kubeza juhudi zilizofanywa mwaka jana. Sekta ya Korosho inahitaji fedha nyingi na ndiyo maana hata baada ya kufanya maamuzi yale aliamua kuvunja Bodi ya Korosho na kuagiza Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko isimamie zoezi lile. Nichukue nafasi hii kuipongeza Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa kazi ambayo waliifanya lakini pia na Benki ya Maendeleo ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze Wakuu wa Mikoa kwa mikoa ambayo inalima korosho, kwa changamoto ya mwaka jana walisimama kidete kuhakikisha kwamba wakulima wanapata haki yao na kusimamia mazoezi mbalimbali yaliyokuwa yanaendelea likiwemo na zoezi lile la uhakiki ambalo Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa walishirikiana kuhakikisha kwamba wakulima ambao ni wakulima wa korosho kweli ndiyo wanaolipwa fedha za korosho na siyo wengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niipongeze Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, ilifanya ziara kwenye mikoa ya kusini na kusaidia kuisimamia Serikali kufanya malipo haraka kwa wakulima wa korosho ambao bado walikuwa wanadai fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi bado kuna changamoto. Sasa hivi bado kuna wakulima ambao bado wanadai fedha zao takribani bilioni 100. Mimi naamini kwa sababu Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo mahsusi alipokuwa kwenye ziara ya mikoa ya kusini, naamini kwamba Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo wataweka mikakati ya kutekeleza agizo hili ili wakulima hawa waweze kulipwa pesa zao kabla ya msimu mpya haujaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nishauri mambo yafuatayo kuhusu zao la korosho. Kwanza tunapomaliza msimu huu, kwa sababu kuna watu bado wanadai, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kama ulivyohamia wakati ule tunaanza kununua, hebu tengeneza timu ya wataalam na watu waadilifu kwa sababu wewe mwenyewe ulishuhudia kwamba katikati pale wakati wa uhakiki kuna vijana wako hawakuwa waaminifu; na nikupongeze kwamba ulichukua ulichukua hatua za makusudi mapema ili kuzuia zile dalili za rushwa ambazo zilitaka kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tumalize msimu vizuri, unda timu ndogo izunguke kila wilaya kusikiliza manung'uniko ya wakulima. Kuna wakulima bado wana manung'uniko, kuna mkulima alipeleka kilo 500 amelipwa kilo 300, akienda kwa viongozi wa *AMCOS* anaambiwa kwamba mwaka huu sisi hatukusimamia. Kwa hiyo, timu yako itasaidia ku-*clear doubts* za wakulima kabla ya msimu mpya haujaanza, nakuomba sana ufanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; kuna changamoto zingine, kuna maeneo, mimi kesi yangu naifahamu kuna Mwenge *AMCOS* kuna akaunti za wakulima 200 zimefungwa, wanatupiana lawama kwamba amefunga fulani. Kwa hiyo, timu yako kama hiyo itatoa suluhisho kwa matatizo madogo madogo ambayo yamebaki katika sekta hii ili tuanze msimu mpya na mambo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri pia kuhusu suala la ubanguaji. Changamoto nyingine tunazipata kwenye zao la korosho kwa sababu bado tunapeleka nje korosho ghafi.

Wenzetu wa Msumbiji wamekaza kamba kuhusu ubanguaji na wanafanya vizuri. Ni muda umefika sasa hivi tujikite katika ubanguaji. Tuna viwanda 12 vya awali vile ambavyo vilijengwa bado havifanyi kazi na wanunuzi wengine wamefanya maghala, kwa hiyo wanyang'anywe. Hata hivyo kuna wawekezaji wapya wameanza kujitokeza sasa hivi kutaka kujenga viwanda vipya vya ubanguaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali yangu sikivu kwanza iweke vivutio kwa wawekezaji hawa lakini pili ipunguze kodi kwa mitambo na mashine mpya wanazoingiza ili gharama za uwekezaji zisiwe kubwa; tukifanya hivyo korosho yetu nyingi tutabangua. Kwanza tutaongeza ajira na tuta-*add value* kwenye korosho zetu na hivyo mkulima atapata fedha ambayo itaongeza kipato chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye tasnia ya korosho kuna mambo mengi na bado tasnia ya korosho inahitaji usimamizi mkubwa. Kwa hiyo nikuombe Waziri wa Kilimo mwaka jana kwa sababu ya uzembe wao ambao walifanya Bodi ya Korosho ilivunjwa, niombe sasa kwamba muda umefika tuunde hiyo Bodi ya Korosho ili isimamie tasnia yetu ya korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilifanya jukumu lile kwa wakati ule kwa dharura iliyojitokeza lakini sasa hivi utafute watu waadilifu, na Tanzania wapo waaminifu, ili waanze kusimamia sekta hii ya korosho ambayo takwimu zipo wazi kwamba inaingiza fedha nyingi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye ushirika. Ushirika kama alivyosema mzungumzaji aliyepita, Mheshimiwa Jitu Soni, tulitarajia kwamba ingekuwa mkombozi kwa mkulima kwa ni ukweli usiopingika kwa Tanzania ushirika bado unamuumiza mkulima, watumishi wa ushirika hawasaidii wakulima. Kwenye zao la korosho ukifuatilia ubadhilifu mwingi unafanywa watumishi wa ushirika wamo ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi katika sekta hii ya ushirika sijui kwa nini; ukienda kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa watumishi wa ushirika na ardhi zamani utakuta wamejitenga pembeni, siku hizi Mheshimiwa Lukuvi amefanya mabadiliko makubwa sana, watumishi wa ardhi wanafuatiliwa. Mheshimiwa Hasunga muda umefika sasa, wafuatilie watumishi wa ushirika, fanya mabadiliko makubwa, wahamishe. Haiwezekani Afisa Ushirika ameanza kusimamia korosho tangu akianza kazi mpaka anastaafu. Mpeleke kwenye pamba akasimamie tasnia ya pamba na pareto atakuwa *active,* lakini Afisa Ushirika amezaliwa kwenye korosho mpaka anastaafu yupo kwenye korosho hata tija yake na ufanisi utakuwa umepungua. Fanya maamuzi magumu wa Mtwara peleka Musoma akasimamie pamba na wa Musoma peleka Songea akasimamie kahawa na hivyo wataongeza tija lakini watakutana na mazingira mapya ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikushauri sana Mheshimiwa Hasungam pamoja na mambo ambayo yanatakiwa ufumue, fumua ushirika, ushirika bado kuna uozo haumsaidii mkulima, ni mzigo kwa mkulima. Mheshimiwa Hasunga tunakuamini na uwezo huo unao; na ulivyoingia tu kwa sababu umeapa tu ukaenda kusimamia korosho, Inshallah utafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la umwagiliaji. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hatua alizochukua juzi kwa kuwasimamisha wale viongozi wa Tume ya Umwagiliaji. Mheshimiwa Hasunga unga mkono pale alipoishia Mheshimiwa Waziri Mkuu, bado kwenye ngazi ya kanda nako kuna madudu vitu, nenda kafumue kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Umwagiliaji kama ingekuwa inafanya kazi yake vizuri tusingehangaika sasa hivi kutafuta chakula kutoka maeneo mengine. Sisi Mtwara tuna *Ruvuma Basin,* Kitere, Rufiji Kusini lakini hayatumiki ipasavyo. Haiwezekani mradi wa mwaka mmoja lakini watu wa tume wanauandaa kwa miaka mitatu na watu wa tume kwa

sababu tuna *organization structure* ambayo ni ya kizamani, wapo kwenye kanda. Kanda ya Kusini ashughulikie Mtwara, Lindi na Ruvuma, hawezi kuwa na ufanisi. Hii tume ivunjwe sasa hivi wawepo kwenye mikoa, yule wa mkoa awajibike kwa *RAS* na wawepo watendaji kwenye Wilaya wawajibike kwa wakurugenzi; lakini sasa hivi wapo wapo tu, wakiwa kwenye kanda hawajibiki kwa *RAS* yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Chikota kwa mchango wako.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, tunaendelea, Mheshimiwa Aida Khenani dakika tano, Mheshimiwa Msigwa dakika tano na Mheshimiwa Bobali ajiandae.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru japo kwa dakika chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kilimo tunazungumzia kiungo kikubwa sana ndani ya taifa. Nitapenda kuchangia vyuo vya utafiti. Hakuna maendeleo ya kilimo kama hatujapeleka fedha na vyuo vya utafiti kuwekwa kipaumbele. Naomba nishauri tu Wizara ya Kilimo, kwamba, kama hamna kipaumbele kipaumbele cha kwanza kwenye Wizara yenu iwe ni vyuo vya utafiti. Huwezi kufanya chochote kwenye kilimo bila kuweka kipaumbele kwenye utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vyuo vichache vya utafiti, lakini hata vilivyopo havipelekewi fedha, na hata fedha zikitengwa hazipelekwi kwa wakati. Kilimo kinachoendelea Tanzania ni kilimo cha mazoea, ukiangalia

mbolea inayotumika kwenye mazao mengi wanatumia vile vidude vya visoda au vikopo vya maji. ni lini walifanya utafiti kwenye udongo kwamba kile ndicho kipimo sahihi? Ni kwa sababu ya mazoea. Hivyo, hatuwezi kuendelea bila kufanya utafiti, ni bora leo tukatenga fedha nyingi kwenye utafiti ili tuweze kuinua kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la vituo vya rasilimali za kilimo. Lengo la kuweka vituo hivi lilikuwa ni kupeleka huduma kwa wakulima; na hivi vituo vilipaswa viwekwe kama vituo vya afya vya kila kata; lakini leo nitolee mfano mdogo tu, Mkoa wa Rukwa una kata 97 hivi vituo vipo 9, kuna kilimo hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la masoko; suala la masoko tumezungumza sana. Wajibu wa mkulima ni kuhakikisha analima au anzalisha kwa tija. Wakulima wetu wamejitoa lakini Serikali imeshindwa kutimiza wajibu wake kuwatafutia masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, uamuzi mlioufanya kwenye korosho ni uamuzi wa dharura sana lakini kama ni uamuzi endelevu wa kutumia Benki ya Maendeleo ya Kilimo mtuambie kwamba itakuja kutumika na kwenye zao la mahindi, kwa sababu ilianza kwenye korosho na ile siyo benki ya korosho peke yake. Kwa hiyo, nashauri Serikali busara iliyotumika itumike tena, kama ilikuwa ni dharura tafuteni soko kabla ya msimu wa mavuno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la miradi ya umwagiliaji; hatuwezi kuwa na kilimo ambacho kinategemea mvua peke yake, lazima wajielekeze kwenye mabwawa ya umwagiliaji. Mengi yaliyopo mengine yamekufa, mengine yamesimama, kosa ni la nani? Serikali wana wajibu wa kupeleka fedha na mambo haya yanafanyika hivi ni kwa sababu Serikali inakosa kipaumbele; inashika pale, inashika hapa, matokeo yake kilimo chetu sijui wanakwenda kukipeleka wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Maafisa Ugani; nimefuatilia kidogo – akija Waziri atanisahisha, yaani mpaka sasa tuna upungufu wa Maafisa Ugani 20,100, hali ya kilimo itakuwaje kama Maafisa Ugani kuna upungufu huo. Nawaomba Wizara ya Kilimo kipindi wanapeleka mapendekezo yao kwa Serikali cha kwanza waombe idadi halisi ya Maafisa Ugani ambao watakwenda kutoa ushauri kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kumekuwa na shida sana kwenye Wizara ya Kilimo; bei ya pembejeo haiendani na hali halisi ya bei ya mazao. Naomba nishauri kwa kuwa *slogan* ya Awamu ya Tano ni Serikali ya viwanda, viwanda wajenge hapa ili bei ya pembejeo ipungue, sasa hivyo viwanda watajenga viwanda gani, hivyo viwanda vitahifadhi nini kama upande wa *materials* wenyewe tumefeli, upande wa umwagiliaji tumeshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ya Kilimo iwe na vipaumbele, kipaumbele cha kwanza kabisa kiwe kuimarisha miradi ya umwagiliaji na hii itasaidia wakulima wetu. Suala pia la danadana la kutokuwalipa mawakala kwa suala la kwamba eti wanafanya utafiti; wanafanya utafiti kwa miaka mingapi? Wale wenye makosa basi wasipewe, wale ambao wanabainika hawana makosa walipwe fedha zao. Uhakiki huu pia ni kama njia mojawapo ya kutegeategea hivi, Serikali kushindwa kutimiza wajibu wake, kama fedha hakuna waseme kwamba fedha hakuna. Kuna watu wameuziwa nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la bima za wakulima lifanyike haraka ili Serikali wajue maumivu ambayo wanayapata wakulima ili makosa wanayofanya Serikali wawe wanawajibika kwa wakulima hawa. Hili jambo liende sambamba na matamko ambayo yanatolewa. Nazungumza hivi kwa sababu, narudia tena leo kwamba tamko la Serikali lililotoka... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Khenani. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze mambo mawili. Jambo la kwanza ni kuhusu kilimo cha parachichi; naomba niishauri Serikali, Nyanda za Juu, hasa Iringa ni *corridor* ya parachichi duniani na naomba tafiti zilizofanyika wahakikishe wanazifanyia kazi kubwa kwa ajili ya kuhakikisha wakazi wa Iringa na maeneo mengine wananufaika na zao la parachichi. Naomba sana wasifanye *business as usual* kwa sababu wanatumia *methods* zilezile, ulimwengu ume-*change,* wanafikiri vilevile, *change* namna ya kufikiri kulingana na ulimwengu unavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, katika kitabu cha hotuba yetu ukurasa wa 24 tumezungumza jinsi ambavyo Mheshimiwa Profesa Kabudi na Gavana wa Benki walisimamia kwenye kuandika ule mkataba wa wanunuzi wa korosho. Profesa ni *authority,* profesa ni mtu ambaye inatarajiwa kwamba anajua mambo mengi, anajua namna ya kufikiri na Mheshimiwa Rais katika Serikali ya Awamu ya Tano amefanya kazi nzuri sana ya kuwaleta wasomi, Maprofesa na Madaktari, tunategemea Madaktari na Maprofesa wanapofanya maamuzi lazima wanakuwa wamepanuka sana ili wasilipotoshe Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kutia aibu mahali ambapo mtu kama Mheshimiwa Profesa Kabudi amekaa, wamekuja na ile kampuni ya kitapeli kabisa, Rais amewaamini kampuni ya kihuni wanalitangazia Taifa kwamba kila kitu kitakuwa safi, korosho itanunuliwa, halafu korosho haijanunuliwa. Hili ni jambo la aibu, hatuwezi kulifumbua macho, lazima Mheshimiwa Profesa Kabudi ajiuzulu kwa kulipotosha Taifa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la aibu sana hili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Hebu ngoja. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, wewe ni *term* yako ya ngapi Bungeni?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Naam?

MWENYEKITI: Muhula wa ngapi huu?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Wa pili.

MWENYEKITI: Ahaa, kwa hiyo unajua sana mambo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Ndiyo.

MWENYEKITI: Haya.

Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kuhusu utaratibu chini ya Kanuni ya 64(1)(e) na 63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kueleza tu ni kwamba Mawaziri hapa Bungeni tunawajibika kwa pamoja mbele ya hili Bunge na hii iko chini ya Ibara ya 53(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Kwa hiyo kumchukua Waziri mmoja mmoja kumtaja na kumrundikia tuhuma sio sahihi hata kidogo kutokana na dhana ya uwajibikaji wa pamoja. Anachokifanya Mheshimiwa Profesa Kabudi ni sisi wote tumekubaliana. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hebu mtulie. Amesimama *on a point of order.*

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kawaida, sisi tunawajibika kwa pamoja wenzetu wanapiga kelele kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusisitiza kwamba niwaombe, badala ya kumchukua Waziri mmojammoja na kumtungia sasa ngonjera za kumlaumu, sio sahihi. Msimamo anaouonesha Waziri yeyote hapa ni msimamo wa *cabinet* nzima, basi tulaumuni sisi wote lakini sio Mheshimiwa Profesa Kabudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe ambaye ndio Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Bunge. Kasema kitu kizuri kwa maana kwamba shughuli zote zinazoendelea sasa hivi humu Bungeni ikiwepo hoja hii ya Wizara ya Kilimo ni ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo wewe unapochangia Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, sema tu Serikali katika haya na haya mimi sijaridhika na hayo yaliyofanyika, maana ni Serikali. Sasa katika uwajibikaji wao Serikali inawajibika kwa pamoja, lakini sio kwamba unam-*single out* Waziri mmoja, kasimama juu ya meza, huyu sijui alikuwa anafanya nini, hapana.

Mheshimiwa Msigwa, endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimem-*single out* Mheshimiwa Profesa Kabudi alikuwa Waziri wa Katiba na Sheria, kwa hiyo *we expected* kwamba yeye angetu-*guide* na angem-*lead* Rais katika njia iliyo sahihi, *he was responsible for that Ministry,* hatuwezi kum-*spare.* Amelipeleka Taifa kwenye sintofahamu kwa ku-*mislead* nchi, ni wajibu wake kusimama hapa na kusema kitu gani kilifanya aingie kwenye mkataba wa hovyo na nchi hii, lazima... *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchungaji Msigwa nimeshaliamulia, sasa unarudi hukohuko, usinilazimishe niangukie kwenye Kanuni ya 73. Haya.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Serikali imekubali kwamba inawadanganya wananchi wa Mtwara na korosho, ina-*mislead* Taifa la Tanzania na kuwapa ahadi hewa... *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: ...kwa sababu inaingia kwenye mikataba ambayo haitekelezeki.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu, niambie Kanuni.

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanzia na 68 nitakwenda mpaka 64 kuhusiana na masuala anayosema ni ya uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mheshimiwa Mbunge anayechangia...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: ...anatenda makosa.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kaa chini.

Mheshimiwa Frank.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, 64 ngapi, hajataja Kanuni.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Subiri nimalize kutoa taratibu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ametaja jumla, hajataja Kanuni kipengele gani.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, unafahamu mimi huwa nawastahi lakini nawasikia vizuri sana sauti zenu na hasa ninyi wawili hapa, naweza nikaamua kuwatoa nje sasa hivi. Hapa hatuko sokoni, tuiheshimu nyumba ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Waziri, unaposimama kwa suala la utaratibu unakwenda tu *straight* kama ni Kanuni ya 64 fasili ya ngapi, mara moja. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa najitahidi ku-*save* muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Kanuni ya 64(1)(a) naomba nizungumze kwamba Mheshimiwa Mbunge anayechangia anasema uongo na ninaomba ni-*prove* kupitia Kanuni ya 63 uongo anaouzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitoe masikitiko yangu kwa niaba ya Watanzania. Ziko habari ambazo tunaendelea kuzithibitisha, kwamba kwa upande huo mwingine wamehusika pia katika kutafuta hata rushwa na kumtishia huyo aliyekuwa anataka kununua hizo korosho.

Hilo tunalifanyia kazi na tutawataja humu mmojammoja na hizo...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: ...rushwa walizokuwa wanataka kuchukua, hilo la kwanza. La pili, ni kwamba taifa halijapata hasara kwa sababu sisi hatujampa korosho huyo...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: ...mwenye kampuni aliyetaka kununua. Mtu kutaka... nakufundisha biashara, nisikilize.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: ...kampuni iliyotaka kununua ilikuwa ilipe, imefika muda haijaweza kulipa, hakuna korosho aliyopewa, hasara hiyo unayoizungumza ni hasara gani?

MBUNGE FULANI: *What is commerce?*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawarudisha sasa kwenye mstari. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa una dakika zako mbili zimebaki, ongelea hoja yako na acha kutupeleka nje, *otherwise* Mheshimiwa Naibu Waziri ameshindwa tu kunifikisha katika *level* ambayo ningekutaka wewe ufanye hivyo, endelea umalize.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kuna kitu gani kimetokea? Kaa chini.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Nasema hivi Mheshimiwa Matiko, kaa chini.

Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: ...rushwa yule.

MBUNGE FULANI: Muone kamdogo kake.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Katoa *allegation* yule.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ninayoijenga hapa, Serikali ina wajibu wa *welfare* za wananchi. Serikali imesababisha tuko *foreign, forex* imeshuka kwa sababu ya mipango ya hovyo ya Serikali kuhusiana na korosho. *For the first time* ninyi Mawaziri, amesema hapa Kaimu Kiongozi, walimshauri Rais wakaamua kutumia Jeshi kuchukua korosho, anakuja Waziri hapa anasema eti anayeleta mkataba amekuja na ndege, anashangaa na ndege, mbona ana *caravan* hapa, *what is* ndege? Wanamshangaa eti kwa sababu amekuja na ndege ndiyo wanaingia kwenye chaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Serikali lazima wasimame waombe radhi kwa wananchi, mnaharibu kilimo, wamewa-*cripple* wananchi kwa sababu ya mikataba ya hovyo, watu wengine kule Mtwara wameshindwa kupeleka watoto wao shule. Walikusanya korosho zao halafu wanasema hapa tuwapigie makofi. Mawaziri waliohusika na Waziri wa Katiba anatakiwa a-*step down,* amei-*mislead* nchi. Kuna wengine wamekufa watoto wao wameshindwa kupeleka shule halafu wanasema hapa tusiseme, tumekuja kufanya nini hapa, *shame on you Government. (Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Haya, kuhusu utaratibu.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nakusomea kuhusu utaratibu kwa Kanuni ya 63(1), ukiniruhusu nitaisoma.

"63.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisimama Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri amesimama ama kumpa taarifa au kuhusu utaratibu ametushutumu Kambi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa kaa chini sasa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: ...naendelea kusema, acha nijenge hoja yangu.

MWENYEKITI: Nimeshasimama. Nimeshaliamulia hilo, usiturudishe nyuma.

Tunaendelea; Mheshimiwa Bobali, dakika kumi.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nianze na suala la minazi; kwetu sisi watu wa Mwambao wa Bahari ya Hindi nazi ni chakula, lakini pia inatumika kupamba miji yetu. Ukifika Lindi, Kilwa, Bagamoyo, Pangani na maeneo mengine, miji inapendeza kwa kuwa na minazi. Minazi inakufa; mwaka jana

nilizungumza humu na bahati nzuri wakati fulani dada yangu pale, Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, wakati akiwa Naibu Waziri wa Kilimo nilizungumza naye nikiwa jimboni kumwonesha masikitiko makubwa ya wananchi ambavyo mashamba yao ya minazi yanakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Wizara ya Kilimo na hili nalo linawashinda? Yapo maeneo ambayo nitakutajia, kwa mfano jimboni kwangu minazi sasa imekufa kabisa. maeneo yale ya Kilangala, Mchinga, Milola, Lutamba, maeneo ya Sinde, lakini hata Kilwa kwa Mheshimiwa Ngombale hapa ukifika Miteja, nenda Kisiju, minazi imekufa, nenda kule Mafia, ukienda Pangani minazi inakufa. Hili nalo linawashinda? Naomba Mheshimiwa Waziri aje na jibu. Waende wakafanye utafiti tujue minazi hii inakufa kwa sababu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ufuta; Mkoa wa Lindi ni wakulima wazuri sana wa ufuta na ufuta wetu ni ufuta mzuri, una mafuta mazuri, mengi. Wananchi baada ya dhoruba kubwa tuliyopigwa kwenye korosho, mategemeo yetu yalibakia kwenye ufuta, tunaanza kutaka kukata tamaa. Kuna jambo limeingizwa katika mfumo wa ununuzi wa ufuta, jambo hili linakwenda kuwaumiza wananchi wakulima wa ufuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matajiri wale kutakiwa kukata vibali kulipa leseni zote, wameandikiwa barua na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa walipe shilingi milioni mbili ya kuchangia Mwenge. Suala la kuchangia Mwenge walilifanya liwe kwenye biashara? Hivi kuna mfanyabiashara gani atalipa shilingi milioni mbili, milioni mbili hii asiihamishie kwa wananchi? Kwa hiyo kuja kuzima Mwenge Lindi mwaka huu wanakwenda kuwatoza wananchi kulipia Mwenge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *this is not fair.* Jambo hili lazima Mheshimiwa Waziri ulitolee maelezo na ni kwamba hatutakubali, Mheshimiwa Waziri lazima uwe ukweli, kwamba sisi tutawaambia wananchi wasikubali na hawatauza ufuta wenyewe kwa sababu kwenye korosho watu wana vidonda

vikubwa na nitavisema hapa. Sasa wakitaka kuturudisha na huku kwenye ufuta haya mambo kwa kweli Mheshimiwa Waziri wayaangalie vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua aliyoandika Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kuwaandikia matajiri wanaokwenda kununua ufuta ambao msimu utafunguliwa tarehe 25, mwezi huu, ile barua suala la kuwaambia walipe shilingi milioni mbili mchango wa Mwenge ufe. Hebu *imagine* kukiwa na matajiri 50 watachangia milioni 100, milioni 100 hii inahamia kwa wakulima, inahamia kwa halmashauri, na mfumo wenyewe mwaka huu tunakwenda kuuza kwa mfumo wa mnada. Kwa hiyo lazima hii tozo itahamia kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, kuhusu korosho; Bunge lako hili tarehe 14, Mwezi Novemba, lilipitisha Azimio la Kuunga Mkono Serikali Kununua Korosho, humu ndani mwaka jana na tukapongeza lile jambo. Leo ukiwaambia Wabunge wanaotoka maeneo yanayolima korosho tulete orodha ya wananchi ambao bado hawajalipwa, orodha hapa tutasoma majina siku nzima. Watu wengi hawajalipwa. Mimi mwenyewe nimeuza korosho zangu, katika milioni 30 nimelipwa milioni tatu, milioni 27 nitalipwa lini, sijui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ninavyoongea, nimetoka jimboni juzi, tayari mikorosho imeanza, msimu wa palizi umeanza na tayari kuna baadhi ya mikorosho imeshaanza kutaka kuonesha kutaka kuzaa. Kama jimboni kwangu wananchi hawajasafisha kabisa na kilio chao kikubwa watu hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mtwara kuliwekwa *centre* ya kulipa wakulima; wakulima walikuwa wanapiga simu pale Mtwara. Sasa hivi nasikia ile *centre* imefungwa kabisa, kwahiyo matumaini kwamba tutalipwa hayapo; na kwa Lindi tumeombwa radhi na Mkuu wa Mkoa kwamba tunawaombeni radhi wakulima wa korosho. Sasa hii inamaanisha nini? Mimi nawaambia, suala la korosho kwetu sisi ndiyo maisha yetu. Leo madiwani wa Halmashauri ya

Wilaya ya Lindi ninakotoka mimi wana miezi sita hawajalipwa posho, wana miezi sita; wanakwenda wanafanya vikao ile posho yao ya mwezi hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendeshaje halmashauri hizi? Halmashauri yetu mpaka leo makusanyo yake mpaka sasa ni asilimia 20, sasa tutatatuaje changamoto za wananchi endapo fedha za ushuru wa korosho hazitapelekwa halmashauri? Kwahiyo hili suala la korosho tusilifanyie siasa kwa mtindo huo maana kila siku tunaambiwa maneno. Jana nimeona Mheshimiwa Waziri wa Biashara anatuambia watu wa Lindi na Mtwara tunazaana sana kwasababu tunakula korosho; huu ni mzaha. Tulipeni fedha zetu, walipeni wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuja Mtwara akasema fedha zitapelekwa bilioni 58, alivyotoka pesa zimepelekwa bilioni 18. Kwa utaratibu huu zitakwisha lini kulipwa? Wengine tuliongea humu ndani ya Bunge kuhusu suala hili tukatolewa humu Bungeni; kwamba huku tunakokwenda siko. Tukapiga na vigelegele, hivi hata Bunge halitaki kujua hatua ambayo Serikali imechukua? Mimi napendekeza kama itakufaa Bunge liunde tume iende ikachunguze, kwenye korosho kuna mambo makubwa, watu hawajalipwa, watu wametiwa umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nakushauri jambo linguine; kwa kuwa msimu umeanza, basi nendeni Benki mkawakopee hawa watu basi walau waweze kufanya palizi; au mkawape bondi waweze kukopesheka. Mtu ana hela zake milioni 30, milioni 20, milioni 10 anashindwa milioni moja ya kufanya palizi shamba lake; nendeni mkawawekee bondi basi Benki waweze kuwakopesha ili kilimo kiendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza suala la korosho tunazungumza maisha yetu. Baadaye mtakuja kutuambia hapa watu wa Lindi na Mtwara tunafeli; watu hawasomi kwasababu wana-*frustrations* nyingi ikiwemo na ya korosho. Mtoto akienda shuleni hawezi akafanya vizuri

wakati nyumbani baba analalamika hajalipwa korosho. Jambo hili Bunge lazima liingilie kati, Serikali inaonesha wazi kwamba imeshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bobali, tunaendelea, Mheshimiwa Khadija Aboud, Mheshimiwa Oran Njeza ajiandae na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: AhsanteMheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa napenda kuipongeza Serikali, napenda kuipongeza pia Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Kilimo kwa juhudi kubwa wanayoifanya kuhakikisha kilimo cha Tanzania kinakua, kinakua endelevu na chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali na Mheshimiwa Rais kwa kuitoa Tume ya Umwagiliaji kwenye Wizara ya Maji na kuipeleka kwenye Wizara ya Kilimo. Tume hii kupeleka kwenye Wizara ya Kilimo imefika hasa pahali pake; kwa maana kwamba Wizara ya Kilimo sasa itaitumia Tume hii ya Umwagiliaji kwa kukuza kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Tume hii ya Umwagiliaji lazima sasa Wizara ijipange vizuri ili kuhakikisha Tume hii watendaji wake wanafanyakazi kwa uadilifu na weledi. Ili kuifanya Tume hii ya Umwagiliaji iweze kufanya kazi zake vizuri ni vyema sasa miundombinu yote ya umwagiliaji inayohusu kilimo iangaliwe upya kuhusu kodi; ikiwemo mitambo ya kuchimbia mabwawa, vifaa vyote vya umwagiliaji pamoja na mitambo ya kuchimbia visima vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiliangalia hili la kodi miradi ya umwagiliaji itakuwa na wananchi watahamasika sana kulima kilimo cha umwagiliaji. Kutokana na hali na mabadiliko ya tabia nchi kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi wetu

wananchi wa Tanzania. Kwasababu kilimo hiki kitakuwa endelevu na cha muda wote kwa maana hiyo viwanda vyetu sasa vitapata malighafi ya kutosha na kwa muda wote. Pia kilimo cha umwagiliaji kitatuweka vizuri katika usalama wa chakula na kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, katika kuimarisha kilimo chetu nchini ni vyema sasa tukawekeza zaidi kwenye utafiti. Tuingize nguvu zetu nyingi katika utafiti katika kupata mbegu bora ambazo zitatoa mazao mazuri yenye tija. Kwa faida ya kilimo hiki ni vyema sasa tukaziimarisha hizi taasisi zetu za utafiti kama TARI, Taasisi zetu za kutayarisha mbenu kama ASA, tukazipa mitaji ya kutosha ili ziweze kufanyakazi zake vizuri kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania na hasa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali na Wizara ya Kilimo kwa kuanzisha kitengo cha kutafuta masoko ya kilimo. Kitengo hiki kitakuwa mkombozi na mtatuzi wa changamoto za mazao yetu ya kilimo katika masoko mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuipongeza Wizara ya Kilimo kwa kuanzisha mradi wa kudhibiti sumu kuvu. Sumu kuvu ilikuwa ni tatizo kwa mazao yetu; na kwa vile mwananchi alikuwa hajui sumu kuvu ni nini kwahiyo baadhi ya wananchi walipoteza maisha kutokana na kula vyakula vilivyokuwa na sumu kuvu. Kwahiyo naipongeza hii Wizara kwa kuliona hili na kuhakikisha kwamba mazao yetu yanakuwa hayana sumu kuvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya kilimo. Bajeti ya kilimo imeongezeka. Pia napenda kuishauri Serikali iendelee kuongeza bajeti ya kilimo ili kukidhi matakwa na mahitaji yote ya Wizara ya Kilimo na taasisi zake zote. Bajeti ikiongezeka taasisi zote zitapata fedha na miradi ya kilimo itaongezeka kwa kupata mbegu bora viuatilifu bora na mengineyo. Naipongeza Serikali kwa kuona nakupunguza tozo mbalimbali za kilimo, lakini pia naishauri Serikali iendelee kuangalia tena uwezekano wa tozo na

vikwazo au changamoto mbalimbali inazokabili sekta hii ya kilimo ili wananchi wahamasike kulima kilimo chenye tija na kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imechambua kwa kina sana kuhusu zao la korosho, naipongeza sana kamati kwa ushauri wake kwa Serikali, na ninaamini kwamba Serikali haina nia mbaya na wananchi au wakulima wa korosho. Wakulima wa korosho watalipwa na watapata haki zao kwasababu najua Serikali iko mbioni sasa kuhakikisha madeni yote yanalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyongeza tu, na mimi napenda kuongeza kwenye korosho kwamba waangalie pia na wadai wa korosho wa mwaka 2017/2018, kwa sababu nako huku kwenye vyama vya ushirika vimewatapeli wananchi wetu wakulima wa korosho kwa madai yao ya mwaka huu. Kwa hiyo Serikali itakapoandaa mchakato wa kuwalipa wananchi na wakulima wa korosho iangalie pia na wale wa mwaka wa jana; kwa sababu tunataka kilimo cha korosho kiwe endelevu na chenye tija mazao yaongezeke tupate mazao ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naipongeza sana Wizara ya Kilimo kwa jitihada mbalimbali za kuendeleza kilimo nchi Tanzania na Serikali yetu kwa ujumla ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais wetu kuhakikisha kwamba kilimo kinakua, kilimo chenye tija kwa ajili ya biashara na mtaji au rasilimali muhimu na mali ghafi kwa viwanda vyetu tunavyovijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, naunga mkono hoja, ahsante sana, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Khadija kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Mwambe na Mheshimiwa Kakoso ajiandae.

MHE.ORAN M. NJEZA: Nashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hii

Wizara muhimu ya Kilimo. Ningependa kuanza kwa kutoa pole kwa wananchi waliopoteza maisha na majeruhi kutokana na ajali ya gari iliyotokea jana pale Mji Mdogo wa Mbalizi Wilaya ya Mbeya. Kwa kweli eneo lile limekuwa ni hatarishi sana, nafikiri Wizara ya Miundombinu pamoja na Mambo ya Ndani pamoja na juhudi wanazozifanya wangejaribu kuangalia namna ya kupunguza ajali katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuisema hiyo nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Hasunga, Naibu wake Mheshimiwa Mgumba, na Naibu wa pili Mheshimiwa Bashungwa; kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana, ni timu nzuri timu ya wataalamu. Ukiangalia na hii hotuba yao ya bajeti kwa kweli imesheheni utaalamu mwingi unaoonesha matarajio mengi, na imekaa kimkakati mno. Kwahiyo inaonesha kabisa ya kwamba wataalamu watatu walikaa vizuri na wakaitengeneza hii hotuba yao vizuri. Mimi ningependa kuongezea kidogo tu katika hicho ambacho nao wametuletea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi nimezungumzia zao la pareto hapa na watu inawezekana wanashangaa hii pareto ni nini. Pareto Tanzania inaongoza Afrika, na sisi ni wa pili duniani. Kwa miaka mingi tulikuwa tunazalisha takriban tani zaidi ya elfu nane lakini leo hii tunazalisha chini ya tani 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilo moja ya pareto huko sokoni duniani ni dola kati ya 150 mpaka dola 300, kwa kilo moja; sasa angalia umuhimu wa hili zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna fursa za kuweza kuzalisha zaidi pareto. Sasa ningemuomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa jicho la kipekee, ni namna gani atusaidie; kwa kuanzia usimamizi wa hili zao sio mzuri tuna Bodi ya pareto na siwezi kuwalaumu sana wataalamu inawezekana katika ule muundo sio mzuri sana. Kwasababu Mheshimiwa Waziri hapa amesema anajaribu kuangalia namna ya kuboresha ile sheria ya kilimo. Ile Bodi ya pareto kwa kweli haijatusaidia.

Mimi kama Mbunge wa Bunge la Mbeya Vijijini tunalima zaidi ya asilimia 85 ya pareto yote inayozalishwa Tanzania, lakini inavyoelekea katika wadau wa pareto Mbeya Vijijini haimo. Sasa ukianzia hapo tu utaona ya kwamba hili ni tatizo, ya kwamba hata wadau wenyewe hawajulikani. Bei ya pareto iliyooneshwa kwenye kitabu cha Waziri kwa kilo ni 3,700, wakulima wanalipwa shilingi 2,300. Sasa unajaribu kuangalia, hizi takwimu zinatoka wapi? Utakwenda kuwaambia nini wakulima? ya kwamba pareto yenu mnayolima mnalipwa shilingi 3,700 wastani ilhali zaidi zaidi wanalipa 2,300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimesema kuwa kilo moja ya *extract* ambayo inatokana na kuichuja ile pareto, kilo moja inakwenda mpaka dola 300; na hata Kenya wenzetu wananunua kwetu kwa dola 70, India kwa dola 90 mpaka 100 na Korea vivyo hivyo. Sasa huyu mkulima unayemlipa 2300 inatoka wapi? Sasa je, kama nchi tunapoteza kiasi gani? Nilikuwa najaribu kuangalia hata ile Kampuni inayonunua pareto, nimegundua katika hisa mle kuna asilimia 15 ambazo ni za wakulima. Hizo asilimia 15 mpaka leo hatujui ni nani anayezifaidi. Asilimia 15 ya hisa ni nyingi. Kwa makusudi kabisa Serikali baada ya kubinafsisha hiki kiwanda ikasema wakulima nao wawe sehemu ya maamuzi ya hiki kiwanda, lakini mpaka leo hizo asilimia 15 hazieleweki nafikiri Waziri labda akiwa pamoja na TR waje watuambie hizo asilimia 15 ziko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vile vile niongelee na kwenye kahawa. Fursa tulizonazo kwenye kahawa bado ni kubwa, bei ya kahawa hapa kwetu ni ndogo. Leo hii sisi tunauza dola mbili kwa kilo, Kenya ni zaidi ya dola tatu, lakini ukiangalia kwenye soko la ICO kule paundi moja ni kama senti 144 ambazo ni dola 1.44 sasa hii tofauti yote inatoka wapi? Hii kahawa yetu ya arabika tunayolima Tanzania ni nzuri sana kwasababu ndiyo inayotumika kwenye *blending* kwenye kahawa nyingine kwa vile sisi tunachuma kwa mkono hizi kahawa, kwa hiyo ina heshima ya kipekee. Sasa hiyo hela tofauti hiyo inayopotea inaenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukienda zaidi kwenye masoko, hata ya mahindi. Nimemsikia msemaji hapa mama Anna Lupembe amezungumzia hoja ya muhimu sana kuhusu soko la mahindi la Kongo. Ni kweli tuna soko zuri Kongo, kuna rafiki zangu na ndugu zangu ambao wame-*access* hilo soko, lakini wamekuwa wakipitishia hiyo mizigo Zambia. Zambia sasa hivi wameweka masharti, lakini sisi tunapakana na Kongo. Sasa kwanini tusitumie njia ya Kongo na barabara za lami hizo zipo?

Sasa haya ndiyo mambo ambayo Wizara ikikaa mkakati kama walivyokuwa Mawaziri, tutumie *brain* zenu kuweza kuwaokoa wakulima tuachane na kufanyakazi kwa mazoea. Kama kuna timu zinawakwamisha huko angalia hizo timu zinazowakwamisha namna gani mzifumue sio wakati wake huu wa kuanza kulea watu ambao hawatusaidia katika kazi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo napenda tu niunge mkono hoja nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Njeza, tunaendelea, Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo na mimi niweze kuchangia mjadala ulioko mbele yetu, wa Wizara ya Kilimo. Ningependa kujikita kwenye mambo mengi sana lakini kwasababu ya muda ninaomba tu niende sehemu chache lakini nitazitaja zile ambazo ningependa nichangie.

Suala la kwanza ambalo nitalizungumzia ni kuhusiana na mkataba wa Indo na hekaya ya Profesa Kabudi suala la pili ambalo ningependa nizungumzie ni suala la *export levy* ambalo tulijadili ndani ya Bunge hili hili, suala la tatu ni madeni ya wakulima ya zamani; na Mheshimiwa Waziri nitaomba u-*note down* wakulima wa korosho walikuwa wanadai pesa ambazo zilifanyiwa *auditing* tukaambiwa watakuja hapa kutakuwa na kesi vitu vingine havijafanyika pesa ya misimu iliyopita, tunaomba hili ulichukulie.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe kabla hujaanza sasa nimeshatoa uamuzi kuhusiana na hilo endelea kuchangia semea, kosoa Serikali.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Kwa hiyo kuna hayo madeni, na nishauri kabisa hapa kwamba sheria ya *export levy* pale ambapo tuliondoa haimaanishi kwamba zile pesa ambazo Serikali ilikuwa inawajibika kuzirudisha kwa wakulima wa korosho zisiende. Kwa hiyo tunaomba na hizo pesa nazo ziende.

Suala lingine ni suala la mradi wa *SAGCOT* tunataka hapo mtakapo kuja mje mtupe majibu kabisa kuna taarifa kwamba mradi wa *SAGCOT* umefutwa kwasababu tumeshinda ku-*comply,* sasa mtueleze ni kwanini. Pia kukosekana kwa pesa kwenye mradi wa *ASDP II* ilhali nimeona kwenye vitabu vyenu mnautaja na mkisema kwamba ni mradi wa kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine; nitaomba utueleze Mheshimiwa Waziri, kama ni wewe unahusika au dada yangu pale Mheshimiwa Manyanya ambaye alituambia mbaazi ni mboga. Yeye tunataka mtueleze waziwazi ni shilingi ngapi mpaka sasa hivi imetumika kwa ajili ya kuwalipa wale askari na gharama zima La zoezi la kukusanya zile korosho na je gharama hii itaingia kwenye bei halisi ya kuuzia korosho na ndiyo maana mnashindwa kuziuza hizi korosho? Tunataka sasa mtupe ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hapa ni suala la Chuo cha Naliendele. Ningependa kabisa Mheshimiwa Waziri utueleze mna mpango gani hasa mahsusi na Chuo cha Naliendele? Kwasababu tumesema tuna nia ya kutaka kuendeleza hapo. Sisi kwenye kitabu chetu cha Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo Waziri wetu alikiweka pale kwenye ukurasa wa 24 kifungu namba 85 ambacho hakikufutwa na Waziri aliyesoma pale hakukisoma kwa wakati ule. Sasa mimi naomba niwasomee na Watanzania wakielewe;

"Katika mazingira ya utatanishi Serikali ilisaini mkataba wa kuuza korosho tani laki moja na Kampuni ya Indo Power ya Kenya mkataba ambao haukutekelezeka licha ya kupigiwa debe na Waziri wa Katiba na Sheria wa wakati huo Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi (Mb) na Gavana wa Benki Kuu., Kambi Rasmi Bungeni inataka Serikali kuwawajibisha wahusika wote kwa kulipotosha Taifa na kuliingiza katika hasara kubwa kutokana na mkataba ambao haukufanyiwa upembuzi yakinifu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndio yalikuwa mawazo yetu sisi Kama Kambi Rasmi Bungeni.

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe hebu keti, kuhusu utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Kanuni

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 53(8): Mbunge yoyote haruhusiwi kufufua jambo ambalo limekwisha kufanyiwa maamuzi. Jambo hili limeshazungumzwa sana toka tumeanza mkutano huu kipindi cha jioni ya leo na limeshatolewa maamuzi.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawaombeni tusilikizane, nawaombeni tusilikizane.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kusisitiza utaratibu ndani ya Bunge

ufuatwe. Huyu Profesa ambaye watu wanataka kuchukua *advantage* ya kumdhalilisha ni mtu mwenye heshima na ameshafanya mambo makubwa katika Taifa hili. Kwa hali hiyo haipendezi, haipendezi, tungeomba sana utaratibu wa kanuni za Bunge ufuatwe na kwa mujibu wa Kanuni ya 53(8) naomba Waheshimiwa Wabunge waheshimu maamuzi ya kiti ambayo yamekwishafanyika.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge mimi ndio naongoza Bunge, kaa chini, hebu Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Frank, narudia mara ya pili mimi huwa napenda sana kuwa-*guide* kwenye kanuni.

Mheshimiwa Esther Matiko ulipoomba utaratibu nikakwambia nimeshaliamulia na ningeweza kukwambia hivi, kanuni ya 63 unayoitumia lazima awepo wakati huo Mbunge anayeongea, lakini hapakuwa na Mbunge anayeongea, nilikuwa nimeshaliamulia hilo ukataka kulifufua.

Narudia Mheshimiwa Mwambe suala la kumtaja Profesa *whether* una hotuba yako au nini, narudia hivi wewe endelea kuchangia ya kwako unavyoona kuhusiana na zao hilo. Mheshimiwa Mwambe endelea.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nisimame nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Kabudi kwa kuwalostisha au kuwasababishia hasara wakulima wa korosho Tanzania na kwa kufanya hivyo...*(Makofi*)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe, usinifanye kama *logic* sizifahamu, nimeshaliamulia, kama wewe tusaidie kutoa ushauri ni nini twende mbele.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshauri...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Hakuna mtu anayeongea hapa, unampa nani utaratibu, kaa chini, kaa chini.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshauri kuna kitu kinaitwa *ministerial responsibilities* na ninachoshauri kabisa kwa Serikali hii kutokana na ubovu wa mkataba ulioingiwa kati ya kampuni ya *Indo Power* pamoja na Tanzania, uliosababishia hasara Tanzania na Serikali ya Tanzania nashauri wale Mawaziri wote waliohusika wawajibishwe. Hawa wana haja ya kupisha, kumwacha Mheshimiwa Rais afanye kazi zake vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa Mheshimiwa wetu mama Manyanya pale akishauri anaongea habari za rushwa, sisi kama Kamati tumefanya ziara kwenye ziara mbalimbali tunaambiwa huyu mama ni mpenda rushwa, mpaka wawekezaji wanashindwa kunakuja kuwekeza hapa Tanzania. Sasa leo kinachokuja hapa kutokea yeye anatuambia tunapenda mambo ya rushwa huku anatuambia mbaazi mboga, anakuja hapa mwingine anesema korosho ni dawa ya kuongeza nguvu za kiume. Wizara hiyo hiyo moja, sisi tunaangalia tu hamuwezi kutudhalilisha hivyo watu wa Mtwara.

MWENYEKITI: Kaa chini. Mheshimiwa Mwambe tuchangie kwa mujibu kwa kuzingatia kanuni za Bunge na kurudisha tena changia hoja yako bila kumtaja Mbunge kwa kumtaja jina.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *control* unayojaribu kuifanya ukweli huu utabaki

kuwa ukweli. Waheshimiwa hawa Mawaziri tunawalaumu watu wa Wizara ya Kilimo, lakini jambo hili la korosho linahusu watu wa biashara huyu mama yupo pale kwa muda mrefu amekaa na Mawaziri wawili hawezi hiyo kazi ampishe Rais afanye kazi hiyo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Hakuna mama humu, hakuna mama humu.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, Mheshimiwa Naibu Waziri yule pale. Tunasema hivyo kwa sababu tuna uhakika sisi tunazunguka kufanya mikutano na wawekezaji wanamlalamikia. Yeye ni mmoja ya watu wanaokwamisha juhudi za watu hata wenye viwanda, anawapa majibu ya hovyo, anakwenda kufanya ziara akiwa na *mood*, kitu ambacho ni kibaya kabisa. *She is out of mood all the time, you see*. Kwa hiyo tuombe kabisa waangalie kabisa namna ya kufanya tumsaidie Rais, Rais anawapenda wakulima, wasiowapenda wa kulima na wasiotaka kuwapa hela wakulima ndio walioanzisha haya matatizo, kuanzia waliotayarisha mikataba na sasa hivi hii Wizara inashindwa kuuza korosho. Msmu wa korosho unaanza karibuni, maghala ya korosho yamejaa korosho kule ndani, wakulima wanadai pesa zao, korosho haziondoki baada ya wiki tatu nne zijazo maghala yale korosho tunakwenda kuweka wapi na yenyewe yataharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa *old stock,* maana yake ni kwamba zitakapoanza korosho mpya hizi za zamani hazitanunuliwa. Hakuna mtu atakayetaka anunue korosho mbovu ambazo hana uhakika nazo. Kwa hiyo, niombe pamoja na kwamba mnazuia hizi taarifa tuliandika vizuri kabisa kwenye taarifa yetu ya Kambi Rasmi lakini zipo kwenye taarifa yetu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine baya kuliko zote, wadau mbalimbali wa korosho hawalipwi pesa zao. Rais ametangaza hata halmashauri hawezi kupewa pesa, halmashauri zetu zitajiendeshaje? Madiwani wanashindwa kulipwa Mheshimiwa Bobali amesema na hiyo sio halmashauri

moja. Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ambapo mimi natokea 85% ya mapato yake yanategemea ushuru wa korosho. Leo hii tunaenda kuambiwa pesa hizi hazitapelekwa, halmashauri zitajiendeshaje, tunashindwa kufanya kazi zetu pale kimsingi. Kwa hiyo tunaomba hili jambo liangaliwe kwa makini itumike busara hata kama bei ni mbovu tunafahamu Serikali wanalazimisha kuuza korosho kwa Sh.3,700 ndio ushauri mbovu unaotolewa na hawa watu tunaosema watoke wamuache Rais asadiwe, sisi tuna uwezo, natamani niwe Naibu Waziri Viwanda na Biashara na ndio nafasi yangu upande wa huku kwa sababu hawawezi waliopo pale na sisi ndio kazi yetu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine baya kuliko yote tuna Vyama vya Ushirika kule kwetu lakini havipewi pesa zao kwa wakati, tunaomba wamsaidie Mrajisi Mkuu, tunafahamu sasa hivi huyu Mrajisi aliyepo ni wa pili baada ya yule wa kwanza kushindwa kutimiza majukumu yake. Naye hapelekewi pesa imeandikwa kwenye vitabu hapa, Serikali hii ndio haimpelekei pesa, atafanyaje kazi zake, atatimizaje wajibu wake kule chini, tunaua Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuja jambo la *kangomba,* nishukuru Mheshimiwa pale amesema kwamba *kangomba* anatambua kwamba ni wajasiriamali lakini tuwaambie kabisa *kangomba* inazaliwa kutokana na ubovu wa kutekeleza mikakati ya Serikali. Serikali zamani ilikuwa na utaratibu wa kupeka pesa kwenye Vyama vya Ushirika, lakini utaratibu huu umeachwa. Sasa wale wananchi kati ya mwezi wa Tano mpaka wa Nane waniishi kwa kutumia nguvu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aibu kabisa, tunazidi kudhalilishwa, Mheshimiwa Waziri anafikiri sisi Mtwara hatuna uwezo wa kuzaana, juzi anaongea na waandishi habari anasema kwamba kuleni korosho kwa wingi zinaongeza nguvu za kiume, sio malengo ya sisi kulima korosho kuongeza nguvu za kiume. Tulikuwa tunalima korosho ili tuweze kupata pesa kigeni, nchi yetu iweze kupata pesa kigeni maendeleo yasonge mbele leo unasimama Waziri ambayo ndio unamsaidia Rais anatuambia kuleni... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Heche na Mheshimiwa Richard Mbogo ajiandae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Kilimo. Awali nimpongeze Mheshimiwa Waziri aliyepewa dhamana ya Wizara hii ameanza na mwanzo mzuri...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Naomba utulilvu Bungeni.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameanza na mwanzo mzuri, naamini akisaidiana na wasaidizi wake watafanya kazi vizuri ya kuisimamia Serikali na Wizara kwa ujumla. Nianze kwa ushauri, Mkoa wa Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe na Ruvuma hii ni mikoa ambayo inazalisha chakula kwa wingi sana. Kazi ya Serikali ni kuwawezesha hawa wakulima wasikate tamaa. Mwaka jana wakulima wa mazao ya mahindi na mpunga wamekula hasara sana kutokana na Serikali kufunga mipaka na kuwazuia wakulima wasiuze mazao yao kwenye masoko ya nje. Nashauri hili kosa tulilolifanya tusije tukalirudia tena, wakulima wanazalisha mazao yao kwa nguvu zao binafsi na hawasaidiwi kitu chochote, muda unapofika mazao yao kuyauza Serikali inaleta vikwazo, tunawaletea umaskini sana. Tunalo soko la kongo, Rwanda na Burundi, sasa hivi maeneo yote hayo yana uhitaji wa kuhitaji mahindi na nafaka nyinginezo. Kwa hiyo nashauri kosa la kuzuia mazao haya lisifanyike tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba waweke mazingira wezeshi ili kusaidia mazao ambayo yanazalishwa kwa wingi hasa Nyanda za Juu Kusini yapate dirisha la kutokea eneo la Sumbawanga kwenye Bandari ya Kasanga

ili yaweze kwenda nchi ya Congo. Nchi ya Congo mazao haya yanahitajika muda wote, wenzetu kule hawalimi kwa sababu ya vita vinavyotokea mara kwa mara. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi eneo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaloshauri kwa Serikali ni kupeleka pembejeo kwa wakati. Mwaka huu uzalishaji wa mazao ya mahindi si mkubwa sana kwa sababu Serikali ilishindwa kupeleka pembejeo kwa wakati. Nimwombe Mheshimiwa Waziri aendelee kufanya utafiti na wawaachie Vyama vya Ushirika viweze kupeleka na kusambaza pembejeo kwa wakulima wake ili waweze kuzalisha kwa wakati. Kuingilia hizi pembejeo kwa Serikali tunaona tunafanya makosa makubwa, tunapeleka kipindi ambacho si cha uzalishaji. Niombe eneo hili wakalifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mazao ya biashara. Jimboni kwangu tunazalisha, tumbaku, kahawa na pamba. Haya mazao ya biashara Serikali inatakiwa kwanza ikae na makampuni ili waweze kuangalia mazingira rafiki yatakayowezesha kusaidia ununuzi wa mazao haya. Zao la pamba ambalo limezalishwa Mpanda hasa katika Wilaya ya Tanganyika ni zao ambalo limepokelewa vizuri kwa wananchi na niipongeze Wizara ya Kilimo kupitia Bodi ya Pamba, wamewasaidia sana wakulima na takribani tuna matarajio ya kuzalisha karibu kilo milioni 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana bado hatujakuwa na uhakika wa soko la zao hili. Makampuni yanayonunua zao hili ni makampuni manne tu kiasi kwamba yanatia wasiwasi kwamba pamba iliyozalishwa Mkoa wa Katavi upo uwezekano ikakosa soko la uhakika. Tunaomba Waziri alifanyie kazi, asukume makampuni mengine yaweze kwenda kununua pamba katika eneo hilo na pamba inayozalishwa kule ni nzuri na walionunua kwa awamu ya kwanza wamesema ni pamba ya *grade one* ambayo imepatikana kwenye mnada wa kwanza uliofanyika kwenye eneo la Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie zao la tumbaku, zao hili ndilo lilikuwa linaongoza hapa nchini kwa kuleta fedha nyingi za kigeni na tulikuwa tuna uzalishaji mkubwa wa zaidi ya kilo milioni mia moja. Ni zao ambalo lilikuwa linaongoza kwa nchi yetu kuleta fedha nyingi za kigeni, lakini kwa sasa linaporomoka siku hadi siku, kutoka uzalishaji wa kilo milioni mia moja kwa sasa uzalishaji ni wa kilo milioni hamsini. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kunusuru hili zao. Kwanza wakae na makampuni ambayo yananunua zao la tumbaku, sasa hivi kuna tetesi kwamba kampuni la *TLTC* ambalo linanunua kwa kiwango kikubwa linaondoka hapa nchini kwa sababu ya mazingira kutokuwa rafiki kwao. Niishauri Serikali yangu wakae na haya makampuni zao la tumbaku ni zao ambalo linalimwa kwenye mikoa mingi katika nchi yetu, watafanya mdololo wa kiuchumi wasipofanya shughuli ya kufuatilia hili zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie miradi ya umwagiliaji, miradi mingi ya umwagiliaji Serikali imeitelekeza na karibu ambao waliopewa dhamana ya kuisimamia wameshindwa kabisa na wengi waliipiga hii miradi, niombe Serikali wafuatilie hii miradi. Ninao Mradi wa Skimu ya Karema, kunaMmradi wa Skim ya Mpailo na Mradi wa Skimu ya Kabage, bado hiyo miradi yote haijakamilika. Niombe Serikali hebu watumeni wataalam waangalie kifo cha fedha zilizotengwa na Serikali ambazo kimsingi mpaka sasa hazionekani kwamba zimefanya shughuli gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa suala la pembejeo, naomba utaratibu wa pembejeo ubadilike na tunaomba sana hasa kwenye suala la tumbaku, utaratibu uliozoeleka huko nyuma hebu waviachie Vyama vya Ushirika viweze kufanya kazi yake ili viweze kupeleka kwa wakati na ni jambo jema kwao wao. Serikali wanapowaachia vyombo vingine vinapofanya kazi hata wakifanya makosa Serikali itakuwa na nafasi ya kuelekeza mkono wake kwamba chombo hiki wakisimamie...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kakoso. Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze na jambo moja hapa. Hakuna kanuni yoyote ya Bunge hili ambayo inamzuia Mbunge kuzungumza kuhusu Waziri yeyote kwenye hili Bunge. Kwa hiyo naomba tafadhali tanapokuja hapa tunalipwa pesa za walipakodi wa nchi hii ili tufanye kazi yao. Sasa haya mambo ya kusumbua watu wakati wanachangia sio mazuri. La kwanza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tumezungumza sana kuhusu kilimo, wazungu walipotaka kuanza kuendelea *Agrarian Revolution* ndio ilikuwa ya kwanza karne ya 16. Kati ya mambo makubwa mawili ambayo Serikali yenu kuyasabishwa yamedharaulika katika nchi hii ni kilimo na ualimu, ambayo ni mambo ya muhimu kweli kweli. Ukiangalia mwanafunzi anayekaribia kufeli shule utasikia familia yake inamwambia ameshindwa hata ualimu, ndipo mlipoufikisha ualimu wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo, mtu akikaribia kuonekana hawezi kusoma vizuri wanamwambia utarudi kupiga jembe, kilimo ndicho kinawatajirisha watu na ndicho kinachotoa chakula cha 100% kwa watu, kinatoa ajira 80%, kinatoa malighafi za viwandani na kilimo ndio kila kitu. Sasa wamefanya *vice versa* na ndio maana tukiwaacha kuendelea kuiongoza nchi hii hata miaka 1,000 hamuwezi kutuondoa hapa, hata miaka 1,000. Ndio maana mwaka 2015 wakati Serikali hii inayojiita ya wanyonge inaingia madarakani, bei ya kahawa pale Tarime ilikuwa Sh.2,200. Sasa hivi tunavyozungumza Mheshimiwa Hasunga bei ya kahawa ni Sh.800, *are we moving forward* au tunarudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama bei ya kahawa ni Sh.800 kwa wakulima ambao wameanza kujitegemea, kwa wakulima ambao alikuja Naibu Waziri Tarime, wamechukua kahawa ya wakulima watu maskini Kata za Muriba, Itiryo, Mbogi, kata nyingi tangu mwezi wa Saba mwaka jana

hawajawalipa mpaka leo na wanasema wao ni Serikali ya wanyonge. Halafu wanasimama watu humu kwa sababu wao wanalipwa pesa za kodi ya watu maskini, wanafungiwa mikanda kwenye gari, wanajisahau wanajiona *ma-queen na ma-king,* wanasahau kwamba hizo ni pesa za walipakodi maskini, sasa wanasimama huku, wanawafanyia maudhi Watanzania waliowapa huo ukubwa wanaotamba nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwamba Waziri anaweza kusimama hapa akapinga kwamba Watanzania hawazidi kuumia kwa sababu ya aina ya jinsi mnavyochukulia Kilimo. Sasa leo mmechukua kahawa ya watu, mwezi wa saba. Nani angeambiwa hapa tangu mwezi wa saba hatulipwi posho au hatulipwi mshahara kama mngekanyaga hapa, hata hela za mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Watanzania wajue, mpaka mafuta mnayokwenda nayo Bungeni na kurudi mnalipwa na Watanzania. *You are being paid millions of money* za walipa Kodi maskini; sasa tunaposimama hapa, hebu tuwafikirie pia waliotusababisha tukaja hapa, la kwanza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu Korosho. Katika hili naanza kwa kuweka mezani kwako hapo watu wako wachukue, gazeti la Daily Nation la Kenya la tarehe 12 lilisema Serikali ya Tanzania yaingizwa chaka na kampuni ya kihuni ya *Indo power*, ambayo leo mnataka mui-*protect*. Ninataka niwaambie, hamtai-*protect* mkii-*protect* humu tunazungumza nje. *(Makofi) (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, hiyo zabuni ya kuanza kuzungumza na hiyo Kampuni ilitangazwa wapi? La kwanza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nani aliyekuwa anafanya mazungumzo ya awali na hiyo Kampuni ya *Indo power*, ambayo gazeti hili la *Daily National* linasema halina hata ofisi kule Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na hili ni jambo la aibu, na tunakuja humu mambo makubwa tunayafanya mambo madogo kwa sababu ya mizaha. Sasa nataka mtuambie hivi kama gazeti mwandishi mmoja tu anaweza kufanya uchunguzi akajua hii Kampuni haina ofisi, ni Kampuni ya kitapeli, Serikali nzima mnampeleka Gavana wetu wa Benki Kuu pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnapeleka Mawaziri watano, mko hapa kwenye picha, mlikuwa pale, akiwemo Profesa Palamagamba Kabudi, ambaye mnam-*protect* hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani alianza kuzungumza na hiyo Kampuni? Nataka mtuambie je, hiyo Kampuni, yaani gazeti la *Daily National* la mwandishi lina uwezo wa kuchunguza kuliko Serikali yetu? Muwaambie Watanzania, muwaambie Watanzania na kama si hasara mtuambie; unakuja unatuambia hapa Kabudi anasema eti huyu mtu alikuja na ndege, so what? Mimi na Esther Matiko tunakodi *helicopter* tunaenda Tarime, kwa hiyo sisi ni wawekezeji? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eti, kwani, yaani mawazo yenu, Waziri kabisa anasimama, eti hii ni Kampuni nzuri kwa sababu huyu mtu ni Mwekezaji, *serious* amekuja na ndege. Freeman Mbowe huyu anamiliki *Caravan*, Godbless Lema anamiliki Ndege ya watu 16, sasa na yeye ni Mwekezaji? *(Makofi/Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Gwajima.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Gwajima, amepaki pale *Helicopter* yake. *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Heche ongea na Kiti wewe, changia, changia. Jielekeze kwenye hoja sasa, mambo, jielekeze kwenye hoja. *(Kicheko)*

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hii Kampuni ilipatikanaje?

MBUNGE FULANI: Dakika za Heche....

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ya muhimu tunataja kujua, nani alianza kuzungumza nao? Tunataka kujua; *common sense* ya kawaida, ukimsikia Profesa Palamagamba Kabudi, na Gavana wa *BOT* Profesa *common sense* inakataa, kwamba hawawezi kufanya maamuzi ya vile, kama si rushwa basi hawawezi kuongoza hata kibanda cha kuuza nyanya hawapaswi kuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawapaswi kabisa, na hili suala Watanzania maskini...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche, hivi mnataka nifanye nini sasa? Nimeshaitolea uamuzi, *you may not like my ruling* lakini ndio uamuzi wangu.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Kule Kusini kuna Watanzania wenzetu ambao ni wakulima wa korosho, na sisi Wabunge tuko hapa ku-*protect* watu wetu. Kuna Watanzania kule korosho ndio mshahara wao, kama ninyi mnavyolipwa kila mwisho wa mwezi. Korosho ndiyo karo ya watoto wao, Korosho ndiyo malipo ya benki wanayodaiwa wamekopa wamejenga. Kwa hiyo tunapozungumza haya masuala tuyazungumze kwa uzito huo. Ndiyo maana sisi tunasema, kama alivyosema mtu anayekaimu nafasi Waziri Mkuu; kama kweli Serikali nzima, mna *collective responsibility* na mnakubali kwamba kosa la kuingiza nchi kwenye aibu gazeti la Kenya linatuandika. Pamoja na mambo yote tunayoweza kufanya humu, Rais wa nchi, nje ya nchi ni *Symbol* ya nchi, na tutam-*protect*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa gazeti hili limesema, pamoja na kwamba umesema hivyo, wewe tunaamini kauli yako ni ya Waziri Mkuu. Leo kama mna uadilifu wa kutosha,

Serikali nzima *resign* kwa sababu mmeaibisha nchi yetu vya kutosha kwa kwenda kuingia na Kampuni.... (*Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Heche. Tunaendelea, Mheshimwa Richard Mbogo na kama muda utaruhusu Mheshimiwa Chikambo. *(Makofi)*

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwanza nianze kumpongeza Waziri wa hii Wizara, Mheshimiwa Hasunga na Manaibu wako, Omary na Innocent na Watendaji wote katika Wizara hii ya Kilimo kwa kazi ambazo mnazifanya ili kuweza kuwanyanyua Watanzania ambao ndio wengi wako kwenye ajira hiyo kwa asilimia 65 kama ulivyoweza kueleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mchango wangu nianze kujielekeza kwenye zao la tumbaku pamoja na mazao mengine ya biashara. Kama wachangiaji wengine ambavyo wameweza kusema, kwenye tumbaku. uzalishaji unaenda unashushwa na wanunuzi, mpaka sasa imefikia tani 50,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kushusha huku kunatokana na soko ambalo wenyewe ndiyo wanalijua, lakini linaathiri sana wakulima wetu, ambao wameshaingia katika hiki Kilimo, lakini sambamba na ushushaji wa uzalishaji; hivi karibuni nilikuwa na swali la msingi tarehe 30 Aprili, kuhusiana na tozo kwa hawa wanunuzi. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi 2017 tulifanya mabadiliko ya sheria tulikuwa na *Amendment of the Local Government Finance Act, (Cap 290)* tuliweza kushusha *produce cess* kutoka asilimia tano mpaka tatu. Kwa kiwango hicho ambacho tulishusha maana yake ni nini? Tulitoa *discount* ya asilimia 40; na hii imepelekea kushusha mapato kwenye halmashauri zetu kwa sababu hii ni *produce cess* iko kwa *buyer. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kushuka huko kwa mapato imesababisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye halmashauri zetu umekuwa ni hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Serikali, mlisema kwamba mtafanya utafiti, haihitaji tuangalie utafiti, sisi tumeshafanya. Kwanza *discount* tu ya asimilia 40 hata kama uzalishaji uko pale pale, tayari mapato yameshuka, kwa hiyo tumeathirika na vitu viwili.

Mheshimimiwa Mwenyekiti, lakini pia, bado makampuni yanayonunua tumbaku katika Mkoa wa Katavi, tukienda Mbeya, Chunya pamoja na Ruvuma Kampuni ya *Premium* imegoma kulipa tozo hizi kwa sababu wanaidai Serikali kwenye marejesho ya *VAT refund (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tangu mwaka jana tumekuwa tukifatilia, sasa tuombe Serikali ije na tamko ni lini, Kampuni hii italipwa, na uhakiki tunajua kufanyika ni rahisi, ili halmashauri zetu na vyama vya msingi viweze kulipwa, maana haya tuna *payables* na *receivables* sasa na wao kwa kweli wamesimamia mahali ambapo wako sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na masoko ya mazao ya wakulima, mazao ya chakula na mazao ya biashara. Mikoa ya Katavi, Rukwa na Songwe, Mbeya mpaka Ruvuma tumekuwa tunazalisha sana mazao na hususan mahindi. Kuna vikwazo vilitokea, hasa kwenye ufungaji wa mipaka; na takwimu hapa wameonesha kwamba tuna ziada, na mkulima ambaye anahangaika ananunua Mbolea, analima hatimaye anahitaji apate bei nzuri ambayo atakuwa na fedha, na aweze kukidhi mahitaji yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke wazi mipaka watu waweze kuuza; na kama ilivyoelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengine, kwamba kuna sehemu nyingi na hususan kwenye nchi jirani ya *Congo DRC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uzalishaji wa tija. Serikali ije ituambie, kwa nini tuna uagizaji mkubwa wa malighafi za viwanda kwenye mafuta na ngano? Kwa nini tunaingia ngano asilimia 95 na tano, ndiyo ambayo inanunuliwa hapa Tanzania? Kwa nini iko hivyo na tunavuka kwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la utafiti. *TARI* iwezeshwe ili waweze kufanya utafiti; kama ni mbegu tuwe na mbegu zilizo bora, na mazao. Kwa mfano mahindi mengine sasa hivi ukishavuna baada ya mwezi mmoja tu yanaanza kubunguliwa. Sasa hebu twende na utafiti wa kutumia hizi taasisi zetu ambazo zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusiana na kilimo cha mara mbili katika mwaka, yaani cha umwagiliaji. Tuna miradi, kwa mfano Kata yangu ya Ugala katika Jimbo la Nsimbo, kuna mradi wa umwagiliaji mpaka sasa hauna ufanisi. Serikali mpitie upya tuone nini kifanyike ili wananchi waweze kufaidika.

Vilevile kutokana na mazingira; hivi tukichimba visima na ambavyo tuka-*reserve* maji haiwezekani kutumia katika umwagiliaji? Kama nchi ya Israel wana ile *drop irrigation* na sisi tuna maji ya visima hakuna uwezekano ili tuondokane na kugombana na Mheshimiwa January Makamba kuhusu uharibifu wa mito? Tuwe na *option* nyingine ya pili kwa maeneo machache, likiwa kama ni *pilot study*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Suala la *Financing*. *Tanzania Agriculture Development Bank* ipanue ku-*finance* na kukopesha watu. Masuala ya vikundi hayana tija; kuna msuguano watu katika kuungana. Sasa waone namna gani ya ku-*finance* mtu mmoja mmoja na *in a long term* na katika *interest* ambayo itakuwa iko ndogo. Maana tukiwezesha tukawa na *commercial farming*, maana yake tutazalisha kwa tija na tutakuwa na ziada ambayo tutaweza kuuza katika nchi hata Kenya. Kenya wanachukua mahindi Tanzania, wanauza South Sudan, kwa nini sisi tusiuze moja kwa moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukiongeza uzalishaji katika nchi yetu, tutaweza kuongeza na kunyanyua uchumi. Tunaona *GDP* kwenye Kilimo ina *90 percent* kwa data za 2013 lakini kwenye Pato la Taifa tuna *28.7 percent.* Kwa hiyo kilimo kwa ardhi tuliyonayo itaenda kuongeza sana. Pia uje utuambie mradi ule wa Mkulazi – Morogoro umefikia wapi? Isiwe kwa suala la uzalishaji wa mazao yanayotokana sukari, yaani miwa, pia mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. *(Makofi)*

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mwongozo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mujibu wa kifungu cha 68(7) niombe Mwongozo wako; labda pengine kwa ajili ya muda sina haja ya kusoma lakini nikihitaji mwishoni uweze kunipa utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Eng. Stella Martin Manyanya, ni mmoja kati Wabunge ambao wanapinga rushwa na wanaichukia rushwa kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo kwa sababu wakati Mheshimiwia Mwambe akichangia amenitamka kwa jina waziwazi kwamba anafahamu Viwanda vilivyonipa rushwa. Sasa kwa sababu ana ushahidi

huo, na mimi kwa sababu sitaki kujitetea, na ikizingatiwa kwamba niko kwenye nafasi ambayo natumikia Watanzania wanaoniamini, naona kwamba nikiliacha hivi hivi, yawezekana watu wakashindwa kuchukua huduma kutoka kwangu kwa sababu ya kujua kwamba mimi nachukua rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa ufahamu na uthibitisho wangu sijawahi kuomba wala kupokea rushwa popote pale. Kwa bahati iliyokuwepo ni kwamba Mheshimiwa Mwambe, angalau angesema amesikia tuhuma zinafanyiwa kazi, lakini amesema ana uhakika na amethibitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa mimi ningeomba kwa heshima kabisa, ataje hivyo Viwanda na rushwa zilizopewa au athibitishe kwa namna yoyote ile ili Watanzania waendelee kuwa na imani name, au kama ikithibitishwa mimi niko tayari kuwajibika katika hilo, ahsante. *(Makofi)*

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wako.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MWENYEKITI: Huwezi ukatoa muongozo juu ya muongozo Mheshimiwa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa hebu kaa chini. Waheshimiwa! Zima hiyo hicho kipazasauti chako. Mheshimiwa Frank Mwakajoka, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa yule wa nyuma yako yule, *please* hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nimeombwa muongozo na Mheshimiwa Stella Manyanya kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kutokana na hayo anayodai kwamba yamesemwa na Mheshimiwa Mwambe, na kama yanaruhusiwa na Kanuni hizi au laa.

Waheshiwa Wabunge, mliona nilivyo hangaika kuzuia tafrani humu, na ndiyo maana Kanuni zetu na hasa Kanuni ya 64 inayoainisha yale makatazo yote. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji aliposimama kuhusu utaratibu nilimruhusu. Akataja Kanuni na akaanza nikamruhusu, maana aliyekuwa anaongea alikuwa ni Mheshimiwa Msigwa, kwamba yeye ndiyo hajasema ukweli.

Sasa nilitegemea yeye angelifika kwenye kiwango cha kulithibitishia Bunge kwamba Mheshimiwa Msigwa hasemi ukweli. Ndiyo maana nilisema kwamba alienda kusema maneno mengine kutuhumu Kambi ya Upinzani, kwamba baadhi yenu; hakutaja majina kwamba baadhi yenu anaweza kuwataja mmoja baada ya mwingine kwamba mlifanya hivyo. Sasa nikasema amekimbia hoja aliyoombea utaratibu ndiyo maana nikasema hajafikia kile kiwango cha kuruhusu niliamulie hilo. Ndiyo maana nikasema akae chini tukaendelea. Sasa Mheshimiwa Mwambe kasimama katika kuchangia, akamwaga tuhuma, ni tuhuma kweli; lakini ningependa mimi niwaongoze kwa Kanuni hizi. Sisi wote ni binadamu, na kila mmoja wetu ana nyongo.

Huwa, ukifikishwa hapo na ndiyo maana Kanuni hizi zinatutaka wewe kama ni Mbunge na tunataka unaitwa huo, Uheshimiwa wako huo, uuonyeshe kwamba huji hapa kusema uongo, huji hapa kuzusha maneno na ukitakiwa kuthibitisha unathibisha au unakuwa muungwana unafuta kauli yako. Sasa katika hali hii mimi ningesema Mheshimiwa Mwambe kwa sababu wewe umeenda kuwa *very specific* sasa unaweza ukasema nina ushahidi wa kuthibitishia hayo niliyoyasema au unakuwa muungwana tu unasema nafuta kauli yangu.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, aanze huyo huyo, aanze yeye.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge naongoza Bunge, tuache matani hapa, Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwanza kwa namna ulivyoniongoza kwenye jambo hili. Mimi niko tayari kulithibitishia Bunge jambo ambalo limeliongea dhidi ya Mheshimiwa Stella Manyanya. Mimi ni Mjumbe wa Kamati; kuna wabangua korosho wametoka kwetu wanamlalamikia. Kwa hiyo niko tayari kuthibitishia Bunge kwamba aliomba rushwa. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa Mwambe, kwa mujibu wa Kanuni zetu sasa nakutaka ulete uthibitisho huo uwasilishe humu Bungeni siku ya Jumatatu kabla ya hoja hii haijahitimishwa, ili suala hili tuliweke vizuri. *(Makofi)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wako.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge hadi siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

(Saa 12:00 Jioni Bunge Liliahirishwa Hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 20 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)